

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 14 Juni, 2022**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (*Monetary Policy Statement*) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Taarifa ya Ukaguzi wa Fedha za Msaada zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa kupitia Programu ya Kudhibiti na Kupambana na Majanga kuanzia Juni, 2020 hadi Aprili, 2022 (*Report on the Audit of Utilization of Funds issued under Catastrophe Containment and Relief Trust Facility from June, 2020 to April, 2022*).

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu sasa aulize swali lake.

Na. 387

**Ujenzi wa Barabara Katika Mji wa Karatu**

**MHE. DANIEL T. AWACK** aliuliza:

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara za ndani za kilometa 10 katika Mji wa Karatu kwa kiwango cha lami iliyotolewa na Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, Mbunge wa Jimbo Karatu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 barabara NBC - Kudu yenye urefu wa kilometa 0.6 ilijengwa kwa gharama ya shilingi milioni 350. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, ujenzi wa barabara za Tarafa - Ari Mpya, TRA - Mahakamani na NBC - Kudu zenye urefu wa kilometa 0.9 kwa

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

gharama ya shilingi milioni 499.99 ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 78 na zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Canivo - Buchani kilometa 0.53; Posta - Malliasili kilometa 0.10 na Bambras - *Continental* kilometa 0.100 zenye jumla ya urefu wa kilometa 0.73 zinaendelea kutekelezwa ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 70. Kwa upande wa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kilometa 0.62 kwa kiwango cha lami kwa barabara za Gorwa, Posta – Mailimbili, Bampras *Continental* na *Rhotia Pharmacy*. Serikali itaendelea kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara za Mji wa Karatu kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Tlemai, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL T. AWACK:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ahadi hii ya kilometa kumi ni toka Rais wa Awamu ya Nne, na leo tuko na Rais wa Awamu ya Sita; je, ni lini ahadi hii ya kilometa kumi itatekelezeka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mji wa Karatu uko *center* ya mji wa kiutalii, kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, *Lake Manyara*, *National Park* na hifadhi ya Serengeti. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kujenga kilometa kumi ili kuimarisha mji uwe wa kiutalii katika Mji wa Karatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVIDE E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daniel Awack, Mbunge wa Jimbo la Karatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Serikali tutaendelea kutenga fedha kila mwaka kuhakikisha ahadi za viongozi wetu wakuu ambazo walizotoa zinatekelezeka katika Jimbo la Karatu. Serikali inaona haja muhimu kabisa ya kuhakikisha kwamba barabara hizo zinakamilika kwa sababu ya umuhimu wa eneo la Karatu hususan katika sekta ya utalii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, katika Mji wa Mbalizi, kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais wa kujenga barabara za mitaa kwa kiwango cha lami; je, ni lini barabara hizo zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika mchakato wa kutafuta fedha, na mara utakapopata fedha hizo maana yake tutaanza ujenzi ili kukamilisha ahadi za viongozi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeahidi kujenga barabara kilometa tano kwenye Mji wa Hyadom; je, ni lini Serikali watatimiza ahadi ya kujenga kilometa hizi za lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua ahadi ambazo viongozi wametoa ikiwemo katika eneo la Hyadom, katika Jimbo la Mbulu Vijijini ambako hadi sasa tunatafuta fedha na tumeendelea kutenga kila mwaka hizo fedha ambapo tutakuwa tunapeleka katika maeneo hayo ili kukamilisha ahadi hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mji wa Nkwenda ni moja kati ya miji ambayo iliahidiwa kujengewa kilometa tano za lami, hata hivyo kilometa tano hazikujengwa ndani ya mji zilijengwa katika barabara ya *TANROADS* ambayo inapita nje ya mji.

Sasa nataka kujua ni lini kilometa tano zilizoahidiwa kujengwa katika barabara za ndani ya Mji wa Nkwenda zitajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua ahadi za viongozi hususan katika maeneo yote ikiwemo eneo la Kwera ambalo umeliainisha hapa Nkwenda na kwa hili ambalo amelieleza ni kwamba Serikali itaendelea kutekeleza kadri ambavyo tutapata fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuiuliza Serikali; ni lini kilometa tano zilizoahidiwa na Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano katika Mji wa Nguruka zitajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa ahadi zote za viongozi tumeshazichukua pale Ofisi ya Rais – TAMISEMI na jukumu letu la sasa ni kuzitafutia fedha ili kuhakikisha kwamba zinaanza kutekelezeka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke sasa aulize swali lake.

Na. 388

### **Kuboresha Barabara za Manispaa ya Temeke**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupanua wigo wa miradi ya kuboresha barabara za mitaa ya Manispaa ya Temeke hasa Jimbo la Temeke kupitia *DMDP*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke kama ifuatavyo:-

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa *DMDP* Awamu ya Kwanza inajenga mtandao wa barabara wenye jumla ya kilometa 48.243 kwa gharama ya shilingi billion 60.9 katika Jimbo la Temeke kwa Kata za Mtoni kilometa 9.623; Makangarawe kilometa 10.402; Yombo vituka kilometa 7.710; Kilakala kilometa 10.53; Keko kilometa 0.462; Buza kilometa 1.7; na Kata za Changombe, Sandali, Temeke na Azimio zimejengwa kilometa 7.8. Kwa sasa kilometa 46.543 zimekamilika na zinatumika na kilometa 1.7 za Buza zilizosalia zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Septemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa *DMDP* Awamu ya Pili katika Jimbo la Temeke imependekezwa kujengwa mtandao wa barabara wa jumla ya kilometa 53.10 kwa kiwango cha lami zinazokadiriwa kugharimu shilingi billioni 69.5. Ofisi ya Rais – TAMISEMI imewasilisha mapendekezo hayo Wizara ya Fedha na Mipango ili iwe sehemu ya mzunguko wa 20 wa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia katika Mkoa wa Dar es Salaam unaotarajia kuanza mwezi Julai, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini kwa kuwa Jimbo letu la Temeke limepata kilometa 53.10; je, huoni haja ya Serikali kufanya mazungumzo na Benki ya Dunia mapema ili kweli Julai hii hizo barabara zianze kujengwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa katika jibu lako la msingi umenijibu kwamba kuna kata ambazo tayari zimeshafanyiwa ukarabati na barabara hizo zinatumika. Niombe kusema kwamba katika Kata ya Chang’ombe, Sambali, Keko, Azimio, Temeke 14 na Miburani sijapata kuona hizo barabara.

Je, uko tayari kuandamana na mimi twende tukazione hizo barabara katika jibu lako la msingi?  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mapendekezo hayo yameshapelekwa na yapo Wizara ya Fedha, na mazungumzo yanaendelea, ni imani yangu kwamba haya mazungumzo yataisha kama ambavyo tulikubaliana mwezi wa saba ili sasa huu mradi wa kwa Halmashauri ya Temeke na Jiji la Dar es Salaam uweze kufanya kazi. Nimhakikishie niko tayari tunaweza tukaongoza na yeye siku ya Jumamosi, *weekend* hii kwenda kuziona barabara hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa Swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuwa Jimbo la Temeke linapakana na Jimbo la Ukonga na sisi ni wanufaikaji wa mradi kwenye Kata za Ukonga na Gongolamboto.

Naomba sasa kujua nini mkakati wa Serikali kuhakikisha mradi huu kwa awamu ya tatu unazinufaisha Kata za Majoe, Kivule, Kitunda na Chanika katika barabara za Pugu, Majohe – Gwera katika barabara ya Kitunda, Kivule, Msongola...

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa hilo ni swali la nyongeza, unataka kumaliza barabara zote kweli? (*Kicheko*)

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali la kwanza kabisa.



**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, aondoe shaka, kuhusu utekelezaji wa mradi huu kwa kuwa ni mradi unaohusu jiji zima la Dar es Saalam ikiwemo katika Jimbolake la Ukonga. Kwa hiyo mara utakapokamilika barabara alizozianisha ziko katika huo mpango, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, Mji wa Mafinga ni miongoni mwa miji 45 itakayonufaika na mradi wa *TACTIC* ambayo pia Jiji la Mbeya lipo.

Je, Mheshimiwa Waziri, uko tayari kukutana na Wabunge wa miji hiyo 45 ili kutueleza maendeleo ya mradi huo kama tulivyofanya kwenye miji 28 maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na kwamba Mbeya imetajwa humo, lakini hapa swali la msingi ni *DMDP*. Kwa hiyo, unao uhuru unaweza kulijibu hilo swali kama majibu unayo, kama huna litakuja kama swali la msingi kwa ajili ya hii miradi ya *TACTIC*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, nitamwambia Waziri wa Nchi na tutakutana na Wabunge wote katika hiyo miji 45 ili kuwaeleza juu ya utekeleza wa mradi huo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi; je, Serikali ina mpango gani wa kuzitumia fedha zilizobaki katika utekelezaji wa mradi huu wa *DMDP* Awamu ya Kwanza katika kuziboresha barabara za Jimbo la Mbagala na Jimbo la Temeke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri na tutakwenda kushauriana na wataalam juu ya utekelezaji wa mabaki wa hizo fedha ambazo zimebakia, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Jimbo la Kawe, katika Wilaya ya Kinondoni lina mtandao mkubwa wa barabara kuliko majimbo yote ya Dar es Salaam; je, Serikali inaweza kusema ina mkakati gani kuongeza nguvu kuongeza barabara kutengeneza kupitia *DMDP* awamu ya pili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Askofu Josephat Gwajima, Mbunge wa Jimbo la Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba tunatambua ukubwa wa Jimbo la Kawe kama ilivyo katika majimbo mengine na tunatambua umuhimu wa kuongeza bajeti. Na katika mradi *DMDP* moja ya vigezo ambavyo umezingatia ni pamoja na ukubwa wa maeneo. Kwa hiyo, mgawanyo utalizingatia ukubwa wa maeneo husika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 389

**Kukarabati na Kupanua Vituo vya Afya Korogwe Vijijini**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kuboresha na kupanua Vituo vya Afya vya Bungu, Magama na Mombo ambavyo vinahudumia wananchi wengi?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza ujenzi wa vituo vya afya kote nchini ikiwemo katika Jimbo la

Korogwe Vijijini. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imepeleka shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya Mnyuzi na Kerenge katika Jimbo la Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vituo vya Afya vya Mombo, Bungu na Magoma Serikali inafanya tathmini ya vigezo stahiki kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza vituo hivi vitatu vya Bungu, Magoma na Mombo ni vituo vya muda mrefu na vinahudumia eneo kubwa; ni lini sasa hiyo tathmini inafayofanya na Serikali itakamilika ili Serikali ipate nafasi ya kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya maboresho?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, vituo hivi nilivyovitaja karibu kila kituo kimoja kinahudumia tarafa nzima, kata zaidi ya tisa. Zipo kata ambazo tumeziainisha kwa ajili ya vituo vya kimkakati; ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya vituo vya mkakati kwenye Jimbo la Korogwe Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vituo hivi vya afya vitatu ni vituo vya siku nyingi na Serikali tayari tulishapeleka wataalamu kufanya tathmini ili kuona majengo yanayohitajika, lakini na gharama ambazo zinazohitajika.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakamilisha mapema iwezekanavyo ili Serikali iweze kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kuongeza majengo yanayopungua katika vituo hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu na vituo vya afya vya kimkakati, Serikali imeshaainisha maeneo yote nchini kote ambayo yanahitaji vituo vya afya vya kimkakati ikiwemo kwenye Jimbo la Korogwe Vijijini na fedha zinatafutwa kwa ajili ya ujenzi kwa hatua kadri ya upatikano wa fedha, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Katika Jimbo la Njombe Mjini kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya kupanua Kituo cha Afya cha Njombe Mjini kwa sababu hakina wodi za wanaume. Ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Njombe Mjini ni moja ya vituo ambavyo Serikali tayari imeanza kufanya tathmini ya majengo ambayo yatahitajika ili utanuzi uweze kufanyika na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hiyo itafanyika na tunatafuta fedha kwa ajili ya kupanua Kituo cha Afya cha Njombe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imejenga kwa mapato yake ya ndani kituo cha afya chenye hadhi ya hospitali eneo la Kalema, Kata ya Ikola, kituo hicho kimekamilika, tatizo lililopo ni ukosefu wa wataalamu na vifaa tiba.

Je, ni lini Serikali itawaunga mkono kwa kuwapelekea vifaa tiba na wataalamu ili kile kituo kianze kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze sana halmashauri hii kwa kujenga kituo cha afya kwa mapato ya ndani, lakini nimwakikishie kwamba katika ajira ambazo zinaendelea hivi sasa ambazo kufikapo Julai Mosi watumishi watapelekwa katika vituo vyetu tutahakikisha kituo hiki pia kinapelekwa watumishi ili kianze kutoa huduma. Lakini katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ambavyo vitapelekwa ili kituo hiki kiendeleo kutoa huduma za afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kufahamu ni lini Serikali itatuboreshea Kituo cha Afya cha Isasa kwa maana ya kutujengea wodi ya akina mama pamoja na wodi ya akina baba? Ahsante.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuainisha vituo vyote ambavyo vina majengo pungufu ili kuyajenga kwa awamu. Kwa hiyo, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Juliana Shonza ili tuweze kuona majengo yapi yanapungua, gharama kiasi gani inahitajika ili tuanze kujenga majengo yanayopungua, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sangu swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Kituo cha Afya Msandamuungano ni kati ya vituo vya afya vilivyoko ndani ya Jimbo la Kwela na kina miundombinu chakavu kimekuwa cha muda mrefu; je, Serikali mna mpango gani wa kuboresha hiki kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumefanya tathmini ya vituo vyote kote nchini, vituo chakavu, hospitali chakavu ambazo zitapangiwa bajeti kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Tumeanza na hospitali za halmashauri, lakini tutakwenda na vituo vya afya ili kuvikarabati au kuviongezea majengo.

Kwa hiyo naomba nichukue hoja yako Mheshimiwa Sangu ili tufanye tathmini pia katika kituo hicho na kutafuta

fedha kwa ajili ya ukarabati na kuongeza majengo ya maeneo hayo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Kata ya Kitanga iko kilometa 77 kutoka yalipo makao makuu ya Wilaya. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kigezo kimojawapo cha kujenga vituo vya afya ni umbali wa eneo hilo husika kutoka kituo cha afya au hospitali ya karibu. Kwa hiyo kwa kilometa 77 bila shaka tunahitaji kuwa na kituo cha afya. Niagize Mkurugenzi wa Halmashauri hii kuhakikisha wanafanya tathmini ya kutafuta eneo, lakini pia watuletee maombi hayo kwa ajili kujenga kituo cha afya katika eneo hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaboresha na kupanua Kituo cha Afya cha Mvomero? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.



**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye mpango mkakati wa kupanua na kuboresha vituo vya afya tutahakikisha pia tunakifanyia tathmini kituo hicho na kutenga fedha ili tuende kukarabati na kupanua kituuo hicho kwa awamu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa pale mkoani Rukwa kwa sababu tayari eneo limetengwa, lakini Serikali bado haijaanza ujenzi. Ni lini Serikali itaanza ujenzi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI hilo nahisi linamuhusu Naibu Waziri wa Afya ama ni la kwako TAMISEMI? Ni la Afya ni la TAMISEMI?

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya au Waziri wa Afya. Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye bajeti ya mwaka huu imepangiwa kwa ajili ya kufanya ujenzi kwenye eneo ambalo amelitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Napenda kuiuliza Serikali je, ni lini Serikali itaanza kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati za Kibata, Kandawale na Miguruwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha peke yake Serikali imeendelea kujenga vituo vya afya katika maeneo ya kimkakati na mpaka Juni hii tayari tumeshajenga vituo vya afya 234 nchini kote na mpango huu ni endelevu, tutahakikisha tunaendelea kujenga vituo vya afya ikiwemo katika Jimbo la Kilwa Kaskazini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela, Kata ya Buswelu walijenga hospitali. Baada ya ukaguzi ikaonekana maeneo yale ni madogo ikahamishiwa Kata ya Sangabuya kwa ahadi kwamba maeneo yale yatakuja kupewa kituo cha afya. Lakini leo ni zaidi ya miaka minne hayajawa kituo cha afya; jje, ni lini Serikali itaweka kituo cha afya katika majengo yale yaliyoko Kata ya Buswelu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi uliopita nilitembelea eneo hili la Kata ya Ilemela eneo la Buswelu na kuona yale majengo ambayo yamejengwa na Wizara ya Afya, lakini na jengo moja ambalo lilijengwa kwa ajili ya kituo cha afya, na nilitoa maelekezo majengo yale ifikapo mwisho wa mwaka ujao wa fedha yaanze kutoa huduma kama kituo cha afya badala ya kubaki bila kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeshalifanyia kazi hilo na nimwakikishie kwamba litakwenda kukamilika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa sasa aulize swali lake.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Buchosa naomba sasa swali langu namba 390 lipate majibu ya Serikali.

Na. 390

**Kupandisha Hadhi Zahanati ya Maisome – Buchosa**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Zahanati ya Maisome kuwa Kituo cha Afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric wewe uko hapa tayari kwa niaba yao hao wananchi wa Buchosa. Kwa hiyo, huna haja ya kurejea kuwa uko hapa kwa niaba yao.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika; kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo Mbunge wa Jimbo la Buchosa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa miongozo ukubwa wa eneo la kituo cha afya linatakiwa kuwa na angalau ekari nne katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali haikuipandisha hadhi Zahanati ya Maisome iliyopo Kijiji cha Kanoni kuwa Kituo cha Afya kwa sababu ya kukosa eneo la ujenzi. Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepeleka shilingi milioni 500 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye Kata ya Maisome, Kijiji cha Kanoni. Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje na jengo la maabara upo katika hatua ya ukamilishaji na ujenzi wa majengo ya wodi ya wazazi, jengo la upasuaji, jengo la kufulia na kichomea taka upo hatua ya awali, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena mwenye swali usiposimama, usipoitwa usilalamike. Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Zangu ni shukrani kwa sababu Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kituo hiki kijengwe baada ya mama mmoja kufia kwenye mtumbwi. Sasa nina swali moja tu la nyongeza.

Je, Serikali iko tayari kuifikiria Kata ya Bukokwa ambayo ina sifa zile zile kama Kisiwa cha Maisome ili iweze kupata kituo cha afya? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchoswa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee shukrani zake nyingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita na Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya katika Jimbo la Buchoswa na nchini kote kwa ujumla, na nimwakikishie tu kwamba kata hii ambayo ameisema ameshakuja kufatilia mara nyingi kuhusiana na uhitaji wa kituo cha afya na tayari tumeanza kufanya tathmini kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya, asante.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Mufindi kwa ujumla makao yake makuu iko kwenye Kata ya Mtwango, lakini eneo hilo mpaka sasa pamoja na kwamba imehamishiwa makao makuu Mafinga Kata ya Mtwango yenye *population* kubwa haina kituo cha afya; je, ni lini Serikali sasa itapeleka kituo cha afya pale kwa ajili kuhudumia kata hiyo na kata jirani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kata hii ya Mtwango ni kata kubwa na ina wananchi wengi na Mheshimiwa Mbunge ameisemea mara nyingi na tumekubaliana tunatafuta fedha kwenda kujenga kituo cha afya katika kata hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi; Kijiji cha Kizota Kata ya Muungano, Kindimbachini wanajenga zahanati tangu mwaka 2013, je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka uliopita peke yake ambao tunaumaliza Juni 30 Serikali imejenga jumla maboma 574 ya zahanati, lakini mwaka ujao wa fedha Serikali imetanga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa maboma 300 ya zahanati kuchangia nguvu za wananchi.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutakwenda kuona pia uwezekano wa kupeleka fedha kwenye boma hilo la zahanati, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 391

**Kiasi cha Fedha ambacho Serikali imekopa  
kutoka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Je, Serikali inadaidwa fedha kiasi gani ilizokopa Mifuko ya Hifadhi za Jamii na kiasi gani cha madeni kimelipwa na kwa utaratibu gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikopa fedha kutoka katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na deni la michango ya wastaafu waliokuwa katika utumishi kabla ya mwaka 1999. Mchanganuo wa madeni na kiasi kilicholipwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Mfuko wa *PSSSF* shilingi bilioni 506.88 na imeshalipwa shilingi bilioni 500 kwa utaratibu wa kibajeti; na deni la michango ya wastaafu waliokuwa katika utumishi kabla ya mwaka 1999 shilingi trilioni 4.46 na shilingi trilioni 2.17 zimeshalipwa kwa utaratibu wa hatifungani maalum. Aidha kiasi kilichobaki cha deni la Mfuko wa *PSSSF* shilingi bilioni 6.88 na shilingi trilioni 2.29 zitalipwa katika bajeti ya mwaka 2022/2023.

(ii) Mfuko wa *NSSF* shilingi bilioni 292.59 zilizokidhi vigezo baada ya uhakiki wa deni la shilingi bilioni 490.16 zitalipwa katika bajeti ya mwaka 2022/2023; na

(iii) Mfuko wa *NHIF* shilingi bilioni 80.68 zilizokidhi vigezo baada ya uhakiki wa deni la shilingi bilioni 209.72, zitalipwa katika bajeti ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuhakiki sehemu iliyobaki ya deni la Mfuko wa *NSSF* na *NHIF* ili yaweze kujumuishwa katika mpango wa malipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima James Mdee swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Waziri yanaonesha kwamba deni la *pre-1999* ni shilingi trilioni 4.4 lakini ripoti ya kikosi kazi cha Serikali yenyewe pamoja na ripoti ya *CAG* ambayo ilitolewa mwaka 2015 inaonesha deni la Serikali la *pre-1999* ni shilingi trilioni 7.1.

Sasa nataka Waziri uniambie hiyo tofauti ilitokea lini na wapi na kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili Mfuko wa *NSSF* umesema Serikali inadaiwa shilingi bilioni 292 ripoti ya *CAG* iliyotoka juzi inasema Serikali inadaiwa shilingi trilioni 1.17 hiyo tofauti kati ya bilioni 200 na trilioni moja imetokana na nini?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza alikuwa anaulizia tofauti imetokeaje, naomba hili tulichukue kama ni ushauri na tutamjibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili pia amehitaji tofauti tunaomba pia tulichukue na kwenda kufanya *review* bila shaka tutapata majibu yaliyo sahihi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge kama kuna kelele kelele hivi yuko sahihi kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu maswali yanayohitaji takwimu huwa anaweza kujibu hapo kama anazo, kama hana takwimu zinatolewa baadaye ndio kanuni zetu zinavyosema. Kwa hiyo, yuko sahihi kabisa majibu aliyoyatoa hapa.



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Bado swali moja Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 392

**Athari za kiuchumi kutokana na hali za kisiasa duniani**

**MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za kukabiliana na athari mbalimbali za kiuchumi zinazotokana na hali ya kisiasa duniani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inafuatilia kwa karibu athari na fursa za kiuchumi na kijamii zinazosababishwa na hali ya kisiasa duniani ikiwemo vita kati ya Urusi na Ukraine. Aidha, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kufanya tathmini ya athari za kiuchumi na jamii zinazotokana na vita ya Urusi na Ukraine kwa Tanzania;

(ii) Serikali kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kupunguza bei ya mafuta kwa kipindi cha kuanzia Juni 1, 2022;

(iii) Kuruhusu wafanyabiashara wenye uwezo wa kuleta mafuta kwa bei nafuu ili kuhakikisha uwepo wa mafuta

nchini. Mpango huu unatarajiwa kupunguza bei ya mafuta kuanzia mwezi Agosti 2022;

(iv) Kuhamasisha wafanyabiashara kuagiza ngano kutoka nchi nyingine zinazozalisha ngano ikiwemo Afrika Kusini, Canada, Australia, Uswiss na Ujerumani;

(v) Kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha mbolea nchini ambapo kutokana na uhamasishaji huo, kampuni ya *Itracom Fertilizers Limited* kutoka Burundi inaendelea na ujenzi wa kiwanda mkoani Dodoma. Kiwanda hicho kitakapokamilika kinatarajiwa kuzalisha tani 500,000 kwa mwaka.

(vi) Serikali kuendelea kutekeleza mikakati mahususi ya kukuza utalii wa ndani na kikanda kupitia fursa za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Kamisheni ya Utalii ya Shirika la Utalii Duniani kwa Kanda ya Afrika.

(vii) Kuimarisha sekta ya uzalishaji ikiwemo kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na tathmini ya hatua mbalimbali zinazopaswa kuchukuliwa kwa kila sekta ili kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na hali ya kisiasa duniani ikiwemo vita ya Urusi na Ukraine, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nancy Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwenye tathmini ya Serikali kati ya bidhaa ambazo zimeathiriwa na vita ya Urusi ya Ukraine ni mafuta ya nishati, mbolea na ngano.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufuta VAT kwa wazalishaji wa mafuta ya kula ndani ya nchi? (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala hili limejadiliwa na suala hili ni ushauri, linahitaji wataalam, tutakaa pamoja tutatoa majibu. Nadhani pengine leo ama kesho tutatoa jibu la suala hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour, Mbunge wa Tumbe sasa aulize swali lake.

Na. 393

**Serikali Kuwasaidia Wamachinga**

**MHE. KHAMIS MBAROUK AMOUR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wamachinga ili waondokane na umachinga na kuongeza mapato ya nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wamachinga ni fursa sahihi ya kujenga uchumi, Serikali itaendelea kusaidia wajasiriamali kifedha na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara, miundombinu na kurasimisha wajasiriamali ikiwemo wamachinga. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour, swali la nyongeza.

**MHE. KHAMIS MBAROUK AMOUR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri, kimsingi nina swali moja tu la nyongeza.

Je, Serikali ipo tayari kuwatambua hawa wajasiriamali wamachinga, nakusudia wa Tanzania nzima, wawe wa Tanzania Bara na Visiwani, halafu wakawaandalia mazingira ya kukopesheka benki? Je, Serikali ipo tayari kufanya hivyo? Ahsante.

**SPIKA:** Kuna kelele nilikuwa nazisikia hapa ndani, sijaelewa ni za simu au za kitu gani? Waheshimiwa Wabunge, tafadhali sana, tusisikilize *video* humu ndani wala tusizitazame *video* humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**  
Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeshaanza kutambua wamachinga Tanzania nzima ikiwemo Visiwani, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anafuatilia sana suala hili, tutaongeza juhudi na kuweka mipango stahiki ya kuwatambua na kuwawezesha wamachinga wote ikiwemo upande wa Zanzibar ambao tunaamini wanatakiwa kupewa fursa sahihi ili waweze

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kuendelea kufanya biashara zao kwa ukamilifu na kwa ufanisi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kati ya changamoto kubwa zinazowapata wafanyabisahara wadogo hawa tunaowaita machinga ni uwezo wa kupata mikopo kwenye hizi *financial institutions* zetu, na sababu kubwa ni kutokidhi vigezo, hasa dhamana na wale wachache ambao wanapata mikopo haswa kwenye hizi *micro-finance* riba ni kubwa sana hivyo inasababisha wao kushindwa kuendeleza biashara zao.

Je, Wizara imejipanga namna gani ili kuweza kuwasaidia watu hawa kwenye sekta hii niliyoitaja? Ahsante. (*Makoff*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, changamoto kubwa ambayo inawakumba wajasiriamali ikiwemo wamachinga ni changamoto ya kupata fedha au mitaji kwa ajili ya kufanya shughuli zao. Serikali inachukua jitihada mbalimbali ikiwemo kuweka fedha mahususi kwa ajili ya kuwasaidia wamachinga, kama ile asilimia 10 ya mikopo kupitia Halmashauri zetu, lakini pia zaidi kupitia taasisi zetu kama *SIDO* ambayo inahudumia viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo, tumeshaweka mahususi kwanza fedha, lakini pili tumekubaliana kupunguza ile riba ambayo mwanzoni ilikuwa

ni kubwa kwa hiyo, itakuwa chini ya asilimia 10, lakini zaidi tunaendelea kuongea na taasisi za kifedha za binafsi na ninyi ni mashahidi, tarehe 11 Aprili Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, alifungua ile kampeni ya teleza kidijitali ambapo mfanyabiashara au mmachinga mdogo anaweza kupata fedha bila kuwa na dhamana au kwenda benki kupitia simu ya kiganjani, wanasema *Mshiko Fasta* kuanzia shilingi 50,000 mpaka 500,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ni jitihada kuhakikisha tunamkomboa mfanyabiashara mdogo au mmachinga kupata fedha kirahisi zaidi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya mwisho ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nilitaka kumuuliza tu swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tunazungumzia sana asilimia kumi kama kuwafikia vijana, na tunatambua vijana wanaozungumzwa kwenye asilimia 10 zile asilimia nne zao ni vijana wanaoishia miaka 35 na machinga wengi wanazidi miaka 35.

Je, ni upi sasa mkakati wa Serikali katika kuwafikia machinga walio wengi zaidi ya hawa wa miaka 35? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, asilimia 10 zile zimelenga zaidi akinamama, vijana na wale wenye ulemavu, lakini kwenye kundi hili la vijana ni kweli wakishavuka ule muda wao maana yake wanakuwa hawawezi kukopesheka.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema Serikali inaendelea na juhudi mbalimbali ikiwemo kupitia taasisi za kifedha ili kuhakikisha wamachinga hawa, hawa wajasiriamali ambao watakosa fursa kwenye ile asilimia 10 ambayo inatengwa katika Halmashauri, basi wapate fedha kupitia taasisi nyingine kama nilivyosema *SIDO* na taasisi za kifedha nyingine ambazo zinatoa mikopo kwa wajasiriamali. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi kwenye Halmashauri wametenga maeneo kwa ajili ya wamachinga, namaanisha wamewajengea vibanda na vibanda hivi wanakwenda kuwapangisha. Hawa wamachinga mtaji wao ni kuanzia shilingi 20,000 mpaka shilingi 4,000,000; je, Halmashauri ziko tayari kuwapatia bure hivi vibanda kwa ajili ya kufanya biashara zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mikakati ya kuhakikisha tunawezesha wajasiriamali na hasa wamachinga ni kuwatengea maeneo, lakini pia kuwawekea miundombinu wezeshi ikiwemo vibanda hivyo ambavyo vinasaidia kufanya biashara zao katika mazingira mazuri, lakini kama ulivyosema katika Halmashauri huenda wanakusanya fedha kidogo kwa ajili ya kuvikarabati au kuhakikisha vile vibanda vinakaa muda mrefu viweze kuwasaidia wajasiriamali au wamachinga hao. Kwa sababu ametoa wazo hilo nadhani tutaongea na wenzetu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuona namna gani ya kuwasaidia vizuri zaidi wajasiriamali

au wamachinga ambao hawana uwezo wa kulipia vibanda hivyo kutokana na hali halisi na maeneo husika. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mariam Azzan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 394

### **Chakechake kuwa na Kituo kimoja tu cha Polisi**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, ni kwa nini hadi sasa Wilaya ya Chakechake ina kituo kimoja cha polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Chakechake ina kituo kimoja cha polisi. Sababu ya hali hiyo ni kwamba, Wilaya ya Chakechake ilikuwa na idadi ndogo ya matukio ya uhalifu na hivyo kituo hicho kilionekana kinatosheleza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu pamoja na shughuli za kiuchumi ikiwemo biashara, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imepanga kujenga vituo vya polisi katika maeneo ya Vitongoji, Pujini, Wesha na



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Gombani. Tayari Idara ya Ardhi imetoa eneo la mita za mraba 1,496 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi eneo la Vitongoji. Serikali itaanza kujenga kituo hicho kulingana na mpango wake wa ujenzi hususani katika mwaka wa fedha 2023/2024. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara imepata ardhi ya kujenga Kituo kimoja cha Polisi; je, ina mkakati gani wa kupata ardhi kujenga vituo vitatu vilivyobaki?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, eneo la Pujini ni miongoni mwa maeneo yenye uhalifu sana; je, Serikali haioni? Ichukue uharaka wa kujenga kituo hicho cha polisi, ili kulinda mali na usalama wa raia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, ardhi inahitajika na kupitia Bunge lako tukufu nimtake Kamishna wa Polisi Zanzibar awasiliane na mamlaka ya ardhi katika Wilaya ya Chakechake ili waweze kumpangia ardhi kwa ajili ya kujenga kwenye maeneo hayo niliyoyabaini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo lenye changamoto ya uhalifu, niseme kwamba kwa sasa kwa sababu hakuna fedha za kujenga Kituo cha Polisi, basi Polisi Wilaya ya

Chakechake waimarishe doria ili kudhibiti makundi yote ya uhalifu kwenye eneo hilo. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabula Shitobela, swali la nyongeza.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kituo cha Polisi Kata ya Kiseke, Ilemela hakina nyumba ya askari na kusababisha kituo kufungwa saa 12.00 jioni. Je, Serikali itakamilisha lini nyumba hiyo ili kuepusha kituo kufungwa saa 12.00 jioni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo la Kiseke ni eneo ambalo lina shughuli nyingi za kiuchumi na kibiashara na msongamano mkubwa wa watu na matukio ya uhalifu yapo, na tunatambua kwa juhudi za Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum na Mbunge wa Jimbo la Ilemela wamekuwa mara kwa mara wakisumbua Wizarani ili waweze kujengewa nyumba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa vile wameshaanza ujenzi niahidi tu kwamba kupitia Jeshi la Polisi chini ya Mfuko wa *IGP* wa Tuzo na Tozo, tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili kupata fedha za kukamilisha kituo hicho hasa baada ya kufanya tathmini ya kiwango cha fedha zinazohitajika. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa Serikali sasa imeamua kujenga vituo hivi vya polisi kuanzia ngazi ya kata. Ni lini sasa Serikali itakuwa

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tayari kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Nyegezi kwa ajili ya Kanda ya Ukanda wa Nyegezi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ni nia ya Serikali kujenga vituo vya polisi, kuimarisha usalama wa raia ngazi ya kata na ni kwa msingi huo tumeweza kutoa askari kata katika kata zote nchini.

Sasa hili suala la ujenzi wa vituo ni suala la gharama na kwamba katika kipindi kifupi hatuwezi kufanya hivyo kulingana na mpango wetu wa ujenzi. Tutaanza na mikoa ambayo haina Ofisi za *RPC*, lakini Wilaya ambazo hazina vituo vya *OCD*. Kwa hiyo, vilivyo kwenye ngazi za kata tumuombe Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na wadau waanze ujenzi ili Serikali ije isaidie kukamilisha vituo hivyo. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu Mkoani Mbeya askari wanafanya kazi nzuri sana ya kulinda rai ana mali zao, lakini askari hawa nyumba zao ni chakavu kweli kweli ukizingatia ni Wilaya zote hakuna nyumba za askari ambazo zinarithisha.

Sasa je, ni lini Serikali itafanya mpango wa kufanya ukarabati kwenye nyumba hizo za askari wetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nitambue kwamba, maeneo mengi ya vituo vya polisi, makazi ya askari katika maeneo hayo ni chakavu sana na ni kwa msingi huo ndio maana tumeanza ukarabati katika maeneo hayo. Na kwa kweli Mbeya kama Mkoa mkubwa ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, kipaumbele kimewekwa kule katika mwaka ujao tutatia kipaumbele ukarabati wa nyumba za askari katika Jiji la Mbeya. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, tatizo la usafiri kwa Kituo cha Polisi cha Mavota ambacho kinahusika na ulinzi wa mgodi wa *Biharamulo Gold Mine* ni kubwa. Tuna kituo pale, lakini hakuna usafiri hata pikipiki.

Sasa ni lini labda Serikali itatusaidia kupata hata usafiri wa pikipiki mbili/tatu ili tuweze kuimarisha ulinzi juu ya wawekezaji ambao wamewekeza katika mgodi ule wa Mavota?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vituo vingi vya polisi havina usafiri wa uhakika, hasa vituo vilivvyo kwenye ngazi ya kata na kwenye maeneo mahususi kama haya ya migodi. Pengine nitumie nafasi hii kueleza kwamba katika mwaka wa fedha huu na ujao tuna magari zaidi ya 300 ambayo yatapatikana na sehemu ya magari hayo ni ku-

*support* usafiri kwenye vituo mbalimbali vya polisi. Sasa pengine niwasiliane na Mbunge kuona uhitaji wa usafiri wa pikipiki katika kituo hiki ili tushirikiane kuzungumza na wadau waweze kutoa fedha kuwezesha ikiwa mpango wa Serikali wa magari hayo utachelewa kufika. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa mara ya kwanza niulize Wizara hii. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Sikonge...

**SPIKA:** Hebu Mheshimiwa George Kakunda, kwa mara ya kwanza kufanya nini?

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza kuuliza swali la nyongeza kwenye Wizara hii ya Mambo ya Ndani. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Sasa ndio maana hayo maneno tunayoyaongeza ni kwamba huwa hupewi nafasi au huna maswali yanayotoka jimboni yanayohusu Wizara hii ama? Maana wananchi hawatajua sasa kwa nini ni mara yako ya kwanza leo? (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ni msisitizo maalum huo, ili Serikali ijue kwamba...

**SPIKA:** Hapana, hebu futa hayo maneno kwa sababu tunapeleka picha huko nje kama vile wewe hupewi nafasi na mimi ndio nimekaa hapa mbele. Nafasi zinatolewa kwa usawa humu ndani kwa hiyo, wewe nenda moja kwa moja kwenye swali, futa mameno ya unauliza kwa mara ya kwanza leo. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Sikonge ambayo ina eneo la kilometa za mraba 27,873 ...

**SPIKA:** Futa kwanza, Mheshimiwa George Kakunda. Futa kwanza ndio unaanza swali lako.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nafuta yale mameno ya mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa niulize swali la nyongeza kwamba Wilaya ya Sikonge ambayo ni miongoni mwa Wilaya kubwa kieneo la kijiografia haina kituo chenye hadhi ya Kituo Kikuu cha Polisi cha Wilaya, badala yake wanatumia jengo dogo ambalo lilijengwa na chifu mwaka 1957. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Kituo cha Polisi cha Wilaya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya nyingi za polisi hazina majengo ya polisi ya ngazi ya Wilaya na ndio maana kama mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge kwenye bajeti hii tumezungumzia haja ya kuanza kujenga vituo vya polisi ngazi ya Mkoa na Wilaya kule ambako vituo hivyo havipo. Sikonge najua ni eneo ambalo pia halina hadhi hiyo, kwa hiyo, tutaweka kipaumbele Mheshimiwa Mbunge ili katika mwaka ujao iweze kuzingatiwa katika bajeti tayari tuanze ujenzi wa kituo hicho. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Kituo cha Polisi cha Kigonga kinahudumia wananchi waliopo mpakani mwa Tanzania na Kenya wa kata

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

za Itirio, Nyanungu, Mlimba na Gorong'a, lakini kituo hiki kilijengwa kwa *full-suit* ya mabati kana kwamba kimechakaa na polisi wamekimbia hawapo tena pale.

Sasa ningetaka kujua ni lini Serikali itajenga kituo hiki kwa sababu ni kituo cha kimkakati ukizingatia kipo mpakani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, viwango vyetu vya kujenga vituo vya polisi siyo kuwa *full-suit* ya mabati, kwa hiyo kama kuna kituo cha aina hiyo hakikidhi viwango pengine sasa niwasiliane na Mheshimiwa Mbunge na mamlaka ya Serikali za Mitaa kule Temeke ili tuanze mkakati wa kujenga kituo kwa kutumia vifaa ya kudumu ikiwa ni matofali na kadhalika...

**MBUNGE FULANI:** Tarime.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Tarime vijijini yes, kwa hiyo nachukua ahadi...

**SPIKA:** Waheshimiwa hapa mnapenda kuwazungumzisha Mawaziri wakiwa wanazungumza mwache amalize jibu lake, ukiwa unaongea naye anaanza kuongea na wewe badala ya kuongea na mimi hapa mbele.

Mheshimiwa Naibu Waziri malizia majibu yako.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nilikuwa nasema hatuna vituo vinavyopaswa kuwa vya polisi vyenye kujengwa kwa *full-suit* za mabati kwa hiyo kituo hiki kama kweli kipo kule mpakani tutashirikiana na uongozi wa Polisi Kanda Maalum ya Tarime Rorya ili kuwa na mpango wa kujenga kituo hiki kwa aina ya

vifaa vinavyostahiki kujengea kituo cha polisi. Kwa hiyo, nimuondoe mashaka Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaweka kipaumbele na kwa vile kituo kiko mpakani, kilete taswira nzuri ya kituo stahiki katika nchi yetu, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsia swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijini hatuna kabisa kituo cha polisi.

Je, ni lini Serikali itatujengea kituo cha polisi katika halmashauri yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza katika maswali niliyojibu muda mfupi uliopita, si wilaya zote zina vituo vya polisi vya ngazi ya wilaya kwa kulitambua hilo ndiyo maana tuna mpango mkakati wa kiwizara wa kujenga vituo vya polisi vya *OCD* katika kila wilaya kulingana na mpango wetu na kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mtwara na kwa umuhimu wa ukanda ule kitapewa kipaumbele, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa sasa aulize swali lake.



Na. 395

**Kurahisishwa Upatikanaji wa Baruti na Zebaki kwa  
Wachimbaji Wadogo**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha utaratibu wa kupata baruti na zebaki unakuwa rahisi na vibali vitolewe kwa ngazi ya kijiji kwa wachimbaji wadogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini imeendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuimarisha usimamizi, upatikanaji na matumizi ya baruti hapa nchini. Ili kurahisisha upatikanaji wa vibali vya baruti Wizara imesogeza huduma hiyo katika Ofisi za Maafisa Madini Wakazi wa Mikoa yote ya kimadini nchini ikiwemo Chunya. Aidha, Serikali imesajili na kutoa vibali vipya vya biashara ya baruti kwa kampuni 25 ambazo hutoa huduma hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini katika kipindi cha mpito kwa matumizi ya zebaki imeendelea kufanya jitihada mbalimbali ikiwemo kushirikiana na Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya ufuatiliaji wa taratibu za uingizaji na usambazaji wa kemikali ya zebaki nchini ili kubaini changamoto za upatikanaji wa kemikali hiyo na kuandaa takwimu za kiasi cha matumizi ya zebaki ili kujua kiasi kinachohitajika nchini ili kurahisisha utoaji wa vibali vya uingizaji na kuwatambua na kuwasajili waingizaji na wasambazaji wa kemikali ya zebaki nchini kwa mujibu wa Sheria ya Kemikali nchini ili biashara hiyo ifanyike kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kemikali ya zebaki kutumika katika shughuli za ukamatishaji wa dhahabu, tafiti za kisayansi zimebainisha kuwa kemikali hiyo isipotumika vizuri ni hatari kwa afya ya binadamu na mazingira, jambo lililosababisha Serikali kusaini Mkataba wa Minamata (*Minamata Convention*) ambao utekelezaji wake unapelekea kupunguza matumizi ya zebaki au kuondoa kabisa pale inapowezekana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na madhara ya matumizi ya zebaki, Serikali kupitia mradi wa *Environmental Health and Pollution Management Program* -imeanza kutafuta njia mbadala ya uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ili kuondokana na madhara yanayotokana na matumizi ya kemikali hiyo. Mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia (*WB*) na kutekelezwa chini ya Baraza la Udhhibiti na Usimamizi wa Mazingira (*The National Environmental Management Council - NEMC*), ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, tunaishukuru Serikali ndani ya muda mfupi imeweza kujenga maghala takribani kumi ndani ya Wilaya ya Chunya kwa ajili ya baruti. Lakini maghala haya yapo pale Chunya mjini na maeneo ya uchimbaji wa dhahabu yako kule vijijini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vibali hivi vinaweza kuwafikia wale wafanyabiashara wa baruti kwenye maeneo yale ya uchimbaji kule vijijini?

Swali la pili kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri, Serikali imeshaingia Mkataba wa Minamata kwa ajili ya kupunguza matumizi ya zebaki na baadaye kuitokomeza kabisa. Lakini kwa kipindi hiki cha mpito matumizi ya kemikali

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

hii ya zebaki bado inaendelea kutumika kwa ajili ya kuchenjua na ukamatishaji dhahabu.

Je, Serikali ina mpango gani kutoa elimu kwa wachimbaji hawa wadogo wa dhahabu ili madhara yasiendelee kutokea zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasaka kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa swali lake la kwanza napenda kumfahamisha kwamba Serikali imeendelea kuboresha utaratibu wa kuweka urahisi wa upatikanaji na matumizi ya baruti katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo na kufikia mwaka huu mwezi huu wa sita Waziri wa Madini kwa mamlaka aliyopewa kwa mujibu wa kifungu cha (8) cha Sheria ya Baruti ya mwaka 1963 Sura ya 45 amepewa mamlaka ya kutoa leseni kwa viwanda vya kutengeneza baruti hapa nchini na tayari kuna viwanda vitatu vimeshapewa hiyo leseni ya kuzalisha baruti jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa upatikanaji wa zebaki kwa wingi nchini, lakini sambamba na hilo kifungu Na. 4 cha Sheria ya baruti Sura ya 45 imempa Waziri mamlaka ya kuteua wakaguzi wa baruti na hao sasa wameshateuliwa na wako katika kila Ofisi ya Madini ya Mikoa yetu yote ya madini nchini na wanafanyakazi chini ya Kamishna wa Madini ambaye anawapa kibali cha kutoa leseni za *store* na masanduku ya kuhifadhia baruti.

Mheshimiwa Spika, kana kwamba hiyo haitoshi, pia anawapa kibali cha kuweza kutoa leseni na mpaka sasa hivi tuna leseni 256 za maghala yaani *magazine*, leseni 338 za *store* yaani *store* yenyewe na leseni 114 za masanduku (*storage boxes*) ya kuhifadhia baruti na Kamishna kwa kutumia hawa wakaguzi wa baruti amewapa mamlaka ya kushirikiana na ofisi zetu za madini kila mkoa kuhakikisha kwamba baruti zinawafikia wachimbaji wadogo kwa njia iliyo

salama na kwa njia rahisi kabisa kupatikana karibu na maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili ambalo anataka kujua kwamba hii zebaki sasa ambayo ni hatarishi kwa mazingira iko katika mikakati ya kwenda kuondolewa matumizi yake, lakini kwa kipindi hiki cha mpito kabla haijaondolewa matumizi yake Serikali inafanya nini kutoa elimu, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka sasa hivi Wizara imeshatoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo zaidi ya 600 na namna salama ya kutumia zebaki.

Katika Mkoa wa Shinyanga tumetoa elimu hiyo katika maeneo ya Mwimbe, Mwambomba, Kalole, Zambazare na Mwakitolyo na katika mwaka huu wa fedha ambayo bajeti yake inakwenda kusomwa leo Bungeni, tunategemea kuendelea kutoa elimu hiyo katika mikoa yote ya kimadini nchini ikiwemo Songea, ikiwemo Chunya, ikiwemo Songwe, Singida, Geita na maeneo mbalimbali ili wachimbaji wadogo waweze kutumia zebaki kwa makini mpaka hapo njia za mbadala zitakapatikana, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana matumizi ya zebaki kwenye maeneo yetu wachimbaji wadogo wadogo hasa Jimbo la Msalala yamekuwa na athari kwa wachimbaji wenyewe, lakini pia kwenye mazingira yanayozunguka pale. Sasa kabla Serikali haijaenda kuzuia matumizi ya zebaki ni teknolojia ipi ambayo mmeianzisha kama mbadala wa matumizi ya zebaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kuna teknolojia mbadala ambayo inaendelea kutumika katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu na teknolojia hiyo inaitwa ni *cyanide* na matumizi ya *cyanide* ni aina ya utaalam

ambao ile kemikali yenyewe inapokuwa imetumika kuchenjua na kukamatwa kwenye mabwawa ya kuchenjulia madini huyeyuka na kupotea hewani bila kuacha madhara yoyote na hiyo ndiyo teknolojia ya kisasa ambayo tunaendelea kutumia na kuendelea kuitambulisha kwa wachimbaji wadogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Robert Maboto swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Halmashauri ya Mji wa Bunda, Kata ya Guta, Mtaa wa Kinyambwiga kuna uchimbaji wa madini pale lakini kwa sasa kuna mgogoro kati ya wenye mashamba na wenye leseni. Je, ni nini kauli ya Serikali kwenye mgogoro huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama unayo majibu ya swali hilo unaweza kujibu, kama huna litakuja kama swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini na kwa ridhaa yako namuomba Mheshimiwa Mbunge alete swali hilo kama swali la msingi halafu tutalijibu hapa Bungeni. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Gambo swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na kwa kuwa madini ya *Tanzanite* yanaruhusiwa kuuzwa duniani kote ikiwa ni pamoja na India na Marekani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vibali ili madini hayo pia yaweze kuuzwa kwenye mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza na nchi ya Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri unao uhuru kama unayo majibu ya swali hilo au lije kama swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kumjibu Mheshimiwa

Gambo kwamba madini ya *Tanzanite* ni madini ya kipekee kabisa ambayo yanapatikana nchini Tanzania tu na kwa ajili hiyo Serikali iliweka utaratibu wa kusimamia uzalishaji, uchakataji, uongezaji wake thamani palepale Mererani. Lakini katika kipindi tulichoko sasa hivi tuko katika hatua za kufanya tathmini ya utaratibu uliowekwa na Serikali ambapo baada ya kujiridhisha kwamba kuna utaratibu mwingine mzuri wa kuruhusu madini hayo yauzwe kila mahali ndani ya nchi na nje ya nchi, bila kuathiri uhalisia wa hali iliyokuwepo ya mwanzo ya utoroshaji wa kiholela tutakwenda kuweka utaratibu mahususi ili madini hayo yaweze kuanza kuuzwa popote pale maadam pia yatakuwa yameshaongezewa thamani na kupewa vibali vya kutoka ndani ya eneo la Mererani ambalo ni eneo tengefu kwa sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kungu swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujua ni njia gani nzuri Serikali inatumia kwenye matumizi ya *cyanide*, kwa sababu madhara ya zebaki ni bora zaidi kuliko madhara ya *cyanide* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nipende tu kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba *handlings* kwa Kiswahili tunasema jinsi unavyo itumia *cyanide* kwa usahihi kwa kutengeneza yale malambo na kuweka *tiling* zile za kuzuia ili isivuje chini ya ardhi, ni njia ya uhakika kabisa kwamba ukishaitumia na ukaiacha ika-*evaporate* ndani ya anga/hewani haiachi madhara yoyote na ni salama zaidi kuliko *zink* ambayo upoteaji wake au *biodegradability* yake ni ngumu zaidi ya kuhifadhi katika maeneo ambayo hakutakaa kuwe na *leakage*.

Kwa hiyo, utalam wa *cyanide* siyo mgumu kama ambavyo yeye anadhani na ni wa uhakika zaidi na ni salama zaidi kuliko zebaki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya swali la nyongeza.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali, ninayo mambo machache hapa na matangazo.

La kwanza kabisa tulishatangaza majibu ya Serikali yale majibu ya msingi yafuate viwango vile tulivyoviweka, Wizara ya Madini na Wizara ya Fedha na Mipango mmeleta majibu marefu.

Kwa hiyo, mrekebishe majibu yenu mnayoyaleta Bungeni, lakini pia Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe maswali ya nyongeza yaendane na maswali ya msingi, kwa sababu si jambo jema sana hapa tukawa kila maswali yanayoulizwa tunayapeleka kwenye maswali ya msingi inaweza ikaonesha kana kwamba Waziri hajajiandaa, lakini Waziri amejandaa kwenye eneo lile la swali la msingi. Kwa hiyo, tufuate huo utaratibu.

Jambo la pili matangazo ya wageni; tunao wageni ambao wametembelea Bunge siku ya leo, kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika na hawa ni viongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Emmanuel Tutuba, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge. Wageni wote wa Wabunge msimame kwa pamoja, karibuni sana sana, karibuni sana nadhani mmewaona Wabunge wenu namna wanavyowawakilisha vizuri. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza ni wanafunzi 70 na walimu kumi kutoka Shule ya Awali ya Msingi *Green Harvest* ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wawakilishi 33 wa Taasisi ya Jamii Mpya ya Jijini Dodoma wakiongozwa na mratibu wao Ndugu Malik Masoud, karibuni sana. Sijapewa maelezo ya ziada hapa ya Taasisi ya Jamii Mpya lakini kila la heri katika yale mnayokusudia kuyafanya. *(Makofi)*

Tunao pia uongozi wa Serikali ya wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao Bungeni asubuhi hii ya leo, lakini lipo jambo moja ambalo nataka nilizungumze halafu nitaleta tangazo la kazi.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba tarehe 9 Juni, 2022 nilitoa maelezo hapa Bungeni kuhusu mawasilisho yaliyowasilishwa kwangu na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara na Mheshimiwa Phillip Augustino Mulugo. Niliwataka Wabunge hawa kuleta Bungeni uthibitisho wa tuhuma walizozitoa wakati walipokuwa wakitoa michango yao Bungeni kuhusu matukio waliyoeleza kuwa yalisababisha watu kuuawa na wengine kujeruhiwa.

Katika maelezo hayo walidai pia kuwa vitendo walivyovilalamikia vilisababisha uharibifu wa mali za wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka hifadhi zilizopo katika majimbo yao.

Baada ya kupokea mawasilisho hayo nilitoa ufafanuzi na maelekezo hapa Bungeni. Katika maelezo hayo nilieleza kwamba mawasilisho ambayo Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara aliyaleta hayakuwa tofauti na madai aliyoyatoa awali wakati akichangia hoja hapa Bungeni. Kwa hali hiyo nilieleza kuwa mawasilisho hayo hayakuweza kuthibitisha tuhuma zake kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kwani baadhi ya picha alizowasilisha kama ushahidi zinaonesha akina mama wajane, akina baba wagane na kueleza kuwa ujane wao au ugane wao umetokana na mauaji ya wenza wao, jambo ambalo halina uthibitisho kwa jambo la mauaji ambalo ni kubwa sana na linahitaji ushahidi wa kutosha kuthibitisha.



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Hata hivyo mimi kama Spika kwa kuzingatia maslahi mapana ya wananchi wa Tarime kwa kuwa nilipokea malalamiko yao na licha ya Mbunge huyu kushindwa kuthibitisha madai yake nilielekeza Serikali ifanye uchunguzi wa jambo hilo na baada ya kukamilisha iwasilishe Bungeni taarifa ya uchunguzi ndani ya siku 90. Kwa kuzingatia manufaa ya uamuzi huo nilitegemea Mbunge huyo husika Mheshimiwa Waitara angeshukuru badala ya kubeza na kupinga.

Waheshimiwa Wabunge, siku moja baada ya uamuzi wangu nimesoma makala inayopinga na kuhoji juu ya uhalali wa uamuzi na maelekezo niliyoyatoa. Makala hiyo imeandikwa katika Gazeti la Raia Mwema Toleo Namba 1031 la tarehe 10 Juni, 2022. Makala hiyo ilitambulishwa kwa wino mweusi katika ukurasa wa kwanza wa gazeti hilo ikisomeka; Waitara apinga uamuzi wa Spika, sehemu ya juu ya kuandikwa kwa kirefu katika ukurasa wa tano wa gazeti hilo.

Waheshimiwa Wabunge, makala hiyo imemnukuu Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara akitumia maneno yafuatayo; "Ni vigumu Serikali inayotuhumiwa kutenda jambo fulani kwenda kujichunguza na badala yake Bunge lilipaswa kuundwa Kamati Teule kuchunguza na taarifa kuwasilishwa kwake si kama alivyofanya Spika."

Maneno mengine yaliyotumika ni kama ifuatavyo; "Hifadhi ya Serengeti ni ya Serikali, sasa Serikali inawezaje kujichunguza, kwa kuwa Serikali inalalamikiwa na Spika amewahi kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitakiwa iundwe Kamati Teule ya Bunge, iende ikachunguze, kisha taarifa iwasilishwe Bungeni, ripoti ikija Bungeni ijadiliwe na maazimio ama mapendekezo yawasilishwe Serikalini. Sasa Serikali kwenda kujichunguza kuna shida." Mwisho wa kunukuu.

Kwa maelezo haya ya Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara kwamba kuna shida kwa Serikali kufanya uchunguzi, inamaanisha kwamba Serikali na vyombo vyake vyote vya

uchunguzi kama vile Polisi, TAKUKURU, Jeshi USU, Usalama navyo vina shida jambo ambalo siyo kweli.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa jambo hili nilishalitolea uamuzi na ni dhahiri gazeti hili lilivyoandika limeweka maneno likimnukuu Mheshimiwa Waitara, jambo alilolifanya linaenda kinyume na kanuni na taratibu za uendeshaaji Bunge ambazo zinaweka wazi ni nini Mbunge anapaswa kufanya anapooona hajaridhishwa na uamuzi wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 5(4) inaeleza wazi kwamba Mbunge ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anatakiwa kuwasilisha malalamiko yake kwa Katibu wa Bunge kwa maandishi ili malalamiko hayo yaweze kufanyiwa kazi kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Mwita Waitara hakutaka kutumia utaratibu huo wa kikanuni na badala yake akaamua kwenda kulalamika kwenye vyombo vya habari.

Waheshimiwa Wabunge, maelezo ya Mheshimiwa Mwita Waitara dhidi ya uamuzi wangu yanakiuka sheria na kanuni zetu. Kwa mujibu wa kifungu cha 24(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296 inazuia Mbunge au mtu yeyote kutoa maneno yanayovunja heshima ya Spika na kudhalilisha kwa makusudi mwenendo wa shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, makosa aliyoyafanya Mheshimiwa Waitara yanaangukia katika Kanuni ya 84(1)(a) na (j) ambayo inasimamia na kutoa adhabu juu ya utovu mkubwa wa nidhamu. Kwa mujibu wa kanuni hiyo makosa ya Mheshimiwa Mwita Waitara yanajidhihirisha kama ifuatavyo:-

(a) Kanuni ya 84(1)(a); Mheshimiwa Mwita Waitara amepuuza uamuzi au maelekezo ya Spika aliyoyatoa kuhusu kuipelekea Serikali tuhuma zilizotolewa ili ifanye uchunguzi na baadaye kuwasilisha taarifa hiyo ya uchunguzi Bungeni.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(b) Kanuni ya 84(1)(j); kitendo cha kueleza kwamba Spika amewahi kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kina lengo la kushusha hadhi ya Spika wa Bunge. Kwa ujumla kwamba Bunge linaongozwa na Spika ambaye anafahamu sheria, lakini hafuati sheria.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi wote mnafahamu na yeye pia anafahamu, kwa kusema tu kwamba mimi niliwahi kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapaswa ajue najua utaratibu kuliko yeye. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hilo tu kwa kuwa analijua alipaswa ajue kwamba hawezi kuwa yeye anazijua sheria kuliko mimi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia athari za kitendo alichokifanya Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara kuvunja hadhi na haki za Bunge. Kwa kutumia mamlaka yangu chini ya Kanuni ya 5(2) ya kusimamia matumizi sahihi ya Kanuni za Bunge; na kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 84 ambayo nimeshawasomea; na kwa sababu hiyo siku ya tarehe 9 Juni, 2022 nilitoa maelezo kwa kirefu sana hapa; na mtu yeyote mwenye akili zake timamu, mtu mzima, mwenye afya ya akili alipaswa kuelewa maana ya yale maelezo niliyoyatoa wakati ule. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge kanuni zetu zipo wazi kabisa adhabu gani anastahili mtu wa namna hii, adhabu gani anastahili mtu wa namna hii kwa sababu kanuni yetu ya 84 inazungumzia utovu mkubwa wa nidhamu na hapa niliwatajia fasili ya (1)(a) inasema; "Mbunge atakuwa ametenda kosa la utovu mkubwa wa nidhamu ikiwa atapuuza uamuzi au maelekezo ya Spika au Mwenyekiti wa Kamati." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nilishaiielekeza Serikali cha kufanya na niliwapa muda wa kufanya hilo jambo, haikubaliki kulivunjia heshima Bunge na haikubaliki kumvunjia heshima Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo niliyoyasema, pamoja na uzito wa hiki kitendo alichokifanya Mheshimiwa Waitara ambaye sio Mbunge mpya ni Mbunge wa kitambo, kwa hiyo nataka kuamini kanuni anazifahamu, hata hivyo nampa onyo, nampa onyo asirudie kudharau maamuzi ya Spika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nampa hilo onyo asirudie kudharau maamuzi ya Spika na kwa sababu kanuni hiyo mnazifahamu adhabu zake ni nzito sasa baada ya kumpa onyo hilo nimemsamehe. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa jambo hili tutasubiri taarifa kama ambavyo nilikuwa nimetoa maelekezo kwa upande wa Serikali.

Nilete tangazo nililionalo hapa mbele kabla hatujaendelea na ratiba yetu; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa na Katibu wa Bunge kwamba Ofisi ya Bunge kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma yaani *Public Finance Management Reform Program* imeandaa mdahalo kuhusu uchumi na kufanya tathmini ya bajeti ya Serikali kesho tarehe 15 Juni, 2022 saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Watoa mada ni Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Sekta Binafsi lakini Taasisi za Utafiti za Uchumi (*ESRF*) na Taasisi ya Utafiti ya *REPOA*.

Waheshimiwa Wabunge wote, kwa sababu bajeti hii itasomwa leo hapa na yale yatakayokuwa yamejiri humo yatakuwa yanajadiliwa kesho, kwa hivyo ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge ili wakati kesho tunapewa nafasi ya kusoma Hali ya Uchumi ambayo tutaambiwa hii asubuhi, lakini pia kusoma bajeti ile ambayo tutakuwa tumesomewa mchana ni muhimu tuje tuwasikilize wataalam wetu wamechambua huko wameona nini.

Kwa hiyo, mafunzo haya ama mdahalo huu utakaofanyika kesho saa 4.00 asubuhi niwaombe sana

Waheshimiwa Wabunge mkumbuke hili, lakini jioni pia tutajitahidi tulirejee tangazo hili muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**SPIKA:** Waziri wa Fedha amekaa mbali nikajua anataka kuletwa, anataka kusindikizwa hata hii asubuhi.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, sasa aje awasilishe Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023. Taarifa hizo ndiyo msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 nitakayowasilisha katika Bunge hili tukufu leo alasiri.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine katika Bunge hili baada ya majadiliano ya bajeti za mafungu mbalimbali. Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania ni muhimu katika kujadili namna ya kuhakikisha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nitumie fursa hii kutoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Chama cha Mapinduzi na Watanzania wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marehemu Irene Alex Ndyamkama. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo mkunjufu, napenda kutoa pongezi zangu za dharti kwako Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wana imani kubwa sana na wewe na hawana shaka na uzoefu wako, weledi wako na umahiri wako katika kusimamia na kuongoza shughuli za Bunge. Aidha, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu kuendelea kuwa na nguvu, ujasiri na afya njema ili muweze kuendelea kutekeleza majukumu yenu ya kuongoza Bunge letu kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nitoe pongezi zangu za dharti, kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na utumishi uliotukuka kwa Watanzania unaolenga kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi na kijamii hapa nchini. Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira yake ya dharti ya kilitumikia Taifa kwa uaminifu ambapo ameendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazolenga kuleta maendeleo kwa Watanzania ikiwemo kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kielelezo na miradi mingine ya kuchochea uchumi na kuimarisha huduma za jamii,

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa akiendelea kutuongoza kwa vitendo kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuchochea ukuaji wa uchumi hususan sekta ya utalii ambayo iliathirika zaidi na UVIKO-19 ikiwemo kushiriki kwenye filamu ijulikanayo kwa jina la *The Royal Tour* kama mwongozaji utalii namba moja nchini. Mheshimiwa Rais amekuwa chachu na kinara wa utalii kupitia filamu hiyo iliyolenga kukuza sekta ya utalii ambayo inatarajiwa kuzalisha takriban ajira milioni 1.3 na fedha za kigeni dola za Kimarekani bilioni 2.6. Filamu hiyo iliyozinduliwa kwa mara ya kwanza Jijini New York tarehe 18 Aprili 2022 na baadaye tarehe 21 Aprili, 2022 Jijini Los Angeles. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu Watanzania wenzangu, hii ni hatua kubwa sana kwa Taifa letu kwa kuwa filamu hii inapatikana kupitia chaneli za *Apple TV Plus* na *Amazon Prime* za nchini Marekani ambazo zinakadiriwa kuwa na watazamaji zaidi ya milioni 200 duniani. Ama hakika kwa msembo wa kisasa mama anaupiga mwingi sana, na hivyo tuna kila sababu ya kuunga mkono jitihada zaidi na zaidi ya hizi ili tuweze kwenda pamoja na mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini kumsaidia kazi katika nafasi ya Waziri wa Fedha na Mipango. Kwa imani hii aliyoionesha kwangu napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa bidii kubwa, weledi, uaminifu, uadilifu na uzalendo wa kiwango cha hali ya juu ili kuhakikisha matamano ya Mheshimiwa Rais na Watanzania wote ya kuleta maendeleo ya ustawi wa kiwango cha juu yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa nchi yetu na dunia kwa ujumla inaendelea kushuhudia athari za UVIKO-

19 ambazo zimesababisha kushuka kwa shughuli za kiuchumi duniani, ikiwemo uzalishaji, biashara za ndani na kimataifa, utalii na usafirishaji wa bidhaa. Katika mwaka 2021 uchumi wa Taifa letu na wa dunia kwa ujumla ulianza kuimarika baada ya kupitia katika kipindi cha kukabiliana na athari za UVIKO-19. Aidha, wakati Serikali ikiendelea na jitihada za kuimarisha uchumi, mwezi Februari, 2022 kuliibuka vita kati ya mataifa ya Urusi na Ukraine ambayo imesababisha Urusi kuwekewa vikwazo na hivyo kusababisha kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali katika soko la dunia zikiwemo mafuta pamoja na gesi.

Mheshimiwa Spika, sanjari na kupanda kwa bei hizo, kumekuwa na uhaba wa baadhi ya bidhaa katika soko la dunia ikiwemo, mbolea, ngano pamoja na mafuta ya kula. Serikali imeendelea kuchukua hatua katika kukabiliana na athari hizo ikiwemo kupokea mkopo wa masharti nafuu wa shilingi triloni 1.3 zilizoelekezwa katika sekta ya afya, elimu, maji pamoja na utalii ili kuchochea uchumi na kukabiliana na UVIKO-19, kingine ni kuongeza bajeti ya kilimo, mifugo, uvuvi, nishati pamoja na miundombinu ya wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama wamachinga ili kuchochea uzalishaji wa ndani na kupunguza nakisi ya urari wa biashara, na kuangalia namna bora ya uagizaji mafuta itakayoleta unafuu wa bei kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue fursa hii kulihakikishia Bunge lako tukufu na Watanzania wote kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na athari hizo kwa lengo la kuleta unafuu wa maisha kwa Watanzania. Nipende kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika mchakato huu nikianza na Bunge lako tukufu chini ya uongozi wako Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri wao mahiri wakati wa uandaaji wa taarifa nilizowasilisha mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 imeandaliwa kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla na sekta mbalimbali kwa mwaka husika ikilinganishwa na mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, aidha, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 yamezingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 na 2025/2026, pamoja na Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akilihutubia rasmi Bunge hili la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 22 Aprili, 2021.

Aidha, Mpango umezingatia sera na mikakati mbalimbali ya kissekta, kikanda na kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Dira ya 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika yaani *SADC 2050*; Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa mwaka 2022/2023, msukumo mkubwa utawekwa katika sekta za uzalishaji ambazo ni kilimo, mifugo, uvuvi na nishati kwani sekta hizi ndizo zinazochochea uzalishaji kwa matumizi ya ndani pamoja na mauzo nje na pia hupunguza nakisi ya urari wa kibiashara pamoja na mfumuko wa bei, lakini pia huzalisha ajira zinazowagusa wananchi walio wengi.

Sambamba na vipaumbele hivyo, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi mingine ya kimaendeleo ikiwemo miradi ya kielelezo kama ya ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa yaani *SGR*, ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Julius Nyerere, uboreshaji wa Shirika la Ndege pamoja na miradi ya elimu, afya, maji, usafiri wa anga nawamajini, bandari, maliasili na utalii, mapinduzi ya TEHAMA, miundombinu ya barabara na madaraja na kuboresha

mazingira ya biashara na uwekezaji ili kukuza ustawi wa sekta binafsi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mwenendo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2021; Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa yaani *IMF* ya Aprili, 2022 inaonesha kuwa uchumi wa dunia ulimarika na kufikia wastani wa asilimia 6.1 kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 3.1 mwaka 2020. Kuimarika kwa uchumi wa dunia kumetokana na hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na nchi mbalimbali katika kuimarisha uchumi, ikiwemo utekelezaji wa sera za fedha na bajeti zinazochochea shughuli za uchumi zilizoathirika na kuendelea kuimarishwa kwa huduma za afya ikiwemo uhamasishaji na usambazaji wa chanjo kwa lengo la kupunguza athari za UVIKO-19. Hata hivyo, uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua na kufikia ukuaji wa asilimia 3.6 kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na uwepo wa vita kati ya nchi ya Urusi na Ukraine ambayo imesababisha kuongezeka kwa bei za vyakula na nishati hivyo kudhoofisha zaidi matarajio ya kurejea kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na UVIKO-19. Ikumbukwe kuwa Urusi ni nchi ya pili kwa hifadhi na uzalishaji wa bidhaa za petroli duniani ambapo inachangia wastani wa asilimia 12 katika mafuta yote yanayozalishwa duniani ikitanguliwa na Marekani yenye mchango wa asilimia 20. Aidha, Urusi ndiyo mzalishaji mkubwa wa nishati ya gesi na mafuta inayotumika katika shughuli za kiuchumi Barani Ulaya.

Vilevile kufikia mwaka 2023 na kuendelea uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua zaidi na kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 3.3 kwa kipindi cha muda wa kati iwapo vita kati ya Urusi na Ukraine vitaendelea pamoja na kuendelea kuzidisha vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Urusi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchumi wa Afrika na Kikanda mwaka 2021, nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilikuwa na ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 4.5 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.7 mwaka 2020.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Hii inatokana na jitihada mbalimbali zilizoendelea kuchukuliwa ili kuimarisha ukuaji wa uchumi ikiwemo kuboresha huduma za afya pamoja na kuimarika kwa bei za bidhaa zinazouzwa nje ya ukanda huo baada ya kuondolewa kwa vikwazo vilivyowekwa ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa UVIKO-19. Ukuaji wa uchumi katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 na utaongezeka kufikia wastani wa asilimia nne mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021 ukuaji wa pato la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.3 wa mwaka 2020. Aidha, ukuaji wa pato la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa asilimia 5.9 kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.1 kwa mwaka 2020. Ukuaji chanya wa uchumi katika nchi wanachama wa jumuiya hizo ulitokana na kulegezwa kwa masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19 pamoja na hatua mbalimbali za sera na kibajeti zilizochukuliwa kwa ajili ya kuchochea shughuli za kiuchumi katika sekta zilizoathirika zaidi na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchumi wa Taifa; ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kipindi cha mwaka 2021 ulikuwa kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 mwaka 2020. Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa uchumi kumetokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 na uwekezaji wa kimkakati hususan katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege pamoja na shughuli zingine.

Mheshimiwa Spika, shughuli zingine za kiuchumi zilizokuwa na ukuaji mkubwa katika kipindi cha mwaka 2021 ni pamoja na sanaa na burudani ambyo asilimia 19.4, umeme asilimia 10.0, uchimbaji madini na mawe asilimia 9.6, habari na mawasiliano asilimia 9.1.

Mheshimiwa Spika, pato ghafi la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 161.5 kwa mwaka 2021, ikilinganishwa na shilingi trilioni 152.1 kwa mwaka 2020. Aidha, mwaka 2021 Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu milioni 57.7 ikilinganishwa na watu milioni 55.9 kwa mwaka 2020. Kwa mantiki hiyo, wastani wa pato kwa mtu lilikadiriwa kufikiwa shilingi bilioni 2,798,224.23, sawa na dola za Kimarekani 1,211.77 kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,701,039.25, sawa na dola za Kimarekani 1,171.51 kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mwenendo wa bei; mfumuko wa bei umeendelea kuwa ndani ya lengo la wigo wa asilimia tatu hadi tano. Mwaka 2021 mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.7 kwa mwaka ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.3 katika kipindi cha kama hicho kwa mwaka 2020. Aidha, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.8 Aprili, 2022 ikilinganishwa na asilimia 3.3 Aprili, 2021. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na sababu zilizo nje ya udhibiti wa kibajeti ama wa kisera zikiwemo kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia kutokana na athari ya vita baina ya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa Sera za Fedha; katika mwaka wa fedha 2021/2022 malengo ya sera ya fedha ni kama ifuatavyo; ukuaji wa fedha taslimu yaani *MO* wa wastani wa asilimia 9.9; ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi yaani *M3* wa asilimia 10.0; ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa wastani wa asilimia 10.6; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza sera za fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi katika uchumi ili kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kusaidia kuimarisha shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na janga la UVIKO-19, hali hiyo ilisaidiwa na mfumuko mdogo wa bei ulioendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia tatu hadi tano.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Ili kufanikisha jukumu hili, Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikitumia nyenzo mbalimbali za kisera za fedha kwa ajili ya kuongeza ukwasi katika sekta ya benki, ikiwemo kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki, kununua fedha za kigeni kwenye soko la jumla na kuingia katika mikataba ya kubadilisha fedha za kigeni na mabenki.

Vilevile Benki Kuu ilichukua hatua za ziada za kisera kwa ajili ya kuchochea ongezeko la mikopo nafuu kwa sekta binafsi, hususan shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu yote hii iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujazi wa fedha na karadha; sambamba na utekelezaji wa sera ya fedha ilivyolenga kuongeza ukwasi, ujazi wa fedha umeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 wastani wa fedha taslimu umeongezeka kwa asilimia 13.8 ikilinganishwa na asilimia 2.7 katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliotangulia na lengo la wastani wa asilimia 9.9 kwa mwaka 2021/2022.

Vilevile ujazi wa fedha kwa tafsiri pana yaani M3 ulikua kwa wastani wa asilimia 13.1, ikilinganishwa ukuaji wa asilimia 6.8 wa lengo asilimia 10. Ongezeko hili la ukwasi kwenye uchumi limesaidia shughuli mbalimbali za uchumi zilizokuwa zimeathiriwa na UVIKO-19 na kuanza kufunguka kwa ujumla na kuongeza kwa mchango kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, upande wa mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi; mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha kutokana na sera wezeshi za kifedha pamoja na za kibajeti, pamoja na hatua hizo zinazoendelea kutekelezwa na Serikali kuboresha mazingira ya biashara na utekelezaji wa hatua za kisera zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu zenye lengo la kuchochea ukuaji wa mikopo na kushusha viwango vya riba za mikopo. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 8.4 katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022

ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mwenendo wa riba; matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha yamesaidia kudumisha kiwango cha kutosha cha ukwasi katika sekta ya benki, na kupelekea utulivu wa riba za masoko ya fedha ya muda mfupi katika viwango vya hapa nchini. Mathalani, riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabanki yaani *the overnight interbank cash market interest rate* ilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 3.42 katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, kutoka wastani wa asilimia 3.6 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, wastani wa riba za mikopo ya benki kwa sekta binafsi kwa ujumla ulipungua japo kwa kasi ndogo hadi kufikia asilimia 16.44 katika kipindi kama hicho Julai 2021 hadi Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya nje; katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili, 2022, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia dola za Kimarekani bilioni 10.62 kutoka dola za Kimarekani bilioni 8.56 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021. Ongezeko hili kubwa lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia pamoja na mapato yanayotokana na shuguli za utalii ikiwa ni matokeo ya hatua zilizochukuliwa na mataifa mengine duniani kufungua mipaka ya kuruhusu safari za kimataifa kutokana na kupungua kwa maambukizi ya UVIKO-19. Aidha, katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ilifikia dola za Kimarekani bilioni 13.23, ikilinganishwa na dola za Kimarekani bilioni 9.27 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa iliongezeka kufikia dola za Kimarekani bilioni 7.03 katika kipindi cha mwaka kinachoishia Aprili 2022 ikilinganishwa na dola za Kimarekani bilioni 6.36 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia ikiwemo, bidhaa za

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

maua na mbogamboga, saruji, bidhaa za plastiki, vipodozi pamoja na nafaka hususan mchele pamoja na mahindi.

Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka na kufikia dola za Kimarekani bilioni 3.59 kwa mwaka unaoishia Aprili, 2022, ikilinganishwa na dola za Kimarekani bilioni 2.20 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021. Ongezeko hili lilichangiwa na idadi kubwa ya watalii waliongia nchini katika kipindi husika. Aidha, katika kipindi husika malipo ya huduma yaliongezeka kutoka dola za Kimarekani bilioni 1.22 na kufikia dola za Kimarekani bilioni 2.20. Ongezeko hili lilichangiwa na ongezeko la gharama za mizigo sambamba na ongezeko la gharama za uagizaji wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa akiba ya fedha za kigeni; akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili, 2022 akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Kimarekani bilioni 5.46 ambayo inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.8. Mahitaji ya nchi kisheria ni kuwa na kiasi cha fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa za kutoka nje kwa muda usiopungua miezi 4.0.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa thamani ya shilingi; thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola za Kimarekani imeendelea kuwa tulivu, ambapo dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,308.87 katika soko la jumla kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,309.48 katika kipindi kama hicho Julai, 2020 hadi Aprili, 2021. Hii ni sawa na kuongezeka kwa thamani ya shilingi kwa wastani wa asilimia 0.03.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa sekta ya kibenki; kwa upande wa mwenendo wa sekta ya kibenki hapa nchini imeendelea kuwa imara, stahimilivu na yenye kutengeneza faida ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 rasilimali za benki zilifikia kiasi cha shilingi bilioni

40,198.2, sawa na ongezeko la asilimia 12.9 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana. Benki zimeendelea kuongeza utoaji wa huduma za kibenki kwa wananchi wengi zaidi kwa kutumia mifumo ya kielektroniki yenye gharama nafuu. Kwa upande mwingine, Benki Kuu imeendelea kuimarisha usimamizi wa benki na taasisi za fedha hapa nchini kwa kutekeleza sera wezeshi na kutoa kanuni na miongozo mbalimbali ili kuendelea kutekeleza sera wezeshi za kutoa kanuni na miongozo mbalimbali ili kulinda uimara wa sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya benki inatarajiwa kubaki salama na tulivu, sambamba na sera zinazotekelezwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali pamoja na Benki Kuu ya Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara na ufanisi katika utoaji wa huduma za fedha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa deni la Serikali; hadi Aprili, 2022 deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 69.44 ikilinganishwa na shilingi trilioni 60.72 kipindi kama hicho kwa mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 14 katika kiasi hicho, deni la nje lilikuwa shilingi trilioni 47.07 na deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 22.37. Ongezeko la deni la Serikali limetokana na kupokelewa kwa mikopo kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2021/2022; kama unavyofahamu Serikali imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 wa Maendeleo wa Taifa kwa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Kutokana na usimamizi thabiti wa Serikali chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM, utekelezaji wa mpango umekuwa na mafanikio makubwa katika nyanja zote ikiwemo kiuchumi, miundombinu, kijamii na uwekezaji. Mafanikio haya yaliyopatikana katika sekta mbalimbali ni pamoja na haya yafuatayo:-



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Moja ya mafanikio kwenye upande miundombinu; ni kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati ya yenye Kiwango cha Kimataifa yaani *Standard Gauge Railway (SGR)* ambapo kipande cha Dar es Salaam – Morogoro kimeshakamilika utekelezaji wake kwa zaidi ya asilimia 96.54 na kipande cha Morogoro – Makutupora zaidi ya asilimia 85.02; kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa kipande cha Makutupora – Tabora chenye kilometa 368 na kuendelea na hatua za ununuzi wa kutafuta mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia za reli kwa kipande cha Tabora – Isaka na kuendelea na ununuzi wa injini, mabehewa pamoja na vifaa vya matengenezo ya njia ya reli.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuzalisha umeme Bwawa la Mwalimu Nyerere; mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa tuta kuu la bwawa ambapo utekelezaji wake umeshafikia zaidi ya asilimia 62.01, njia za kupitishia maji ya kufua umeme ambayo imeshafikia asilimia zaidi ya 74.16, nyumba ya mitambo ya kufua umeme ambayo imeshafikia asilimia 44.22, kingo za bwawa asilimia 42.82 na kituo cha kupokelea na kusafirisha umeme wa kV 400 ambayo imeshafikia zaidi ya asilimia 75.44. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umeshafikia zaidi ya asilimia 60.22.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uboreshaji wa Shirika la Ndege; baadhi ya mafanikio yaliyopatikana na ni pamoja na kupokelewa kwa ndege tatu ambapo ndege moja ni aina ya *Dash 8 Q400* na mbili aina ya *Airbus A220 300* na kufanyika kwa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege tano mpya ambapo ndege moja aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner*, ndege mbili aina ya *Boeing 737-9*, ndege moja aina ya *De Havilland Dash 8-Q400* na ndege moja ya mizigo aina ya *Boeing 767- 300F* na kuendelea na ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege ya *KIMAFa* katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya umeme, mafanikio yaliyopatikana ni kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Rusumo megawati 80 ambapo utekelezaji wake umeshafikia asilimia 91.6;

kuendelea na utekelezaji wa mradi wa *Kinyerezi / Extension* megawati 185 ambapo utekelezaji wake umeshafikia asilimia 88; kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kupoozea umeme vya Singida na Dodoma katika mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kV 400 Iringa – Singida – Shinyanga pamoja na *transmission investment project*; kuendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa kV 400 Singida – Arusha – Namanga ambapo utekelezaji wake umeshafikia zaidi ya asilimia 96.1.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, moja ya mafanikio ni kusainiwa kwa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato awamu ya kwanza itakayoanzisha ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege pamoja na jengo la abiria; kukamilika kwa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita; kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka na kufungwa kwa mfumo wa kuongoza ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; kukamilika kwa usanifu na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege mfano Songea zaidi ya asilimia 96, Mtwara zaidi ya asilimia 89, Iringa zaidi ya asilimia 44, Songwe zaidi ya asilimia 95 na Musoma zaidi ya asilimia 10; kuendelea na maandalizi ya ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vitakavyogharimu *Euro* takribani milioni 50 sawa na zaidi ya shilingi bilioni 136.5.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na upande wa Bandari ya Dar es Salaam ambapo kumekuwepo na kuboreshwa kwa gati namba 1 hadi 7; kukamilika kwa ujenzi wa gati maalumu la kuhudumia meli za magari na yadi ya kuhudumia makasha.

Kwa upande wa Bandari ya Mtwara ni kukamilika kwa ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300 na kuendelea na ujenzi wa uzio na sakafu ngumu katika eneo la mita za mraba 75,807.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kwa upande wa Bandari ya Tanga kukamilika kwa uongezaji wa kina wenye lengo la kuingia meli kutoka mita nne hadi mita 13 pamoja na kuweka vifaa vya kuongoza meli.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maziwa makuu ni kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Nyamirembe, Magarine, Lushamba, Ntama na Mwigobero pamoja na gati mbili za majahazi katika Bandari ya Mwigobero.

Kwa upande wa Ziwa Tanganyika, kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Kagunga, Sibwesa na Kabwe na kwa upande wa Ziwa Nyasa ni kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari ya Kiwira na Itungi na kukamilika kwa ujenzi wa gati na miundombinu yake katika Bandari ya Ndumbi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za usafiri na usafirishaji abiria na mizigo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili za *New Butiama Hapa Kazi Tu* na *New Victoria Hapa Kazi Tu* na kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya *MV Mwanza Hapa Kazi Tu* yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ambao umeshafikia zaidi ya asilimia 66.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kujengwa kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilometa 216.26 na kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe jumla ya kilometa 1,124.3 za barabara za mikoa. Kwa upande wa barabara zinazosimamiwa na *TARURA*, jumla ya kilometa 232.94 za lami na kilometa 8,181.65 za changarawe pamoja na madaraja 405 na makalavati 206 yakiwa yamejengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya moja ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri 127, ujenzi wa vituo vya afya 70, ukamilishwaji wa maboma ya zahanati 564; kukamilika kwa ukarabati wa wodi namba 18 katika jengo la Sewa Haji katika

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ajili ya wodi za kulaza wagonjwa binafsi; kukamilika kwa ujenzi na ufungaji wa mitambo ya kuzalisha tiba hewa pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa maabara maalumu na ufungaji wa mitambo ya kisasa katika Taasisi ya Mifupa yaani *MOI*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu moja ya mafanikio ni kuendelea na sera ya kutekeleza elimu bila ada ili kuongeza fursa za elimu hapa nchini. Hadi Aprili, 2022 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 244 na kuchapisha na kusambaza kwa vitabu vya kiada 15,609,515 na kiongozi cha mwalimu 538,006 kwa masomo yote ya darasa la sita pamoja na la saba ili kuimarisha uwiano kati ya wanafunzi pamoja na kitabu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji mjini na vijijini, moja ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na upatikanaji wa huduma za maji. Hadi Aprili, 2022 umefikia wastani wa asilimia 74.5 vijijini kutoka asilimia 72.3 mwezi Juni, 2021 na mijini imefikia asilimia 86.5 kutoka asilimia 86 katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo, mifugo na uvuvi, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuzalishwa kwa mbegu bora tani 35,199.39 na miche 32,301,995 ya mazao mbalimbali; kutolewa kwa pikipiki 7,000 kwa Maafisa Ugani kwa ajili ya kuimarisha huduma za ugani; kupatikana kwa mbolea tani 436,452; kuanzishwa kwa mashamba 67 yenye ukubwa wa hekta 205,432.45 ambayo kila moja lina ukubwa wa kuanzia hekta 20; kuhakikiwa na kutambuliwa kwa mashamba matano ya *NAFCO* yenye ukubwa wa ekari 18,980 na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu tatu za umwagiliaji ambazo ni Mkombozi, Idudumo pamoja na Ilemba.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, ni kuendelea na utafiti wa tathmini ya teknolojia bora ya ng'ombe chotara wa maziwa na uzalishaji wa nyama; kukamilika kwa ujenzi wa majosho 95 katika mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa; kuanza kwa ujenzi wa majosho

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

73 katika halmashauri 58; kuzalishwa na kusambazwa kwa dozi 43,409,600 za chanjo dhidi ya magonjwa ya mdondo, homa ya mapafu ya ng'ombe na mbuzi, kimeta cha mbavu mchanganyiko na kimeta na cha mbavu na kutupa mimba.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, kusainiwa kwa mkataba na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko kule Lindi; kuendelea na maandalizi ya ununuzi wa meli mbili za uvuvi kati ya zile nne zilizopangwa na kukamilika kwa mpango wa kibiashara wa ufufuaji wa Shirika la Uvuvi la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa viwanda; katika kutekeleza mkakati wa kuendeleza sekta ya viwanda kwa kuweka mazingira wezeshi, hatua iliyofikiwa ni pamoja na kuendelea na majadiliano na wawekezaji watakaowekeza kwenye miradi ya msingi mitatu katika eneo maalumu la uwekezaji la Bagamoyo ambalo ni bandari ya kisasa, sehemu ya kanda maalumu kwa ajili ya mizigo na usafirishaji pamoja na sehemu ya mji wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa vituo vitatu vya umahiri katika shughuli za uchimbaji wa madini vya Chunya, Songea pamoja na Mpanda; kuanzishwa kwa masoko mapya manne ya madini na vituo vipya nane vya ununuzi wa madini, hivyo kufanya jumla ya masoko ya madini kuwa 42 na vituo vya ununuzi wa madini kufikia 75. Mafanikio mengine ni kusainiwa kwa mikataba ya ubia kwa ajili ya uwekezaji wa kiasi cha takribani dola za Kimarekani milioni 1,672.57 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kampuni za madini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa habari, mawasiliano na TEHAMA baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa kilometa 409 ambapo kilometa 72 zimeunganishwa nchi ya Msumbiji kupitia mpaka wa Mtambaswala na kilometa 72 zimeunganishwa na watumiaji wa mwisho katika ofisi za Serikali za Msalato, Mtumba na

Kikombo hapa Dodoma na kilometa 265 zimeunganishwa Manyoni – Kambi Katoto; kukamilika kwa ukarabati wa kilometa 105 za ujenzi wa mkongo wa Arusha – Namanga kupitia miundombinu ya *TANESCO* na kukamilika kwa uandaaji wa ramani za mipaka ya kiutawala katika Halmashauri 20.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maliasili na utalii baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana ni pamoja na kuanzishwa kwa mara ya kwanza kwa programu ya *Royal Tour* iliyoasisiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambayo imelitangaza Taifa na utalii katika nyanja mbalimbali za kimataifa; kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka nje ya nchi kutoka watalii 620,867 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 922,692 kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 48.6. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kukuza biashara na uwekezaji, wateja 13,836 walipatiwa huduma katika kituo cha huduma za uwekezaji mahala pamoja ambapo jumla ya miradi 206 ya ubia kati ya wageni na watanzania ilisajiliwa yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 769 na inatarajiwa kutoa ajira kwa Watanzania wapatao 37,451.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utawala bora na utawala wa kisheria; katika kuhakikisha kuwa utawala bora na utawala wa sheria unashamiri hapa nchini, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo na miundombinu ya kitaasisi ya utoaji haki, uwazi na uwajibikaji wa utumishi wa umma, shughuli za Mfuko wa Bunge pamoja na Mfuko wa Mahakama; mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kulijengea Bunge uwezo kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi katika maeneo ya usimamizi wa bajeti, masuala ya kodi, utungaji wa sheria, kuendesha shughuli za Bunge kupitia Bunge Mtandao, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo, pamoja na ujumuishwi wa masuala ya jinsia katika bajeti.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19; kama tunavyofahamu katika kipindi cha mwaka 2019 dunia ilikumbwa na mlipuko wa janga la UVIKO-19 ambapo kwa kiasi kikubwa uliathiri afya za jamii pamoja na uchumi wa nchi. Katika kukabiliana na athari hizo za mlipuko huo, Serikali iliandaa mpango wa maendeleo kwa ajili ya ustawi wa jamii na mapambano dhidi ya UVIKO-19. Mpango huo ulizinduliwa rasmi tarehe 10 Oktoba, 2021 na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mpango huo ulitekelezwa kwa kugharamiwa na mkopo nafuu usio na riba wenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 567.25 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa la *IMF*.

Mheshimiwa Spika, kupitia fedha hizo Serikali imeweza kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi hususan katika sekta ya elimu ambayo ilipokea shilingi bilioni 368.9; afya ambayo ilipokea shilingi bilioni 466.9; utalii ilipokea shilingi bilioni 90.2; sekta ya maji ilipokea shilingi bilioni 139.4; na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ulipokea shilingi bilioni 5.5.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 – 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Mpango umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 na sera na mikakati mbalimbali ya kissekta, kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) 2050 na Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu yaani 2030.

Mheshimiwa Spika, malengo na shabaha ya uchumi katika mwaka 2022 ni kama ifuatavyo: -

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(i) Ukuaji wa pato halisi la Taifa kufikia asilimia 4.7 kwa mwaka 2022 na asilimia 5.3 kwa mwaka 2023.

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei pamoja na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi saba katika muda wa kati.

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya pato la Taifa kwa mwaka 2022/2023.

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 11.7 ya pato la Taifa kwa mwaka 2022/2023.

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, misingi itakayozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo: -

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za maendeleo.

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili kama vile vita pamoja na magonjwa ya mlipuko.

(iii) Kuendelea kuwa na utoshelevu wa chakula hapa nchini.

(iv) Uwepo wa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na katika nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2022; katika mwaka 2022 Serikali itaendelea kuimiriha miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati inayoendelea. Miradi hiyo inatarajiwa kuwa na matokeo mapana ya haraka katika uchumi, ikiwemo kuzalisha ajira,



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kipato na kuchangia zaidi kupunguza hali ya umaskini kwa wananchi wetu. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa reli, mradi wa kufua umeme, kuboresha shirika la ndege, kuchakata gesi asilia katika baadhi ya vyanzo na ujenzi wa barabara na madaraja makubwa ili kuendeleza kanda maalumu za kiuchumi ikiwemo eneo maalumu la uwekezaji la Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, miradi ambayo inatarajiwa kutekelezwa ni pamoja na kuendeleza sekta ya kilimo; kutekeleza miradi ya kimkakati ya umwagiliaji, mbegu, maghala pamoja na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kukuza biashara na uwekezaji, kipaumbele kitakuwa katika kusimamia utekelezaji wa mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara ikiwemo kuimarisha mazingira ya kisera na kisheria kuhusu uwekezaji pamoja na mifumo ya uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuchochea maendeleo ya watu, miradi itakayotekelezwa inalenga kuboresha maisha ya watu kwa upande wa sekta ya elimu. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kugharamia elimu ya msingi bila ada pamoja na kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuendeleza rasilimali watu, baadhi ya mambo yatakayotekelezwa ni pamoja na kuendeleza utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya kukuza ujuzi hapa nchini ili kuongeza ajira kwa vijana kwa kutoa mafunzo ya ufundi na stadi za kazi kupitia programu mbalimbali zikiwemo kuimarisha Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi nchini; kuboresha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu; na utekelezaji wa programu ya Taifa ya kukuza staha.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2022/2023 yanapatikana katika kitabu cha Mpango, Sura ya Nne.

Mheshimiwa Spika, vihatarishi vya utekelezaji wa mpango kwa mwaka 2022/2023; utekelezaji wa mpango unaweza kuathiriwa na vihatarishi vya ndani na nje. Vihatarishi vya ndani ni pamoja na ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo; ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika mipango ya maendeleo; uharibifu wa mazingira, mabadiliko ya tabia ya nchi na uhalifu wa kimtandao pamoja na rushwa. Vihatarishi vya nje ni pamoja na majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko; mitikisiko ya kiuchumi duniani; kubadilika kwa teknolojia na kutopatikana kwa misaada na mikopo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango, Serikali itachukua hatua mbalimbali ikijumuisha kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa kodi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti za kielektroniki wanapouza bidhaa na wanaonunua kudai risiti wanaponunua bidhaa; kuendelea kuimarisha na kuhamasisha wananchi kuhusu uelewa wa huduma za sekta ya fedha ikiwemo utoaji wa mikopo, uwekezaji, mitaji pamoja na bima. Mambo mengine ni pamoja na kuendelea kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi wa ndani na nje ili kupunguza gharama za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ugharamiaji wa Mpango; kwa mwaka 2022/2023 inakadiriwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 15,004.8 sawa na asilimia 36.2 ya Bajeti yote ya Serikali zitatumika kugharamia miradi ya maendeleo ikijumuisha miradi ya huduma za jamii. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 12,305.8 sawa na asilimia 82.0 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,699.1 sawa na asilimia 18.0 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje. Katika kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kama *engine* muhimu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo Serikali itahakikisha miradi yote inayovutia uwekezaji wa sekta binafsi inatekelezwa kwa

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

utaratibu wa Ubia kati ya sekta ya umma pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, narudia, katika kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kama *engine* muhimu ya utekelezaji wa miradi, Serikali itahakikisha miradi yote inayovutia uwekezaji wa sekta binafsi inatekelezwa kwa utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma pamoja na sekta binafsi yaani *joint ventures* kwa kutumia utaratibu wa Kampuni Maalumu yaani *Special Purpose Vehicle*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ukusanyaji wa mapato ya kugharamia Mpango, Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo; kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa kodi kwa kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wanatoa risiti za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya kufuatilia mizigo inayokwenda nchi jirani ili kuimarisha uwezo wa usimamizi wa mizigo inayopita kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mashirikiano na washirika wa maendeleo kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo yaani *Development Cooperation Framework* ili kuhakikisha kuwa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo zinaendelea kupatikana kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kugharamia miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia wa sekta ya binafsi kama nilivyotoka kusema Serikali imepanga kuwezesha Mamlaka za Serikali Mitaa zenye miradi ya *PPP* iliyopo katika hatua mbalimbali za maandalizi ikiwemo upembuzi yakinifu na ununuzi wa wabia kukamilisha miradi hiyo iweze kuanza utekelezaji wake. Katika mwaka 2022/2023

Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji; Serikali itahakikisha kuwa mipango ya maendeleo inatekelezwa kama ilivyokusudiwa, suala la ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji limeendelea kupewa msukumo wa kipekee katika shughuli za kila siku za Serikali. Katika kutekeleza hilo, mwaka wa fedha 2021 Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya ufuatiliaji na tathmini wa miradi 225 katika sekta za uchukuzi, viwanda, elimu, afya, ujenzi, utawala bora, kilimo, mifugo, maji pamoja na biashara ikitekelezwa na Serikali pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uwepo wa ushirikishwaji wa kutosha katika masuala ya ufuatiliaji na tathmini; Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kushirikiana na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Sekta Binafsi katika kuratibu na kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

Mheshimiwa Spika, Serikali inazielekeza Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutafsiri malengo na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 katika Mipango na Bajeti za kissekta kwa mwaka 2022/2023. Aidha, Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo pamoja na Programu za Maendeleo wa mwaka 2022 ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango kazi wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inazielekeza Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuaandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, majumuisho; kama nilivyoelezea hapo awali, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 – 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Utekelezaji wa Mpango utaendelea kuimarisha viashiria vya uchumi jumla, kuboresha mazingira ya uwekezaji viwandani ikiwemo kuimarisha majadiliano na wawekezaji wa ndani na nje, kuimarisha mahusiano ya kisiasa, ulinzi na diplomasia ya uchumi na nchi nyingine na kuendelea kutekeleza kwa kasi miradi ya maendeleo na kuendeleza mashirikiano na sekta binafsi pamoja na sekta ya umma wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuchochea uwekezaji wa viwandani hususani kwa kutumia rasilimaliwatu pamoja na malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini ikiwemo mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, madini, misitu pamoja na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada za kukabiliana na athari za majanga mbalimbali ya asili na yasiyo ya asili yakiwemo magonjwa, vita na mabadiliko ya tabianchi. Mathalani, tutaendelea kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Athari za UVIKO-19 na kuweka mpango madhubuti wa kupunguza athari zinazotokana na vita vinavyoendelea kati ya Urusi pamoja na Ukraine ikiwepo kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa mbalimbali na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kwa niaba ya Serikali ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Sekta

Binafsi, Taasisi za Elimu na Tafiti, Asasi za Kiraia, Taasisi za Kidini, Washirika wa Maendeleo na Wananchi wote kwa namna walivyojitoa na kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuimarisha uchumi wa Taifa letu. Wadau hao wamekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kwa msingi huo, ninawaomba na kuwasih wadau wote waendele kushirikiana na Serikali yetu inayoongozwa na mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi yaani CCM ili kuweza kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii isingeweza kukamilika bila jitihada kubwa zilizofanywa na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, hivyo, kwa dhati ya nafsi yangu naomba nitoe shukrani zangu za kipekee kwa Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mawaziri na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu wa Wizara zote na Naibu Makatibu Wakuu na viongozi wote wa Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya taarifa hii ya Hali ya Uchumi wa Taifa letu kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023.

Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Emmanuel Mpawe Tutuba, kwa kujitoa usiku na mchana kukamilisha kwa wakati na kwa ubora Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwa kutenga muda wao kusikiliza hotuba hii na niwaombe wajiandae. Aidha, napenda kuwataarifu wadau wote kuwa hotuba hii na vitabu vya

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ni [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz). Na niwaombe wajiandae kwa hotuba ya bajeti ambayo nitarudi nayo leo alasiri ambayo itakuwa imebeba matumaini ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA  
DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA  
UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2021 NA MPANGO WA  
MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2022/23 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23. Taarifa hizo ndiyo msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 nitakayowasilisha katika Bunge hili Tukufu leo alasiri.

**2. Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine katika Bunge hili baada ya majadiliano ya bajeti za mafungu mbalimbali. Mkutano huu wa Saba wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muhimu katika kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

**3. Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena, nitumie fursa hii kutoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Chama cha Mapinduzi na Watanzania wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marehemu Irene Alex Ndyamkama. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, Amina.

**4. Mheshimiwa Spika**, kwa moyo mkunjufu, napenda kutoa pongezi zangu za dharti kwako Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla wana imani kubwa sana na wewe na hawana shaka na uzoefu, weledi na umahiri wako katika kusimamia na kuongoza shughuli za Bunge. Aidha, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu, ujasiri na afya njema ili muweze kuendelea kutekeleza majukumu yenu ya kuliongoza Bunge letu.

**5. Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya kipekee, nitoe pongezi zangu za dharti, kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na utumishi uliotukuka kwa watanzania unaolenga kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi na kijamii. Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira yake ya dharti ya kilitumikia Taifa kwa uaminifu ambapo ameendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazolenga kuleta maendeleo kwa Watanzania ikiwemo: kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kielelezo na miradi mingine ya kuchochea uchumi na kuimarisha huduma za jamii; kuendelea mapambano dhidi ya rushwa; na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

**6. Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais amekuwa akiendelea kutuongoza kwa vitendo kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuchochea ukuaji wa uchumi hususan sekta ya utalii



ambayo iliathirika zaidi na UVIKO-19 ikiwemo kushiriki kwenye filamu ijulikanyo kwa jina la *The Royal Tour* kama Mwongoza Utalii Namba Moja Nchini. Mheshimiwa Rais amekuwa chachu na kinara wa utalii kupitia filamu hiyo inayolenga kukuza sekta ya utalii ambayo inatarajiwa kuzalisha takriban ajira milioni 1.3 na fedha za kigeni dola za Marekani bilioni 2.6. Filamu hiyo iliyozinduliwa kwa Mara ya Kwanza Jijini New York tarehe 18 Aprili 2022 na baadaye tarehe 21 Aprili 2022 Jijini Los Angeles. Ndugu Watanzania wenzangu, hii ni hatua kubwa sana kwa Taifa letu kwa kuwa filamu hii inapatikana kupitia chaneli za *Apple TV Plus* na *Amazon Prime* za nchini Marekani ambazo zinakadiriwa kuwa na watazamaji zaidi ya milioni 200 duniani. Ama kwa Hakika Mama Anaupiga Mwingi; na hivyo tuna kila sababu ya kuunga mkono jitihada hizi na kwenda pamoja na Mama.

**7. Mheshimiwa Spika**, kipekee natoa shukrani zangu za dhiti kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kumsaidia kazi katika nafasi ya Waziri wa Fedha na Mipango. Kwa imani hii aliyoionesha kwangu napenda kuwahakikishia Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa bidii kubwa, weledi, uaminifu, uadilifu na uzalendo wa kiwango cha hali ya juu ili kuhakikisha matamano ya Mheshimiwa Rais na Watanzania wote ya kuwa na maendeleo na ustawi wa kiwango cha juu yanafikiwa.

**8. Mheshimiwa Spika**, Sote tunafahamu kuwa, nchi yetu na dunia kwa ujumla inaendelea kushuhudia athari za UVIKO-19 ambazo zimesababisha kushuka kwa shughuli za kiuchumi duniani, ikiwemo uzalishaji, biashara za ndani na kimataifa, utalii na usafirishaji wa bidhaa. Katika mwaka 2021, uchumi wa Taifa letu na wa dunia kwa ujumla ulianza kuimarika baada ya kupitia katika kipindi cha kukabiliana na athari za UVIKO-19. Aidha, wakati Serikali ikiendelea na jitihada za kuimarisha uchumi, mwezi Februari 2022 kuliibuka vita kati ya mataifa ya Urusi na Ukraine ambayo imesababisha Urusi kuwekewa vikwazo na hivyo kusababisha kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali katika soko la dunia zikiwemo mafuta

na gesi. Sanjari na kupanda kwa bei hizo, kumekuwa na uhaba wa baadhi ya bidhaa katika soko la Dunia ikiwemo, mbolea, ngano na mafuta ya kula. Serikali imeendelea kuchukua hatua katika kukabiliana na athari hizo ikiwemo kupokea Mkopo wa Masharti nafuu wa shilingi trilioni 1.3 zilizoelekezwa katika sekta ya afya, elimu, maji na utalii ili kuchochea uchumi na kukabiliana na UVIKO-19; kuongeza bajeti ya kilimo, mifugo, uvuvi, nishati na miundombinu ya wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga ili kuchochea uzalishaji wa ndani na kupunguza nakisi ya urari wa biashara; na kuangalia namna bora ya uagizaji mafuta itakayoleta unafuu wa bei kwa wananchi. Aidha, nichukue fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na athari hizo kwa lengo la kuleta unafuu wa maisha kwa Wananchi.

**9. Mheshimiwa Spika**, Nipende kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika mchakato huu nikianza na Bunge lako Tukufu chini ya uongozi wako Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Sillo Daniel Baran (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri wao mahiri wakati wa uandaaji wa taarifa nilizowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

**10. Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 imeandaliwa kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla na sekta mbalimbali kwa mwaka husika ikilinganishwa na mwaka 2020. Aidha, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 yamezingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akilihutubia rasmi Bunge hili la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021. Aidha, Mpango

umezingatia Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda na kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050; Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

**11. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza Mpango wa mwaka 2022/23, msukumo mkubwa utawekwa katika sekta za uzalishaji ambazo ni kilimo, mifugo, uvuvi na nishati kwa kuwa sekta hizi huchochea uzalishaji kwa matumizi ya ndani na mauzo nje ya nchi, hupunguza nakisi ya urari wa biashara, mfumuko wa bei na huzalisha ajira zinazowagusa wananchi wengi. Sambamba na vipaumbele hivyo, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo ikiwemo miradi ya kielelezo ya ujenzi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR), ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere - MW 2,115, uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) pamoja na miradi ya elimu, afya, maji, usafiri wa anga na majini, bandari, maliasili na utalii, mapinduzi ya TEHAMA, miundombinu ya barabara na madaraja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kukuza ustawi wa sekta binafsi nchini.

## **MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021**

### **Uchumi wa Dunia**

**12. Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili 2022 inaonesha kuwa, uchumi wa dunia uliimarika na kufikia wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 3.1 mwaka 2020. Kuimarika kwa uchumi wa dunia kumetokana na hatua zilizochochuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na nchi mbalimbali katika kuimarisha uchumi, ikiwemo utekelezaji wa sera za fedha na bajeti zinazochochea shughuli za uchumi zilizoathirika na kuendelea kuimarishwa kwa huduma za afya ikiwemo uhamasishaji na usambazaji wa chanjo kwa lengo la kupunguza athari za UVIKO-19. Hata hivyo, uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua na kufikia ukuaji wa asilimia 3.6 mwaka 2022. Hii inatokana na uwepo wa vita kati ya nchi ya

Urusi na Ukraine ambayo imesababisha kuongezeka kwa bei za vyakula na nishati hivyo, kudhoofisha zaidi matarajio ya kurejea kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na UVIKO-19. Ikumbukwe kuwa Urusi ni nchi ya pili kwa hifadhi/uzalishaji wa bidhaa za petroli duniani ambapo inachangia wastani wa asilimia 12 katika mafuta yote yanayozalishwa dunia ikitanguliwa na Marekani yenye mchango wa asilimia 20. Aidha, Urusi ndiyo mzalishaji mkubwa wa nishati ya gesi na mafuta inayotumika katika shughuli za kiuchumi barani Ulaya. Vilevile, kufikia mwaka 2023 na kuendelea uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua zaidi na kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 3.3 kwa kipindi cha muda wa kati iwapo vita kati ya Urusi na Ukraine vitaendelea pamoja na kuendelea kuzidisha vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Urusi.

## **Uchumi wa Afrika na Kikanda**

**13. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2021, nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilikuwa na ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 4.5, ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.7 mwaka 2020. Hii ilitokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa ili kuimarisha ukuaji wa uchumi ikiwemo kuboresha huduma za afya pamoja na kuimarika kwa bei za bidhaa zinazouzwa nje ya ukanda huo baada ya kuondolewa kwa vikwazo vilivyowekwa ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa UVIKO-19. Ukuaji wa uchumi katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 na utaongezeka kufika wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2023.

**14. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2021, ukuaji wa Pato la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.3 mwaka 2020. Aidha, ukuaji wa Pato la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa asilimia 5.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.1 mwaka 2020. Ukuaji chanya wa uchumi katika nchi wanachama wa jumuiya hizo ulitokana na kulegezwa kwa masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19 pamoja na hatua mbalimbali za sera na kibajeti

zilizochukuliwa kwa ajili ya kuchochea shughuli za kiuchumi katika sekta zilizoathirika na ugonjwa huo.

### **Uchumi wa Taifa Pato la Taifa**

**15. Mheshimiwa Spika**, Ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kipindi cha mwaka, 2021 ulikuwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 mwaka 2020. Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa uchumi kumetokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 na uwekezaji wa kimkakati hususan katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege. Shughuli za kiuchumi zilizokuwa na ukuaji mkubwa katika kipindi cha mwaka 2021 ni pamoja na Sanaa na Burudani (asilimia 19.4), Umeme (asilimia 10.0), Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 9.6) na Habari na Mawasiliano (asilimia 9.1).

**16. Mheshimiwa Spika**, Pato Ghafi la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 161.5 mwaka 2021, ikilinganishwa na shilingi trilioni 151.2 mwaka 2020. Aidha, mwaka 2021, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu milioni 57.7, ikilinganishwa na watu milioni 55.9 mwaka 2020. Kwa mantiki hii, Wastani wa Pato kwa Mtu lilikadiriwa kufikia shilingi 2,798,224.23, sawa na dola za Marekani 1,211.77 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi 2,701,039.25, sawa na dola za Marekani 1,171.51 mwaka 2020.

### **Mwenendo wa Bei**

**17. Mheshimiwa Spika**, Mfumuko wa Bei umeendelea kuwa ndani ya lengo la wigo wa asilimia 3 hadi 5. Mwaka 2021, mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.7 kwa mwaka ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.3 katika kipindi cha mwaka 2020. Aidha, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.8 Aprili 2022 ikilinganishwa na asilimia 3.3 Aprili 2021. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na sababu zilizo nje ya udhibiti wa Serikali zikiwemo kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na

usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia kutokana na athari za vita baina ya Urusi na Ukraine.

### **Utekelezaji wa Sera ya Fedha 2021/22**

**18. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, malengo ya sera ya fedha yalikuwa ni kama ifuatavyo:

- (i) Ukuaji wa fedha taslimu (M0) wa wastani wa asilimia 9.9;
- (ii) Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;
- (iii) Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa wastani wa asilimia 10.6; na
- (iv) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

**19. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi katika uchumi, ili kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kusaidia kuimarisha shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na janga la UVIKO-19, hali iliyosaidiwa na mfumuko mdogo wa bei ulioendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Ili kufanikisha jukumu hili, Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikitumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha kwa ajili ya kuongeza ukwasi katika sekta ya benki, ikiwemo kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki, kununua fedha za kigeni kwenye soko la jumla, na kuingia mikataba ya kubadilishana fedha za kigeni na mabenki (*foreign exchange swap*). Vilevile, Benki Kuu ilichukua hatua za ziada za kisera kwa ajili ya kuchochea ongezeko la mikopo nafuu kwa sekta binafsi, hususan shughuli za kilimo. Aidha, kufuatia athari za vita vya Ukraine ambayo imeongeza changamoto ya kuvurugika kwa minyororo ya ugavi na kusababisha kuongezeka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, pamoja na bei ya vyakula kama ngano na mafuta ya kula, imesababisha kuongeza kwa

mfumuko wa bei ya bidhaa hizo nchini na kuhatarisha kupanda zaidi kwa mfumuko wa bei. Hali hii imeilazimu Benki Kuu kuanza kupunguza kiasi cha ukwasi inachoongeza kwenye uchumi ili kuanza kudhibiti hatari ya kuanza kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei nchini.

## **Ujazi wa Fedha na Karadha**

**20. Mheshimiwa Spika**, sambamba na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi, ujazi wa fedha umeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, wastani wa fedha taslimu uliongezeka kwa asilimia 13.8 ikilinganishwa na asilimia 2.7 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia, na lengo la wastani wa asilimia 9.9 kwa mwaka 2021/22. Vilevile, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 13.1, ikilinganishwa ukuaji wa asilimia 6.8 na lengo asilimia 10. Ongezeko hili la ukwasi kwenye uchumi limesaidia shughuli mbalimbali za uchumi zilizokuwa zimeathirika na UVIKO-19 kuanza kufunguka kwa ujumla na kuongeza mchango kwenye Pato la Taifa.

## **Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi**

**21. Mheshimiwa Spika**, mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha kutokana na sera wezeshi za fedha na bajeti, pamoja na hatua zinazoendelea kutekelezwa na serikali kuboresha mazingira ya biashara, na utekelezaji wa hatua za kiseru zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu zenye lengo la kuchochea ukuaji wa mikopo na kushusha viwango vya riba za mikopo. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 8.4 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21, na lengo la ukuaji wa asilimia 10.6 kwa mwaka 2021/22. Miezi ya hivi karibuni kasi ya ukuaji wa mikopo imeongezeka na kufikia asilimia 13.4 kwa mwaka ulioishia Aprili 2022. Sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa katika shughuli binafsi ambazo zilipata asilimia 39.3 ya mikopo yote, ikifuatiwa na shughuli za biashara asilimia 16.7, uzalishaji viwandani asilimia 10.1 na kilimo asilimia

7.9. Ni matarajio ya serikali kuwa lengo la wastani wa asilimia 10.6 kwa mwaka 2021/22 litafikiwa kufuatia hatua za kisera na maboresho ya mazingira ya biashara yanayoendelea kutekelezwa nchini.

## Mwenendo wa viwango vya riba

**22. Mheshimiwa Spika**, matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha yamesaidia kudumisha kiwango cha kutosha cha ukwasi katika sekta ya benki, na kupelekea utulivu wa riba za masoko ya fedha ya muda mfupi katika viwango vya chini. Mathalani, riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabanki (*overnight interbank cash market interest rate*) ilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 3.42 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, kutoka wastani wa asilimia 3.60 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Vilevile, riba ya dhamana za muda mfupi (*Overall Treasury bills rate*) ilipungua hadi wastani wa asilimia 4.17 kutoka wastani wa asilimia 4.62 katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

**23. Mheshimiwa Spika**, wastani wa riba za mikopo ya benki kwa sekta binafsi kwa ujumla ulipungua japo kwa kasi ndogo hadi asilimia 16.44 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.59 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Aidha, wastani wa riba za amana kwa ujumla ulikuwa asilimia 6.85 katika, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.70. Ni matarajio yetu kuwa hatua za kisera zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu zitasaidia kuendelea kupungua kwa riba za mikopo nchini na kusaidia kukuza uchumi wa nchi na mazingira bora zaidi ya kufanya biashara.

## Sekta ya Nje

**24. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka kinachoishia Aprili 2022, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia dola za Marekani bilioni 10.62 kutoka dola za Marekani bilioni 8.56 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ongezeko hili kubwa lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia pamoja na mapato yatokanayo na shuguli za utalii ikiwa



ni matokeo ya hatua zilizochukuliwa na mataifa mengine duniani kufungua mipaka yao kuruhusu safari za kimataifa kutokana na kupungua kwa maambukizi ya UVIKO-19. Aidha, katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ilifikia dola za Marekani bilioni 13.29, ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 9.27 katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za walaji hususan petroli na dawa ambapo thamani ya petroli iliongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na ongezeko la bei katika Soko la Dunia pamoja na kiwango kilichoagizwa katika kipindi hicho.

**25. Mheshimiwa Spika**, Thamani ya mauzo ya bidhaa iliongezeka kufikia dola za Marekani bilioni 7.03 katika kipindi cha mwaka kinachoishia Aprili 2022 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 6.36 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia ikiwemo, bidhaa za maua na mbogamboga, saruji, bidhaa za plastiki, vipodozi pamoja na nafaka hususan mchele na mahindi.

Aidha, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ziliongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 8.06 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021 hadi dola za Marekani bilioni 11.09 Aprili 2022. Hali hiyo ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa malighafi, bidhaa za viwandani, mitambo na bidhaa za petroli.

**26. Mheshimiwa Spika**, mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka na kufikia dola za Marekani bilioni 3.59 kwa mwaka unaoishia Aprili 2022, ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 2.20 katika kipindi kama hicho mwaka 2021, ongezeko hili lilichangiwa na idadi kubwa ya watalii waliongia nchini katika kipindi husika. Aidha, katika kipindi husika malipo ya huduma yaliongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.22 na kufikia dola za Marekani bilioni 2.20. Ongezeko hili lilichangiwa na ongezeko la gharama za mizigo sambamba na ongezeko la gharama za uagizaji wa mafuta.

## Akiba ya Fedha za Kigeni

**27. Mheshimiwa Spika**, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili 2022, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 5.46 ambayo inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.8. Mahitaji ya nchi kisheria ni kuwa na kiasi cha fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa muda usiopungua miezi 4.0. Aidha, kiwango kilichopo kinakidhi pia lengo la kuwa na miezi isiyopungua 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

**28. Mheshimiwa Spika**, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani imeendelea kuwa tulivu, ambapo dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,308.87 katika soko la jumla kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,309.48 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021. Hii ni sawa na kuongezeka kwa thamani ya shilingi (*appreciation*) kwa wastani wa asilimia 0.03. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwepo kwa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, utulivu wa mfumuko wa bei nchini, mwendelezo wa nakisi ndogo katika urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje, pamoja na utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti.

## Mwenendo wa sekta ya kibenki

**29. Mheshimiwa Spika**, sekta ya kibenki nchini imeendelea kubaki imara, stahimilivu na yenye kutengeneza faida ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, rasilimali za benki zilifikia kiasi cha Shilingi bilioni 40,198.2, sawa na ongezeko la asilimia 12.9 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka jana. Aidha, amana za benki ziliongezeka hadi kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 28,603.3, sawa na ongezeko la asilimia 11.8, ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2020/

21. Vilevile, hali ya mitaji ya mabanki na ukwasi vimeendelea kuimarika hadi kufikia faida ya mtaji ya asilimia 18.4 Aprili 2022, ikilinganishwa na faida ya asilimia 10.3 kipindi kama hiki mwaka 2020/21.

**30. Mheshimiwa Spika**, benki zimeendelea kuongeza utoaji wa huduma za kibanki kwa wananchi wengi zaidi kwa kutumia mifumo ya kielektroniki yenye gharama nafuu. Kwa upande mwingine, Benki Kuu imeendelea kuimarisha usimamizi wa benki na taasisi za fedha nchini kwa kutekeleza sera wezeshi na kutoa kanuni na miongozo mbalimbali ili kulinda uimara wa sekta hiyo. Vilevile, benki zimeelekezwa kutekeleza mipango ya kuongeza mitaji juu ya kiwango kinachotakiwa kisheria, ili kuongeza uwezo kwenye utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi na huduma nyingine za benki.

**31. Mheshimiwa Spika**, sekta ya benki inatarajiwa kubaki salama na tulivu, sambamba na sera zinazotekelezwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali pamoja na Benki Kuu ya Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara na ufanisi katika utoaji wa huduma za fedha nchini. Aidha, Benki Kuu imeendelea kuimarisha jitihada za kupunguza kiwango cha mikopo chechefu ambapo, hadi kufikia mwezi Aprili 2022 kiwango cha mikopo chechefu kilipungua kufikia asilimia 8.23 ikilinganishwa na asilimia 9.77 mwezi Aprili 2021. Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kufuatilia kwa karibu mikakati ya mabanki katika kupunguza mikopo chechefu hadi kufikia kiwango kisichozidi asilimia 5.

## **Deni la Serikali**

**32. Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2022, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 69.44 ikilinganishwa na shilingi trilioni 60.72 kipindi kama hicho mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 14.4. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa shilingi trilioni 47.07 na deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 22.37. Ongezeko la deni la Serikali lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipya kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, ongezeko la deni lilitokana na kutolewa kwa hatifungani maalumu yenye

thamani ya shilingi trilioni 2.18 kwa ajili ya deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) lililotokana na michango ya watumishi wa kabla ya mwaka 1999. Taarifa ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba 2021 inaonesha kuwa deni la Serikali bado ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia ukomo wa viashiria vyote vinavyokubalika kimataifa.

## **MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2021/22**

**33. Mheshimiwa Spika**, kama unavyofahamu Serikali imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ambao ni Mpango wa Kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Kutokana na usimamizi thabiti wa Serikali chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, utekelezaji wa Mpango umekuwa na mafanikio makubwa katika nyanja zote ikiwemo kiuchumi, miundombinu, kijamii na uwekezaji. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbalimbali ni pamoja na:

**(i) Miundombinu ya Reli:** Kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR) ambapo kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) utekelezaji umefikia asilimia 96.54 na kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 85.02; kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa kipande cha Makutupora – Tabora (km 368); kuendelea na ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Tabora – Isaka (km 165); kuendelea na ununuzi wa injini, mabehewa na vifaa vya matengenezo ya njia ya reli; na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia za reli za Tabora – Kigoma (km 411), Uvinza – Musongati - Gitega (km 282) na Kaliua – Mpanda – Karema (km 321) kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Mafanikio mengine ni: Kukamilika kwa ukarabati wa njia ya reli ya Tanga – Moshi - Arusha (km 470); kukamilika kwa ukarabati wa mabehewa ya mizigo 200

yanayotumika kutoa huduma ya usafiri kwa njia ya reli ya *Meter Gauge* iliyopo; kukamilika kwa uundaji wa vichwa vya injini saba (7) vya sogeza; na kupokelewa kwa vichwa vya treni vitatu (3), mabehewa 44 ya mizigo na mtambo wa kupima ubora wa njia ya reli.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere – MW 2,115:**

Kuendelea na ujenzi wa tuta kuu la bwawa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 62.01, njia za kupitisha maji ya kufua umeme asilimia 74.16, nyumba ya mitambo ya kufua umeme asilimia 44.22, kingo za bwawa asilimia 42.82 na kituo cha kupokea na kusafirisha umeme kV 400 asilimia 75.44. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 60.22.

**(iii) Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania:**

Kupokelewa kwa ndege tatu (3) ambapo ndege moja (1) ni aina ya Dash 8 Q400 na mbili (2) ni aina ya Airbus A220 300; kufanyika kwa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege tano (5) mpya ambapo ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner, ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9, ndege moja (1) aina ya De Havilland Dash 8-Q400 na ndege moja (1) ya mizigo aina ya Boeing 767- 300F; kuendelea na ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege ya KIMAFa katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa Kilimanjaro (KIA); kuanzisha safari katika vituo vitatu (3) vipya vya nje ya nchi vya Lubumbashi, Nairobi na Ndola; kurejesha safari za ndani na nje kwa abiria; kuanzisha safari za mizigo za kwenda Guangzhou; na kutolewa kwa mafunzo kwa marubani 102 na wahudumu 108 wa ndani ya ndege.

**(iv) Miradi ya Umeme:**

kuendelea na ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Rusumo - MW 80 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 91.6; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Kinyerezi I Extension MW 185 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 88; kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kupooza umeme vya Singida na Dodoma katika mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Iringa – Singida – Shinyanga (Backbone Transmission Investment Project - BTIP II); kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kV 400 Singida – Arusha – Namanga ambapo utekelezaji umefikia

asilimia 96.1; kuendelea na ujenzi wa njia ya usafirishaji wa umeme wa Kv 400 kutoka Rufiji – Chalinze – Kinyerezi – Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 37; kuendelea na ujenzi wa mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 (Rusumo – Nyakanazi) ambapo ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme umefikia asilimia 61 na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi umefikia asilimia 95; na kuunganishwa umeme kwa jumla ya vijiji 8,688 kati ya vijiji 12,345 sawa na asilimia 70.4 ya vijiji vyote Tanzania Bara.

**(v) Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege:** kusainiwa kwa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato awamu ya kwanza itakayohusisha ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege pamoja na jengo la abiria; kukamilika kwa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita; kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongoza ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; kukamilika kwa usanifu na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Songea (asilimia 96), Mtwara (asilimia 89), Iringa (asilimia 44.65), Songwe (asilimia 95) na Musoma (asilimia 10); kuendelea na maandalizi ya ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vitakavyogharimu Euro milioni 50 sawa na shilingi bilioni 136.85.

**(vi) Uendelezaji wa Bandari: Bandari ya Dar es Salaam:** Kuboreshwa kwa gati namba 1 – 7; na kukamilika kwa ujenzi wa gati maalumu la kuhudumia meli za magari (RoRo) na yadi ya kuhudumia makasha. **Bandari ya Mtwara:** kukamilika kwa ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300; na kuendelea na ujenzi wa uzio na sakafu ngumu katika eneo la mita za mraba 75,807. **Bandari ya Tanga:** kukamilika kwa uongezaji wa kina kwenye lango la kuingia meli kutoka mita nne (4) hadi mita 13 pamoja na kuweka vifaa vya kuongoza meli.

**Bandari za Maziwa Makuu: Ziwa Victoria:** Kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Nyamirembe, Magarine, Lushamba,

Ntama na Mwigobero pamoja na gati mbili (2) za majahazi katika bandari ya Mwigobero. **Ziwa Tanganyika:** kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Kagunga, Sibwesa na Kabwe (Nkasi); kukamilika kwa ujenzi wa bandari ya Lagosa pamoja na upanuzi wa bandari ya Kasanga; na kuendelea na ujenzi wa Bandari za Karema, Kibirizi, Kigoma na Ujiji. **Ziwa Nyasa:** kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari ya Kiwira na Itungi; na kukamilika kwa ujenzi wa gati na miundombinu yake katika bandari ya Ndumbi.

**(vii) Kuboresha Huduma za Usafiri na Usafirishaji wa Abiria na Mizigo katika Maziwa Makuu**

Kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili (2) za *New Butiama Hapa Kazi Tu* na *New Victoria Hapa Kazi Tu*; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ambao umefikia asilimia 66; na kukamilika kwa ujenzi wa chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza chenye uwezo wa kubeba meli au chombo chenye uzito kuanzia tani moja (1) hadi tani 4,000.

**(viii) Barabara na Madaraja Makubwa:** Kujengwa kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilomita 216.26; na kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe jumla ya kilomita 1,124.3 za barabara za mikoa. Kwa upande wa barabara zinazosimamiwa na TARURA, jumla ya kilometa 232.94 za lami, kilomita 8,181.65 za changarawe, madaraja 405 na makalvati 206 yamejengwa. Miradi iliyokamilika ni pamoja na: ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami sehemu za Tabora – Nyahua (km 85), Nyahua – Chaya (km 85.4) na Manyoni - Itigi - Chaya (km 89.35); barabara za Mbeya – Lwanjilo (km 36) na Lwanjilo – Chunya (km 36), sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 39); na barabara za Mtwara – Mnivata (km 50). Barabara zinazoendelea ni pamoja na ujenzi sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 83.79, Kidatu – Ifakara (km 68) asilimia 54.5, Makutano – Sanzate (km 50) asilimia 94.1, Mto wa Mbu – Loliondo sehemu ya Waso – Sale Jct (km 50) asilimia 98, na Moronga – Makete (km 53.5)

umefikia asilimia 86. Aidha, Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya mzunguko katika jiji la Dodoma (Dodoma outer ring road) yenye urefu wa kilometa (112.3) na kuendelea na maandalizi ya upanuzi wa barabara kutoka Dodoma kwenda Singida (km 50), Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Arusha (km 50) na Dodoma – Morogoro (km 70). Kwa upande wa madaraja hatua zilizofikiwa ni: kuzinduliwa na kuanza kutumika kwa daraja la Tanzanite Dar es Salaam; kuanza kutumika kwa daraja la Kiyegeya (Morogoro); na kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Kitengule (Kagera) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90; Wami (Pwani) asilimia 72.88; Msingi (Singida) asilimia 82; Lower Malagarasi asilimia 65; na ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi umefikia asilimia 40.2.

**(ix) Huduma za Afya:** Kuendelea na ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 127, ujenzi wa vituo vya afya 70, ukamilishaji wa maboma ya zahanati 564; kukamilika kwa ukarabati wa wodi namba 18 katika jengo la Sewa Haji katika hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya wodi za kulaza wagonjwa binafsi; kukamilika kwa ujenzi na ufungaji wa mtambo wa kuzalisha tiba hewa (Oxygen generating plant) katika hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila; kukamilika kwa ujenzi wa maabara maalumu na ufungaji wa mtambo wa kisasa (Angio-Suite) katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili - MOI; kukamilika kwa wodi ya watoto katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete; ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi (asilimia 70), chumba cha kufunga mashine ya MRI (asilimia 80) na kujengwa kwa kituo cha habari kwa magonjwa ya saratani (Patient Information Centre) katika Taasisi ya Saratani Ocean Road; ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi katika hospitali ya rufaa ya magonjwa ya kifua kikuu Kibong’oto; ukarabati wa chumba cha *X-ray na Utra-sound* katika hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe; kujengwa kwa majengo ya kutolea huduma za afya ya Mama na Mtoto (Maternal and Newborn Wing) katika hospitali ya Rufaa Kanda ya Mashariki CCBRT; kuendelea na ujenzi wa wodi za wagonjwa wa saratani (asilimia 57) na kliniki ya wagonjwa wa macho (asilimia 65) katika hospitali ya rufaa kanda ya ziwa Bugando; kuendelea na ujenzi wa vyumba nane (8) vya



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

upasuaji (asilimia 80) katika hospitali ya kanda ya kaskazini (KCMC); kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) la afya ya uzazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 93 katika hospitali ya rufaa Mbeya; kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa UVIKO - 19 (asilimia 95) katika hospitali ya rufaa Shinyanga; kununuliwa na kusambazwa kwa chanjo za polio, surua, rubella, kifaduro, pepopunda, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo na kichomi na chanjo dhidi ya UVIKO – 19.

**(x) Elimu:** Kuendelea kutekeleza Sera ya elimumsingi bila ada ili kuongeza fursa za elimu nchini ambapo hadi Aprili 2022, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 244.5; kuchapishwa na kusambazwa kwa vitabu vya kiada 15,609,515 na kiongozi cha mwalimu 538,006 kwa masomo yote ya Darasa la VI na VII ili kuimarisha uwiano kati ya mwanafunzi na kitabu; kuendelea na ujenzi wa shule mpya 232 za Sekondari za kata katika kata zisizokuwa na shule za Sekondari; ujenzi wa shule 10 kati ya lengo la shule 26 maalumu za bweni za wasichana kwa masomo ya Sayansi; kutolewa kwa mafunzo kazini kwa walimu 10,000 wa sekondari wa masomo ya hisabati na sayansi; kuwezesha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kuchapisha na kusambaza miongozo ya masomo tisa (9); kukusanywa kwa mikopo ya shilingi bilioni 156.81 kutoka kwa wanufaika wa mikopo iliyoiva na kugharamia mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 569.0 kwa wanafunzi 177,777; na kuimarishwa kwa Tume ya Nguvu za Atomiki kwa kuendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa maabara changamano.

**(xi) Maji Mijini na Vijijini:** Upatikanaji wa huduma ya maji hadi Aprili 2022 umefikia wastani wa asilimia 74.5 vijijini kutoka asilimia 72.3 Juni, 2021 na mijini asilimia 86.5 kutoka asilimia 86 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na hatua zilizofikiwa ni: kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Kigoma (asilimia 95), Arusha (asilimia 80) na mradi wa Mugango – Kiabakari – Butiama (asilimia 42). Aidha, katika eneo linalohudumiwa na DAWASA (mikoja ya Dar es Salaam na Pwani) utekelezaji wa miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 95. Vile vile, Serikali imeanza hatua za kutafuta suluhu ya kudumu ya tatizo la maji katika

majiji ya Dodoma na Dar es Salaam kwa kutekeleza miradi ya Bwawa la Kidunda, bwawa la Farkwa na mradi mkubwa wa maji kutoka ziwa Victoria hadi Dodoma.

**(xii) Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

**Kilimo:** Kuzalishwa kwa mbegu bora tani 35,199.39 na miche 32,301,995 ya mazao mbalimbali; kutolewa kwa pikipiki 7,000 kwa Maafisa ugani kwa ajili ya kuimarisha huduma za ugani; kupatikana kwa mbolea tani 436,452; kuanzishwa kwa mashamba 67 yenye ukubwa wa hekta 205,432.45 ambayo kila moja lina ukubwa wa kuanzia hekta 20; kuhakikiwa na kutambuliwa kwa mashamba matano (5) ya NAFCO yenye ukubwa wa ekari 18,980; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu tatu (3) za umwagiliaji za Mkombozi (Iringa), Idudumo (Nzega) na Ilemba (Sumbawanga); kutolewa kwa mafunzo kwa maafisa ugani 2,486 kuhusu kilimo bora cha alizeti na pamba katika mikoa ya Dodoma, Singida, Simiyu, Kilimanjaro, Kigoma na Manyara; kukamilika kwa ukarabati wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 za mazao katika Wilaya ya Kiteto; kukamilika kwa ukarabati wa vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 38,000 katika Mkoa wa Arusha na ghala la Mbugani - Dodoma lenye uwezo wa kuhifadhi tani 30,000 za nafaka; kutolewa kwa vibali 681 kwa wafanyabiashara wa viuatilifu; kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha FOMI Mkoani Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka; NFRA na CPB zilifanikiwa kununua mahindi ya wakulima ambapo kiasi cha shilingi bilioni 114 zilitumika; na kufanyika kwa majaribio 88 ya kisayansi (*bioefficacy field trials*) kwa viuatilifu vipya.

**Mifugo:** Kuendelea na tafiti na tathmini za teknolojia bora za ng'ombe chotara wa maziwa na uzalishaji wa nyama; kukamilika kwa ujenzi wa majosho 95 katika mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa; kuanza kwa ujenzi wa majosho 73 katika halmashauri 58; kuzalishwa na kusambazwa kwa dozi 43,409,600 za chanjo dhidi ya magonjwa ya Mdondo, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe na Mbuzi, Kimeta, Chambavu, Mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu na Kutupa Mimba; kuzalishwa kwa jumla ya dozi 50,261 za mbegu za mifugo na kusambazwa kwa dozi 31,380

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

katika mikoa 19 kwa ajili ya uhimilishaji; kununuliwa na kusambazwa kwa jumla ya pikipiki 300 ili kurahisisha utoaji wa huduma za ugani kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mifugo katika minada 18 nchini; kulimwa kwa hekta 800 za malisho ya mifugo katika ranchi za Kongwa, Ruvu na West Kilimanjaro; na kuzalishwa kwa jumla ya ndama 3,119 katika Ranchi za Kikulula, Misenyi, Kongwa, Ruvu, Mkata, West Kilimanjaro, Mzeri na Kalambo.

**Uvuvi:** kusainiwa kwa Mkataba na Mkandarasi *China Harbour Engineering Co. Ltd* kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko, Lindi; kuendelea na maandalizi ya ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi kati ya nne (4) zilizopangwa; kukamilika kwa mpango biashara wa ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO); kujenga ofisi tano (5) katika Halmashauri tano (5) kwa ajili ya kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi; kufanyika kwa kaguzi 1,863 za kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi kwenye viwanda vya kuchakata samaki, mialo, magari ya kusafirisha samaki, maghala ya kuhifadhi samaki na masoko ya samaki; kujenga na kuimarisha miundombinu ya mialo na masoko ikiwemo kukamilika kwa ujenzi wa baadhi ya mialo na kuendelea na ujenzi wa mialo pamoja na ujenzi wa soko la samaki la Mbamba Bay; kuvuliwa kwa tani 324,752.45 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.18; kuuzwa nje kwa tani 34,841.72 za samaki na Samaki hai 169,089 wa mapambo wenye thamani ya shilingi bilioni 475.01; kujengwa kwa maabara ya utafiti wa uvuvi katika kituo cha TAFIRI - Dar es Salaam; na kufanyika kwa tafiti mbalimbali za mazao ya samaki ikiwemo tafiti kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la tindikali baharini.

**(xiii) Uendelezaji wa Viwanda:** Katika kutekeleza mkakati wa kuendeleza sekta ya viwanda kwa kuweka mazingira wezeshi, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kuendelea na majadiliano na wawekezaji watakaowekeza kwenye miradi ya msingi mitatu (3) katika eneo maalumu la uwekezaji Bagamoyo ambayo ni Bandari ya kisasa (*Modern Seaport Component*), sehemu ya kanda maalumu kwa ajili ya mizigo

na usafirishaji (*Logistics Park*) na sehemu ya mji wa viwanda (*Port side Industrial City*); kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa manne (4) ya kuvuna na kuhifadhi maji yenye uwezo wa kuhifadhi maji ya mita za ujazo 1,750,000 na kuendelea na upanuzi wa mashamba ya miwa katika kiwanda cha Sukari Mbigiri ambapo utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 75 kwa upande wa mashamba ya miwa na asilimia 45 kwa upande wa ujenzi wa kiwanda; kuendelea kuimarisha Sekta Ndogo za ngozi, nguo na mavazi, chuma na bidhaa za chuma, mbolea na kemikali za viwandani na uchakataji wa bidhaa zinazotokana na kilimo kama vile mafuta ya kula, korosho, matunda, maziwa na bidhaa za maziwa. Aidha, kupitia maonesho ya Dubai Expro Serikali ilifanikiwa kusaini mikataba 36 ya uwekezaji yenye thamani ya shilingi trilioni 17 pamoja na mikataba yenye thamani ya shilingi trilioni 11.7 ilisainiwa wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais ya uzinduzi wa filamu ya *Royal Tour*.

**(xiv) Madini:** kukamilika kwa ujenzi wa vituo vitatu (3) vya umahiri katika shughuli za uchimbaji madini vya Chunya, Songea na Mpanda; kuanzishwa kwa masoko mapya manne (4) ya madini na vituo vipya nane (8) vya ununuzi wa madini, hivyo kufanya jumla ya masoko ya madini kuwa 42 na vituo vya ununuzi wa madini kufikia 75; na kusainiwa kwa mikataba ya ubia kwa ajili ya uwekezaji wa kiasi cha takribani dola za Marekani milioni 1,672.57 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kampuni za Madini za: Nyanzaga (NMCL) kwa ajili ya uchimbaji mkubwa wa madini ya dhahabu na madini ambata ya shaba, chuma, nickel, zinc na lead kwenye eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 23.36 Sengerema; Kampuni ya Jacana Resources Limited (Strandline Resources Limited) kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya *Heavy Mineral Sand* (Beach Sands) Kigamboni kwenye eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 4.45; Kampuni ya Mahenge Resources Limited (Black Rock Mining Ltd) kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya graphite; na Kampuni ya Petra Diamond Ltd inayoendelea na uchimbaji wa madini ya Almasi katika mgodi wa Williamson Diamonds Limited eneo la Mwadui. Katika mikataba hiyo Serikali itamiliki asilimia 16 ya hisa za kila kampuni.

**(xv) Habari, Mawasiliano na TEHAMA:** kukamilika kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kilomita 409 ambapo kilomita 72 zimeunganisha nchi ya Msumbiji kupitia mpaka wa Mtambaswala, kilomita 72 zimeunganisha watumiaji wa mwisho katika ofisi za Serikali za Msalato, Mtumba na Kikombo Dodoma na kilomita 265 zimeunganisha Manyoni – Kambi katoto (Chunya); kukamilika kwa ukarabati wa kilomita 105 za ujenzi wa mkongo Arusha – Namanga kupitia miundombinu ya TANESCO; kukamilika kwa uandaaji wa ramani za mipaka ya kiutawala katika Halmashauri 20; na kuendelea na uwekaji wa miundombinu ya anwani za makazi nchini.

Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kuongeza upanuzi na usikivu wa shirika la utangazaji TBC ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kituo cha kurushia matangazo ya masafa ya FM katika kituo cha Kisaki mkoani Morogoro; kukamilika kwa ujenzi na ufungaji wa mitambo ya kituo cha Redio ya Jamii Makao Makuu Jijini Dodoma; kuendelea na ujenzi na ufungaji wa mitambo ya masafa ya FM katika mikoa mipya ya Njombe, Songwe na Simiyu, sambamba na wilaya za Kilwa, Serengeti pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40; kununuliwa na kufungwa kwa mitambo miwili (2) ya kurushia matangazo kwa njia ya Satelaiti (FLY AWAY) pamoja na mtambo wa kurusha mubashara matangazo ya redio kwa njia ya mtandao (LIVE U); na kukamilisha ujenzi wa jengo la Studio na ununuzi wa vifaa vya Chaneli ya Televisheni ya TBC 2 katika ofisi za Mikocheni Dar es Salaam.

**(xvi) Maliasili na Utalii:** Kuanzishwa kwa mara ya kwanza kwa *Programu ya Royal Tour* iliyoasisiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambayo imelitangaza Taifa na utalii katika Nyanja za kimataifa; kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka nje ya nchi kutoka watalii 620,867 mwaka 2020 hadi watalii 922,692 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 48.6; Hifadhi ya Taifa Serengeti ilitangazwa na shirika la *Mainland Aggregates Limited* la nchini Marekani mwaka 2021 kuwa mshindi wa pili

barani Afrika na wa 12 duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya watumiaji wa mtandao wa kijamii wa instagram; kampuni 11 za uwekezaji zilipatiwa maeneo ya kujenga huduma ya malazi ya hoteli za hadhi ya kitalii katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Mikumi, Serengeti na Arusha; na Tanzania kuwa mwenyeji katika Onesho la Kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Regional Tourism Expo - EARTE 2021*);

**(xvii) Kukuza Biashara na Uwekezaji:** wateja 13,836 walipatiwa huduma katika kituo cha Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja (OSC) ambapo jumla ya miradi 206 (73 wageni, 69 Watanzania 64 ubia kati ya wageni na Watanzania) ilisajiliwa yenye thamani ya dola za Marekani milioni 769.5 na inatarajiwa kutoa ajira kwa watanzania wapatao 37,451; kushiriki katika mikutano tisa (9) ya ndani ikiwemo Maonesho ya Utalii ya Kanda ya Afrika Mashariki (EA Regional Tourism Expo), Dubai Expo 2020, Jukwaa la Viwanda lililofanyika Zanzibar na maonyesho ya viwanda vidogo (SIDO Trade Fair) yaliyofanyika Kigoma; na kutolewa kwa mikopo kwa kampuni 31 zinazozalisha na kuchakata bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo na kilimo kupitia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kutumia Mpango wa SANVN (SIDO, AZANIA Bank, NEEC, VETA na NSSF).

**(xviii) Utawala Bora na Utawala wa Sheria:** katika kuhakikisha kuwa utawala bora na utawala wa sheria unashamiri nchini, Serikali imeendelea kuimarisha Mifumo na Miundombinu ya Kitaasisi na utoaji haki, uwazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma, shughuli za Mfuko wa Bunge pamoja na Mfuko wa Mahakama. Mafanikio yaliyopatikana ni: kulijengea Bunge uwezo kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi katika maeneo ya usimamizi wa bajeti, masuala ya kodi, utungaji wa sheria, kuendesha shughuli za Bunge kupitia Bunge mtandao, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo, pamoja na ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika bajeti; na kununuliwa na kufungwa kwa vifaa vya kuhifadhi taarifa ili kuimarisha Mamlaka ya Serikali Mtandao. Aidha, kwa upande wa mahakama Serikali imekamilisha ujenzi wa vituo vitano (5)

Jumuishi vya utoaji Haki katika Mikoa ya Dar es Salaam (Temeke na Kinondoni), Dodoma, Arusha na Morogoro; kuendelea na ujenzi wa makao Makuu ya Mahakama Dodoma, Mahakama za Mwanzo sita (6), Mahakama za Hakimu Mkazi tatu (3) na Mahakama za wilaya sita (6); kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya 26, Mahakama za Mwanzo sita (6) na kituo kimoja (1) jumuishi cha utoaji haki katika Mkoa wa Mwanza. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa haki za watoto, wasichana, wanawake na wanaume; mapambano dhidi ya rushwa; na kuendelea na ujenzi wa majengo 24 ya Wizara katika mji wa Serikali Dodoma ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi kutokea makao makuu ya nchi Dodoma.

## **UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19**

**34. Mheshimiwa Spika**, kama tunavyofahamu katika kipindi cha mwaka 2019, dunia ilikumbwa na mlipuko wa janga la UVIKO – 19 ambapo kwa kiasi kikubwa uliathiri afya za jamii na uchumi wa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania. Katika kukabiliana na athari za mlipuko huo, Serikali iliandaa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 (Tanzania COVID-19 Socio-economic Response and Recovery Plan – TCRP). Mpango huo ulizinduliwa rasmi tarehe 10 Oktoba, 2021 na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mpango huo unatekelezwa kwa kugharamiwa na mkopo nafuu usio na riba wenye thamani ya dola za Marekani milioni 567.25 sawa na shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Kati ya fedha hizo, dola za Marekani milioni 467.3 sawa na shilingi bilioni 1,079.6 zilielekezwa Tanzania Bara na dola za Marekani milioni 100 sawa na shilingi bilioni 231.0 zilielekezwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**35. Mheshimiwa Spika**, kupitia fedha hizo Serikali imeweza kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi hususan katika sekta ya elimu ambayo ilipokea shilingi bilioni 368.9, afya shilingi bilioni 466.9, utalii shilingi bilioni 90.2, maji shilingi

bilioni 139.4 na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) shilingi bilioni 5.5.

**36. Mheshimiwa Spika**, katika sekta ya elimu, Serikali imeweza kupunguza msongamano wa wanafunzi kwa kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 12,000 katika shule za sekondari, madarasa 3,000 ya vituo shikizi katika shule za msingi na mabweni 50 ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu pamoja na ununuzi wa madawati, viti na meza. Aidha, ujenzi wa Vyu vya Ufundi Stadi - VETA unaendelea katika wilaya 25 ikijumuisha upatikanaji wa vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika vyuo 11.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika sekta ya afya, hatua iliyofikiwa ni kuanza kwa ujenzi na ukarabati wa majengo 26 ya wagonjwa mahututi (ICU), majengo 80 ya huduma za dharura - EMD na nyumba 150 (3 in 1) za watumishi katika ngazi ya msingi chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na ujenzi wa wodi 38 za wagonjwa mahututi - ICU; wodi 20 za huduma za dharura - EMD; nyumba 26 za watumishi, uboreshaji wa hospitali za rufaa za mikoa saba (7), hospitali maalumu ya Mirembe; kituo cha magonjwa ya kuambukiza Kisopwa - Dar es Salaam na kituo cha mfano cha utoaji elimu ya afya kwa umma Njedengwa – Dodoma ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, maandalizi ya ununuzi wa vifaa tiba vya UVIKO - 19 yamekamilika ikiwemo ununuzi wa mashine 130 za Kidigitali za *X – Ray*, *CT – Scan* 31, MRI nne (4) na *Portable Echo Cardiography* saba kwa ajili za Hospitali ya Taifa Muhimbili, Ocean Road, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, hospitali za kanda, Hospitali za Rufaa za Mikoa pamoja na hospitali ya Emilio Mzena Memorial na Lugalo.

**38. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa sekta ya Maji, Serikali imekamilisha taratibu za ununuzi wa seti 25 za mitambo ya kuchimba visima katika mikoa yote nchini, seti tano (5) za mitambo ya ujenzi wa mabwawa na seti nne (4) za vifaa vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi. Aidha, utekelezaji wa miradi 218 ya kuboresha huduma za maji unaendelea katika maeneo ya mijini na vijijini yenye thamani ya shilingi bilioni



139.4, ambapo miradi 46 ni kwa maeneo ya mijini na miradi 172 kwa maeneo ya vijijini.

**39. Mheshimiwa Spika**, sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta zilizopata athari za moja kwa moja kutokana na UVIKO-19. Katika kuimarisha sekta hiyo, Serikali inaendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo malango, barabara, njia ya watembea kwa miguu, *Trails, campsite* na bandas katika hifadhi zilizo chini ya TANAPA ikiwemo Nyerere National Park, Saadani National Park, Kilimanjaro (trails) pamoja na majengo ya kale na nyumba za kihistoria. Vilevile, Serikali imetoa mafunzo kwa waongoza watalii 1,060 katika Hifadhi za Taifa Tarangire, Saadani, Serengeti, Ngorongoro na Manyara ili kuimarisha udhibiti wa ubora wa huduma za utalii katika kukabiliana na janga la UVIKO - 19.

**40. Mheshimiwa Spika**, kupitia Mpango wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi zitokanazo na UVIKO – 19, Serikali imewezesha kaya maskini 51,290 katika Halmashauri 35 kupitia Mfuko wa TASAF ambapo shilingi bilioni 5.5 zimetumika. Aidha, Serikali imewawezesha wajasiriamali vijana, wanawake, na wenye ulemavu jumla ya shilingi bilioni 5 kupitia Mpango wa biashara wa kuboresha miundombinu na mazingira ya wafanyabiashara wadogo katika Halmashauri za Jiji la Dodoma, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya na Dar es Salaam pamoja na Halmashauri za Manispaa za Kinondoni, Temeke, Ubungo na Morogoro. Vilevile, Serikali imeendelea na hatua za upatikanaji wa mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa vyuo vinne (4) vyenye mazingira hatarishi vya watu wenye ulemavu katika mikoa minne (4) ya Tanzania Bara kwa gharama ya shilingi bilioni 3.5.

## **MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2022/23**

**41. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) wenye dhima ya ***Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***. Mpango umeandaliwa kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango

wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23; na Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda na kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050, Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

### **Malengo na Shabaha za Uchumi Jumla kwa Mwaka 2022/23**

**42. Mheshimiwa Spika**, Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi katika kipindi cha mwaka 2022/23, ni kama ifuatavyo:

(i) Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 4.7 mwaka 2022 na asilimia 5.3 mwaka 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 hadi 7.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 11.7 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23; na

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**43. Mheshimiwa Spika**, Misingi itakayozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za maendeleo;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili kama vile ukame, vita na magonjwa ya mlipuko;

(iii) Kuendelea kuwa na utoshelevu wa chakula nchini; na

(iv) Uwepo wa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na katika nchi jirani.

### **Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2022/23**

**44. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea kukamilisha miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati inayoendelea. Miradi hiyo inatarajiwa kuwa na matokeo mapana na ya haraka katika uchumi, ikiwemo kuzalisha ajira, kipato na kuchangia zaidi kupunguza hali ya umaskini nchini. Miradi hiyo inajumuisha: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR); Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) – Njombe; Daraja la JPM - Kigongo – Busisi (Mwanza); Ujenzi wa barabara na Madaraja Makubwa; kuendeleza Kanda Maalumu za Kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo; na programu ya kuendeleza ujuzi adimu.

**45. Mheshimiwa Spika**, miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2022/23 itakaendelea kuzingatia maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 – 2025/26 kama ifuatavyo:

**(a) Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi:** Msisitizo utawekwa katika kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji ikijumuisha kuimarisha utulivu wa uchumi jumla. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: uendelezaji wa miundombinu na huduma; ukarabati wa njia kuu za reli ikiwemo kukamilisha ukarabati wa njia ya reli kwa maeneo yaliyobaki kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Isaka (km 970); ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi na zile za kuunganisha Tanzania na nchi jirani ikiwemo Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499), Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni (Mkiwa) (km 528), Barabara ya Itoni – Ludewa -

Manda (km 211); barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460); barabara ya Mafinga – Mtwango – Nyololo – Mgololo; Kibaha - Mlandizi – Chalinze - Morogoro *Express Way* (km 158); barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) na mchepuo wa Mbeya (Uyole – Songwe (km 48.9); barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389); kukamilisha madaraja makubwa ya *New Wami* (Pwani), *Kitengule* (Kagera), *Lower Malagarasi*, *Mkundi* (Morogoro), *Godegode* (Dodoma) na *Mtera* (Iringa); ujenzi wa meli katika ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa; kuendelea kuboresha bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Bandari Kavu ya Ruvu; ujenzi wa viwanja vya ndege vya Msalato, Shinyanga, Tabora, Kigoma na Lindi; kujenga njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 ya Rufiji - Chalinze - Dodoma; kujenga njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 ya Singida - Arusha – Namanga; kujenga njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 ya Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi (North West Grid Extension); kusambaza umeme vijijini kupitia REA; uimarishaji wa Gridi ya Taifa ikijumuisha ujenzi wa vituo vipya 57 vya kupoza umeme; ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa; kuimarisha huduma za bima hususan bima za mazao na huduma za fedha ili kuimarisha shughuli za uwekezaji nchini; na kuimarisha mapinduzi ya kidigitali kwa kukuza teknolojia ya habari na mawasiliano.

**(b) Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Huduma:**

miradi itajielekeza katika kuendelea kukuza sekta ya kilimo kwa kutekeleza miradi ya kimkakati ya umwagiliaji, mbegu na maghala kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo kufikia wastani wa asilimia 10 na mchango wa shughuli za umwagiliaji kwenye kilimo kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2030. Aidha, Serikali inalenga kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta 8,500,000 pamoja na kuongeza mauzo ya bidhaa za kilimo nje kutoka dola za Marekani bilioni 1.2 hadi dola za Marekani bilioni 5 ifikapo mwaka 2030. Baadhi ya mikakati mahsusi itakayotekelezwa ni pamoja na kujenga skimu za umwagiliaji, kuanzisha Mfuko wa

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kutengamaza Bei za Mazao (*Price Stabilisation Fund*) na mifuko ya kuendeleza mazao, kujenga maghala ya kuhifadhi mazao kwenye vijiji ili kukabiliana na changamoto ya upotevu wa mazao baada ya mavuno na kuanzisha *Youth Agricultural Parks*; kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji, kuimarisha huduma za ugani; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo; kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji katika sekta ya kilimo; kuimarisha afya ya mifugo; kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo za TARI na ASA; kuimarisha miundombinu ya masoko ya mifugo na mazao yake; kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania – TAFICO na kuliwezesha kujendesha kibiashara; ujenzi wa bandari ya uvuvi – Kilwa Masoko; kununua boti 250 za kisasa aina ya *fibre* kwa ajili ya vyama vya ushirika vya wavuvi; na kujenga na kukarabati vituo vya ukuzaji viumbe maji.

Kwa upande wa viwanda, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: kuendelea kuboresha Kituo cha Kuendeleza Teknolojia ya Magari Tanzania – TATC; kuendelea kufufua Kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC; kuimarisha Kiwanda cha Viuadudu; Uendelezaji wa Viwanda Vidogo – SIDO; kuendelea Eneo la Kongano ya Viwanda – TAMCO; Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ/EPZ) ya Dodoma, Manyara na Bunda; na kuendelea kuweka sera na mazingira wezeshi kwa uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda.

Kwa upande wa eneo la madini na huduma, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: kuendelea kufungua masoko na vituo vya madini; kuendelea wawekezaji wadogo wa sekta ya madini; kuendelea utalii kanda ya kusini na kuimarisha utalii hususan kwa kuanzisha mazao mapya ya utalii wa fukwe, mikutano pamoja na kuimarisha utalii wa ndani; na kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya wanyamapori kwa lengo la kulinda urithi na maliasili za Taifa.

**(c) Kukuza Biashara na Uwekezaji:** Kipaumbele kitakuwa katika kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara ikiwemo kuimarisha mazingira ya kisera na kisheria kuhusu uwekezaji pamoja na mifumo ya uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji kitaifa; kuondoa

utozaji kodi mara mbili; na kulinda biashara na uwekezaji wa sekta binafsi. Aidha, shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na: kutekeleza Programu za Kuboresha Mifumo ya Udhhibiti wa Biashara; Kukuza Ushiriki wa Watanzania kwenye Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji; Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Kukuza Sekta Binafsi; Uendelezaji wa Masoko ya Bidhaa; Udhhibiti wa Ubora wa Bidhaa; na kuimarisha masoko, maonesho na makongamano ya uwekezaji wa kikanda na kimataifa.

**(d) Kuchochea Maendeleo ya Watu:** Miradi itakayotekelezwa inalenga kuboresha maisha ya watu: Kwa upande wa sekta ya elimu shughuli zitakazo tekelezwa ni pamoja na: kuendelea kugharamia elimumsingi bila ada; kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; kuimarisha vyuo vya elimu ya juu, vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vya ualimu; kuboresha Elimu ya Sekondari; uboreshaji wa maktaba; kukamilisha maboma ya vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi; kuboresha mitaala ili iendane na mahitaji ya soko; kujenga shule mpya katika maeneo yenye mahitaji; na kugharamia uboreshaji wa lische shuleni.

Kwa upande wa eneo la afya, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: kuimarisha huduma za afya hususan ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda na za Mikoa, zahanati, vituo vya afya na hospitali za Halmashauri za Wilaya; kuimarisha upatikanaji wa chanjo, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa kuongeza bajeti, kutoa fedha na kuimarisha udhibiti; kuimarisha huduma za ustawi na maendeleo ya jamii, hususan haki za wazee, watoto na makundi maalumu; na kuendelea na hatua za utelezaji wa ahadi ya utoaji wa bima za afya kwa wote;

Kwa upande wa eneo la maji safi na usafi wa mazingira miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: kuimarisha huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini; ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa, wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa; ujenzi wa bwawa la Farkwa kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji katika jiji la Dodoma; bwawa la

Kidunda kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa maji jijini Dar es Salaam; na kutekeleza mradi wa kimkakati wa kutoa maji kutoka ziwa Victoria hadi jijini Dodoma.

Kwa upande wa eneo la ardhi, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: kuendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchi nzima; kuimarisha mipaka ya kimataifa; kuimarisha miundombinu ya upimaji na ramani; na kuendeleza upangaji wa matumizi ya ardhi nchini ili kuondoa migogoro katika matumizi ya ardhi.

**(e) Kuendeleza Rasilimali Watu:** Kuendelea na utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya kukuza ujuzi nchini ili kuongeza ajira kwa vijana kwa kutoa mafunzo ya ufundi na stadi za kazi kupitia programu mbalimbali zikiwemo: kuimarisha programu ya taifa ya kukuza ujuzi nchini; kuboresha mfuko wa maendeleo ya vijana; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu; na kutekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha.

**46. Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2022/23 yanapatikana katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Nne.

### **Vihatarishi vya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2022/23**

**47. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango unaweza kuathiriwa na vihatarishi vya ndani na nje. Vihatarishi vya ndani ni pamoja na: ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo; ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika mipango ya maendeleo; uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; na uhalifu wa kimtandao na rushwa. Vihatarishi vya nje ni pamoja na: majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko; mitikisiko ya kiuchumi duniani; kubadilika kwa teknolojia; na kutopatikana kwa misaada na mikopo kwa wakati.

**48. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango, Serikali itachukua hatua mbalimbali

ikijumuisha: Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa kodi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti za kielektroniki wanapouza bidhaa na wanunuzi kudai risiti wanaponunua bidhaa; kuhamasisha ulipaji kodi katika sekta isiyo rasmi kwa kujumuisha kwenye mfumo rasmi wa ulipaji kodi; kuendelea kuimarisha na kuhamasisha wananchi kuhusu uelewa wa huduma za sekta ya fedha ikiwemo utoaji wa mikopo, uwekezaji, mitaji na bima; kuendelea kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji wa sekta Binafsi wa ndani na nje ili kupunguza gharama za uwekezaji; kusimamia miongozo na kanuni za usimamizi wa mazingira; kuendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa ikijumuisha kuchukua hatua za kisheria kwa wanaobainika kuhusika na vitendo vya rushwa; kuboresha mifumo ya kuzuia na kukabiliana na majanga; na kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji hususan viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa kutumia teknolojia na malighafi za ndani ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

### **Ugharamiaji wa Mpango 2022/23**

**49. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2022/23, inakadiriwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 15,004.8 sawa na asilimia 36.2 ya Bajeti yote ya Serikali zitatumika kugharamia miradi ya maendeleo ikijumuisha miradi ya huduma za jamii. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 12,305.8 sawa na asilimia 82.0 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,699.1 sawa na asilimia 18.0 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje. Katika kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kama injini muhimu ya utekelezaji wa miradi, Serikali itahakikisha miradi yote inayovutia uwekezaji wa sekta binafsi inatekelezwa kwa utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) na Joint Venture kwa kutumia utaratibu wa Kampuni Maalumu (*Special Purpose Vehicle*).

**50. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza ukusanyaji wa mapato ya kugharamia Mpango, Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo: Kuimarisha ukusanyaji



na usimamizi wa kodi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti za kielektroniki wanapouza bidhaa na wanunuzi kuchukua risiti wanaponunua bidhaa; kuendelea kutoa elimu kwa mlipakodi kupitia runinga, redio, mitandao ya kijamii na semina; kupanua wigo wa kodi kwa kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi kupitia kampeni ya Mlango kwa Mlango; kuendelea kutumia Mpango wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (*Compliance Risk Management Plan*) ili kubaini na kutambua wakwepaji wa kodi; kuendelea kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa mipaka yote kwa kuongeza ushirikiano baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na vyombo vya ulinzi na usalama nchini ili kudhibiti bidhaa za magendo na kupunguza tatizo la ukwepaji wa kodi; na kuimarisha mazingira rafiki ya ulipaji kodi kwa hiari kwa kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo itakayosaidia na kurahisisha ulipaji kodi.

**51. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kufuatilia Mizigo inayokwenda nchi jirani (*Electronic Cargo Tracking System*) ili kuimarisha uwezo wa usimamizi wa mizigo inayopita kwenda nchi jirani; kuhamasisha ulipaji kodi katika sekta isiyo rasmi kwa kuijumuisha kwenye mfumo rasmi wa ulipaji kodi; kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wapya, kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi utakaowezesha kuongeza wigo wa kodi pamoja na kuendelea kusimamia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (*Government Electronic Payment Gateway - GePG*) ili kurahisisha ulipaji na kudhibiti upotevu wa mapato.

**52. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuimarisha mashirikiano na Washirika wa Maendeleo kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework - DCF*) ili kuhakikisha kuwa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinaendelea kupatikana kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali nchini. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa Maendeleo imeanza maandalizi ya kufanya

tathmini na mapitio ya Mwongozo wa Ushirikiano itakayoivezesha nchi kujipanga kimkakati ili kunufaika zaidi na fursa zilizopo kwa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali, Sekta binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali katika masuala ya ushirikiano wa kimataifa.

Vile vile, kwa kutambua uwepo wa pengo la rasilimali fedha zinazohitajika katika kufikia shabaha ya maendeleo ya Taifa, Serikali imeainisha vyanzo mbadala na bunifu vitakavyotumika kugharamia miradi ya maendeleo na hivyo kupunguza mzigo kwa bajeti ya Serikali. Vyanzo hivyo ni utekelezaji wa Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano sanjari na Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa mwaka 2020/21- 2029/30. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itafanya maboresho ya sheria mbalimbali pamoja na kuweka miongozo itakayowezesha kunufaika na vyanzo mbadala na bunifu katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

**53. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ugharamiaji wa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa utaratibu wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Serikali imepanga kuwezesha Mamlaka za Serikali zenye miradi ya PPP iliyopo katika hatua mbalimbali za maandalizi ikiwemo Upembuzi Yakinifu na Ununuzi wa wabia kukamilisha miradi hiyo iweze kuanza utekelezaji. Katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Baadhi masuala yatakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea kutafuta wabia wa miradi mitano (5) iliyofikia katika hatua za ununuzi (*procurement stage*) kwa kuitangaza katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Miradi hiyo ni: ujenzi wa viwanda vya dawa muhimu (Kibaha), vifaa tiba vitokanavyo na pamba (Mwanza) na maji tiba (Mbeya); uendeshaji wa huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza; ujenzi wa hoteli ya nyota nne katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; ujenzi wa kituo changamani cha biashara (commercial Complex) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;

na ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza simu za mkononi chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika Mkoa wa Mwanza.

### **Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji**

**54. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa mipango ya maendeleo inatekelezwa kama ilivyokusudiwa, suala la ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji limeendelea kupewa msukumo wa pekee katika shughuli za kila siku za Serikali. Katika kutekeleza hilo, mwaka 2021/22, Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 225 katika sekta za Uchukuzi, Viwanda, Elimu, Afya, Ujenzi, Utawala Bora, Kilimo, Mifugo, Maji na Biashara inayotekelezwa na Serikali pamoja na Sekta Binafsi. Katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea kutumia mbinu na viashiria vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 pamoja na Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo kupima utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na miradi ya maendeleo na kuchukua hatua za kutatua changamoto zitakazobainika katika utekelezaji. Vile vile, Serikali itaendelea kuzingatia miongozo mbalimbali ya ufuatiliaji na tathmini ya Mpango ikiwemo Sheria ya Ununuzi wa Umma, SURA 410, Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348. Pamoja na Sheria hizo, Serikali pia imeanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ili kutatua changamoto za uratibu wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini Serikalini.

**55. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha uwepo wa ushirikishwaji wa kutosha katika masuala ya ufuatiliaji na tathmini, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kushirikiana na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Sekta Binafsi katika kuratibu na kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

**56. Mheshimiwa Spika**, Serikali inazielekeza Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutafsiri malengo na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 katika Mipango na Bajeti za kisekta kwa mwaka 2022/23. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo wa Mwaka 2022 ikiwa ni pamoja na: kuandaa Mpango Kazi wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini, kutenga rasilimali fedha zitakazowezesha shughuli za ufuatiliaji na tathmini; kuimarisha mifumo ya ndani ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo; kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo kwa kuzingatia mipango kazi iliyowekwa; kuendelea kuwajengea uwezo watumishi katika tasnia ya ufuatiliaji na tathmini; na kuwa na mfumo mmoja wa kielektroniki unaoratibu taarifa za utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini katika kutekeleza mipango ya maendeleo.

**57. Mheshimiwa Spika**, Serikali inazielekeza Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuaandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwasilisha taarifa husika Wizara ya Fedha na Mipango.

## **MAJUMUISHO**

**58. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya *“ Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo*

ya Watu". Utekelezaji wa Mpango utaendelea kuimarisha viashiria vya uchumi jumla, kuboresha mazingira ya uwekezaji viwandani ikiwemo kuimarisha majadiliano na wawekezaji wa ndani na nje, kuimarisha mahusiano ya kisiasa, ulinzi na diplomasia ya uchumi na nchi nyingine, kuendelea kutekeleza kwa kasi miradi ya maendeleo, kuendeleza mashirikiano na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuchochea uwekezaji viwandani hususan kwa kutumia rasilimali watu na malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini ikiwemo mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, madini, misitu na gesi asilia.

**59. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea na jitihada za kukabiliana na athari za majanga mbalimbali ya asili na yasiyo ya asili yakiwemo magonjwa, vita na mabadiliko ya tabianchi. Mathalani, tutaendelea kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Athari za UVIKO-19 pamoja na kuweka mipango madhubuti ya kupunguza athari zitokanazo na vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine ikiwemo kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa mbalimbali na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi.

**60. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuboresha upatikanaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi zikiwemo huduma za afya, elimu, umeme na maji safi na salama mijini na vijijini, kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo na ya kimkakati, kuimarisha miundombinu wezeshi ya uwekezaji na biashara kwa ajili ya masoko ya kimataifa hususan ya nchi jirani, kuimarisha sekta za uzalishaji ili kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi, kufungua fursa zaidi za ajira na maendeleo ya watu.

## HITIMISHO

**61. Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu na Tafiti, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Washirika wa Maendeleo na Wananchi wote kwa namna walivyojitoa na kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa

miradi ya maendeleo na kuimarisha uchumi wa Taifa letu. Wadau hao wamekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Kwa msingi huo, ninawaomba na kuwasihii wadau wote waendeleo kushirikiana na Serikali yetu inayoongozwa na Rais shupavu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

**62. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii isingeweza kukamilika bila jitihada kubwa zilizofanywa na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, kwa dhati ya nafsi yangu naomba nitoe shukrani za pekee kwa Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Viongozi wote wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakuu wa Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23. Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba kwa kujitoa usiku na mchana kukamilisha kwa wakati na kwa ubora Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23.

**63. Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwa ujumla kwa kutenga muda wao kunisikiliza. Aidha, napenda kuwataarifu wadau wote kuwa, hotuba hii pamoja na vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ni [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz).

**64. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23.

**65. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge hoja hii huamriwa baadaye si sasa pamoja na kwamba ametoa hoja na imeungwa mkono ndiyo utaratibu wetu, lakini kuwahoji kutakuja baadaye tutakapomaliza utaratibu wetu.

Na kwa kusema hayo, kwa ratiba yetu ya leo akishamaliza hapa Waziri amemaliza tunaendelea kwenda kusoma tukitafakari haya tukitafakari tutakayoyasikia sasa baadaye kwenye hotuba yake atakayoleta, hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taifa na tunaita bajeti.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na pia ratiba ya siku kama ya leo huwa tunaanza saa kumi ndiyo kanuni zetu zinavyosema. Kwa hiyo, watu wasije wakasema mbona amesema saa kumi halafu hatujatengua kanuni hapana, kanuni zetu zinataja saa kumi.

Kwa hiyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni Leo.

*(Saa 5.30 asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10:00 Jioni)*

*(Saa 10:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumuita sasa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba aje awasilishe hoja yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi. Lakini leo kwa sababu ni siku maalum ataletwa na *Sergeant-At-Arms*. Kwa hiyo amlete humu ndani sasa tuko tayari sasa kwa ajili ya kumsikiliza. (*Makofi/Vigelegele*)

*(Hapa Waziri wa Fedha na Mipango - Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba Aliingia Ukumbini akisindikizwa na Sergeant-At-Arms)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, karibu uje uwasilishe hoja yako.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Hii ni Bajeti ya Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu yoyote kwenye hotuba ambayo mtaona imekidhi matarajio hayo ndiyo maono yake Rais wetu na sehemu yoyote mtakayoona maelekezo hayo ndiyo maelekezo yake, na pale yamkini mkiona haijakidhi sana matarajio basi hayo ni mapungufu yetu Wizara ya Fedha katika kutafsiri maono yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Bajeti hii inawasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kifungu cha 124 (4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina bajeti ya Serikali. Kitabu cha kwanza ni Makadirio ya Mapato; kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kitabu cha nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2022 nayo ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 yameandaliwa kwa kuzingatia nyaraka na miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 na 2025/2026 ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030, Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo pamoja na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeyaridhia nayo ni sehemu iliyozingatiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM kwa kuendelea kuniamini katika dhamana hii ya kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa mapato na matumizi kwa mwaka 2021/2022; kwa upande wa mwenendo wa mapato katika bajeti ya mwaka 2021/2022 Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi trilioni 37.99 kutoka katika vyanzo vyote vya ndani na nje ambapo hadi Aprili 2022 kiasi cha shilingi trilioni 29.84 kilikuwa kimekusanywa. Mchanganuo wa mapato yaliyopatikana hadi Aprili, 2022 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) yalikuwa ni shilingi trilioni 17.20, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 21.78;

(ii) Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi trilioni 2.03 ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 3.05;

(iii) Mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 759.0 ambapo lengo la mwaka ni shilingi bilioni 863.9;

(iv) Misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia shilingi trilioni 3.93 ikiwa ni sawa na asilimia 92.0 ya lengo la kukusanya trilioni 4.27;

(v) Mikopo kutoka vyanzo vya ndani ilifikia shilingi trilioni 4.12 ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 4.99; na

(vi) Mikopo yenye masharti ya kibiashara ilifikia shilingi trilioni 1.81 ambapo lengo la mwaka ni kukopa shilingi trilioni 3.05.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 jumla ya shilingi trilioni 29.40 zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 18.79, zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zilijumuisha shilingi trilioni 6.73 kwa ajili ya mishahara; shilingi trilioni 4.79 matumizi mengineyo na shilingi trilioni 7.27 kugharamia deni la Serikali. Jumla ya shilingi trilioni 10.61 sawa na asilimia 74.1 ya lengo la mwaka zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kiasi hiki hakijumuishi baadhi ya fedha zilizopelekwa moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Fedha hizi zinajumuishwa kwenye hesabu za Serikali mwishoni mwa mwaka wa fedha pindi taratibu za kihisibu zitakapokuwa zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa; hadi Aprili, 2022 deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 69.44, sawa na ongezeko la asilimia 14.4 ikilinganishwa na shilingi trilioni 60.72 Aprili, 2021. Kati ya kiasi hizo, deni la ndani ni shilingi trilioni 22.37 sawa na asilimia 32.2 na deni la nje ni shilingi trilioni 47.07 sawa na asilimia 67.8. Kati ya deni la nje, deni lenye masharti ya kibiashara ni shilingi trilioni 14.27, sawa na asilimia 30.3. Hivyo, sehemu kubwa ya deni la nje ni mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali kufikia Novemba, 2021 kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura Namba 134 ilionesha kuwa viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Tathmini hiyo, ilionesha kuwa uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa pato la Taifa ni asilimia 31 ukilinganishwa na ukomo wa asilimia 55, uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa pato la Taifa ni asilimia 18.8 ikilinganishwa na ukomo ambao ni asilimia 40 na uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 142.46 ikilinganishwa na ukomo ambao ni asilimia 180.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya kukopesheka; katika mwaka 2021/2022, zoezi la tathmini na ukadiriaji wa kukopesheka kwa nchi (*credit rating*) ambalo lilisimama awali lilianza tena kupitia benki ya Citibank ambayo ilikuwa mshauri wa Serikali. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 Serikali imefikia hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za ununuzi ambapo imefanikiwa kuchagua kampuni mbili ambazo zinatambulika kimataifa na kupitia mikataba yao. Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na kampuni hizo pamoja na kuandaa takwimu mbalimbali ambazo zitatumika katika zoezi la tathmini na ukadiriaji wa kukopesheka. Serikali inategemea kukamilisha zoezi hili ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023. Naomba nichukue fursa hii kuziomba taasisi za Serikali na

binafsi na mabenki zitakazopata nafasi ya kuhojiwa na wataalamu wa kampuni hizo kutoa ushirikiano kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu. Kukamilika kwa zoezi hili kutatuwezesha kuongeza wigo wa wakopeshaji kwa Serikali na makampuni binafsi hususan katika masoko ya mitaji ya kimataifa (*International Capital Markets*).

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023; bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 ni ya pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 hadi 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Aidha, dhima kuu ya bajeti ya mwaka huu 2022/2023 kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuongeza kasi ya kufufua uchumi na kuimarisha sekta za uzalishaji kwa ajili ya kuboresha maisha.

Katika utekelezaji wa dhima hiyo kwa mwaka 2022/2023 kipaumbele kikubwa katika sekta za uzalishaji kitawekwa ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, uwekezaji na biashara. Lengo la Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania ni kujenga uchumi, kukabiliana na umasikini pamoja na ukosefu wa ajira hasa kwa vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shabaha za uchumi jumla; kutokana na mambo yanayozingatiwa katika uandaaji wa bajeti hii, shabaha za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo: -

(i) Ukuaji wa pato halisi la Taifa kufikia asilimia 4.7 mwaka 2022 na asilimia 5.3 kwa mwaka 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya tatu hadi saba katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya pato la Taifa kwa mwaka 2022/2023;

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 11.7 ya pato la Taifa kwa mwaka 2022/2023; na

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu kwa mwaka wa fedha 2022/2023; nchi zote duniani zinapita kwenye athari kubwa za UVIKO-19 na vita kati ya Urusi na Ukraine iliyoanza Februari, 2022 ambayo imeendelea kuleta athari katika mataifa mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania kutokana na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Madhara ya UVIKO-19 yamekuwa na makali zaidi baada ya uchumi kuanza kurejea, kwa kuwa nchi zilikuwa katika *lockdown* na wengine kupunguza katika uzalishaji. Uchumi ulipoanza kurejea katika hali ya uzalishaji wote walihitaji bidhaa ambazo ziliachwa kuzalishwa hivyo kusababisha upungufu.

Kungali hali iko hivyo, vita kati ya Urusi na Ukraine imeongeza upungufu wa bidhaa hizo hizo kutokana na kuathiri uzalishaji na mnyororo wa usambazaji. Kwa mujibu wa Shirika la Chakula Duniani, nchi za Urusi na Ukraine ni kati ya nchi zenye uzalishaji na uuzaji mkubwa wa mazao mbalimbali ikiwemo ngano, pamoja na mafuta ya kula pamoja na shayiri.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Urusi ni ya pili katika uzalishaji wa gesi asilia na bidhaa za mafuta ya petroli duniani. Kadhalika, nchi ya Ukraine ni miongoni mwa nchi zinazozalisha mafuta ya alizeti kwa wingi duniani. Kufuatia madhara haya ya vita, ni dhahiri kuwa uchumi na maisha duniani havitabaki kama vilivyokuwa. Ndio maana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM ameelekeza bajeti hii ya Serikali ijkite kuchukua hatua za kutoa unafuu kwa wananchi na kufufua uchumi. Bajeti hii itatilia mkazo Sera za Mapato, Sera za Matumizi, kujali ufanisi (*value for money*), mapambano ya vitendo vya rushwa na kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji ili kuweza kutengeneza ajira hasa kwa vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkakati ya kuongeza mapato kwa mwaka 2022/2023; nawapongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania na Taasisi zingine zinazokusanya mapato na maduhuli ya Serikali. Tumepiga hatua kubwa kwenye makusanyo ya ndani. Hadi Aprili, 2022 ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa umefikia shilingi trilioni 19.99, sawa na asilimia 93.3 ya makadirio ya kukusanya shilingi trilioni 21.42 katika kipindi kama hicho. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yamefikia shilingi trilioni 17.20 sawa na asilimia 94.5 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 18.2; mapato yasiyo ya kodi yamefikia shilingi trilioni 2.03 sawa na asilimia 81.2 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 2.5 na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yamefikia shilingi bilioni 759.0 ikiwa ni asilimia 104.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 724.1 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado kuna vitendo vya rushwa kwenye ukusanyaji wa mapato hasa kwenye kodi kubwa, mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Ardhi. Kuna mapato ya Serikali bado yanaingia kwenye mifuko ya watu binafsi. Hii inafanyika hasa panapotokea ukadiriaji wa viwango vya juu ili kuruhusu majadiliano ya kwenda kwenye kodi stahiki yanayotakiwa kupunguza kiasi na kiasi kinachopunguzwa chini ya kile kilichostahili ndicho kinachopunguzwa kinaingia katika mifuko binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshapokea taarifa kadhaa za matukio ya aina hii na inaendelea kulifuatilia kwa umakini sana jambo hili. Wale wanaokataa kutoa rushwa ndio wanaoonewa zaidi na ndio wanaobambikwa makadirio yasio halisi kwa kuwakomoa, ndio wanaotishiwa kufilisiwa. Jambo hili halikubaliki. Nitoe rai jambo hili liachwe mara moja. Tuache utaratibu wa kufanya majadiliano kwenye kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumishi wa umma wanaokusanya kodi na maduhuli ya Serikali wanaowaomba wafanyabiashara wawapunguzie kiasi wanachotakiwa kulipa ili kisichoingia Serikalini wapate wao wanafanya makosa ya uhujumu uchumi. *(Makofi)*

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kadhalika wapo wafanyabiashara na wauza maduka wanawaambia wananchi nikupe bei ya risiti ya *TRA* au nikupe bila risiti? Na bei ile isiyo na risiti inakuwa ndogo kuliko ile yenye risiti, kwa maana hiyo wanakuwa wanawashawishi wakwepe kulipa mapato ya Serikali, wao wenyewe wao wenyewe wabaki na kodi ya Serikali. Huu ni uhujumu uchumi kama mwingine niliosema. Naagiza vitendo hivyo navyo vikome mara moja na ambaye hataacha atakutana na mkono wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Watanzania wote kulipa kodi unayostahili kulipa, wala wasiogope vitisho, wala usidhanie kuwa kama utatoa taarifa watakulipizia kwa kiasi kwa kuwa umetoa taarifa hiyo. Toa taarifa TAKUKURU iliyo karibu nawe kwa siri, ama toa taarifa Idara ya Usalama wa Taifa iliyo karibu nawe. Watumishi wa aina hiyo watakaobainika hautawakuta tena kwenye ofisi za umma, wala hatutawahamisha, tutawafukuza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais anachukizwa sana na vitendo vya ukosefu wa maadili na uaminifu kwa baadhi ya watumishi wa umma na wala asitokee anayedhani ana haki sana ya kuwa kwenye utumishi wa umma, hii ni dhamana tu na wala asitokee anayedhani vijana waliohitimu wa Kitanzania walioko mitaani hawana haki za kuwa kwenye ofisi za watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao hata uwezo wa kupangua safu nzima ya utumishi wa umma na tukapanga safu mpya ya vijana walioko mtaani. Kwenye masuala ya uadilifu na uaminifu wala hata tusibabaishane, tutawakamata, tutawashitaki na tutawafunga. Lazima tukomeshe kabisa vitendo vya rushwa kwenye mapato na matumizi na jambo hili tatalifuatilia, anayetaka kumjaribu mama na ajaribu na hii ndio kauli aliyotoa na mimi naipigia mstari hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mengine tunayotarajia kuyafanya kwenye sera ya mapato ni kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kufanya makadirio ya kodi kwa wafanyabiashara wadogo ambao hawana uwezo wa

kutunza kumbukumbu na kutengeneza hesabu za biashara zao, kuweza kuweka kwenye matumizi ya kiteknolojia ili kurahisisha uwasilishaji wa ritani zao kielektroniki na ulipaji kodi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuimarisha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (*GePG*) na kuhimiza malipo ya Serikali kutumia Namba ya Kumbukumbu ya Malipo; na kuimarisha mifumo ya usimamizi katika Mashirika, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati. Ili kukuza mchango wa sekta binafsi Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuipa nafasi zaidi sekta binafsi.

Aidha, Serikali imepanga kuendeleza uanzishwaji wa vituo vya pamoja vya utoaji huduma ili kuwezesha huduma muhimu zinazohitajika katika kuanzisha biashara ziweze kupatikana sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kubana matumizi; kwa upande wa Sera za Matumizi katika mwaka 2022/2023 sera zitakuwa za kubana na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali inatarajia kudhibiti ununuzi na matumizi ya magari kwa kuzingatia Waraka wa Rais Na.1 wa mwaka 1998 kuhusu hatua za kubana matumizi ya Serikali na Waraka Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina za stahili za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma ili kubana matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo yenye gharama kubwa sana kwa Serikali ni ununuzi wa magari, ununuzi wa mafuta ya uendeshaji, ununuzi wa vipuri na matengenezo. Tunapanga kuchukua hatua za muda mfupi na za muda mrefu. Lazima matumizi ya Serikali na matumizi ya watumishi wa umma yote yaakisi ugumu wa maisha wanayopitia wananchi wetu, kufuatia athari za majanga hususani UVIKO-19 ili fedha zinazopatikana ziweze kufanya mambo muhimu hapa nchini. *(Makofi)*



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, hatua za muda mfupi zitakazochukuliwa ni pamoja na kupunguza safari za ndani na nje, kukata fedha za ununuzi usio wa lazima, kupunguza ukubwa wa uwakilishi kwenye mikutano ya ndani na nje, tutapimiana mafuta ya magari ya Serikali kila mwezi kufuatana na shughuli za lazima. Utaratibu huu unatumika hata kwa Wabunge na hawajawahi kuacha kufanya ziara, ndio utaratibu pia unaotumika kwa Benki Kuu na baadhi ya Taasisi za Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemwelekeza Mlipaji Mkuu wa Serikali afanye uchambuzi wa wastani wa mahitaji ya mafuta kufuatana na aina ya majukumu, ulazima wa majukumu pamoja na ngazi katika utumishi. *(Makofi)*

Kwa upande wa hatua za muda wa kati na wa muda mrefu, napendekeza Serikali kubadili kabisa utaratibu uliopo ili kuwakopesha magari watumishi wenye hadhi ya kuwa na gari la Serikali wawe na magari yao wenyewe wayalipie, wafanye matengenezo wao wenyewe, wanunue vipuri wao wenyewe na masuala ya mafuta yaangaliwe kwa utaratibu utakaonekana unafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia, napendekeza Serikali kubadili kabisa utaratibu uliopo ili kuwakopesha magari watumishi wenye hadhi ya kuwa na gari la Serikali. Wakopeshwe na walipe, wakishalipia magari yale yanakuwa ya kwao, wafanye matengenezo wao wenyewe, wanunue vipuri wao wenyewe na masuala ya mafuta yaangaliwe kwa utaratibu utakaonekana unafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ina magari zaidi ya 15,742, pikipiki zaidi ya 14,047 na mitambo 373 na inatumia zaidi ya shilingi bilioni 558 kwa mwaka kwa ajili ya ununuzi, ununuzi wa mafuta ya uendeshaji, ununuzi wa vipuri pamoja na matengenezo. Ukiondoa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na Mahakama, upande wa Serikali ubaki na viongozi wakuu wachache wa kila Wizara, Mashirika, Wakala, Mikoja, Wilaya pamoja na miradi ambayo inahitaji usimamizi na wasimamizi wanatakiwa kuwa katika maeneo ya mradi yaani

kuwa kule (*site*) kwa muda mwingi, ambapo kwenye makundi haya hawatazidi watano kwa Taasisi na wengine wote wenye stahili za kuwa na magari wakopeshwe, watumie magari yao, watasimamia vizuri matumizi ya magari hayo, watasimamia vizuri matengenezo, watasimamia vizuri mafuta na watasimamia vizuri vipuri. Tutaondoa utaratibu uliozoeleka, dereva na gari anapitishwa chini, boshi anapanda ndege labda kutoka Mwanza au Mbeya anasema tukutane Dar es Salaam na kurudi hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna utafiti uliwahi kufanywa na nikaweza kuupata, siku moja yalibainika magari ya Serikali yalitokea Dodoma kwenda Dar es Salaam kwa siku yalikuwa 132 na yaliyokuwa yanatoka Dar es Salaam yakipishana na yale yanayokuja Dodoma yalikuwa 76. Magari 132, magari 76 kwenye *route* hiyo hiyo na njiani humo nane yalikuwa yamepinduka, je, kwa mwezi gharama ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, tuna nchi ambazo zinatumia utaratibu huo na hata Benki Kuu ndivyo wanavyofanya, yule ambaye anastahili ya gari ndivyo wanavyofanya lakini hata Wabunge wameweza kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge ni viongozi wakubwa tu kwenye Taifa hili, lakini ndivyo wanavyofanya kwenye magari, tena majukumu yao ni ya kusafiri kutembelea wananchi ndivyo wanavyofanya kwenye mafuta, ndivyo wanavyofanya kwenye vipuri na kazi inafanyika kama kawaida. (*Makofi*)/*Vigelegele*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amedhamiria kupunguza matumizi kwenye Serikali yake, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono. Kama utaratibu huo wa kuwakopesha magari watumishi wenye stahili za magari na gharama za matumizi na mambo mengine, gharama zitashuka Serikalini takribani kutoka shilingi bilioni 550 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 50.5 kwa mwaka. Hiyo ni *serving* ya zaidi ya shilingi billioni 500 na fedha hizo zitakazookolewa zitafanya shughuli ya ununuzi wa madawa muhimu hospitalini watu wetu wasikose dawa

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wanapokwenda hospitalini; na zinaweza zikatoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati ambavyo hatujaanza kutoa mikopo hiyo na kutekeleza shughuli zingine za maendeleo. Tumezidi mno kupenda ubosi, magari makubwa kwa kila mtu Serikalini, matumizi ya starehe, wakati katika nchi hiyo hiyo bado kuna watu ambao wanapata shida kupata mlo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelelekeza Wizara ya Fedha na Mipango ifanye kazi kwenye jambo hili na iweze kuleta mapendekezo ya namna ya fedha hizi ziweze kutumika kwenye matumizi ya msingi tu.

Mheshimiwa Spika, wengine wanaweza wakajiliza jambo hili niwahakikishie halitaathiri mtumishi bali litafanyika *gradually*, litafanyika kwa hatua yaani *by phasing out* yaani tutabadilisha kadri watu wanavyopanda madaraja. Wakipanda wakifikia stahili hiyo wanakopeshwa na hatutaajiri dereva akistaafu, wale wachache watakaobaki watabaki kwenye maeneo ya viongozi, watabaki kwenye magari ya miradi na watabaki kwenye *pool*/kwenye mahitaji ambayo yanahitaji magari hayo na wala mtu asing' ang' anie hiyo kwa sababu mtoto wa dereva sio lazima naye aje kuwa dereva.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, tutaachana na mfumo wa sasa wa Ununuzi wa Umma (*Transactional Procurement*) ambao umeshindwa kuleta tija kwa kuwa msingi wake mkubwa unalinganisha zabuni zilizofunguliwa... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri makofi yamepigwa sana hapo kwa hiyo anza hiyo sehemu ya sambamba. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo tutaachana na mfumo wa sasa wa manunuzi wa umma (*Transactional*

*Procurement*) ambao umeshindwa kuleta tija kwa kuwa msingi wake mkubwa ni ulinganishaji wa zabuni zilizofunguliwa badala ya bei za bidhaa na huduma ambazo tunazijua. (Makofi/Vigelele)

Mheshimiwa Spika, mara nyingi bei hizi za ununuzi zimekuwa kubwa kuliko zile zilizopo sokoni kwa ujumla hata kwa rejareja na ingekuwa tunanunua kwa ajili ya nyumbani kwetu au kwa ajili ya makampuni ama kwa ajili ya kampuni zetu bei hizo tusingezikubali. (Makofi)

Napendekeza kuwa, ununuzi wa umma uwe wa kimkakati (*strategic sourcing*) kwa kuzingatia ukubwa wa ununuzi wa serikali na sekta ya umma kwa ujumla (*economies of scale*) pamoja na uwiano na mfanano wa bidhaa za huduma zinazotumika serikalini na sekta ya umma yaani *synergies*. (Makofi/Vigelele)

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ni moja, bidhaa zinafanana, hata ofisi ambazo ziko mkoa mmoja, imekuwa ikitokea kila mmoja anakuwa na bei yake licha ya bidhaa hizo kufanana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, unaweza ukawa unaikuta bei ya maji unaijua kabisa lakini kwa sababu mchakato umeshafanyika na umefuata sheria, unakuta bei ya maji labda imeongezeka mara mbili au mara tatu kwa ile ya soko ambayo tunaijua.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti matumizi ya Serikali, Serikali imepanga kufanya maboresho katika mfumo wa manunuzi wa umma ili kuhakikisha ununuzi wa umma unakuwa wenye tija na unaoendana na ubora na thamani ya fedha. Tutaendelea kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (*TANePS*) ikiwemo kuweka ukomo wa bei za bidhaa za huduma zinazotumika Serikalini ili kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango itahakikisha kuwa, bei zote za bidhaa na huduma

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

zinazotumika sokoni kwa ujumla na rejareja zinakuwa na *price catalogue*, inaingizwa kwenye mfumo wa *TANePS* na kuwa na ukomo (*limit*) kuwa na kikomo cha bei zitakazotumika Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia kuhakikisha kwamba mfumo wa *TANePS* hauruhusu watoa huduma, wakandarasi au wauza bidhaa wanaotoa bei hizo zilizo zaidi ya soko kwa ajili ya kupata zabuni kwenye sekta ya umma wakishaona tu ni Serikali wanapandisha bei.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza hatua hii, Wizara ya Fedha na Mipango itatoa Waraka wa Hazina kuelekeza Idara na Taasisi za ununuzi kununua bidhaa zinazofanana kwa bei ya kikomo. Endapo kutakuwa na ulazima wa kununua magari kwa wingi Serikali itafanya mazungumzo na Toyota Tanzania na Japan hasa magari ya maeneo ya taasisi zile nilizozitaja vyombo vya ulinzi pamoja na maeneo mengine, ili kufanya makubaliano ya jumla (*framework agreement*) yatakayowezesha Serikali kupata bei nafuu kama ilivyo kwa mashirika makubwa ya Kimataifa kama vile *UNDP* na mengine. Hii itasaidia kuokoa fedha katika manunuzi ya magari pamoja na vipuri na zoezi hili litafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napendekeza matumizi ya mifumo ya TEHAMA iwe chaguo namba moja katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kuondoa hizi *paper work operations* kwenye shughuli zake. Kila shughuli zifanyike kwa mtandao, mbona Bunge mmeweza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumbi za Mikoa na kumbi za Wilaya zote ziwe na miundombinu ya mikutano kwa njia ya mtandao (*virtual meeting*) pamoja na *zoom*. Hata wabunge wataweza kushiriki vikao vya Mabaraza ya Madiwani wakiwa hapa Dodoma na wataweza kuendelea na shughuli za Bunge hapa Dodoma au kushiriki vikao vya Mabaraza ya Madiwani wakiwa hata nje ya nchi au katika maeneo mengine kwenye majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuita Wakuu wa Mikoa nchi nzima, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Watendaji wa Halmashauri magari kwa nchi nzima umbali wote huu kuja kukaa mahali na kusikiliza ni mzigo mkubwa kwa walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekopa fedha kwa ajili ya Mkongo wa Taifa na tunaendelea kulipa deni, ila tunatumia gharama zingine kubwa kufanya kazi *manually*. Mheshimiwa Rais anajenga Chuo Kikuu cha TEHAMA, lakini tunaogopa TEHAMA. Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo tutafute utaratibu wa kuweza kuhamia kwenye TEHAMA. Tunataka kufuta usemi ambao ulizoeleka wa *Government works on papers* sasa tuseme *Government works on records*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeongea na Wizara ya Kisekta kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais kujadili utekelezaji wa jambo hili, Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo Wizara ya TEHAMA tafuteni mtu wa kusimika hiyo mitambo kila Wilaya tutapunguza matumizi yasiyo ya lazima. Eti inatokea Mkurugenzi anakuja tokea Wilaya ya pembezoni gharama yote ile eti ameleta barua au kuja kutoa ufafanuzi wa jambo au wanakuja nchi nzima kwenye kikao ila anaongea ni mmoja tu kwa uwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, au mtu anasafiri siku nne kuja kushiriki kikao cha masaa au nusu saa hadi masaa matatu anaacha kuhudumia wananchi na hatari zote za njiani na gharama zote kwa karne hii jambo hili sio muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kuna wakati kwenye magereza yetu tulishuhudia mwaka juzi hivi kuna wakati ndugu yangu Bwana Biswalo Mganga alitembelea gereza moja Mwanza, alipowasikiliza mahabusu alikuta takribani 82 hawastahili kuwa ndani na kuwaachia. Sasa swali utatembelea magereza mangapi *physically*, watu wangapi wanakaa ndani kwa sababu tu hawajatembelewa? Mahakama wameonesha TEHAMA inaweza kufanyakazi vizuri kwa kuendesha kesi na kuamua kwa njia ya mtandao, lazima

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tutumie vizuri maeneo mengi kwenye TEHAMA ili kuweza kuongeza ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufanisi katika miradi ya maendeleo, Mheshimiwa Rais ameelekeza kuangalia upya utaratibu wa ununuzi na thamani ya fedha kwenye miradi ya maendeleo. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha bado kuna dosari katika matumizi ya Serikali hususani kwenye ununuzi mkubwa na miradi ya maendeleo. Serikali imefuatilia eneo hili na kugundua mfumo wa kufanya ukaguzi wa taratibu za ununuzi (*compliance audit*) na wa fedha (*financial audit*) una mapungufu. Yapo mazingira ya taratibu zote kufuatwa katika ununuzi na sheria zote za ununuzi kufuatwa na hatua zote za ukaguzi kufuatwa lakini fedha inakuwa imeibiwa. Hii inatokana na baadhi ya watumishi wa umma wasio waaminifu kupanga njama na wafanyabiashara wasio wazalendo, kupandisha bei za bidhaa kwenye zabuni na kujipangia hata huyo aliyeshindania kwa kiwango cha chini anakuwa bado yuko mbali na bei ya soko au gharama halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mchezo wa aina hii, wanafuata sheria zote za ununuzi, wanafuata taratibu zote za kumchagua aliyeshinda kwa bei ya chini, ila kwa kuwa hiyo iliyoshindaniwa kuwa bei ya chini ni ya chini tu ikilinganishwa na wale wengine walioshindana kwenye zabuni hiyo. Inakuwa wamefanya njama basi bei hizo zinakuwa juu ukilinganisha na bei za bidhaa hizo katika soko. Hawa ni watu wanaoiba japo wamezingatia sheria, ni watu wanaoiba kwa mujibu wa sheria. Serikali itaendelea kumjengea uwezo CAG ili kumuwezesha kukagua kwa kufuata thamani ya fedha kwenye miradi yote mikubwa (*value for money*) na kufanya ukaguzi kwa wakati ili kukabiliana na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kumuongezea fedha CAG ili apate watumishi wa kutosha kwa kuajiri au kuwahamisha watumishi kutoka idara yoyote ya Serikali na kuwajengea uwezo. *(Makofi)*

Narudia, napendekeza kumuongezea fedha CAG ili apate watumishi wa kutosha kwa kuajiri au kuwahamisha watumishi kutoka idara yoyote ya Serikali na kuwajengea uwezo kwa mafunzo na weledi wa ukaguzi wa thamani ya fedha ili kuweza kukabiliana na tatizo hili. Nimemtengoa fedha CAG kama alivyoomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kuziba mianya inayotoa fursa ya miradi kutekelezwa bila kujali thamani ya fedha (*value for money*) kama alivyoelekeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Serikali itaendelea kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani ili kuweza kuvijengea uwezo wa kitaaluma na kuongeza idadi ya watumishi katika fani mbalimbali kama vile TEHAMA, uhandisi, ukadiriaji majenzi, wakemia, wanasheria na fani nyingine ili kuondokana na dhana ya wakaguzi wa ndani kuwa na taaluma ya fedha pekee.

Aidha, Serikali itafanya marekebisho ya Kanuni za Fedha za Umma kwa kuziwezesha Kamati za Ukaguzi kuwa na wajumbe wa nje watatu ikiwemo Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi ili kuongeza uhuru na ufanisi wa Kamati za Ukaguzi kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022. Pamoja na mambo mengine, marekebisho ya kanuni hizo yatazitaka Kamati za Ukaguzi kuwasilisha taarifa za ukaguzi wa ndani kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu kila robo mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya tathmini pia ya muundo wa majukumu ya Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali ikiwemo kufanya stadi za kujifunza kutoka nchi nyingine zenye Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kama ilivyo kwa hapa Tanzania na kuangalia muundo unaostahili na kukidhi mahitaji ya Idara zinazotekeleza majukumu yake.

Vilevile napendekeza Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kuwa na fungu lake (*independent vote*) pamoja na



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kuongeza idadi ya wakaguzi wa ndani ili kuimarisha na kuboresha ufanisi katika utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuanzia mwaka wa fedha 2022 taarifa za wakaguzi wakuu wa ndani zipelekwe moja kwa moja kwa *Internal Auditor General* kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais wakati akipokea Taarifa ya CAG. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkaguzi Mkuu wa Ndani atakuwa anawasilisha taarifa hizi mbele ya Baraza la Kazi chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kila Waziri wa kisekta aweze kupokea hoja zinazomhusu, kuzifanyia kazi na kuchukua hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi wa ndani wa ofisi mbalimbali watatoa msaada na ushauri kwa maafisa masuhuli husika ila taarifa ziende kwa *Internal Auditor General* na nakala zipelekwe kwa viongozi wakuu wa Maafisa Masuuli bhao. Kwa mfano, kwenye ngazi za Halmashauri, nakala ziende iwepo iende kwa DC, iende kwa Wenyeviti au mamea, Wakuu wa Wilaya; kwa Sekretarieti za Mikoa nakala ziende kwa Wakuu wa Mikoa na kwa Wizara, nakala ziende kwa Mawaziri, kwa taasisi, mashirika pamoja na wakala nakala hizo ziende kwa bodi zinazosimamia mashirika hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wakati inatokea tunaona miradi inakamilika, fedha zote zimetumika, lakini miradi inakuwa chini ya kiwango; jengo au mradi unakamilika au mradi ungali bado unanukia rangi, lakini ukipita pale unakuta nyufa kila kona, simenti na tofali zikiwa ni mchanga. Katika kukabiliana na jambo hilo Serikali imemuelekeza Mkaguzi Mkuu wa Ndani pamoja na vitengo vingine vya ukaguzi kuanza kufanya *Technical Audit* badala ya kufanya *Financial Audit* peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la usimamizi wa fedha za umma, Serikali itahakikisha Sheria ya Fedha ya Umma Sura Namba 348 inasimamiwa na ipasavyo. Pale

itakapotokea sheria ama taratibu za usimamizi wa fedha zimekiukwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kujibu hoja zinazotolewa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ama hoja za wakaguzi wa ndani, Afisa Masuuli wa Fungu husika pamoja na Maafisa wake wa chini watachukuliwa hatua kulingana na kanuni za fedha zinazohusisha adhabu (*Surcharge and Penalties*) za mwaka 2005. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuwakata mshahara kati ya asilimia tano hadi 30 kwa mwezi kulingana na uzito wa kosa alilolifaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali imetoa mwongozo wa ufuatiliaji na tathimini (*Monitoring Evaluation*) yaani *M&E*. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania anakerwa sana na udhaifu uliopo katika eneo hili. Eneo hili tumelitengea rasilimali watu pamoja na fedha ili kuweza kupewa malengo yanayoweza kupimika waweze kufanya kazi hiyo. Napendekeza kuanzia mwaka huu wa fedha unaokuja taarifa za *M&E* ziwasilishwe kwenye Baraza la Kazi la Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwako Mheshimiwa Spika, ili zipelekwe kwenye Kamati za Bunge, ili kamati zinapotembelea miradi ziwe na taarifa za kuweza kusaidia kufanya ukaguzi wa miradi, ili kuepusha vitendo vya kutokuwepo kwa taarifa za fedha kutumika ilihali kule *site* mradi haupo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vitendo vya rushwa vinasababisha utekelezaji wa miradi kuwa chini ya viwango kwa kuwa fedha zilizopangwa kutumika kwenye miradi kwenda kwenye mikono ya watumishi wasio wazalendo. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amelikemea jambo hili vikali. Watu wanapanga kuanzia wakati wa maandalizi ya bajeti, wanafuatilia mchakato wote, siku ikipitishwa na Bunge wanakesha wakisherehekea kwamba bajeti yao imepita, mradi unaposainiwa wanaanza kugawana fedha kabla ya utekelezaji wa mradi. Serikali itaendelea kuimarisha *Technical Audit, Value for Money* na *Real Time Audit* katika mwaka wa fedha unaokuja. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Aidha, Serikali haitawanyima wananchi wa halmashauri yoyote fedha kwa sababu ya hati chafu, wala haitarudisha fedha kwenye mfuko kwa sababu hazikutumika kwa ajili ya uzembe wa baadhi ya waliopewa dhamana ya kutekeleza miradi hii, wananchi hawahusiki na hati chafu. Tutawabaini wazembe, tutawakamata, tutawashitaki na tutawafunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kukazia, watumishi wa umma ndio kiungo muhimu sana katika maendeleo ya nchi. Mikataba yote wanaingia wao, ununuzi wote Serikalini wanafanya wao, miradi yote wanatekeleza wao, mapato yote wanakusanya wao na wananchi walijinyima wakawasomesha kwa kujinyima, ili wakusanye na kutumia kwa ajili ya maendeleo ya wote. Bado kuna vitendo vingi kwenye utumishi wa umma vinavyopunguza ufanisi. *wage bill* yetu ni kubwa kuliko ufanisi tunaoupata, *wage bill* ni kubwa kuliko viwango vinavyotakiwa kiuchumi na wakati huo huo ikama hazijatimia na wakati huohuo kila mtaa tuna vijana hawana kazi. Hii ina maana kuna watu wanalipwa bila kufanya kazi ya ufanisi na wapo kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imezoeleka kwa mfano Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, Makatibu Tawala, wakuu wa taasisi mbalimbali, wakuu wa idara mbalimbali ipo tangu siku zote, wakitenguliwa huendelea kulipwa mshahara ule ule sawa na yule aliyeko kazini. Unaweza kukuta nchi ina Wizara 25, lakini ina Makatibu Wakuu 50 au zaidi. Unaweza ukakuta tuna Halmashauri 184, lakini ukakuta tuna Wakurugenzi 300 au zaidi na hivyo hivyo kwa taasisi nyingine kwa sababu, hata waliotolewa wanaendelea kulipwa kama wako ofisini. Wanaziba nafasi za vijana wapya na vilevile hawako kwenye ofisi zile ambazo walikuwa kule. Wengine walishasababisha upotevu na hasara kwa Taifa letu, lakini wote wanaendelea kubebesha mzigo Watanzania wa kuwalipa, tunalipia nafasi mpya tunalipa na waliotoka. *(Makofi)*

Napendekeza yeyote aliyeko kwenye nafasi ya kuteuliwa akitolewa, lakini akabaki kwenye utumishi wa

umma arejee pia kwenye mshahara aliokuwa analipwa kabla ya kuteuliwa. Hii itawapunguzia mzigo Watanzania kulipa watu walioko *bench*, lakini pia itapunguza kuziba nafasi za vijana wanaotakiwa kuajiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo haya hayavutii, lakini ni lazima tuambizane ukweli. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anakerwa sana kuona fedha nyingi zinaelekezwa kwenye matumizi yasiyo ya lazima. Mbona Mawaziri tukitoka hapa *front bench* wote tukitoka, kesho yake tunarudi kwenye mshahara wa Ubunge. Utaratibu wa kumlipa aliyechukua nafasi yako na wewe uendelee kulipwa kwenye nafasi ile ile ambayo ulishatoka unaibebesha Serikali mzigo na inawabebesha walipa kodi waw a Tanzania mzigo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mashirika ya umma, napendekeza mashirika ya umma yote yenye kufanya kazi za misingi kibiashara yafanye kazi kwa ufanisi na faida. Yale yasiyofanya kazi kibiashara tutayapima kwa namna yanavyoweza uchumi kuchangamka na jinsi wanavyoimarisha huduma wanazozitoa kwa jamii. Mashirika mengi yamekuwa ni mzigo kwa kutegemea ruzuku kutoka Serikalini ili yajiendeshe. Kwa nchi zilizoendelea, mapato makubwa ya Serikali yanatoka kwenye mashirika yake ili kupunguza mzigo kwa maskini kulipa kodi ili kuweza kuendesha mashirika hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napendekeza wakuu wa mashirika ya umma wafanyiwe usaili kwa ushindani. Napendekeza nafasi zianze kutangazwa punde nafasi inapokuwa wazi, wenye sifa wajitokeze, wafanyiwe usaili na bodi hivyo hivyo wenye sifa ndio wafanyiwe upekuzi, ili uteuzi uweze kufanyika na wapewe mikataba na malengo yanayopimika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, imezoeleka baadhi ya mashirika mengi kuwa muda mwingi yanakuwa bila bodi na mengine yana menejimenti dhaifu na mengine hata bodi hazijasimama vizuri. Unakuta mashirika pamoja na taasisi nyingine bodi na menejimenti zimezidisha sana urafiki,

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wanaendesha ofisi kiurafiki, hakuna uwajibikaji wa kutosha na hii inakiuka misingi ya mashirika kuwa na bodi za wakurugenzi. Hii inasababisha watu wakikabidhiwa shirika la umma wanageuza kuwa ni mali yao au duka lao. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametuelekeza tuangalie upya utaratibu utakaoleta ufanisi wa mashirika ili yaweze kujijendesha na kutoa gawio kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kuna maeneo yatakayogusa sheria na kanuni mbalimbali, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametuelekeza isiwepo sheria yoyote inayotumika kama kikwazo cha kuwaletea Watanzania ufanisi. *(Makofi)*

Serikali, itafanyia marekebisho ya Sheria mbalimbali na kanuni zitakazoguswa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanayolenga kuongeza ufanisi Serikalini yaweze kufanyika. Najua masuala ya udhibiti wa matumizi, udhibiti wa vitendo vya rushwa, udhibiti wa uzembe, udhibiti wa ununuzi usiozingatia thamani ya fedha (*value for money*) yanagusa maslahi ya watu na yatanifanya niwe *unpopular Finance Minister*, hata siku nikitoka kwenye nafasi marafiki wakaona nilikwamisha *deal* zao, potelea mbali, watabaki wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale marafiki watakaona nilikwamisha dili zao nikiwa Waziri wa Fedha siku nikitoka wakiniacha, potelea mbali, watabaki wananchi wangu wa lamba ambao huwa wanabaki na mimi hata nisipokuwa Waziri. Mheshimiwa Rais amenielekeza nifanyie kazi maeneo haya ya mapato na matumizi ya nchi, nami nitayasimamia na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu, hii ni nia njema ya Mheshimiwa Rais ya kuwakwamua Watanzania kwenye umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nihamie kwenye sekta za uzalishaji; kuhusu sekta za uzalishaji na ajira kwa vijana, Taifa letu ni Taifa la Vijana, wastani ni wa miaka 18. Miaka ya 1960 na miaka ya 1970 na miaka ya 1980 vijana wengi walikuwa

wanahudumia wazee na watoto. Njia ilikuwa rahisi kwa wahitimu wakitafutwa wangali masomoni wachague wanataka wafanye wapi kazi ama taasisi gani, hali haiko hivyo sasa, kwa sasa wazee ndio wanahudumia vijana na watoto wao. Ni kawaida kukuta mzee kijijini ama mstaafu akiwahudumia vijana wake wahitimu. Uwiano huu si mzuri kwa Taifa letu kuwa na nguvu kazi kubwa ambayo haiko kazini, kwa maana hiyo mipango yetu sasa na sera zetu lazima zijibu mahitaji ya vijana wa Kitanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sekta ya kilimo; katika kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji zinazotengeneza ajira kwa vijana, Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294 hadi shilingi bilioni 954 na itaendelea kuongeza kwa kila mwaka. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo inakua kwa angalao zaidi ya asilimia 10 ifikapo 2030. Bajeti ya mwaka 2022/2023 ni msingi muhimu kufikia jambo hilo. Malengo mengine ni kujitoshesheza kwa mahitaji ya chakula cha ndani na nje, kuongeza thamani ya mauzo ya mazao nje kutoka dola za Kimarekani bilioni 1.2 hadi bilioni tano ifikapo 2030, hii itatusaidia pia kwenye uhimilivu wa deni la Taifa, kuongeza mazao ya bustani pamoja na mengine kutoka dola za Kimarekani milioni 750 hadi angalao dola bilioni mbili ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza umaskini Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inalenga kuongeza ajira za vijana na wanawake zaidi ya milioni tatu katika sekta ya kilimo ifikapo mwaka 2025. Hii itafanyika kwa kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta milioni 8.5 sawa na asilimia 50 ya eneo lote linalotumiwa hapa nchini ifikapo 2030. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo itatekeleza skimu ndogo za umwagiliaji kote nchini. Tunataka vijana watoke mjini waelekee kwenye mashamba ya umwagiliaji kwa kuwajengea miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi wa mabwawa ya kuvunia maji pamoja na mvua. Tutatoa maji Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na mito mikubwa, kama Malagarasi, Ruvuma na Rufiji, Mara, Pangani, pamoja

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

na Ruvu na haya maji tutayatumia kwenye skimu za umwagiliaji. Kwa ardhi na maji na watu tulionao ni jambo la aibu Tanzania kulia shida ya ngano, shida ya mafuta ya kula eti kwa sababu Urusi na Ukraine wanapigana. Tunayo fursa ya kuilisha Afrika, Ulaya na Asia na baadhi ya nchi kwenye baadhi ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuongeza idadi ya mashamba makubwa (*block farms*) kutoka 110 kwa mwaka 2020 hadi 10,000 ifikapo 2030. Kufanya mwelekeo wa uzalishaji wa kilimo kuwa wa kibiashara. Kwa kilimo cha michikichi, tuache kung'ang'ania mchikichi mmoja mmoja kwa kila familia, Mkoa wa Kigoma ndio kitovu cha Michikichi. Tumekaa na Wabunge wa Kigoma tumekubaliana kuruhusu uwekezaji utakaowahusisha wenye mashamba na upanuzi utafuata kwa mikoa ya Tabora, Katavi, Pwani, Geita na Kagera. Wenye mashamba na wenyewe wawekeze, si mbaya ukiiga kauli mbiu ya Yanga kwamba mwekezaji ni mwananchi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakulima wawezeshwe kuunganisha mashamba ili yawe mashamba makubwa (*plantations*), kila mmoja atakuwa mmiliki ili itengenezwe miundombinu ya pamoja. Ni ngumu sana kuwatoa vijana wahitimu leo wakalime *style* waliyokuwa wanalima babu zetu, lazima wao walime kwa njia ya kisasa na hapo ndipo tunapoweza kuitikisa dunia. Serikali itaendelea kufanya tathmini ya kutumia ardhi kwa tija; kwa mfano sasahivi tunaongea na Wizara ya Mifugo, hata ninyi mtasema, tunazo hekta 38,000 pale kongwa, hivi kwa nini wasipunguze ama wakahamisha kiasi cha mifugo ili lile eneo lote lile tukafanya *plantation* kubwa ya alizeti na kiwanda kikiwa palepale. Na lile eneo kama la Mtanana ambalo watu wanasumbuka kila siku kuweka madaraja na maji yanakata na yanaenda kukata reli kule, tukatengeneza bwawa kubwa, ili bonde lote lile liwe *outgrowers* wa alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazao yafuatayo nyanayoagizwa kutoka nje tutaanzisha utaratibu wa ndani wa kuwauliza wale wanaoagiza kutoka kule wametumia kwa kiwango gani

mazao ambayo tunayapata ndani hapa, kwa mfano ngano, shayiri, mafuta ya mchikichi pamoja na mafuta ya alizeti. Mpaka sasa Tanzania bado haijajitosheleza kwa vitu vingi ambavyo tunao uwezo wa kuzalisha, bidhaa nyingi ambazo tunaagiza tunao uwezo wa kuzalisha hapa. Tunataka tujitosheleze kwa chakula, tunataka kujilisha, tunataka kuilisha Afrika pamoja na Mashariki ya Kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Oman inaagiza chakula kwa zaidi ya dola za Kimarekani bilioni tano kwa mwaka. Hizi ni ajira ambazo zimekaa tu sebuleni tunataka angalau katika miaka mitano ijayo tuwalishe ndugu zetu wa Oman hata kwa dola za Kimarekani bilioni 1.5 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya mifugo; tumeongeza bajeti kwenye sekta ya mifugo, tunachotaka kukifanya ni kuongeza uwekezaji ili tuweze kui-*modernize* sekta ya mifugo. Sasa hivi takwimu za mifugo tunazo nyingi kama mnavyoziona, lakini pia ndani ya nchi tunakosa malighafi kwenye viwanda vya nyama.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na malengo yanayotofautiana, mwenye viwanda ana malengo tofauti, na wafugaji wenye mifugo wana malengo tofauti. Ndugu zangu wa usukumani kule Mwanhuzi huko hata ng'ombe akivunjika mguu anafungwa *POP*, hata akiwa na shughuli ya kifamilia hachinji ng'ombe muulizeni Kalemmani, hachinji ng'ombe wa zizini, anakwenda kununua ng'ombe mnadani ili afanyie hiyo shughuli ya kifamilia, ng'ombe wa zizini wote wamepewa majina utasikia Shita Makui, Magulya, Kishosha Ugali, Shosha Nghwiye, Ntongeji wengine wana majina ya shangazi wengine ya mjomba hawachinjwi hawa wala hawana lengo la kupeleka mnadani. (*Makofi*)

Kwa hiyo mwenye kiwanda ana lengo tofauti na mwenye ng'ombe ana malengo tofauti, Wizara ya Mifugo tumeiongezea bajeti ili kuweza kufanya *modernization* waweke *modernization* kwenye sekta ya mifugo ili kuweza kuzalisha ng'ombe ambao wanatakiwa wapelekwe kwenye viwanda vyetu ili viweze kupata malighafi. Wizara ya Mifugo



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tumeiongezea shilingi bilioni 100 ambapo shilingi bilioni 40 zitaenda sekta ya mifugo na shilingi bilioni 60 zitakwenda kwenye sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakusudia kuanzisha vituo nane vya kukuza ujuzi kwa vijana (*Youth Incubation Center*) kwa kuanzia na wanufaika takribani 1000 kwa ajili ya vijana watakaofanya kazi ya kunenepesha ng'ombe na kuuza kwenye viwanda vinavyokosa malighafi. Serikali imepanga kutumia mitambo ya kuchimba mabwawa kwa ajili ya wafugaji wadogo wadogo.

Aidha, napendekeza Wizara inayohusika na mifugo itunge kanuni za kukusanya na kulinda fedha (*ring fencing*) fedha ambazo zitatumika kwenye kila Wilaya kwenye mifugo waweze kutengeneza miundombinu ya mifugo (majosho pamoja na mabwawa).

Mheshimiwa Spika, Serikali itatoa mitambo kwa sababu kila ukanda utakuwa na mitambo ya kuchimbia mabwaw. Mheshimiwa Rais ameendelea kuhamasisha uwekezaji zaidi katika viwanda vya kuchakata na kusindika nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya uvuvi tumeiongezea fedha ili kuweza kuongeza pato la Taifa na kazi ambazo zitafanyika ni pamoja na usambazaji wa boti zaidi ya 250 za kisasa za *fiber* kwa ajili ya ushirika wa wavuvi ili kuendelea na ufufuaji wa shirika la uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya fedha imeendelea kutoa mikopo kwa wafanyabiashara na uchumi. Pamoja na juhudi hizo, kumekuwepo na wafanyabiashara wasiolipa mikopo yao kwa wakati na kupelekea kudhoofisha ustawi wa mabenki na ustawi wa kiuchumi kwa ujumla. Hadi kufikia Machi, 2022 mikopo chechefu ilifikia asilimia 8.12. Hiki ni kiwango kikubwa sana kwenye vigezo vya usimamizi wa mabenki. Jambo hili linasababishwa na ukopaji usiozingatia

kanuni na ukosefu wa weledi na uaminifu kwa baadhi ya watumishi wa mabenki. Unakuta mtu amekopa mabenki zaidi ya matano na kote hajalipa. Akidaiwa sana anajificha, akichoka kujificha anapeleka mahakamani. Tuache utapeli unatuharibia nchi ukikopa lipa. Nitoe rai kwa vyombo vya dola vyote na vyombo vya sheria kuwa wakali kwenye utapeli wa aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana wanawake, taarifa za kitafiti nilizopewa zinaonesha wanawake wengi wanajitahidi kurejesha mikopo, hata mikopo ya familia ikikopwa wanawake kama wanajua mikopo hiyo itafanyakazi na uwezekano mkubwa mikono hiyo italipwa tofauti na wanaume walio wengi. Niweke sawa pale niliposema wanaume walio wengi ni ukimuondoa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Naibu Spika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tujenge utaratibu wa kuzingatia kanuni na uwezo wa kulipa na tujenge utaratibu wa kurejesha mikopo kwa uaminifu ili kuimarisha sekta ya fedha na kukuza uchumi wetu.

Kwa upande mwingine wapo pia watumishi wa mabenki wasio waaminifu, wanashirikiana na madalali, wanapenda kutamani dhamana za wateja wao, wanatafuta wateja haraka haraka wa kununua dhamana ambazo ziliwekwa na wateja angali mteja ameshalipa zaidi ya asilimia tisini ya deni lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tena wanauza kwa kiwango ambacho hakihusiani kabisa na thamani ya dhamana iliyowekwa. Jambo hili linawatia umaskini watanzania na nitoe rai kwa vyombo vya ulinzi na usalama kufuatilia kwa karibu kila kunapofanyika minada ili kuweza kuangalia uhalali wa kile kinachofanyika kwa madalali pamoja na bandarini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nishati mafanikio ni kama ambavyo yalielezwa na Wizara ya kisekta. Katika sekta ya nishati Serikali ina kusudia kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kwa mwaka 2022/2023 Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM inakusudia kutekelezaji mradi mkubwa wa kuimarisha Gridi ya Taifa (*The National Grid Stabilization Project*) kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa umeme na kuwa na uhakika hapa nchini. Miradi mingine itakayotekelezwa ni kama ilivyoorodheshwa na Wizara ya kisektas

Mheshimiwa Spika, Serikali itakamilisha uunganishwaji wa mkoa miwili ya Kigoma na Katavi kwenye Gridi ya Taifa. Mradi wa Nyakanazi – Kakonko – Kasulu hadi Kigoma KV 33 unaojengwa na Mkandarasi Sinotech, Mradi wa Nyakanazi - Kigoma KV 400 Mkandarasi yuko *site* kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 168 na fedha hizo zipo. Kadhalika mradi wa kufua umeme wa Malagarasi Mw 49.5 fedha zipo tayari kwa ajili ya mradi huo. Serikali itaendelea na miradi mingine mikubwa miwili ambayo ni ule wa Sumbawanga - Katavi - Kigoma na ule wa Tabora – Katavi - Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mkoa wa Katavi, tayari mkandarasi yuko *site* kwa ajili ya kutengeneza *sub-stations* pale Ipole – Sikonge - Inyonga wenye thamani ya bilioni 124. Napenda kuwahakikishia wananchi wa mkoa hiyo kuwa umeme wa Gridi ya Taifa utafika kama Waziri wa Nishati alivyoelekeza. Wabunge wa mkoa ya Kigoma na wale wa Katavi mliokuja kuweka kambi Wizara ya Fedha kufuatilia ahadi ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan mtarudi mikoani kwenu mkiwa mashujaa na mtatembea kifuambele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi na uchukuzi; mafanikio ni kama yalivyoainishwa na Wizara ya kisekta. Serikali imeshaanza mchakato wa kutafuta mkandarasi kwa kipande cha Tabora - Kigoma angali imeshasaini kipande cha Makutupora - Tabora na iko hatua za mwisho kusaini kipande cha Tabora - Isaka. Serikali itakapokamilisha itasaini mkataba wa kipande cha Tabora - Kigoma ambacho ni cha takribani dola za Kimarekani bilioni 2.1 na kipande cha Uvinza - Malagarasi - Msongati - Itega -

Kindu kwa upande wa Tanzania nacho wako kwenye hatua za kutafuta mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha jumla ya kilometa 216 kama ambavyo nilitoa katika hotuba ya Hali ya Uchumi leo. Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania inaweka msisitizo kwenye ujenzi wa barabara hasa zinazofungua uchumi na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani kwa utaratibu wa *EPC+F* ikiwemo barabara ya Kidatu - Ifakara - Lupilo - Malinyi - Londo mpaka Lumecha kule Songea yenye kilometa 499; na ya pili ni ile barabara ya Handeni - Kibirashi - Kibaya - Kwa Mtoro hadi Singida kilometa 460 ili Mheshimiwa Reuben aache kuja kupiga kambi pale Wizara ya Fedha na nyingine ni ile ya Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti - Lalago hadi Maswa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Flatei alivyomaliza sarakasi hapa alihamia Wizarani na sisi Wizara ya Fedha tumeiweka barabara hii kwenye orodha ili aweze kuwapelekea majibu sahihi wananchi wake barabara hiyo itajengwa pamoja na rafiki yangu Issay. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni ya daraja la juu la Magomeni -Jangwani hadi *Fire* hadi kule Bibi Titi; na nyingine ni barabara ya Kibaha - Mlandizi - Chalinze - Morogoro ambayo ni *expressway* kilometa 158 na ile ya Igawa Songwe Tunduma ambayo ni *expressway* kilometa 218.

Mheshimiwa Spika, narudia hii ya sita ni ile ya Igawa Songwe hadi Tunduma *expressway*. Pamoja na hii barabara ya *expressway* hizi ambazo ni ya Morogoro ya Kibaha - Mlandizi - Chalinze - Morogoro ambayo itakuwa ya *expressway* na ya Igawa Songwe Tunduma pamoja na daraja la Tanzanite zitawekewa *road toll* pamoja na taratibu zingine kwa sababu zina sifa hizo za kuweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itamalizia barabara zinazounganisha Mikoa ambayo wakandarasi wako kazini ikiwepo Tabora - Kigoma - Nyakanazi - Kigoma kuweka

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kipaumbele kwenye kujenga barabara na miundombinu ya kiuchumi ambazo tuna uchumi mkubwa unaofanyika katika maeneo yale kwa mfano barabara ya Makongorosi - Itigi – Mokiwa; barabara ya Mafinga – Mtwango - Nyololo – Mgololo; barabara ya Kahama - Nyanghwale - Geita na nyinginezo. Serikali ya Awamu ya Sita ina dhamira ya dharti ya kutekeleza miradi hiyo ya bandari kama ambavyo ilielezwa na Wizara ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, sayansi na teknolojia mafanikio ni kama ambavyo yalielezwa na Wizara ya kisekta. Hata hivyo katika mwaka 2022/2023 Serikali itaenda kutekeleza mradi wa *Higher Education for Economic Transformation (HEET)* wenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 425.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utahusisha ujenzi wa miundombinu katika vyuo vikuu mama na katika mikoa kadhaa ambayo haina vyuo vikuu ikiwemo Lindi, Kagera, Rukwa, Katavi, Manyara na kukamilisha ujenzi wa *Institute of Marine Science Zanzibar* na kujenga Chuo Kikuu kipya cha TEHAMA Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 244 zitatumiwa. Rais anakusudia kujenga chuo cha TEHAMA huyo ndiyo Samia kitajengwa Chuo cha TEHAMA hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na utaratibu wa kugharamia elimu ya msingi bila ada ambapo hadi Aprili, 2022, jumla ya shilingi bilioni 244 tayari zilishatumika. Ili kukabiliana na utoro (*drop out*) za watoto ambao wanatoka katika familia maskini, bado tuna watoto wanaoshindwa kumudu mahitaji ya lazima licha ya uwepo kwa programu ya elimu bila malipo, hivyo wanabaki kusaidiwa na Wabunge pamoja na Madiwani pamoja na wengine.

Napendekeza kuanzisha dirisha maalum kupitia *TASAF* itakayosaidia watoto wanaotoka familia maskini. Kwa kuanzia napendekeza kutenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya watoto wanaotoka familia maskini, hii itawapunguzia *message* na simu na vilio Waheshimiwa Wabunge ambao ndiyo mmekuwa wafadhili wakuu wa watoto hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutoa fursa kwa watoto wasioendelea na kidato cha tano na vidato vingine Serikali itaendelea kuimarisha elimu ya ufundi hususan katika vyuo vya kati na vile vya *VETA*. Serikali inakusudia kujenga Vyuo vya *VETA* katika mwaka huu wa fedha hadi sasa tuna vyuo 77 katika wilaya ambazo zina *VETA* tuna wilaya 77 ambavyo vina vyuo vya *VETA*, kati ya Wilaya 138 kote ikiwepo mkoa 25 yenye vyuo hivyo vya Ufundi. Bado mkoa wa Songwe hauna chuo kabisa na Wabunge wa mkoa wa Songwe wamekuwa wakipiga kambi ofisini kufuatilia ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, bado tuna wilaya karibu 62 ambazo hazina vyuo vya *VETA*. Napendekeza kutenga shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi tukianza na mkoa wa Songwe na wilaya zingine 36 ambazo hazina vyuo vya (*VETA*). Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio Samia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine elimu ya kidato cha tano na sita kuna vijana wanaotoka vijijini kwenye shule za kata wanafaulu kwenda mkoa ya mbali. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM anaguswa sana na tatizo hilo kwa watoto pamoja na wazazi wanaopata shida kutokana na ukweli kwamba hakuna shule za *high school* kwenye kata.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa wanafunzi wa kidato cha tano ni takribani 90,000 na kidato cha sita ni takribani 56,000 na mahitaji ya kifedha ni takribani bilioni 10.3. Ili kupunguza gharama za watoto hao kama Mheshimiwa Rais alivyoielekeza Wizara ya Fedha, napendekeza kufuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita. (*Makofi/Vigelegele*)

*(Hapa Mhe. Jacqueline N. Msongozi Aliimba Wimbo wa Tuna Imani na Samia)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, tafadhali simameni tu mpige makofi habari ya nyimbo humu ndani hairuhusiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri rudia kidogo hapo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa tuna takribani wanafunzi 90,825 wa kidato cha tano na wanafunzi takribani 56,880 wa kidato cha sita mahitaji ya kifedha ni takribani bilioni 10.3. Ili kuwapunguzia gharama watoto hao kama Mheshimiwa Rais alivyonielekeza baada ya kuguswa sana na shida wanazozipata napendekeza kufuta ada ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita. *(Makofi)*

Kwa hatua hiyo, elimu bila ada itakuwa kuanzia shule za msingi mpaka kidato cha sita. Serikali itajipanga kuangalia namna ya kusaidia vyo vya kati kadri hali ya uchumi itakavyokuwa inatengemaa. Nani kama Samia? Nani kama mama? CCM ni *number one*, Samia ni *number one*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango subiri kidogo. Humu ndani wewe huwezi kuwauliza Wabunge ili wakujibu ndiyo utaratibu Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za afya kama ambavyo ilielezwa kwa kina na Wizara ya kisékta. Serikali inakusudia kuendelea kuboresha sekta ya afya kwa kujenga na kukarabati na kupanua miundombinu katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo hospitali maalum ya mama na mtoto ya Jijini Dodoma pamoja na hospitali zingine kama ambavyo ilielekezwa na Wizara ya kisékta. Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Magharibi kukamilisha ujenzi wa hospitali tano za rufaa, mikoa na mikoa mipya Katavi, Geita, Njombe, Songwe, Simiyu na kukamilisha upanuzi wa hospitali nane za Rufaa za Mikoa.

Aidha, Serikali itaendelea kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa na ubobezi katika hospitali ya Taifa.

Kama ambavyo tulishaelezea tutakuwa na mitambo ya *MRI* minne, *CT Scan* 31 maana yake kila mkoa *Digital X-Rays* 130 pamoja na vifaa vingine vinavyohitajika katika matibabu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya maji Mheshimiwa Rais amewezesha kukamilika kwa miradi 303 na tutaendelea na utekelezaji wa miradi mingine kama ambavyo Wizara ya kisekta ilielezea kwa kina. Serikali pia imekamilisha taratibu za kununua seti 25 za mitambo ya kuchimba visima ambayo itasambazwa kila mkoa isipokuwa Dar es Salaam na seti tano za mitambo ya ujenzi wa mabwawa ambayo itapelekwa kila ukanda na seti nne za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi pamoja na vitendea kazi vingine. Mitambo hiyo inatarajiwa kupokelewa mwishoni mwa mwezi huu wa Juni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maliasili na utalii hadi Aprili mwaka huu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua filamu ya *Royal Tour* ambayo imelenga kuonesha uwezo na fursa ambazo Tanzania inazo katika sekta ya utalii. Hivyo, kupitia Bunge hili, napenda kuendelea kuwakaribisha *diaspora* wa Tanzania na wengine wengi waje wawekeze Tanzania, lakini pia wafanye shughuli za utalii. Tanzania tuna jambo letu, Tanzania ni Kitovu na ni mfano wa sehemu ya uwekezaji na sehemu ya utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande madini mafanikio ni kama ambavyo Wizara ya kisekta ilielezea. Kwa upande wa wachimbaji wadogo mafanikio kwa wachimbaji wadogo ni kushiriki uchumi wa madini, Serikali imezihamasisha taasisi za kifedha hapa nchini kutoa mikopo kwa wachimbaji hao ili kuwawezesha kukua na kufanya uchimbaji wenye tija. Baadhi ya mabenki ambayo tayari yameonesha nia wakiwemo kwenye uchimbaji mdogo ni *NMB*, *NBC*, *CRDB* na *KCB* zimeridhia kuanza kutoa mikopo ambapo jumla ya shilingi bilioni 36 zimekopeshwa kwa wachimbaji hao. Hizi ni miongoni mwa juhudi ambazo Serikali imezifanya kuhakikisha wachimbaji wadogo wanakua na kufikia hadhi ya kiwango



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

cha kati na hatimaye kuwa wakubwa nao pia waweze kushiriki kwenye uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia Tanzania imeweza kufanikisha ugani wa jiolojia kwa asilimia 96 ya nchi nzima, ugani wa jiofizikia kwa skeli ndogo asilimia 100 na skeli kubwa asilimia 16 na ugani wa jiokemia asilimia 25 kwa nchi nzima. Kupitia tafiti hizo Serikali imefanikiwa kugundua maeneo mengine mapya ambayo yatatusaidia. Wizara itaendelea kuratibu masuala hayo ili waweze kugundua maeneo mengine mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bunge Serikali inatambua kazi kubwa ambazo Bunge inafanya na tumeiongezea Bunge kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya matumizi mengineyo ili kuliwezesha Bunge ikiwemo kuwajengea Wabunge uwezo waweze kuisimamia vizuri Serikali. Serikali imeongeza bajeti ya Mfuko wa Jimbo ili kuwawezesha Wabunge kushiriki kikamilifu katika shughuli za kuchochea shughuli za maendeleo kwenye majimbo yao. Serikali itahakikisha kuwa fedha kwa ajili ya shughuli za Bunge zinatolewa kwa wakati kama Mheshimiwa Rais alivyotuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utawala bora; upande wa Mahakama Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa mifumo ya haki na utoaji haki na itaendelea kuwezesha mihimili kama Mahakama ili kuweza kusikiliza kesi na mashauri na kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya utoaji haki kwa kupitia TEHAMA kama ambavyo nimetoka kusema ambavyo wamekuwa wakifanya.

Kwa upande wa Mwanasheria Mkuu, Serikali itaendelea kugharamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zinazolenga utoaji wa haki kwa wananchi na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ulinzi na usalama Serikali kupitia majeshi yetu imeendelea kudumisha amani na usalama hapa nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kiulinzi na majeshi mengine mbalimbali, sambamba na zoezi la anuani za makazi linaloendelea, Serikali itaimarisha shughuli za usalama ngazi ya kaya ili kudhibiti aina mpya ya uhalifu ambao tumekuwa tukiusikia katika baadhi ya majirani zetu. Utaratibu huo ni pamoja na kuhakikisha viongozi wa mitaa na shehia wanahusika kwenye upangishaji wa nyumba kuhusika ili kuweza kujua nani anapanga wapi na mikataba ya Serikali za Vijiji na mikataba inayopangiwa ipigwe mihuri na Ofisi za Serikali ya vijiji na mitaa husika. Kadhalika, mauziano ya mali zisizohamishika lazima zihusishe uongozi wa Serikali za Vijiji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uhusiano na washirika wa maendeleo; jitihada za kuimarisha ushirikiano na washirika wa maendeleo zimeendelea kama ambavyo tumeeleza wakati Wizara ya Kisekta ilipowasilisha taarifa kupitia Wizara ya Mambo ya Nje. Serikali inakamilisha majadiliano ya mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia upatao dola za Kimarekani milioni 500, sawa na takribani shilingi bilioni 1.16, makubaliano tayari yapo hatua za juu na tunaendelea na makubaliano na wenzetu wa *IMF* kwa ajili ya *ECF*, Shirika la fedha la *IMF* ambapo ni dola la Kimarekani bilioni 1.1 ili kuweza kusaidia shughuli za maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, upande wa maslahi ya watumishi wa umma pamoja na wastaafu; ilikuwa ikisikika tuzo ya watumishi wa umma nani ni mchapakazi na nani ni mzalendo na *criteria* ipi inatumika? Matunda ya utumishi wa kujitua na uadilifu wa watumishi hao ni yapi? Je, ni nani kayatambua na kuyapa thamani halisi mambo hayo? Sauti zenye maswali haya zilisikika kwa mama yetu mwenye usikivu, unyenyekevu na anayejali, na hatimaye maswali haya yakapata majibu kwenye jambo letu. Kalamu yenye mamlaka ya Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akaongeza kima cha chini cha mshahara kwa asilimia 23.3 hii ilifunika maongezeko yote mliyoyasikia hapa Afrika. (Makofi)

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kuonesha kujali watumishi wa umma Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amefanya maboresho kwenye viwango vya posho, katika mema na kujali, kutenda na kuuishi mema. Hivyo, Mheshimiwa Rais wetu amekuwa ni mfano wa maneno haya katika jambo hili, ahsante sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada za kulipa madeni ya Watumishi wa Umma na kupandisha madaraja watumishi wanaostahili. Tutaendelea kuboresha mazingira ya kazi na maslahi kadri kadri uchumi wa nchi utakavyokuwa unaruhusu katika kuhakikisha maslahi ya wastaafu wetu waliotumikia Taifa letu kwa uzalendo, uadilifu na bidii kubwa wananufaika nayo. Serikali sikivu ya Mama Samia Suluhu Hassan imeridhia kuongeza malipo ya mkupuo kwa wastaafu katika asilimia 33 badala ya asilimia 25 iliyopendekezwa mwaka 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira ya biashara ndogo ndogo; katika kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuhakikisha anasimamia na kuwalinda na kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wadogo, Serikali itaendelea jitihada mbalimbali za kuhakikisha wajasiriamali hao wadogo almaarufu wamachinga wanapata mazingira bora ya kufanyia kazi. Serikali itaendelea kuwatambua na kuwaunganisha na taasisi za kifedha, vile vile Serikali itaendelea kutenga maeneo ya ujenzi wa miundombinu wa wajasiriamali hao wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameahidi kutoa shilingi milioni kumi kila Mkoa kwa ajili ya kuimarisha uongozi wa machinga pamoja na ujenzi wa ofisi zao. Aidha, Mheshimiwa Rais amenituma nipendekeze kama ifuatavyo; kutenga fedha takribani shilingi bilioni 45 kwa ajili ya miundombinu pamoja na mikopo kwa ajili ya wamachinga katika mikoa yetu. *(Makofi)*

Aidha kupitia sheria ya fedha ya mwaka huu, Serikali inapendekeza kufanya maboresho ya jumla ya sheria 19 za

sheria mbalimbali ambazo zipo kwenye kuboresha mazingira ya biashara yaani *blueprint* zianze kutekelezwa katika muswada huu ambao nitausoma hapo baadae. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sensa na Makazi, kipaumbele kingine cha bajeti ya itakuwa ugharamiaji wa Sensa na Makazi na niwaombe Waheshimiwa Wabunge waendeleo kuwahamasisha wananchi kwa ajili ya sensa itakayofanyika tarehe 23 Agosti, mwaka huu. Ili kuwezesha zoezi hili muhimu, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 400.9 ili kuweza kufanikisha zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni lugha ya Kiswahili; lugha ya kiswahili ndio lugha ya Taifa letu, ndio lugha ya ofisini, ndio lugha ya pili kwa watoto wa vijijini na ndio lugha ya kwanza kwa watoto wa sasa, ndio lugha ya msingi, ndio lugha ya Bunge, ni wazi kwamba nikiwa Waziri wa Katiba na Sheria nilipendekeza itumike kama lugha ya Mahakama. Kiswahili ndio lugha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo tuliipeleka sisi wenyewe, pia ni lugha ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika yaani *SADC* pamoja na Umoja wa Afrika na huko tuliipeleka wenyewe. *UNESCO* wameitambua na watakuwa wanaiadhimisha kila tarehe 7 Julai kwa mwaka. Hii ndiyo lugha yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini usaili wa watoto wa Kitanzania huwa unafanyika kwa Kiingereza? Yaani Afisa Kilimo, Afisa Mifugo, Mtumishi wa Serikali za Mitaa anakwenda kuwahudumia Watanzania lakini ili tuweze kupima uwezo wake wa akili tunapima kingereza chake. Napendekeza saili zote zifanyike kwa Kiswahili, na kumbi zote za mikutano na ofisi za Serikali ziwe na vifaa vya kutafsiria lugha za kigeni na watafsiri ili tuweze kukienzi Kiswahili chetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo, Serikali itarejesha Bahati Nasibu ya Taifa kwa utaratibu wa kutumia sekta binafsi. Sambamba na hivyo Serikali kupitia Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, na *TRA* pamoja na sekta binafsi wataanza kuendesha bahati nasibu kwa kupitia risiti za *EFD* ili kuchochea wananchi kudai risiti wanaponunua bidhaa.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Aidha, Serikali itatumia sehemu ya mchango wa wajibu yaani *Corporate Social Responsibility* kwa kiwango kisichozidi asilimia mbili kwa ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya fedha kuweza kuendeleza michezo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwahakikishia Watanzania kuwa tutaweka nyasi bandia kwenye viwanja vitano kama alivyosema Waziri mwenye sekta ya michezo, sanaa na utamaduni kwa kuanzia tutaweka Mwanza, Arusha, Tanga, Dodoma na Mbeya. Katika mwaka wa fedha msamaha wa kodi kwenye nyasi bandia pia na vifaa vyake ambata utakwenda mpaka ngazi za Halmashauri. Nitumie fursa hii nizipongeza timu zetu za *Serengeti Girls* pamoja na *Tembo Warriors* ambao wamefanikiwa kwenda mashindano ya dunia niitakie kila la kheri timu ya *Taifa Stars* ambayo bado inatafuta tiketi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kupunguza makali ya maisha kwa wananchi wetu; Serikali itachukua hatua za makusudi kupunguza makali ya maisha kwa wananchi wetu yaliyotokana na athari za vita. Hatua hiyo inayochukuliwa ni pamoja na zile za kuhusu ongezeko la bei za mafuta, Serikali imepunguza tozo mbalimbali zilizokuwa kwenye ukokotoaji wa bei ya nishati ya mafuta. Aidha, Serikali itatoa ruzuku ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kupunguza ya kupunguza bei ya nishati ya mafuta hapa nchini. Vilevile Serikali inachukua hatua nyingine katika suala ikiwemo kuendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya kugharamia bei ya nishati ya mafuta kwa kutoa fedha kama hizo huko tunapoelekea na baadaye kwenda kwenye utaratibu wa *Fuel Price Stabilization*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa zao la mafuta ya kula nitaisema tutakapokwenda kwenye hatua za kikodi, hivyo hivyo na kwa upande wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo mbalimbali pamoja na hatua nyingine za mapato. Napendekeza kufanya marekebisho ya sheria zifuatazo; Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Namba 148; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Namba

332; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Namba 147; Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura Namba 438; Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura Namba 290; Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura Namba 263; Sheria ya Madini, Sura Namba 123; Sheria ya Korosho, Namba 18; Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura Namba 196; Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura Namba 306; Sheria ya Bima, Sura Namba 394; Sheria ya Magari ya Kigeni Sura Namba 84; Sheria ya Benki Kuu, Sura Namba 197; Sheria ya Usimamizi wa Forodha na Afrika Mashariki ya mwaka 2004; Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti yaani *Blueprint* na marekebisho madogo madogo ya baadhi ya sheria za kodi na sheria nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Kodi napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria za Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura Namba 148 kama ifuatavyo; kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye miti ambayo hajachakatwa yaani *standing tree*. Lengo la hatua hii ni kuchochea ukuaji wa sekta ya misitu, kuongeza ajira na kuwa na usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu. Hatua hii itapunguza mapato kama tulivyoelekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi zinazotumika kuzalisha mitungi ya gesi zinazotambulika kwa *HS Code 7229.90.00, 3810.90.00, 3401.19.00, 7904.00.00, 4016.93.00, 8481.10.00* na *8309.90.90*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mitungi ya gesi ili kulinda viwanda vya ndani.

Pia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kutambua mikopo mbadala inayofuata misingi ya taratibu zilizo nje ya fedha za asili ambayo asili yake ishughulikiwe sawa sawa na mikopo inayotolewa na benki katika utaratibu wa kawaida. Lengo la hatua hii ni kuchachua ukuaji wa bidhaa nyingine zenye lengo la kuchochea ukuaji wa biashara, uchumi pamoja na kuweka usawa katika ulipaji kodi.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Kiwango cha asilimia sifuri kwenye bidhaa za mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa mwaka mmoja ili kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula iliyopanda kutokana na mdororo wa uchumi; kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye mbolea inayozalishwa nchini kwa mwaka mmoja. Kiwango hiki kitahusu tu wazalishaji wa mbolea wa hapa ndani. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa uchumi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, mamlaka ya kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa mwekezaji mahiri maalumu baada ya kuridhiwa na *NISC* kwa mujibu wa kifungu cha 20(8) cha Sheria ya Uwekezaji Sura Namba 38 pamoja na kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la hatua hii ni kufanikisha maendeleo ya sekta ya uwekezaji nchini na kuondoa mgongano wa kisheria kuhusu utoaji wa vivutio vya ziada vya kikodi kati ya Sheria ya Uwekezaji na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 11(10) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuhusisha bidhaa za mtaji zinazotambulika kwa *heading 87.16* kwenye bidhaa za mtaji yaani *capital goods* zinazostahili kupata ahirisho la kodi ya ongezeko la thamani. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uwekezaji na kuchochea maendeleo ya viwanda hapa nchini.

Pia kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vya kupima kiwango cha maji na unyevunyevu kwenye udongo zinazotambulika kwa *HS Code 9026.10.00*, kifaa cha kupima kiasi kilichochukuliwa na udongo hasa katika eneo la mizizi ya mmea kinachotambulika kwa *HS Code 9031.80.00*, kifaa cha kupima kiwango cha chumvi katika maji kinachotambulika kwa *HS Code 9027.80.00*, na kifaa cha kupima kiwango cha naitrojeni katika hali ya naitreti

kinachotambulika kwa *HS Code 9027.90.00*. Lengo la hatua hii ni kukuza utafiti hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vyandarua vinavyotumika katika uzalishaji wa mbogamboga na maua vinavyotambulika kwa *HS Code 56.08*. Lengo la hatua hii ni kukuza sekta ya kilimo na kuongeza tija kwenye uzalishaji; kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vya kupima kiwango cha unyevunyevu yaani *moisture meter* vinavyotambulika kwa *HS Code 9003.18.00*, kifaa cha kupima kiwango cha mvua iliyonyesha *rain gauge for weather stations* kinachotambulika kwa *HS Code 9023.00.90*.

Mheshimiwa Spika, kifaa kinachopima hali ya hewa *alkaline* na tindikali *PH meters* kinachotambulika kwa *HS Code 3822.00.90*, kifaa cha kuzalisha miche/mbegu kwa chupa kinachotambulika kwa *HS Code 8419.89.60* na kifaa cha kupima uwezo wa kuvutika kinachotambulika kwa *HS Code 9031.80.00*. Pia kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye magari yenye jokofu yanayotambulika kwa *HS Code* kama nilivyozirodhesha ili kuweza kusaidia utekelezaji wa jukumu la aina hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye malighafi za kutengeneza mbolea zinazotambulika kwa *HS Code 2528.00.00*, *HS Code 2710.99.00* na *HS Code 3505.20.00*; kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vanila ya kijani isiyochakatwa inayotambulika kwa *HS Code 0905.10.00* ili kuleta usawa kwenye mazao mengine; kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye kamba za katani zinazozalishwa nchini. Lengo la hatua hii ni kukuza zao la katani na kuongeza ajira.

Pia kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mtindi na maziwa yanayozalishwa kwa joto la juu na kudumu kwa muda mrefu. Hatua hii inalenga kuwawezesha wazalishaji wa ndani kushindana kikanda na kimataifa. (*Makofi*)



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifungashio vya maziwa vinavyotambulika kwa *HS Code 3923.30.00, 4819.10.00, HS Code 4819.20.00* na *HS Code 4819.20.90*; kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye hereni za mifugo za kieletroniki zinazotambulika kwa *HS Code* ambazo tumeziainisha.

Pia kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vya machinjio vinavyotambulika kwa *HS Code* ambazo tumeziainisha; kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mbegu za malisho zinazotambulika kwa *HS Code 1209.25.00, HS Code 1209.21.00* na *HS Code 1209.29.00*; kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 18 cha Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Msamaha ili kuhuishia vifaa na mashine zinazotumika kwa vyombo vya ulinzi na usalama yaani *military and armed forces*, lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwenye ununuzi wa mashine hizo.

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa na mitambo ya hali ya hewa vinavyoingizwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyavu za kuvulia zinazotambulika kwa *HS Code* hizo ambazo tumezibainisha, lengo la hatua hii ni kukuza uvuvi wa wavuvi wadogo wadogo na kuchochea ukuaji wa Sekta ya Uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Namba 148 ili kuiwezesha Serikali kukusanya Kodi ya Ongezeko la Thamani katika biashara ya mtandao yaani *digital services* bila kuathiri uwajibikaji chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Namba 338.

Aidha, marekebisho haya yanalenga kurahisisha utaratibu wa usajili wa mlipakodi wanaotoa huduma za kidijitali na hapa niwapongeze watu wa *Jamii Forum* kwa kufanya *coordination* ya mazungumzo ya kuweza kukamilisha hatua hii.

Mheshimiwa Spika, kufuta msamaha wa kodi wa ongezeko la thamani kwenye simu janja pamoja na vishikwambi zenye *HS Code 8517.12.00* na *HS Code 8471.30.00* au *HS Code 8517.12.00* na Modemu zenye *HS Code 8517.62.00* au *HS Code 8517.69.00* kwa kuwa msamaha husika haujawezesha kupatikana bidhaa hizo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake umewanufaisha wafanyabiashara. Hata hivyo, hatua hii inategemea kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kufuta msamaha wa kodi wa ongezeko la thamani kwenye huduma za kukodi ndege (*air charter services*) kwani huduma hizi hutolewa kibiashara kama huduma za kukodi vyombo vingine vya usafiri ambazo kisheria hulipiwa kodi ya ongezeko la thamani. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 36,545.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria wa Mapato; napendekeza kufanya marekebisho ya jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuweza kuweka kiwango cha asilimia 3.5 kwa walipakodi wenye mauzo yanayozidi shilingi 11,000,000.00 lakini yasiyozidi milioni 100,000,000.00 kwa mwaka kwa lengo la kuweka uwazi na kurahisisha makadirio ya ulipaji wa kodi. Hatua hii itaongeza ulipaji wa kodi kwa hiari na hivyo pendekezo hili litaongeza ufanisi katika masuala ya ulipaji wa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 10 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya fedha mamlaka ya kusamehe kodi ya mapato kwa wawekezaji mahiri maalumu baada ya kuidhinishwa na *NISC* kwa mujibu wa Sheria 20 kifungu cha 8 na Sheria ya Uwekezaji ya 38 pamoja na kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri kama nilivyoielezea kwa upande wa *VAT*.

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya Zuio, kuondoa msamaha wa kukata kodi ya zuio kwenye malipo ya upangishaji wa nyumba, vyumba na majengo ya kibiashara, lengo la hatua hii ni kuwezesha

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wapangaji kukusanya kodi ya zuio kwenye pango na kuiwasilisha Serikalini. Aidha, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato ataingia makubaliano ya uwakala na Ofisi ya Rais, TAMISEMI juu ya usimamizi na ukusanyaji wa kodi hii.

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji katika uhamishaji wa haki na taarifa za madini kwenda kwenye kampuni za ubia zinazoundwa baina ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji kwenye hisa ambazo Serikali imepata kupitia Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi ya zuio kwenye kuponi za hati fungani za makampuni na manispaa yaani *Coupon for Corporate and Municipal Bond*. Pendekezo hili linalenga kuongeza vyanzo mbadala vya kugharamia miradi ya maendeleo hasa kwenye manispaa zetu.

Mheshimiwa Spika, kupunguza kiwango cha kodi ya zuio kwenye tasnia ya filamu kwa malipo yanayofanywa kwenda kwa watoa huduma wa nje ya nchi kutoka asilimia 15 hadi asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kukuza tasnia ya filamu na kuchochea uhamishaji wa ujuzi kwenye tasnia hiyo kwa lengo la kuongeza ajira na kuboresha maisha.

Mheshimiwa Spika, kutoza kodi ya mapato ya asilimia mbili kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wa kigeni. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi kwa kuzingatia kanuni na usawa za kodi. Nimpongeze Ndugu Max wa *Jamii Forum* kama nilivyosema aliwakusanya hawa watu na tukaweza kuongea nao.

Mheshimiwa Spika, kutoa kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye malipo ya wachimbaji wadogo wa madini (*Small Scale Miners*), hatua hii inalenga kuweka utaratibu maalum wa utozaji kodi kwa wachimbaji hao na kutatua changamoto zilizopo kwenye sekta ya uchimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kutoza kiwango cha mfuto (*flat rate*) cha shilingi 3,500,000 ikiwa ni kodi ya mapato inayopaswa kulipwa kwa magari ya mizigo na mabasi ya abiria kwa mwaka. Lengo la hatua hii ni kuongeza uwazi katika makadirio ya kodi baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipakodi na kuweka mfumo wa kodi unaotabirika na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya awali ya mapato (*Advance Income Tax*) ya shilingi 20 kwa lita kwa wafanyabiashara rejareja wa mafuta ya petroli hapa nchini itakayokusanywa na waingizaji wa mafuta hayo kwa jumla na kulipwa Serikalini. Lengo la hatua hii ni kurahisisha ulipaji wa kodi ya mapato kwenye vituo vya mafuta na kupunguza gharama za matumizi. Hatua zingine za kikodi zinatarajiwa kutuletea milioni 102.593.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kifungu cha 124 napendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:-

(i) Kupunguza ada ya leseni kwa wazalishaji na waingizaji wa bidhaa zinazotowwa Ushuru wa Bidhaa kutoka shilingi milioni 500 hadi shilingi milioni 300. Hatua hii inalenga kuwapa unafuu wazalishaji na waingizaji wa bidhaa hizo pamoja na kusaidia kurejesha ukuaji wa sekta baada ya athari za UVIKO-19.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri samahani kidogo hapo kwenye kupunguza ada ya leseni hebu soma hicho kiwango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kupunguza ada ya leseni kwa wazalishaji na waingizaji wa bidhaa zinazotowwa Ushuru wa Bidhaa kutoka shilingi milioni 500 hadi shilingi milioni 300. Hatua hii inalenga kuwapa unafuu...

**SPIKA:** Ngoja ngoja vitabu vinaonesha kutoka shilingi laki tano hadi shilingi laki tatu. Kwa hiyo, umefanya

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

marekebisho au tuchukue hii tunayoiona kwenye vitabu. Ni milioni 500 au ni laki tano?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, laki tano kwenda laki tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusamehe ushuru wa bidhaa kwenye vifungashio vya maua, matunda, na mbogamboga vinavyotambulika kwa *HS Codes 3923.29.00* pamoja na *HS Code* zingine ambazo tumeziandika.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa bidhaa wa shilingi 700 kwa kila bidhaa za sukari zinazolingizwa kutoka nje ya nchi na shilingi 500 kwa kilo ya bidhaa za sukari zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa bidhaa kwenye betri za maji kwa kiwango cha asilimia tano zinazotambulika kwa *HS Code 8507.10.00*, *HS Code 8507.20.00*. Hatua hii inalenga kupunguza madhara ya kimazingira yanayosababishwa na matumizi ya betri hizo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura Namba 348; napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura Namba 290 ili kugawanya asilimia 10 ya mapato yanayokusanywa na Serikali za Mitaa kwa utaratibu ufuatao; asilimia tano ipelekwe TAMISEMI kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya wajasiriamali wadogo wadogo na hizi zingine zifanye kazi zilizokuwa zikifanya kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusamehe ushuru wa mazao kwenye mbegu, hatua hii inalenga kuwapa unafuu wakulima na kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa mazao ya misitu ambayo nilishaisema kutoka asilimia tano hadi asilimia tatu.

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 16(7) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura Namba 290 ili kubainisha kwamba makampuni na taasisi za biashara na watu binafsi wanaotakiwa kulipa ushuru wa huduma kwenye Halmashauri moja watatakiwa kulipa ushuru kwenye Halmashauri nyingine ambako wananunua mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho ya kifungu cha 16 ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa mamlaka ya kuandaa Kanuni za ugawaji mapato yatokanayo na ushuru wa huduma kwenye makampuni.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mfuko wa Fidya kwa Wafanyakazi kwa kupunguza kiwango cha mchango kwa sekta binafsi kutoka asilimia 0.6 inayotozwa sasa hadi asilimia 0.5 ya mapato ghafi ya wafanyakazi. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa katika uchangiaji kati ya wafanyakazi wa sekta binafsi na sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, kupunguza kiwango cha mrabaha kutoka kwenye makaa ya mawe yanayotumika kama malighafi ya kuzalisha nishati viwandani kutoka asilimia tatu hadi asilimia moja. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Spika, kupunguza kiwango cha kutoza mrabaha (*royalty*) kutoka asilimia sita hadi asilimia nne kwa dhahabu inayouzwa kwenye vituo vya kusafishia madini, lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa vituo vyetu vilivyoanzishwa vinapata malighafi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Korosho ili mapato yanatokana na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi yagawanywe kama ifuatavyo; asilimia 50 ipelekwe Wizara ya Kilimo kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo na Mfuko wa Kilimo; na asilimia 50 ipelekwe Mfuko Mkuu wa Serikali. Lengo la

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

hatua hii ni kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo na kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kama ruzuku na tafiti.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Posta na Mawasiliano ambapo tutapunguza tozo kwenye miamala kutoka kiwango kilichokuwa hakizidi shilingi 7,000 hadi kiwango kisichozidi shilingi 4,000 katika kila muamala wa kutuma na kutoa pesa. Punguzo hilo ni sawa na asilimia 43 ya kiwango cha sasa nani sawa na asilimia 60 ya tangu tulipoanzia, sasa itakayobakia itakuwa ni asilimia 40. Lengo la hatua hii ni kupunguza makali ya maisha kwa Watanzania hasa katika kipindi hiki ambacho dunia inapita katika changamoto za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Bima kwa kuongeza wigo wa bima za lazima kwa kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara, bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje, vyombo vya baharini pamoja na vivuko.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Magari ya Kigeni ili kupunguza tozo ya magari yasiyozidi ekseli tatu kutoka dola za Kimarekani 16/100 kwa kilometa hadi dola za Kimarekani 10/100 kwa kilometa. Lengo la hatua hii ni kuwianisha utozaji wa viwango hivyo na ukanda wa *EAC, SADC na COMESA*.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Benki Kuu ili kuweza kuongeza wa ukomo wa Serikali kukopa kwa kiasi kisichozidi asilimia 18 ya mapato ya ndani yaliyoainishwa katika mwaka husika badala ya kiwango cha sasa cha mara moja ambacho kinatumika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza hatua mpya kwenye viwango vya ushuru wa forodha kama ifuatavyo; kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 au dola za Kimarekani 1.5 kwa kila mita moja ya mraba kutegemea na kiwango kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za marumaru zenye *HS Code 6907.21.00, HS Code*

2907.22.00 na HS Code 6907.23.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 au Dola za Marekani 125 kwa kila tani moja kutegemea na kiasi kilicho kikubwa kwenye mabati yanayotambulika kwa HS Code 7212.22.00 na HS Code 7226.99.00 kwa mwaka mmoja badala ya ushuru wa sasa wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kuvilinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kurejesha utozaji wa ushuru wa forodha wa kiwango cha asilimia sifuri kutoka kiwango kilichokuwa kinatumika cha sasa cha asilimia 25 kwenye mafuta ghafi ya kula yaani *Crude Palm Oil* yanayotambulika kwa HS Code 1511.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa mafuta ghafi hapa nchini na wananchi waweze kupata bidhaa hiyo kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 0 kwenye mafuta ghafi ya soya, karanga, nazi na haradali zinazotambulika kwa HS Code 1507.10.00; HS Code 1508.10.00; HS Code 1513.11.00; HS Code 1514.91.00; na HS Codes 1515.11.00. Lengo la hatua hii ni kuoanisha viwango vya mafuta haya ghafi vifanane na viwango vya mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 500 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea na kiwango kilichokikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwa mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati na cha mwisho yaani *semi-refined*. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani. HS Code hizo tumeziorodhesha katika jedwali ambalo linaonekana kwenye hotuba.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru wa bidhaa kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye taalo za watoto (*diapers*) zinazotambulika kwa HS Code



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

9619.00.90. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (*cotton yarn*) zinazotambulika kwa *HS Code 52.05*, *HS Code 52.06* na *HS Code 52.07*.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwenye milango na madirisha ya *aluminium* na chuma inayoingizwa kutoka nje zenye *HS Codes 7610.10.00* na *HS Code 7308.30.00*. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza viongeza ladha kwenye vyakula na vinywaji zinazotambulika kwa *HS Code 1901.90.10*; *HS Code 3302.10.00*; na *HS Code 3505.10.00*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji.

Mheshimiwa Spika, kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 25 hadi 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa *HS Code* ambazo tumezirodhesha kwenye jedwali hilo hapo.

Mheshimiwa Spika, kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengenezea vioo vizito zinazotambulika kwa *HS Code 7005.10.00*; *HS Code 7005.21.00*; *HS Code 7005.29.00*; na *HS Code 7005.30.00*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa vioo.

Mheshimiwa Spika, kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye

malighafi za kutengeneza nyaya za umeme (*electrical cables*) zinazotambulika kwa *HS Code* ambazo tumezitaja kwenye jedwali hili. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa nyaya hizo pamoja na kuvutia uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (*toilet soaps*) zinazotambulika kwa *HS Code 3401.20.10*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya kiwango cha asilimia 100 au dola za kimarekani 460 katika kila tani moja ya ujazo kutegemea kiwango kilicho kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwenye hema za chuma zinazotambulika kwa *HS Code 9406.20.90* zitakazoagizwa na wafugaji, kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwenye nywele bandia zinazotambulika kwa *HS Code 6704*. Hatua hii inalenga kulinda wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo na kuongeza ajira moja moja na kuongeza mapato ya Serikali. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hatujasikia vizuri au..., hebu rudia hapo. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwenye nywele bandia zinazotambulika kwa *Heading 6704*. Hatua hii inalenga kulinda wazalishaji wa

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ndani wa bidhaa hizo na kuongeza ajira moja moja na kuongeza mapato ya Serikali. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwenye mafuta mengineyo ya petroli yanayotambulika kwa *HS Code 2710.19.10*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu na kulinda watumiaji wa bidhaa hii.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 kwenye sigara za kielektroniki zinazotambulika kwa *HS Code 8543.10.40.00*. Lengo la hatua hii ni kulinda mnyororo wa thamani.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kufanya marekebisho kwenye tafsiri ya *HS Code 7310.29.20* na *HS Code 7612.90.10* ambazo awali zilikuwa zinatafsiri makasha ya kufungashia vinywaji.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali yaani *EFD Machines za Point of Sale* yaani *POS* zinazotambulika kwa *HS Code 8470.50.00* na *HS Code 8470.90.00*. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya vifaa hivi katika uhasibu wa mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa maziwa kwa joto la juu vinavyodumu kwa muda mrefu kama *HS Code* hizo nilizoitaja 4819.50.00.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka viwango vya asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye chupa za mvinyo zinazotambulika kwa *HS Code 4003.10.00*.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia sifuri hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye unga wa kakao unaoingizwa kutoka nje unaotambulika kwa *HS Codes* hizo. Lengo la kufanya hivyo ni kuchochea kilimo cha zao la kakao hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia kahawa vinavyotambulika kwa *HS Codes* ambazo tumezitaja hapa.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia korosho.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia pamba yaani *cotton lint*. Vifungashio hivyo vinavyotambulika kwa *HS Code* tulizozitaja hapa.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha asilimia 25 kwenye malighafi za kutengeneza taulo za watoto zinazotambulika kwa *HS Code* hizo ambazo tumeziorodhesha hapa.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifaa vinavyotumika katika kukata, kung'arisha na kuongeza thamani ya madini kama tulivyoorodhesha kwenye *HS Code* hizo hapo.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya mbegu vinavyotambulika kwa *HS Code* ambazo tumeziorodhesha kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha kwa asilimia 10 au dola za Kimarekani 125 kwa tani moja ya ujazo

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kwenye bidhaa za chuma kutegemea na kiwango kilicho kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 10 kwa mwaka mmoja kama ambavyo tumeorodhesha kwenye *HS Code* zilizopo kwenye jedwali hili.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 ama dola za Kimarekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea na kiwango kilicho kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa *HS Code* hizo tulizozitaja kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 au dola za Kimarekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo kwa mwaka mmoja kutegemea na kiwango kilicho kikubwa kwa bidhaa za mabati kama tulivyoorodhesha *HS Code* za kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 ama dola za Kimarekani 250 kwa kila ujazo wa mita kutegemea na kiwango kilicho kikubwa badala ya asilimia 25 ama dola za Kimarekani 200 kwa kila tani kama tulivyoorodhesha kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 ama dola za kimarekani 250 badala ya 25 ama dola za Kimarekani 200 kwa kila tani ya ujazo wa *metric ton* kutegemeana na kilicho kikubwa kama tulivyoonesha kwenye jedwali hilo hapo.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 ama dola za Kimarekani 250 badala ya kiwango cha asilimia 10 kwenye bidhaa ya chuma kama ambavyo tumeonesha kwenye jedwali hilo hapo.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia sifuri hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za fito za plastiki zijulikanazo kama *PVC profiles* zinazotambulika kwa *HS Code 3916.10.00* na hizo tulizozionesha kwenye jedwali.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini ambazo zinatambulika kwa *HS Code* 48.29.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa *HS Code* 1001.99.10 na *HS Code* 1001.99.90 kama ambavyo tumeonesha kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia sifuri kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa *remission* kwenye bidhaa inayojulikana kama *printed aluminium barrier laminates* ambazo tumezionesha kwenye *HS Code* hizo hapo.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia sifuri kutoka kiwango cha awali cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa *duty remission* kwenye malighafi za kutengeneza sabuni ijulikanayo kama *RBD palm stearin*.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 ama dola za Marekani 1.35 kwa kila kilo moja ya viberiti vinavyotambulika kwenye *HS Code* ambazo tumezionesha kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea na iliyo kikubwa kwenye moja ya bidhaa za chuma ambazo tumetambulisha kwenye *HS Code* hizo hapo.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye maji ya kunywa yanayotambulika kwa *HS Code* hizo. Kwa hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia sifuri kwenye *gypsum powder* inayotambulika kwa *HS Code* ambazo tumezitambulisha kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mitumba inayoingia kutoka nje badala ya asilimia 35 ama dola za kimarekani 0.4 kwa kilo kutegemea na kiwango kilicho kikubwa. Lengo la hatua hii ni unafuu kwa watumiaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwenye malighafi za vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza viatu vya ngozi pamoja na nguo kama tulivyobainisha.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotambulika kwa *HS Code* hizo hapo.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi 25 kwa mwaka kwenye matairi mapya ya pikipiki.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka kwenye nyaya za umeme.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka kwenye *milk cans* zinazotambulika kwa *HS Code* ambazo tumezionesha hapo.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye *LABSA* inayotambulika kwa *HS Code* ambazo tumezionesha hapo.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 au asilimia sifuri kwa mwaka

kutoka malighafi za kuchakata ngozi zinazotambulika kwa *HS Code* hizo hapo.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengenezea mbolea zinazotambulika kwa *HS Code* hizo hapo.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha wa asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka kwenye vifungashio vya tumbaku ilinayochakatwa vinavyotambulika kwa *HS Code 5310.10.00*.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha wa asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka kwa waunganishaji wa pikipiki za matairi matatu bila kujumuisha fremu ili ziweze kutengenezwa na kuunganishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa forodha kwa asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia sifuri mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengenezea mabomba ya plastiki.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa forodha wa kiwango cha asilimia 10 kutoka kiwango cha asilimia 100 ama dola za Kimarekani 460 kwa kila tani moja kutegemeana na iliyo kubwa kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya viwandani.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekubaliana kiwango cha juu cha ushuru wa forodha cha zaidi ya asilimia 25 kuwa ni asilimia 35. Hivyo, miundo mipya ya ushuru wa *EAC* katika mpangilio wa viwango vya *four tariff* yaani asilimia sifuri, 10, asilimia 25 na asilimia 35 lakini utekelezaji wake utanza tarehe 1 Julai, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara za kisekta napendekeza kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye sekta ya mifugo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali namba moja; kwa sekta ya uvuvi kama ilivyooneshwa kwenye



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

jedwali namba mbili; kwa Wizara ya Kilimo kufuta tozo ya shilingi 200 inayotozwa kwa kila mita ya mraba ya eneo la uso wa maji na kuongeza ada ya kibali cha kusafirisha mbolea ya nje ya nchi kutoka dola za Kimarekani 0.2 kwa tani hadi dola za Kimarekani 0.5.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia kuanzisha utaratibu wa tozo ya ada ya shilingi 1,000 hadi shilingi 3,000 kwenye ada ya matumizi ya king'amuzi kulingana na kiwango cha utumiaji.

Kwa upande wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo napendekeza kuanza tozo ya asilimia 1.5 kwenye vifaa vinavyotumika kuzalisha, kusambaza, kudurufu na kutunza kazi za sanaa, uandishi na ubunifu mwingine kama vile mziki, filamu, vitabu, picha na aina nyingine za kazi. Vifaa hivi kama *radio, tv set, enabling recording, analogy radio recorders, analogy video recorders, CD, DVD, copier, digital jokebox, MP3 player*. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 9.6. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shirika la Vivango Tanzania napunguza tozo ya kudhibitisha ubora wa shehena za sukari zinazoiingizwa nchini kutoka shilingi sita kwa kilo hadi shilingi 2.5 kwa kilo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), nafuta tozo ya kipimio cha mzio inayotozwa shilingi 10,000 na tozo ya kipimo cha kilele inayotozwa kwa shilingi 25,000. Pendekezo hili linatarajia kuchochea mazingira wezeshi ya biashara.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mionzi; napunguza ada ya utambuzi wa mionzi kutoka asilimia 0.2 hadi asilimia 0.1 ya malipwani kwenye mizigo yote ya vyakula inayosafirishwa. Nafanya maboresho ya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Tume ya Nguvu za Mionzi kama zilivyoainishwa kwenye kiambatanisho namba tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi ya Zimamoto na Uokoaji Sura Namba 426 kwa kupunguza ada Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi ya Zimamoto na Uokoaji Sura Namba 426 kwa kupunguza ada na tozo mbalimbali kama ilivyooneshwa kwenye jedwali namba nne.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha napendekeza kufanya marekebisho ya Jedwali la viwango vya tozo na ada ya michezo ya kubahatisha chini ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Namba 41 kama ilivyooneshwa kwenye jedwali namba tano.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji; napendekeza mwaka wa fedha huu Serikali ipitishie uamuzi wa kuondoa ada ya kibali cha kuingia nchini (*Visa/Pass Fee*) kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka nchi ya Msumbiji kwa ajili ya mpango wa kubadilishana wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia kufanya maboresho ya sheria mbalimbali ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kupunguza muingiliano wa sheria ni kama ifuatavyo: -

(i) Kufuta kifungu cha 6(10)(b)(ii) na (iii) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania namba 12 ili kuwa na viwango vya kitaifa (*national standards*) kwa kuzingatia kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Viwango Namba Mbili. Lengo la hatua hii ni kufanya jumla la viwango vya kitaifa kubaki kwa Shirika la Viwango Tanzania pekee.

(ii) Kufuta kifungu cha 7(1)(b)(ii) na (iii) cha Sheria ya Udhhibiti wa Nishati na Maji, Sura Namba 414 ili kubakisha jukumu la viwango kwa Shirika la Viwango.

(iii) Kufuta kifungu cha 5(1)(c)(i) na (ii) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Namba Tatu ili kazi hiyo ifanywe na Shirika la Viwango Tanzania.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(iv) Kufuta kifungu cha 5(2)(c) cha Sheria ya Pamba Namba Mbili ya mwaka 2001 ili kubakiza jukumu hilo kwenye Shirika la Viwango.

(v) Kufuta kifungu cha 12(1)(b) na (c) cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania Namba 14 ya mwaka 2017 ili jukumu hilo liweze kufanywa na sheria ya viwango.

(vi) Kufuta kifungu cha 5(1)(i) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba Moja ya mwaka 2003 ili viwango hivyo vibaki kwenye sheria namba mbili ya mwaka 2009 ili mahitaji ya viwango vya *TMDA* yatawasilishwa na Shirika la Viwango Tanzania.

(vii) Kufuta kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba Moja ya mwaka 2003 ili kazi ya udhibiti wa machinjio ifanywe na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pekee.

(viii) Kufuta kifungu cha 3(2)(g) cha Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Namba 17 ya mwaka 2003 ili chanjo zisajiliwe na *TMDA* pekee.

(ix) Kufanya marekebisho ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Tasnia ya Maziwa ili Bodi ya Maziwa iweze kufanya ukaguzi huo.

(x) Kufanya marekebisho kwenye *marginal note* ya kifungu cha 46 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi ili kuondoa mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza majukumu hayo.

(xi) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 51 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi ili kuongeza sehemu mpya ya saba inayoweka hitaji la *collective management organisations* kutoa taarifa ya hesabu zilizokaguliwa kwa *copyright* ya ofisi ya kila mwaka.

(xii) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Tasnia Ya Pamba Sura Namba 201 ili jukumu

hilo la kusimamia viwango vya pamba liweze kufanywa na Shirika la Viwango pekee.

(xiii) Kufanya marekebisho ya sheria ya kifungu cha 23 cha Sheria ya Utalii Sura Namba 65 ili kumpa Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii mamlaka ya kutoa vibali vya kuridhiwa na Bodi.

(xiv) Kufanya marekebisho kwenye kifungu 28 cha Sheria ya Mbolea Sura Namba 378 ili jukumu la kuandaa kanuni za viwango liweze kufanywa na Shirika la Viwango.

(xv) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 17 cha Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Sura Namba 297 ili kuweka sharti la OSHA kutoa leseni.

(xvi) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 35 cha Sheria ya Serikali za Mitaa ili kuweka sharti la Mamlaka ya Miji kuanzisha vituo vya pamoja kwa ajili ya utaratibu, uhamasishaji na uboreshaji wa mazingira ya kibiashara.

(xvii) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 113 cha Sheria ya Serikali za Mitaa ili kuweka sharti la Mamlaka za Vijiji kuanzisha vituo vya pamoja kwa ajili ya utaratibu wa uhamasishaji wa mazingira bora ya biashara.

(xviii) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 6, 7 na 8 cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Sura Namba 290 ili kupunguza kiwango cha tozo kwa kitanda.

(xix) Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 3 cha Sheria ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi Sura Namba 220 ili kuondoa mkanganyiko uliopo katika sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, sheria hizo 19 ni sheria ambazo tunazibadilisha kama matakwa ya *blueprint* yetu inavyoelekeza ili kutengeneza mazingira bora ya ufanyaji wa biashara. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua nilizozitaja hapo, napendekeza kutoa tamko la kibiashara ya bima hapa nchini kwamba ushindani ufanyike kufuatia msingi wa soko huria. Kwa maana hiyo, biashara nyingine zinaweza kuelekeza mashirika ya bima yanayoaminika na Serikali ambayo ni Shirika la Bima la Taifa pamoja na Shirika la Bima Zanzibar kufanya biashara kiushundani kwa kutoa huduma bora tofauti na maelekezo yaliyokuwepo sasa ambayo yalitambua Shirika la Bima la Taifa pekee na fursa ya kupata taasisi za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe ya kuanza kutekelezwa sheria hizo ni tarehe Mosi mwezi wa Julai, isipokuwa pale itakavyopendekezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, sura ya bajeti ya mwaka 2022 inaonesha jumla ya shilingi trilioni 41.48 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika. Jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 28.02, sawa na asilimia 67.5 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 23.65 na mapato yasiyo ya kodi yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 4.37.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 4.65, sawa na asilimia 11.2 ya bajeti yote. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 5.78 kutoka soko la ndani ambapo shilingi trilioni 3.0 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na kiasi cha shilingi trilioni 2.48 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vilevile, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 3.03 kutoka soko la nje kwenye masharti ya kibiashara kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 41.48 kwa matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 26.48 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63.8 ya bajeti yote, ikijumuisha shilingi

trilioni 11.31 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na gharama nyingine za mfuko mkuu na shilingi trilioni 9.83 kwa ajili ya mishahara ikiwemo nyongeza ya mishahara, upandishaji wa madaraja kwa watumishi na ajira mpya. Aidha, shilingi trilioni 5.34 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ikijumuisha shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa kwa watumishi na wazabuni.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 15.0, sawa na asilimia 36.2 ya bajeti yote. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 12.31 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 82.0 ya bajeti ya maendeleo na shilingi trilioni 2.70 ni fedha za nje. Fedha za maendeleo za ndani zinajumuisha shilingi trilioni 1.11 kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge*, shilingi trilioni 1.44 kwa ajili ya kugharamia mradi wa kufua umeme wa Mwalimu Julius Nyerere, shilingi trilioni 1.18 kwa ajili ya mfuko wa barabara, shilingi bilioni 944.1 kwa ajili ya mifuko ya reli, maji na REA na shilingi bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, shilingi bilioni 230 kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madeni yaliyohakikiwa ya wakandarasi na shilingi bilioni 346.5 kwa ajili ya kugharamia elimu bila ada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza hapo awali, sura ya bajeti kwa mwaka 2022/2023 ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali hilo namba moja.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, maendeleo endelevu ya Taifa lolote duniani hujengwa kwa ushiriki wa wananchi wote nchini chini ya uongozi madhubuti na shupavu. Bajeti hii ni muendelezo wa kuiishi dhana hiyo kwani imeandaliwa kwa kushirikisha makundi yote katika jamii yetu ya Tanzania. Makundi hayo ni wawakilishi wa wananchi ambao ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, watalaamu mbalimbali kutoka taasisi za umma na binafsi pamoja na wananchi wa kawaida. Maoni yaliyowasilishwa na makundi hayo jamesaidia katika kuboresha bajeti hii. Kwa msingi huo,

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ni dhahiri kabisa hii ni bajeti ya wananchi, ni bajeti ya watu wote kwa ajili ya maendeleo ya watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, bajeti ya mwaka 2022/2023 inalenga kuongeza kasi ya kufufua uchumi na kuimarisha sekta za uzalishaji kwa ajili ya kuboresha maisha ya watu, hivyo nguvu kubwa itaelekezwa katika maeneo hayo chini ya kaulimbiu ya Kazi lendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele nilivyovianisha awali, wote tunafahamu kuwa tafsiri ya dhana ya ukuaji wa uchumi ni lazima ifungamane na maendeleo ya mtu mmoja mmoja na familia za Watanzania wote na tunajua kuwa mama hawezi kumuacha mwanae apate taabu, mama ana huruma, mama anajali na mama ana upendo kwa wanae. *(Makofi)*

Hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM imehakikisha kuwa bajeti hii inaenda kugusa na kuboresha maisha ya Watanzania wa hali zote kwa kuboresha sekta za uzalishaji. Hii itasaidia kuongeza ajira na vipato, kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo mfumuko wa bei uliotokana na mabadiliko ya kiuchumi duniani na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM inalenga kujenga misingi ya kiuchumi, matunda na mikakati hiyo yatafikiwa na kutunufaisha wote ili kila Mtanzania kwa nafasi yake ashiriki kwenye shughuli za uzalishaji mali zinazofuata sheria za nchi na kuchangamkia fursa za kiuchumi ili kujiongezea kipato na kuongeza mapato ya ndani ya Serikali.

Hivyo, nawahimiza wananchi wote, taasisi za umma na binafsi kudai risiti sahihi wanapofanya ununuzi wa bidhaa

na huduma ili kuhakikisha kuwa Serikali inakusanya kodi stahiki kutoka kwenye shughuli zinazofanyika. Vilevile nawahimiza wafanyabiashara na kampuni zote kuwajibika kwa hiari katika ulipaji wa kodi kwa Serikali kutokana na shughuli wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kumaliza naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza majukumu ya kuiletea maendeleo nchi yetu. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thati ya kuleta maendeleo huko Zanzibar. *(Makofi)*

Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia na kuratibu kazi za kila siku za Serikali na utendaji wa Serikali hapa Bungeni kwa umahiri mkubwa pamoja na kumsaidia vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuiletea Taifa letu maendeleo. *(Makofi)*

Naomba nikupongeze wewe binafsi kuwa mwanamke wa pili kushika uongozi wa mhimili huu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza Naibu Spika ambaye pia amechaguliwa kwa kishindo nafasi ya kuliongoza Bunge letu tukufu. *(Makofi)*

Tunategemea kuwa umakini wenu na weledi wenu na busara na hekima ambayo mmeshaionyesha itasaidia katika utekelezaji wa shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

chini ya Mwenyekiti wake mtani wangu Daniel Baran Sillo - Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua - Mbunge wa Kilindi pamoja na Kamati nzima kwa ushauri wao ambao wameutoa katika kuboresha taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa kazi nzuri ya kuongoza mhimili wa Mahakama. Kazi yenu ni nzuri sana na ni ya muhimu sana kwenye ustawi wa jamii, upendo na amani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, neno la Mungu linasema; haki huinua Taifa, bali dhambi ni aibu ya watu wote utaipata kwenye Mithali 14:34. Endeleeeni kusimamia sheria na kutenda haki mnapotekeleza majukumu yenu. *(Makofi)*

Niwapongeze vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Tanzania vikiongozwa na JWTZ kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya, wameiheshimisha nchi yetu na kuifanya kuwa nchi ya tofauti duniani kote. Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kila wakati anatumia Wakazi wa Fedha kutekeleza mahitaji yenu ya kibajeti sawasawa na mahitaji yenu, na sisi tutafanya hivyo ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Mwanasheria wa Serikali, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na wataalam wote wa Wizara zote na Taasisi zote. *(Makofi)*

Kwa unyenyekevu nawashukuru viongozi na waumini wa dini zote kwa kuendelea kuliomba Taifa. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwaomba viongozi wote na waumini wote tuendeele kumuomba Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ili Mungu aendeele kumjalilia afya njema hekima na unyenyekevu na dhamira yake njema ya kusimamia rasilimali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge wa Jimbo la Kojani ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano na msaada anaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumshukuru Bwana Emmanuel Mpawe Tutuba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa usimamizi wa kazi za kila siku za Wizara na uratibu mzuri wa maandalizi ya bajeti hii, akisaidiwa na Naibu Makatibu Wakuu. *(Makofi)*

Ninawashukuru pia wakuu wa taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango; Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara; pamoja na watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, nipende kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwaletea maendeleo wananchi wake. Washirika hao kuchangia bajeti ya Serikali ni pamoja na Serikali za Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uingereza, Ujerumani na Uswisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mashirika na Taasisi za Kimataifa ambazo kuchangia bajeti hii ni Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kuwait, Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, Umoja wa Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Umoja wa Mataifa na Mashirika yote yaliyopo chini yake, Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa, pamoja na Shirikisho la GAVI.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninapenda kuyatambua Mashirika yote yasiyo ya Kiserikali ambayo yamesaidia katika uendelezaji. *(Makofi)*

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha, nitumie fursa hii kuipongeza sana timu ya Yanga kwa mwenendo wake mzuri wa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Yanga kwa mwenendo mzuri wa mwaka huu, naomba nitumie fursa hii kumwomba radhi boshi wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kitendo alichokifanya mwanangu Fei Toto kule Mwanza. *(Kicheko)*

Boshi niwie radhi, nilipompeleka Fei Toto kule Yanga sikujua atakuja kuwafanyia kitu mbaya kama hivi, mpaka nasikia anatafutwa maliasili eti kaua mnyama bila kibali. *(Makofi)*

Nakupongeza Mheshimiwa Anthony Mavunde wewe ndio ulikuwa Mwenyekiti wa kuisaidia Yanga ikiwa kwenyea mapito. Nampongeza GSM kwa kurejesha furaha ya wananchi hasahasa kwa usajili wa Fiston Mayele. Mayele amekuwa maarufu kuliko Makatibu Wenezi wa baadhi ya vyama vya siasa. *(Kicheko)*

Nawapongeza sana na marafiki zangu wa Simba kwa kuwakilisha vyema kwenye mashindano ya kimataifa, wananjua kimataifa huwa tupo pamoja siwezi kukana Bendera ya Taifa langu kwa ajili ya utani wa jadi. Nampongeza sana Mheshimiwa Mavunde pamoja na wengine wote pamoja na Antony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuwasilisha hotuba hii. Kwa moyo wa dhati napenda kuishukuru familia yangu, ikiongozwa na mke wangu Neema Nchemba nadhani yupo hapa leo, pamoja na kijana wangu, Joshua Mwigulu ambaye amewakilisha watoto pamoja na mdogo wangu Perpetua kwa kuendelea kunitia moyo na kuniombea wakati wote ninapokuwa katika majukumu yangu. *(Makofi)*

Vilevile nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi, marafiki zangu wa majira yote, kwa kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge nitakuja kuwatembelea nikishamaliza majukumu ya Kimataifa, *songe lizigizigi mukembyetui*.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania Wote kwa kunisikiliza.

Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania. Kazi lendelee!

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo naomba sasa kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO,  
MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA  
MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI  
MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2022/23 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako *Tukufu* lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022/23. Bajeti hii inawasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kifungu cha 124 (4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020.

**2. heshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii ninawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina Bajeti ya Serikali. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato; Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa

Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2022 nayo ni sehemu ya bajeti hii.

**3. Mheshimiwa Spika**, makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 yameandaliwa kwa kuzingatia nyaraka na miongozo mbalimbali ikiwemo: Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020; Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo; na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeyaridhia.

**4. Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23. Kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumshukuru sana ***Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*** kwa kuendelea kuniamini katika dhamana hii ya kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango.

## **I. MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI 2021/22**

### **Mwenendo wa Mapato**

**5. Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka 2021/22, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi trilioni 37.99 kutoka katika vyanzo vyote vya ndani na nje

ambapo hadi Aprili 2022, kiasi cha shilingi trilioni 29.84 kimekusanywa. Mchanganuo wa mapato yaliyopatikana hadi Aprili 2022 ni kama ifuatavyo:

(i) Mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), yalikuwa ni shilingi trilioni 17.20, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 21.78;

(ii) Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi trilioni 2.03, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 3.05;

(iii) Mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 759.0, ambapo lengo la mwaka ni shilingi bilioni 863.9;

(iv) Misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia shilingi trilioni 3.93, sawa na asilimia 92.0 ya lengo la mwaka la shilingi trilioni 4.27;

(v) Mikopo kutoka vyanzo vya ndani ilifikia shilingi trilioni 4.12, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 4.99; na

(vi) Mikopo yenye masharti ya kibiashara ilifikia shilingi trilioni 1.81, ambapo lengo la mwaka ni kukopa shilingi trilioni 3.05.

## **Mwenendo wa Matumizi**

**6. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, jumla ya shilingi trilioni 29.40 zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 18.79, zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha shilingi trilioni 6.73 kwa ajili ya mishahara, shilingi trilioni 4.79 Matumizi Mengineyo na shilingi trilioni 7.27 kugharamia deni la Serikali. Jumla ya shilingi trilioni 10.61, sawa na asilimia 74.1 ya lengo la mwaka zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kiasi hiki hakijumuishi baadhi ya fedha zilizopelekwa moja kwa

moja kwenye utakelezaji wa miradi (D-fund). Fedha hizi zitajumuishwa kwenye hesabu za Serikali mwishoni mwa mwaka wa fedha pindi taratibu za kihesabu zitakapokamilika.

### **Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Serikali**

**7. Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2022, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 69.44, sawa na ongezeko la asilimia 14.4 ikilinganishwa na shilingi trilioni 60.72 Aprili 2021. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 22.37, sawa na asilimia 32.2 na deni la nje ni shilingi trilioni 47.07, sawa na asilimia 67.8. Kati ya deni la nje, deni lenye masharti ya kibiashara ni shilingi trilioni 14.27, sawa na asilimia 30.3. Hivyo, sehemu kubwa ya deni la nje ni mikopo yenye masharti nafuu.

**8. Mheshimiwa Spika**, tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali iliyofanyika Novemba 2021 kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134 ilionesha kuwa viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika Tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa: uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 31.0 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 18.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; na uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 142.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180.

### **Tathmini ya Kukopesheka kwa Nchi (Credit Rating)**

**9. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, zoezi la tathmini na ukadiriaji wa kukopesheka kwa nchi (credit rating) ambalo lilisimama hapo awali lilianza tena kupitia benki ya Citibank ambayo ilikuwa mshauri wa Serikali. Hadi kufikia mwezi Mei 2022, Serikali imefikia hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za

ununuzi ambapo imefanikiwa kuchagua kampuni mbili ambazo zinatambulika kimataifa na kupitia mikataba yao. Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na kampuni hizo pamoja na kuandaa takwimu mbalimbali ambazo zitatumika katika zoezi la tathmini na ukadiriaji wa kukopesheka. Serikali inategemea kukamilisha zoezi hili ndani ya mwaka 2022/23. Naomba nichukue fursa hii kuziomba taasisi za Serikali, za binafsi na benki zitakazopata nafasi ya kuhojiwa na wataalamu wa Kampuni hizo kutoa ushirikiano kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi. Kukamilika kwa zoezi hili kutatuwezesha kuongeza wigo wa wakopeshaji kwa Serikali na makampuni binafsi hususan katika masoko ya mitaji ya kimataifa (International Capital Markets).

## II. BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**10. Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 ni ya pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye dhima ya *“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”*. Aidha, dhima kuu ya bajeti ya mwaka 2022/23 kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni *“Kuongeza Kasi ya Kufufua Uchumi na Kuimarisha Sekta za Uzalishaji kwa ajili ya Kuboresha Maisha”*. Katika utekelezaji wa dhima hiyo kwa mwaka 2022/23 kipaumbele kitakuwa katika sekta za uzalishaji zikiwemo Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Nishati, Uwekezaji na Biashara. Lengo la Serikali ya CCM inayoongozwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM ni *kujenga uchumi, kukabiliana na umasikini pamoja na ukosefu wa ajira hasa kwa vijana*.

### Shabaha za Uchumi Jumla

**11. Mheshimiwa Spika**, kutokana na mambo yaliyozingatiwa katika uandaaji wa bajeti hii, shabaha



za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:

(i) Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 4.7 mwaka 2022 na asilimia 5.3 kwa mwaka 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 hadi 7.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 11.7 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23; na

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4);

### III. MAMBO MUHIMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**12. Mheshimiwa Spika**, nchi zote duniani zinapita kwenye athari kubwa za UVIKO 19 na vita kati ya Urusi na Ukraine iliyoanza Februari 2022 ambayo imeendelea kuleta athari katika mataifa mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania kutokana na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Madhara ya UVIKO-19, yamekuwa na makali zaidi baada ya uchumi kuanza kurejea, kwa kuwa nchi zilikuwa katika "lockdown" na nyingine kupunguza uzalishaji wa bidhaa. Uchumi unaporejea katika hali ya uzalishaji mataifa yote yanahitaji bidhaa ambazo ziliachwa kuzalishwa hivyo kusababisha upungufu. Kungali hali iko hivyo, vita kati ya Urusi na Ukraine imeongeza upungufu wa bidhaa kwa kuathiri uzalishaji na mnyororo wa usambazaji. Kwa mujibu wa Shirika la Chakula Duniani, nchi za Urusi na Ukraine ni kati ya

nchi zenye uzalishaji na uuzaji mkubwa wa mazao mbalimbali ikiwemo ngano, mafuta ya kula na shayiri.

**13. Mheshimiwa Spika**, nchi ya Urusi ni ya pili katika uzalishaji wa gesi asilia na bidhaa za mafuta ya petroli duniani. Kadhalika, nchi ya Ukraine ni miongoni mwa nchi zinazozalisha mafuta ya alizeti kwa wingi duniani. Kufuatia madhara haya ya vita, ni dhahiri kuwa uchumi na gharama za maisha duniani hazitabaki zillivyokuwa awali. Ndio maana **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM** ameelekeza bajeti hii ya Serikali ijikite kuchukua hatua za kutoa unafuu kwa wananchi na kufufua uchumi. Bajeti hii itatilia mkazo Sera za Mapato, Sera za matumizi, kujali ufanisi (Value for Money), mapambano ya vitendo vya rushwa na kuwekeza kwenye Sekta za uzalishaji ili kutengeneza ajira kwa vijana.

#### **Mikakati ya kuongeza Mapato Mwaka 2022/23**

**14. Mheshimiwa Spika**, nawapongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania na taasisi zingine zinazokusanya mapato na maduhuli ya Serikali. Tumepiga hatua kubwa kwenye makusanyo ya ndani. Hadi Aprili 2022, ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa umefikia shilingi trilioni 19.99, sawa na asilimia 93.3 ya makadirio ya kukusanya shilingi trilioni 21.42 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yamefikia shilingi trilioni 17.20, sawa na asilimia 94.5 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 18.2, mapato yasiyo ya kodi yamefikia shilingi trilioni 2.03, sawa na asilimia 81.2 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 2.5 na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yamefikia shilingi bilioni 759.0, ikiwa ni asilimia 104.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 724.1 katika kipindi hicho.

**15. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, bado kuna vitendo vya rushwa kwenye ukusanyaji wa

mapato, hasa kwenye kodi kubwa, mapato ya Mamlaka za Serikali za mitaa na ardhi. Kuna mapato ya Serikali yanaingia kwenye mifuko ya watu binafsi. Hii inafanyika kwa kukadiria viwango vya juu ili katika majadiliano ya kwenda kwenye kodi stahiki kinapunguzwa kiasi chini ya kile kinachostahili na kilichopunguzwa kinaingia mifuko binafsi. Serikali imeshapokea taarifa kadhaa za matukio ya aina hii na inaendelea kulifuatilia kwa umakini sana jambo hili. Wale wanaokataa kutoa rushwa ndio wanaoonewa zaidi, ndio wanaobambikwa makadirio yasio halisi kwa kuwakomoa, ndio wanaotishiwa kufilisiwa. Jambo hili halikubaliki. Nitoe rai jambo hili liachwe mara moja. Tuache utaratibu wa kufanya majadiliano (bargaining) kwenye kulipa kodi. Watumishi wa umma wanaokusanya kodi na maduhuli ya Serikali wanaowaomba wafanyabiashara wawapunguzie wanachotakiwa kulipa ili kisichoingia serikalini wapate wao wanafanya makosa ya uhujumu uchumi. Kadhalika wapo wafanyabiashara na wauza maduka wanaowaambia wananchi “nikupe bei ya risiti ya TRA au bila risiti”, na bei ile isiyo na risiti inakuwa ndogo kuliko bei ya risiti ili kuwashawishi wakwepe kulipa mapato ya Serikali na wao wenyewe wabaki na kodi ya Serikali. Huu ni uhujumu uchumi. Naagiza vitendo hivyo vikome mara moja na ambaye hataacha atakutana na mkono wa sheria.

**16. Mheshimiwa Spika**, nitoe rai kwa watanzania wote kulipa kodi wanayostahili kulipa, wala wasiogope vitisho, na wala wasidhanie kuwa kuna wakati watakulipizia kisasi, toa taarifa ofisi ya **TAKUKURU** iliyo karibu nawe, ama toa taarifa Idara ya Usalama wa Taifa iliyo karibu nawe. Watumishi wa aina hiyo watakaobainika hutawakuta tena ofisi za umma, wala hatutawahamisha, **Tutawafukuza kazi**. Mheshimiwa Rais anachukizwa sana na ukosefu wa maadili na uaminifu wa baadhi ya watumishi wa umma. Asitokee anayedhani ana haki sana ya kuwa mtumishi wa

umma, hii ni dhamana tu. Wala asitokee anayedhani vijana wahitimu wa kitanzania walioko mtaani na hawana kazi akadhani hawana haki ya kuwa watumishi wa umma. Tunao uwezo wa kupangua safu nzima ya utumishi wa umma na tukapanga safu mpya ya vijana hawa walioko mtaani. Kwenye uadilifu na uaminifu, hata tusibabaishane, ***Tutawakamata, Tutawashitaki na Tutawafunga. Lazima tukomeshe kabisa vitendo vya rushwa kwenye mapato na matumizi.***

**17. Mheshimiwa Spika**, mambo mengine tunayotarajia kuyafanya kwenye sera ya mapato ni kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kufanya makadirio ya kodi kwa wafanyabiashara wadogo ambao hawana uwezo wa kutunza kumbukumbu na kutengeneza hesabu za biashara zao (Presumptive Regime), kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia ili kurahisisha uwasilishaji wa ritani za kodi kielektroniki (electronic filing) na ulipaji kodi kwa wakati; Kuimarisha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) na kuhimiza malipo ya Serikali kutumia Namba ya Kumbukumbu ya Malipo; na kuimarisha mifumo ya usimamizi katika Mashirika, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati. Ili kukuza mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi, kutoa ajira na kuongeza mapato, Serikali inapanga kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuipa nafasi zaidi sekta binafsi. Aidha, Serikali imepanga kuendeleza uanzishwaji wa vituo vya pamoja vya utoaji huduma ili kuwezesha huduma muhimu zinazohitajika katika kuanzisha na kufanya biashara kupatikana sehemu moja.

### **Mkakati wa Kubana Matumizi**

**18. Mheshimiwa Spika**, Sera za matumizi katika mwaka 2022/23 zitakuwa za kubana na kuondoa matumizi

yasiyo ya lazima. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali inatarajia kudhibiti ununuzi na matumizi ya magari kwa kuzingatia Waraka wa Rais na.1 wa mwaka 1998 kuhusu hatua za kubana matumizi ya Serikali na Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina na stahili za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma ili kubana matumizi. Baadhi ya maeneo yenye gharama kubwa sana kwa serikali ni Ununuzi wa magari, Ununuzi wa mafuta ya uendeshaji, Ununuzi wa vipuri na matengenezo. Tunapanga kuchukua hatua za muda mfupi na za muda mrefu. **Lazima**, matumizi ya Serikali na matumizi ya watumishi wa umma yote yaakisi ugumu wa maisha wanayopitia wananchi wetu kufuatia athari za majanga hususan ya UVIKO-19 ili fedha zinazopatikana zifanye mambo muhimu hapa nchini. Hatua za muda mfupi zitakazochukuliwa ni kupunguza safari za ndani na nje, kukata fedha za ununuzi usio wa lazima, kupunguza ukubwa wa uwakilishi kwenye mikutano ya ndani na nje, na tutapimiana mafuta ya magari ya Serikali kila mwezi kufuatana na shughuli za lazima. Utaratibu huu unatumika kwa wabunge, na hawajaacha kufanya shughuli majimboni mwao, BOT wanapimiwa, baadhi ya Taasisi za UN wanapimiwa. **Namwelekeza Mlipaji Mkuu** wa Serikali afanye uchambuzi wa wastani wa mahitaji ya mafuta kufuatana na aina ya majukumu, ulazima wa majukumu na ngazi katika utumishi.

**19. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa hatua za muda wa kati na muda mrefu, napendekeza Serikali kubadili kabisa utaratibu uliopo kwa kuwakopesha magari watumishi wenye hadhi ya kuwa na gari la Serikali wawe na magari yao wenyewe, wafanye matengenezo wenyewe, wanunue vipuri wenyewe na masuala ya mafuta yaangaliwe kwa utaratibu utakaonekana unafaa. Kwa sasa Serikali ina magari **zaidi ya 15,742, pikipiki 14,047 na mitambo 373** na inatumia zaidi ya shilingi **558,453,134,226.05** kwa

mwaka kwa ajili ya ununuzi wa magari, ununuzi wa mafuta ya uendeshaji, ununuzi wa vipuri na matengenezo ambapo kwa sasa ni **zaidi** ya shilingi bilioni 500. Ukiondoa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na Mahakama, upande wa Serikali wabaki viongozi wakuu wa Wizara, Mashirika, wakala, mikoa, wilaya na Miradi ambao wasimamizi watakuwa eneo la mradi (site) muda mwingi ambapo kwenye makundi haya hawatazidi watano kwa taasisi, wengine wote wenye stahili ya gari la Serikali wakopeshwe, watumie magari yao, watasimamia vizuri matumizi, matengenezo, mafuta na vipuri. **Tutaondoa utaratibu uliozoeleka, dereva na gari anapitishwa chini, boshi anapanda ndege mpaka Mwanza au Mbeya kutoka Dar es Salaam na kurudi hivyo hivyo. Kuna utafiti wa siri ulifanywa, kwa siku moja yalibainika magari ya Serikali yaliyotoka Dodoma kwenda Dar es Salaam yalikuwa 132, na yaliyokuwa yanatoka Dar es Salaam yakipishana kuja Dodoma yalikuwa 76, na mengine 8 yalikuwa yamepinduka. Je kwa mwezi ni gharama kiasi gani?**

**20. Mheshimiwa Spika**, kwa utaratibu huo gharama za matumizi ya magari serikalini zitakuwa takribani **shilingi 50,508,038,843.09**. Zaidi ya shilingi **billion 500** zitaokolewa na kuelekezwa kwenye ununuzi wa dawa muhimu hospitalini, kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati, na kutekeleza miradi ya maendeleo. *Tumezidi kupenda ubosi, magari makubwa kwa kila mtu serikalini, matumizi ya starehe, wakati katika nchi yetu bado kuna watu wanapata shida kupata mlo mmoja.* Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania ameielekeza Wizara ya Fedha na Mipango ifanyie kazi jambo hili la kuelekeza fedha kwenye matumizi ya msingi tu. *Jambo hili halitaathiri mtumishi bali litafanyika gradually, yaani by phasing out, yaani tunabadilisha kadri watu wanavyopanda kustahili kukopa na kutokuajiri madereva kadri wanavyostaafu na kadri maafisa wanavyohamia*

*skimu za kukopa. Madereva wengine watabaki kwa viongozi, magari ya miradi ya site, na magari ya pool. Mtoto wa Dereva sio lazima naye aje awe dereva.*

**21. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hayo, Serikali itaachana na mfumo wa sasa wa Ununuzi wa Umma (Transactional Procurement) ambao umeshindwa kuleta tija kwa kuwa msingi wake mkubwa ni ulinganishaji wa zabuni zilizofunguliwa badala ya bei za bidhaa na huduma ambazo tunazijua. Mara nyingi bei hizi za ununuzi zimekuwa kubwa kuliko zile zilizopo sokoni kwa jumla na hata rejareja (wholesale and retail) na ingekuwa tunanunua kwa ajili ya nyumbani kwetu au kwa ajili ya kampuni zetu tusingekubali bei hizo. Napendekeza kuwa, ununuzi wa umma uwe wa kimkakati (Strategic Sourcing) kwa kuzingatia ukubwa wa ununuzi wa Serikali na sekta ya umma kwa ujumla (Economies of Scale) pamoja na uwiano na mfanano wa bidhaa na huduma zinazotumika serikalini na sekta ya umma yaani *synergies*. **Sasa Serikali ni moja, bidhaa zinafanana, hata ofisi zilizoko mkoa mmoja, ila inatokea kila mmoja anakuwa na bei zake licha ya bidhaa kufanana.**

**22. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti matumizi, Serikali imepanga kufanya maboresho katika mfumo wa ununuzi wa umma ili kuhakikisha ununuzi wa umma unakuwa wenye tija na unaoendana na ubora na thamani ya fedha. Tutaendelea kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) ikiwemo kuweka ukomo wa bei za bidhaa na huduma zinazotumika serikalini ili kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali; Wizara ya Fedha na Mipango itahakikisha kuwa, bei zote za bidhaa na huduma zinazotumika sokoni kwa jumla na rejareja (Price Catalogue) zinaingizwa kwenye mfumo wa TANePS na kuwa kikomo (limit) cha bei zitakazotumika Serikalini. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba mfumo wa TANePS hauruhusu watoa huduma na wakandarasi au wauza

bidhaa wanaotoa bei zilizo zaidi ya soko kupata zabuni (tender) kwenye sekta ya umma.

**23. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza hatua hii, Wizara ya Fedha na Mipango itatoa Waraka wa Hazina kuelekeza idara na taasisi nunuzi kununua bidhaa zinazofanana kwa bei ya kikomo. Endapo kutakuwa na ulazima wa kununua magari kwa wingi, Serikali itafanya mazungumzo na Toyota Tanzania na Japan (kwa njia za kidijitali) ili kufanya makubaliano ya jumla (framework agreement) yatakayowezesha Serikali kupata bei nafuu kama ilivyo kwa mashirika makubwa ya kimataifa kama vile UNDP. Hii itasaidia kuokoa fedha katika ununuzi wa magari pamoja na vipuri. Zoezi hili litafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi. **Fedha zitakazookolewa kutokana na hatua hizi Serikali itazielekeza katika ujenzi wa vyuo vya ufundi kwenye Wilaya zetu kwa ajili ya watoto wetu.**

**24. Mheshimiwa Spika**, napendekeza matumizi ya mifumo ya TEHAMA iwe chaguo namba moja katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kubana matumizi. Kuanzia mwaka ujao wa fedha ofisi za serikali zianze *paperless operations* kwenye shughuli zake. Kila shughuli zifanyike kwa mtandao, **mbona Bunge mmeweza?** Kumbi za Mikoa na Wilaya zote ziwe na miundombinu ya mikutano ya njia ya Mtandao (Virtual Meeting). Hata wabunge mtaweza kushiriki vikao vya Mabaraza ya Madiwani mkiwa Dodoma au hata nje ya nchi. Utaratibu wa kuitana Wakuu wa Mikoa nchi nzima, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, na magari kwa nchi nzima na umbali wote kuja kukaa mahali na kusikiliza ni mzigo kwa walipa kodi. Tumekopa fedha kwa ajili ya mkongo wa taifa, tunalipa deni, ila tunatumia gharama kubwa kwa kufanya kazi *manually*. Mheshimiwa Rais anajenga chuo kikubwa cha TEHAMA, lakini tunaogopa TEHAMA. Tunataka kufuta usemi wa *“Government works on papers”* Sasa



tunasema “*Government works on records*”. Tumeongea na Wizara ya Kisekta kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais kujadili utekelezaji wa jambo hili, Wizara tafuteni mtu wa kusimika hiyo mitambo kila Wilaya. Eti mkurugenzi anakuja tokea Wialaya ya pembezoni gharama yote ile eti ameleta barua, au anakuja kutoa ufafanuzi, au wanakuja nchi nzima kwenye kikao ila anaongea mmoja kwa uwakilishi.

**25. Mheshimiwa Spika**, kuhusu ufanisi katika Miradi ya Maendeleo, Mheshimiwa Rais ameelekeza kuangalia upya taratibu za ununuzi na thamani ya fedha kwenye Miradi ya Maendeleo. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - CAG ilionesha bado kuna dosari katika matumizi ya Serikali hususani kwenye ununuzi mkubwa na miradi ya maendeleo. Serikali imefuatilia eneo hili na kugundua mfumo wa kufanya ukaguzi wa taratibu za ununuzi (Compliance Audit) na wa kifedha (Financial Audit) ina upungufu. Yapo mazingira ya taratibu zote kufuatwa katika ununuzi, sheria zote za ununuzi kufuatwa, na hatua zote za ukaguzi kufuatwa lakini fedha ya umma kuibiwa. Hii inatokana na baadhi ya watumishi wa umma wasio waaminifu kupanga njama na wafanyabiashara wasio wazalendo kupandisha bei za bidhaa kwenye zabuni na kujipangia hata huyo aliyeshindania kwa kiwango cha chini anakuwa mbali na bei ya soko au gharama halisia.

**26. Mheshimiwa Spika**, kwenye mchezo wa aina hii, wanafuata sheria ya ununuzi, wanafuata taratibu za kumchagua aliyeshinda bei ya chini, ila kwa kuwa hiyo iliyoshindaniwa kwa bei ya chini ni ya chini tu ikilinganishwa na wazabuni wengine ambapo zabuni imefanywa kwa njama basi bei hizo zinakuwa juu sana ikilinganishwa na bei za bidhaa hizo kwa bei ya soko. ***Hawa ni watu wanaoiba japo wamezingatia sheria. Serikali itaendelea kumjengea uwezo*** CAG ili kumwezesha kukagua thamani ya fedha kwenye miradi yote mikubwa (**Value for Money**) na kufanya

ukaguzi kwa wakati ili kukabiliana na tatizo hili. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kumwongezea fedha **Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)** ili apate watumishi wa kutosha kwa kuajiri na kuwahamisha watumishi kutoka idara yoyote ya Serikali na kuwajengea uwezo kwa mafunzo na weledi wa ukaguzi wa thamani ya fedha ili kuweza kukabiliana na tatizo hili. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itafanyia marekebisho Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kuziba mianya inayotoa fursa ya miradi kutekelezwa bila kujali thamani ya fedha (Value for Money) kama alivyoelekeza **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania**.

**27. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani kwa kuvijengea uwezo wa kitaaluma na kuongeza idadi ya watumishi katika fani mbalimbali kama vile TEHAMA, uhandisi, ukadiriaji majenzi, wakemia, wanasheria na fani nyingine ili kuondokana na dhana ya wakaguzi wa ndani kuwa na taaluma ya fedha pekee. Aidha, Serikali itafanya marekebisho ya Kanuni za Fedha za Umma kwa kuziwezesha Kamati za Ukaguzi kuwa na wajumbe wa nje watatu ikiwemo Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi ili kuongeza uhuru na ufanisi wa kamati za ukaguzi kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022. Pamoja na mambo mengine, marekebisho ya Kanuni hizo yatazitaka Kamati za Ukaguzi kuwasilisha taarifa za ukaguzi wa ndani kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kila robo mwaka.

**28. Mheshimiwa Spika**, Serikali itafanya tathmini ya muundo na majukumu ya Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali ikiwemo kufanya stadi ya kujifunza kutoka nchi nyingine zenye Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu Serikali kama Tanzania ili kuangalia muundo unaostahili na kukidhi mahitaji ya Idara hiyo kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na ufanisi. Vilevile napendekeza Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kuwa na fungu lake (Independent Vote) pamoja na

kuongeza idadi ya wakaguzi wa ndani ili kuimarisha na kuboresha ufanisi katika utendaji. Napendekeza kuanzia mwaka wa fedha 2022/23 taarifa za wakaguzi wa ndani zipelekwe moja kwa moja kwa *Internal Auditor General* (IAG) kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais wakati anapokea taarifa ya CAG. IAG atakuwa anawasilisha taarifa hizi kwenye Baraza la Kazi chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kila Waziri wa kisekta aweze kupokea hoja zinazomhusu, kuzifanyia kazi na kuchukua hatua za kinidhamu. Wakaguzi wa ndani wa ofisi mbalimbali watatoa msaada na ushauri kwa maafisa masuhuli husika ila taarifa zote ziende kwa IAG na nakala zipelekwe kwa viongozi walio juu ya maafisa masuhuli. Kwenye ngazi za Halmashauri, nakala ziende kwa wenyeviti, mamea na wakuu wa Wilaya; kwa Sekretarieti za Mkoa, nakala ziende kwa Mkuu wa mkoa; Kwa wizara, nakala ziende kwa mawaziri; na kwa taasisi, mashirika na wakala, nakala ziende kwa wenyeviti wa Bodi.

**29. Mheshimiwa Spika**, kuna wakati inatokea tunaona miradi ikikamilika, fedha zote zikiwa zimetumika lakini miradi ikiwa chini ya viwango, jengo au mradi unakamilika ungali bado unanukia rangi lakini ukiwa umetapakaa nyufa kila kona, sementi na tofali zikiwa ni mchanga. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali inamwelekeza IAG pamoja na vitengo vya ukaguzi wa ndani kuanza kufanya *Technical Audit* badala ya (Financial Audit) peke yake na kuanza kufanya ukaguzi kwa wakati (Real Time Audit) na ukaguzi wa mifumo (Systems Audit) ili kupunguza uwezekano wa upotevu fedha kupitia mifumo ya ukusanyaji au matumizi mabaya ya fedha za umma.

**30. Mheshimiwa Spika**, kwenye eneo la usimamizi wa fedha za umma, Serikali itahakikisha kuwa Sheria ya Fedha za Umma SURA 348 inasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo na pale itakapotokea sheria na taratibu za usimamizi wa fedha zimekiukwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kujibu hoja zilizotolewa na

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na hoja za wakaguzi wa ndani, Afisa Masuuli wa Fungu husika pamoja na Maafisa wake wa chini watachukuliwa hatua kulingana na Kanuni za fedha zinazohusiana na adhabu (Surcharge and Penalties) za mwaka 2005. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuwakata mshahara kati ya asilimia 5 hadi 30 kwa mwezi kulingana na uzito wa kosa waliloshiriki kulitenda na kupendekeza kwa Mamlaka zao za nidhamu, kuvuliwa wadhifa alionao au kuondolewa dhamana ya kuwa Afisa Masuuli wa fedha za Fungu husika.

**31. Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Serikali imetoa mwongozo wa ufuatiliaji na tathimini (**Monitoring Evaluation**) yaani (M&E), na sasa inaandaa Sera ya M&E, na baadae Sheria ya M&E. **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania** anakerwa sana na udhaifu uliopo katika eneo la M&E serikalini. Eneo hili litaongezewa rasilimali watu na fedha na litapewa malengo yanayopimika. Pamoja na hayo, napendekeza kuanzia mwaka ujao wa fedha taarifa za M&E ziwasilishwe kwenye Baraza la Kazi chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**32. Mheshimiwa Spika, Vitendo vya Rushwa** vinasababisha utekelezaji wa miradi kuwa chini ya viwango kwa kuwa fedha zilizopangwa kwenda kwenye mradi mingine zinachepushwa na kwenda kwenye mikono ya watumishi wasio wazalendo. **Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** amelikemea vikali jambo hili. Watu wanapanga kuanzia wakati wa maandalizi ya bajeti, wanafuatilia mchakato wote, siku ikipitishwa na Bunge wanakesha wakishangilia bajeti yao imepita, mradi unaposainiwa wanaanza kugawana fedha kabla ya utekelezaji wa mradi. Serikali itaendelea kuimarisha **Technical Audit, Value for Money Audit** na **Real Time Audit** katika mwaka ujao wa Fedha. Aidha, Serikali haitawanyima fedha

wananchi wa halmashauri yoyote kwa sababu ya hati chafu, wala haitarudisha fedha kwenye Mfuko Mkuu kwa sababu hazijatumika kutokana na sababu za uzembe wa baadhi ya watumishi wa umma. **Wananchi hawahusiki na hati chafu. Tutawabaini wazembe, Tutawakamata, Tutawashitaki na Tutawafunga.**

**33. Mheshimiwa Spika**, watumishi wa umma ni kiungo muhimu sana katika maendeleo ya nchi. Mikataba yote inaingiwa na watumishi wa umma; ununuzi wowote wa Serikali unafanywa na watumishi wa umma; miradi yote ya Serikali inatekelezwa na watumishi wa umma; na mapato yote yanakusanywa na watumishi wa umma. Wananchi waliwasomesha watumishi wa umma kwa kujinyima, wamewaamini wakusanye na kutumia kodi zao kwa kuwapa huduma. Bado kuna vitendo vingi kwenye utumishi wa umma vinavyopunguza ufanisi katika Taifa lao. "*Wage bill*" yetu ni kubwa kuliko viwango vinavyotakiwa kiuchumi na wakati huo huo ikama hazijatimia na kila mtaa tuna kijana anatafuta kazi. Hii ina maana kuna watu wanalipwa bila kufanya kazi au wanalipwa bila kuwa na ufanisi kazini.

**34. Mheshimiwa Spika**, imezoeleka kwa mfano Makatibu Wakuu, Manaibu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, Makatibu Tawala wa Wilaya, wakurugenzi, wakuu wa taasisi mbalimbali, wakuu wa idara mbalimbali tangu uhuru wakitenguliwa huendelea kulipwa mshahara ule ule sawa na aliyeko kazini mpaka anastafu. Unaweza kukuta nchi ina Wizara 25 ila ina Makatibu Wakuu 50 au zaidi, au Halmashauri 184 lakini kuna wakurugenzi 300 au zaidi na hivyo hivyo kwa nafasi nyingine. Wengine wamesabaisha upotevu na hasara kwa Taifa, wote wanaendelea kuwabebesha mzigo watanzania na wanaziba nafasi ya ajira mpya kwa vijana kwa kulipwa mshahara wa nafasi walizotolewa. Napendekeza yeyote aliyetokea kwenye nafasi yake ya

kuteuliwa akitolewa akabaki kwenye utumishi wa umma arejee pia kwenye mshahara wake wa zamani ili kuwapunguzia watanzania mzigo wa kuwalipa watu waliokaa benchi huku wakiziba nafasi za vijana wanya kuajiriwa. Mambo haya hayavutii lakini lazima tuambizane ukweli. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anakerwa kuona fedha nyingi zinakwenda kwenye matumizi ya kawaida

**35. Mheshimiwa Spika**, napendekeza mashirika yote ya umma yenye kufanya kazi kwa misingi ya kibiashara yafanye kazi kwa ufanisi na faida. Yale yasiyofanya kazi kibiashara tutayapima kwa namna wanavyoweza uchumi kuchangamka na jinsi wanavyoimarisha huduma wanazozitoa kwa jamii. Mashirika mengi ni mzigo kwa Serikali kwa kutegemea ruzuku kutoka serikalini ili yajiendeshe. Kwa nchi zilizoendelea, mapato makubwa ya Serikali yanatoka kwenye mashirika yake ili kuwapunguzia mzigo maskini wa kulipa kodi ili ziendeshe mashirika hayo lakini pia kupunguzia Serikali kutegemea kukusanya fedha kutoka kwa watu maskini. Napendekeza wakuu wote wa mashirika ya umma wafanyiwe usaili kwa ushindani. Napendekeza nafasi zianze kutangazwa punde nafasi ikiwa wazi ili wenye sifa wajitokeze na wafanyiwe usaili na iwe hivyo hivyo kwa bodi. Wenye sifa ndio wafanyiwe upekuzi kufanyiwa uteuzi na kupewa mkataba wenye malengo yanayopimika. **Mashirika na taasisi zingine, bodi na Menejimenti zimezidisha urafiki sana na wanaendesha ofisi kirafiki, hakuna uwajibikaji wa kutosha, hii inakiuka misingi ya mashirika kuwa na bodi za wakurugenzi.** Hii inasababisha watu wakikabidhiwa shirika la umma wanageuza ni mali yao au duka.

**36. Mheshimiwa Spika**, natambua kuna maeneo yatakayogusa sheria na kanuni mbalimbali, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametuelekeza isiwepo sheria yoyote inayotumika kama kikwazo cha kuwaletea watanzania ufanisi. Serikali, itafanyia

marekebisha Sheria mbalimbali na kanuni zitakazoguswa na maelekezo ya mheshimiwa Rais yanayolenga kuongeza ufanisi Serikalini. Najua maswala ya udhibiti wa matumizi, udhibiti wa vitendo vya rushwa, udhibiti wa uzembe, udhibiti wa ununuzi usiozingatia thamani ya fedha (value for money) yanagusa maslahi ya watu na yatanifanya niwe *unpopular Finance Minister*, na hata siku nikitoka kwenye nafasi hii marafiki watakaoona nilikwamisha dili zao potelea mbali watabaki wananchi wa Iramba ambao huwa wanabaki nami hata nikiwa nje ya uwaziri. **Mheshimiwa Rais amenielekeza niyafanyie kazi maeneo haya ya mapato na matumizi ya nchi, nami nitayasimamia, nawaomba waheshimiwa wabunge tumuunge mkono mheshimiwa Rais wetu, hii ni nia njema ya kuwakwamua watanzania kwenye umasikini.**

### **Sekta za Uzalishaji**

**37. Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta za Uzalishaji** na Ajira kwa Vijana, **Taifa letu ni Taifa la Vijana, (wastani wa miaka 18)**. Miaka ya sitini, miaka ya sabini na miaka ya themanini vijana walikuwa wanahudumia wazee na watoto. Njia ilikuwa rahisi kwa wahitimu wakitafutwa wangali masomoni wachague wanataka kwenda kufanya kazi taasisi gani. Hali haiko hivyo sasa. Kwa sasa, wazee ndio wanahudumia vijana na watoto wao. Ni kawaida sasa kukuta mzee wa kijijini au mstaafu akiwahudumia vijana wahitimu. Uwiano huu sio mzuri kwa Taifa letu kuwa na nguvu kazi kubwa ambayo haiko kazini licha ya uwekezaji mkubwa uliowekwa katika sekta za uzalishaji. ***Mipango yetu sasa na Sera zetu sasa lazima zijibu mahitaji ya vijana wa Tanzania.***

### **Sekta ya Kilimo**

**38. Mheshimiwa Spika**, katika kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji na zinazotengeneza ajira kwa

vijana, Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeongeza bajeti ya Kilimo kutoka shilingi billion 294 hadi shilingi bilioni 954 na itaendelea kuongezeka kila mwaka. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo inakua kwa zaidi ya asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Bajeti ya mwaka 2022/23 ni msingi muhimu kufikia lengo kuu hilo. Malengo mengine ni kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula ndani ya nchi na kuuza nje ya nchi, kuongeza thamani ya mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka dola za Marekani bilioni 1.2 hadi zaidi ya dola za Marekani bilioni 5 ifikapo mwaka 2030 ili kuongeza uhimilivu wa deni la Taifa. Serikali inakusudia kuongeza mauzo ya Mazao ya Bustani (Horticulture) kutoka dola za Marekani milioni 750 kwa mwaka hadi dola za Marekani bilioni 2 mwaka 2030.

**39. Mheshimiwa Spika**, ili kupunguza umaskini kwa watazania, Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inalenga kutengeneza ajira kwa vijana na wanawake zaidi ya milioni 3 katika sekta ya kilimo ifikapo mwaka 2025. Hii itafanyika kwa kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta 8,500,000, sawa na asilimia 50 ya eneo lote linalolimwa nchini ifikapo 2030. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo itatekeleza *Schemes* ndogo za umwagiliaji kote nchini. Tunataka vijana watoke mjini kuelekea kwenye mashamba ya umwagiliaji kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo ujenzi wa mabwawa ya kuvunia maji ya mvua. Tuna **Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na mito mikubwa, kama Malagarasi, Ruvuma, Rufiji, Mara, Pangani, Ruvu nk**, haya maji tutayatumia kwenye skimu za Umwagiliaji. Kwa ardhi, maji na watu tulio nao, ni jambo la aibu kwa Tanzania kulia shida ya ngano, shida ya mafuta ya kula kwa sababu ya vita vya Ukraine na Urusi, sisi tunayo fursa ya kuilisha Afrika, Ulaya na Asia katika baadhi ya mazao.



**40. Mheshimiwa Spika**, Serikali inakusudia kuongeza idadi ya mashamba makubwa (Block Farms/ Commercial Farms) kutoka 110 mwaka 2020 hadi 10,000 mwaka 2030 na kufanya mwelekeo wa uzalishaji wa kilimo kuwa cha kibiashara. Kwa kilimo cha **michikichi, tuache kung'ang'ania mchikichi mmoja mmoja kila familia, Mkoa wa Kigoma ndio kitovu cha Michikichi na upanuzi utafuata mikoa ya Tabora, Katavi, Pwani, Geita na Kagera**. Wakulima wawezeshwe kuunganisha mashamba ili yawe mashamba makubwa (plantations). Kila mmoja anakuwa mmiliki ili itengenezwe miundombinu ya pamoja. Hivyo ndivyo tunavyoweza kuitikisa dunia. Kwa alizeti hivyo hivyo. Serikali inatarajia kufanya tathmini ya kupunguza au kuhamisha mifugo michache **iliyopo katika ranchi ya Kongwa** ili hekta karibu elfu 38 zitumike kwa kilimo cha alizeti na kiwanda kikubwa kuliko vyote Afrika Mashariki. Aidha, eneo la Mtanana ambapo huwa tunasumbuka kuweka madaraja pale maji yanapokata barabara tuweke Bwawa kubwa ili bonde lote liwe la "*outgrowers*" wa alizeti.

**41. Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa Tanzania hatujajitosheleza kwa vitu vingi tu ambavyo tuna uwezo wa kuzalisha. Bidhaa nyingi tunazoagiza kutoka nje tuna uwezo wa kuzizalisha hapa, hizo ni ajira za vijana wa kitanzania ambazo tumewapa vijana wa mataifa tunakoagiza bidhaa. Serikali imekusudia kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa za kilimo kufikia asilimia 100 ifikapo 2030, na kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kupitia kilimo cha umwagiliaji kutoka asilimia 10 hadi asilimia 50. Mafuta ya alizeti yale ni mengi tu yakipangwa pembezoni mwa barabara, machungwa, mananasi, ni mengi tu yakipangwa pembezoni mwa barabara, ukiweka viwanda vya masaa 24 kwa siku 7, vya kuwafanya vijana wafanye kazi kwa zamu (shift), viwanda

vitawashwa wiki tatu tu, upungufu wote wa malighafi ni ajira za vijana tunazozikosa.

## Sekta ya Mifugo

**42. Mheshimiwa Spika**, idadi ya mifugo hapa nchini ni takriban ng'ombe milioni 35.3; mbuzi milioni 25.6; na kondoo milioni 8.8; kuku milioni 92.8; na nguruwe milioni 3.2. Hata hivyo, mchango wa sekta hii kwenye fedha za kigeni bado mdogo, na mchango wa kubadilisha maisha ya wafugaji bado ni mdogo. Licha ya idadi hiyo ya mifugo, viwanda vyetu vilivyopo Rukwa, Longido, Kibaha, na Mwanza havina malighafi, na wakati huo huo tuna vijana hawana ajira. Sababu kubwa ni utofauti wa malengo kati ya mfugaji na mwenye kiwanda. Malengo ya wafugaji wengi tulionao siyo ya kibiashara, anafuga ili idadi iongezeke, hana mpango na kiwanda. **Mheshimiwa Spika**, ndugu zangu wa usukumani hata ng'ombe akivunjika mguu anafungwa POP, hata akiwa na shughuli ya kifamilia hachinji ng'ombe wa zizini, anakwenda kununua mnadani. Wale wa kwenye zizi wote wana majina, **chitamakuwi, maagulya, nshoshawiye na majina ya shangazi**, mjomba, bibi, hawachinjwi halafu mwenye kiwanda anaweka kiwanda kutokana na takwimu tu za mifugo katika mkoa huo.

**43. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezewa ukomo wa bajeti kwa kiasi cha shilingi bilioni 100. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 40 ni za sekta ya mifugo na shilingi bilioni 60 ni za sekta ya uvuvi. Hivyo, bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezeka kutoka shilingi 168,252,007,000 hadi kufikia shilingi 268,252,007,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 92,050,824,000 ni kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na shilingi 176,201,183,000 ni kwa ajili ya sekta ya uvuvi. Ongezeko hilo la bajeti linalenga kuimarisha sekta ya mifugo ili ufugaji uwe wa kisasa zaidi na wenye tija (modernization). Katika mwaka 2022/2023, Serikali

itaimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba ya Sao Hill, Kitulo na Mabuki kwa kuyapatia ng'ombe wazazi na vitendea kazi, ikiwemo matrekta matatu (3) na vifaa vyake. Aidha, Serikali itanunua madume ya mbegu 366 kwa ajili ya kuboresha mbari za mifugo; na itazalisha mitamba 3,500 na kuisambaza kwa wafugaji. Serikali inakusudia kuongeza uzalishaji wa vyakula ambapo mpaka sasa uzalishaji wa vyakula vya mifugo umeongezeka kutoka tani 1,200,000 mwaka 2020/2021 hadi tani 1,380,000 mwaka 2021/2022.

**44. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM inayoongozwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM inakusudia kuanzisha vituo nane (8) vya kukuza ujuzi wa vijana (Youth Incubation Center) kwa kuanzia na wanufaika takriban 1000 kwa ajili ya vijana watakaofanya kazi ya kunenepesha ng'ombe na kuuza kwenye viwanda hivi vinavyokosa malighafi. Serikali imepanga kutumia mitambo ya kuchimba mabwawa kwa ajili ya wafugaji wadogo wadogo. Aidha, napendekeza Wizara inayohusika na mifugo itunge kanuni za kukusanya na kulinda fedha kwa kila Wilaya kwa makundi ya mifugo yanayozidi mia moja kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji zaidi katika viwanda vya kuchakata na kusindika nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi hususani nchi za Mashariki ya Kati ambapo kwa sasa kuna machinjio na viwanda 24 vinavyokidhi vigezo vya kuuza nyama nje ya nchi ambapo vitano kati ya hivyo vimeanza kufanya mauzo nje ya nchi. Viwanda vya kutengeneza bidhaa za ngozi vina uwezo wa kuzalisha jozi 2,855,600 za viatu kwa mwaka. Kwa upande wa maziwa, idadi ya viwanda vya kusindika maziwa nchini imeongezeka kutoka 99 mwaka 2020/2021 vilivyosindika lita milioni 75.9 hadi viwanda 105 mwaka 2021/2022 vilivyosindika lita milioni 77.6 ikiwa ni ongezeko la asimilia 2.3

## Sekta ya Uvuvi

**45. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021, sekta ya uvuvi ilikua kwa asilimia 2.5 na ilichangia asilimia 1.8 kwenye Pato la Taifa. Aidha, sekta ya uvuvi inatoa ajira kwa watazania takriban milioni 4.5 katika mnyororo mzima wa thamani ambapo ajira za moja kwa moja kwa wavuvi ni 194,804 na wakuzaji viumbe maji ni 31,998. Serikali imepanga: Kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko - Lindi; ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari; ununuzi wa vifaa vya kuvutia samaki (Fish Aggregate Device - FADs); ununuzi na usambazaji wa boti 250 za kisasa za aina ya *fibre* kwa vyama vya ushirika wa wavuvi; kuendelea na ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO; kuwajengea uwezo wataalamu wa uvuvi; kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi - FETA; kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania - TAFIRI; kukamilisha ujenzi wa mialo ya kupokelea samaki ya Igabiro, Mbamba Bay na Chifunfu na kujenga masoko sita (6) ya samaki kwenye maeneo mbalimbali ya kimkakati; kukarabati kituo cha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi cha Bukoba; kununua boti mbili (2) kwa ajili ya utalii wa baharini; ujenzi na ukarabati wa vituo vya ukuzaji viumbe maji; na kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya sekta ya uvuvi ili kuhakikisha mradi unatekelezwa kama ulivyopangwa.

## Sekta ya Fedha

**46. Mheshimiwa Spika**, sekta ya fedha imeendelea kutoa mikopo kwa wafanyabiashara na uchumi. Pamoja na juhudi hizo, kumekuwepo na wafanyabiashara wasiolipa mikopo yao kwa wakati na kupelekea kudhoofisha ustawi wa mabanki na ustawi wa uchumi kwa ujumla. Hadi kufikia Machi 2022, mikopo chechefu ilikuwa asilimia 8.12. Hiki ni kiwango kikubwa sana ikilinganishwa na vigezo vilivyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania. Jambo hili linasababishwa

na ukopaji usiozingatia kanuni na unaohusisha ukosefu wa weledi na uaminifu wa baadhi ya watumishi wa benki. Unakuta mtu amekopa mabenki zaidi ya matano na kote hajalipa. Akidaiwa anabakia kuonesha ufundi wa kujificha, baadae akichoka kujificha anakimbilia mahakamani. Tuache utapeli unatuchafulia nchi na unapozesha uchumi, "Ukikopa Lipa". Nitoe rai kwa vyombo vya dola na vyombo vya sheria kuwa wakali kwenye utapeli wa aina hii.

**47. Mheshimiwa Spika**, niwapongeze sana wanawake, taarifa za kitafiti nilizopewa zinaonesha wanawake wengi wanajitahidi kurejesha mikopo kwa uaminifu. Hata mikopo ya familia kama imekopwa na wanawake, mingi huwa inafanya kazi iliyokusudiwa na hivyo inarejeshwa kwa uaminifu kuliko iliyokopwa na wanaume wengi ambao huwa hawarejeshi. (Niweke sawa, Niliposema wanaume wengi ni ukimwondoa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu). Tujenge utaratibu wa kukopa kwa kuzingatia kanuni, uwezo wa kulipa na tujenge utaratibu wa kurejesha mikopo kwa uaminifu ili kuimarisha sekta ya fedha na kukuza uchumi. Kwa upande mwingine, wako baadhi ya watumishi wa mabenki wasio waaminifu kwa kushirikikiana na madalali wao wanapenda kutamani dhamana za wateja wao na kutafuta wateja wa kununua dhamana za wateja wangali wameshalipa zaidi ya asilimia tisini ya deni. Tena wanauza dhamana kwa kiwango cha chini ukilinganisha na thamani ya dhamana iliyowekwa. Jambo hili linawatia umaskini watanzania. Nitoe rai kwa vyombo vya ulinzi na usalama kufuatilia kwa karibu kila inapofanyika minada kwa madalali wa dhamana na bandarini.

### **Sekta ya Nishati**

**48. Mheshimiwa Spika**, mafanikio tuliyoyapata katika sekta ya nishati ni pamoja na kuendelea kutekeleza: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115 ambapo hadi Aprili 2022 utekelezaji umefikia

asilimia 60.22; miradi ya Kupeleka Umeme Vijijini - REA; mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (East African Crude Oil Pipeline - EACOP) kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania; na mradi wa kusindika na kuongeza kasi ya usambazaji gesi asilia. Aidha, Serikali imeendelea kuwashirikisha wazawa ambapo shughuli za uendeshaji wa mitambo ya uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia unafanywa na watanzania.

**49. Mheshimiwa Spika**, katika sekta ya nishati, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme. Kwa mwaka 2022/23, Serikali ya CCM inayoongozwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM itaendelea na utekelezaji wa mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (**National Grid Stabilization Project**) kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini pamoja na kutekeleza miradi ya nishati vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Miradi mingine itakayotekelezwa inahusisha Ruhudji (MW 358), Kinyerezi I - Extension (MW 185), Rusumo (MW 80) na Kikonge (MW 300). Aidha, Serikali itaendelea kujenga njia za mzunguko pete (ring circuit) ili kuzuia upotevu wa umeme kwa kuwezesha umeme kupita njia mbadala pale miundombinu inapopata hitilafu. Miradi ya njia ya umeme wa msongo itakayoendelea kutekelezwa ni pamoja na kV 400 Rufiji - Chalinze - Dodoma na Chalinze - Kinyerezi; kV 400 Singida - Arusha - Namanga; kV 400 North - West Grid Extension (Iringa - Mbeya - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Nyakanazi); pamoja na kujenga miundombinu ya umeme kwa ajili ya SGR.

**50. Mheshimiwa Spika**, Serikali itakamilisha uunganishaji wa mikoa miwili yaani Kigoma na Katavi kwenye Gridi ya Taifa. Mradi wa Nyakanazi - Kakonko - Kasulu - Kigoma KV33 unaojengwa na Mkandarasi Sinotech, Mradi wa Nyakanazi - Kigoma KV 400 Mkandarasi yuko *site* kwa gharama ya dola za

Marekani milioni 168, fedha zipo! Kadhalika mradi wa kufua umeme wa Malagarasi mw 49.5 fedha tayari zipo kwa ajili ya mradi huo. Serikali itaendelea na miradi mikubwa miwili pia ya kuunganisha umeme kutokea Sumbawanga – Katavi - Kigoma na ule wa Tabora -Katavi - Kigoma. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mkoa wa Katavi, tayari mkandarasi yuko site ukianza na ujenzi wa *sub station Ipole* Sikonge, Inyonga wenye thamani ya billion 124. Napenda niwahakikishie wananchi wa mikoa hiyo kuwa umeme wa Grid ya Taifa utafika kama alivyoeleza Waziri wa Nishati. Wabunge wa Kigoma na wabunge wa Katavi mliokuja kuweka kambi Wizara ya Fedha na Mipango mkifuatilia ahadi ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, mtarudi mikoani kwenu mkiwa mashujaa na mtatembea kifuatele.**

## Ujenzi na Uchukuzi

**51. Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2022, ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa - SGR kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) umefikia asilimia 96.54; na kipande cha Morogoro - Makutupora (km 422) asilimia 85.02. Aidha, Serikali imesaini mkataba wa ujenzi wa SGR kwa kipande cha tatu cha kutoka Makutupora mpaka Tabora (km 368) wenye thamani ya shilingi trilioni 4.4. Serikali iko katika hatua za mwisho ya kusaini mktaba wa kipande cha Tabora - Isaka (km 163) (dola za Marekani milioni 695.7). **Serikali imeanza mchakato wa kutafuta mkandarasi kwa kipande cha Tabora - Kigoma km 514 (dola za Marekani bilioni 2.1) na kipande cha Uvinza – Malagarasi – Msongati – Gitega - Kindu (DRC)**

**52. Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha ujenzi wa jumla ya kilometa 216.26 za barabara kuu na kilometa 34.8 za barabara za mikoa kwa kiwango cha lami. Aidha, kilometa 307.41 za barabara za mikoa zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Vilevile,

Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje - *Outer Ring Road* (km 112.3) katika Jiji la Dodoma pamoja na kuendelea na upanuzi wa njia nane wa barabara ya Kimara - Kibaha (km 19.2). Kadhalika, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja ya Tanzanite (Dar es Salaam), Kiyegeya (Morogoro), na Ruhuhu (Ruvuma) na kuendelea na ujenzi wa madaraja ikijumuisha daraja la J.P Magufuli (Kigongo - Busisi, Mwanza) ambalo ujenzi umefikia asilimia 40.2, Kitengule, Kagera (asilimia 90) na Wami, Pwani (asilimia 72.9). Serikali pia imeendelea na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Songea, Mtwara, Iringa, Musoma na Songwe.

**53. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM inayoongozwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM itaweka msisitizo katika ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi na zile za kuunganisha Tanzania na nchi jirani kwa utaratibu wa **EPC + F** ikiwemo

(1) barabara za Kidatu - Ifakara - Lupilo- Malinyi - Londo - Lumecha (Songea), (km 499);

(2) Handeni - Kibirashi - Kibaya - Kwa Mtoro - Singida (km 460);

(3) Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti River - Lalago - Maswa (Simiyu) (km 389);

(4) Daraja la Juu la Magomeni-Jangwani-Fire-Bibi Titi  
(5) Kibaha - Mlandizi - Chalinze - Morogoro *Expressway* (km 158);

(6) Igawa - Songwe - Tunduma (*Expressway*) (km 218.0), ambazo zitawekewa *road toll* pamoja na daraja la Tanzanite kwa kuwa lina sifa zote za kufanya hivyo. Serikali itamalizia barabara zinazounganisha Mikoa ambayo wakandarasi wako kazini ikiwepo Tabora - Kigoma na Nyakanazi - Kigoma



na kuweka kipaumbele kwenye kujenga barabara muhimu za kiuchumi kama Barabara ya Makongorosi-Itigi - Mokiwa, Mafinga-Mtwango-Nyololo - Mgololo, Kahama - Nyang – wale - Geita na nyinginezo.

**54. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya awamu ya sita imeonesha dhamira ya dharti ya kuboresha bandari ili kurahisisha shughuli za kiuchumi za usafirishaji kwa njia ya maji na uvuvi katika kina kirefu cha bahari. Katika kufanikisha hilo, Serikali imendelea na miradi ya ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya bandari zilizopo katika ukanda wa Bahari ya Hindi. Miradi hiyo ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa gati maalumu la kuhudumia meli za magari (RoRo), yadi ya kuhudumia makasha pamoja na kuboresha gati namba 1 - 7 katika Bandari ya Dar es Salaam; kusainiwa kwa mkataba na mkandarasi *China Harbour Engineering Co. Ltd* kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Uvuvi, Kilwa Masoko - Lindi; kukamilika kwa ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300; kuendelea na ujenzi wa uzio na sakafu ngumu katika eneo la mita za mraba 75,807 katika Bandari ya Mtwara; na kukamilika kwa uongezaji wa kina kwenye lango la kuingia meli kutoka mita nne (4) hadi mita 13 pamoja na kuweka vifaa vya kuongoza meli katika Bandari ya Tanga. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na wawekezaji watakaowekeza kwenye Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo hususani katika miradi ya msingi mitatu (3) ambayo ni: Bandari ya kisasa (Modern Seaport Component); Sehemu ya Kanda Maalum kwa ajili ya mizigo na usafirishaji (Logistics Park); na Sehemu ya Mji wa Viwanda (Port side Industrial City).

**55. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Serikali ilikamilisha ujenzi wa chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza pamoja na ukarabati wa meli za New Butiama Hapa Kazi Tu na New Victoria Hapa Kazi Tu. Aidha, serikali imeendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na

tani 400 za mizigo, ambapo ujenzi umefikia asilimia 66. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali inatarajia kujenga meli mpya: moja (1) katika Ziwa Victoria; mbili (2) katika Ziwa Tanganyika; na moja katika Bahari ya Hindi. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa meli ya MV. Mwanza katika ziwa Victoria pamoja na ukarabati wa Meli za MV Umoja, MT Sangara, MV Liemba - Ukerewe, MT. Nyangumi na boti moja (1) ya mwendokasi (Sea Warriors) - Ziwa Tanganyika. Aidha, Serikali itafanya ukaguzi wa kina wa Meli ya MV Mwongozo katika Ziwa Tanganyika pamoja na kuendelea kufungua mifumo ya TEHAMA katika vituo vya Maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa).

**56. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa kuboresha Shirika la Ndege Tanzania ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/22 Serikali imepokea ndege tatu (3). Kati ya hizo, ndege mbili (2) ni aina ya Airbus A220 300 na ndege moja ni aina ya Dash 8 Q400. Vilevile, Serikali imefanya malipo ya awali ya ununuzi wa ndege mpya tano (5) ambazo ni ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9, ndege moja (1) aina ya De Havilland Dash 8-Q400, ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner, na ndege moja (1) ya mizigo aina ya Boeing 767-300F.

**57. Mheshimiwa Spika**, uboreshaji wa viwanja vya ndege unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kutekeleza hilo, Serikali imesaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato awamu ya kwanza itakayohusisha ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege pamoja na jengo la abiria. Aidha, Serikali imekamilisha upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongoza ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; pamoja na usanifu na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Viwanja vinavyoendelea kufanyiwa ukarabati na ujenzi ni viwanja vya ndege

vya Songea (asilimia 96), Mtwara (asilimia 89), Iringa (asilimia 44.65), Songwe (asilimia 95) na Musoma (asilimia 10). Vilevile, Serikali inaendelea kufanya maandalizi ya ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vitakavyogharimu Euro milioni 50 sawa na shilingi bilioni 136.85.

## **Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**58. Mheshimiwa Spika**, Serikali imewezesha ujenzi wa madarasa 15,000 katika shule za sekondari na vituo shikizi na mabweni 50 kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ujenzi wa miundombinu hii umewezesha wanafunzi wote 907,803 waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2021 kupata nafasi ya kuanza kidato cha kwanza Januari 2022 bila kusubiri chaguo la pili. Kadhalika, Serikali imekamilisha maboma 560 ya vyumba vya madarasa katika shule za sekondari kutokana na tozo za miamala ya simu ambapo shilingi bilioni 7.0 zilitolewa; Aidha, Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 569 kwa wanafunzi 177,777 wa elimu ya juu.

**59. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23 Serikali itaenda kutekeleza mradi wa "*Higher Education for Economic Transformation*" (HEET) wenye thamani ya dola za Marekani milioni 425. Mradi huu utahusisha ujenzi wa miundombinu katika vyuo vikuu mama na katika mikoa kadhaa ambayo haina vyuo vikuu ikiwemo Lindi, Kagera, Rukwa, Katavi, Manyara na kukamilisha ujenzi wa *Institute of Marine Science Zanzibar* na kujenga chuo kipya cha TEHAMA Dodoma.

**60. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kugharamia programu ya elimumsingi bila ada ambapo hadi Aprili 2022, jumla ya shilingi bilioni 244.5 zilitolewa. **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mwenyekiti

wa CCM ameguswa sana na watoto kukatisha masomo kwa ajili ya sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu zinazosababisha kukatisha masomo ni umaskini wa kipato kwenye familia zetu, mimba za utotoni, mwamko duni wa elimu kwa baadhi ya jamii na utoro na wale wasioendelea kufuatana kwa mujibu wa sheria (Ufaulu). **Ili kukabiliana na utoro (drop out) wa wanafunzi wanaotoka familia maskini**, bado tuna watoto wanaoshindwa kumudu mahitaji ya lazima licha ya kuwepo kwa programu ya elimu bila malipo na hivyo wanasaidiwa na wabunge, madiwani na wengine kuchangiwa na wasamaria wema. **Napendekeza kuanzisha dirisha maalum (Special Fund) kupitia TASAF itakayosaidia watoto wanaotokea familia maskini.** Kwa msingi huo napendekeza kuanza na bilion 8 kwa ajili ya watoto masikini watakaopatikana kwenye database ya TASAF na taarifa za wabunge na madiwani.

**61. Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na mimba za utotoni, Serikali itaendelea kujenga mabweni kwenye maeneo hatari kwa watoto wa kike. Aidha, ili kutoa fursa kwa watoto wasioendelea na vidato na vyuo, Serikali itaendelea kuimarisha elimu ya ufundi hususan katika vyuo vya kati kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujajiri ama kuajiriwa. Mpaka sasa Wilaya 77 zina vyuo vya Ufundi VETA kati ya Wilaya 138 nchini kote. Tuna mikoa 25 ina Vyuo vya Ufundi kati ya mikoa 26. Bado mkoa wa Songwe hauna kabisa Chuo cha VETA na wabunge wa mkoa wa Songwe wamekuwa wakishinda Ofisini wakifuatilia ahadi waliopewa na Mheshimiwa Rais. Bado kuna wilaya 36 ambazo hazina vyuo wala vyuo vya Mkoa. Napendekeza kutoa bilioni 100 kwa ajili ya ujezi wa vyuo vya ufundi kwa Mkoa wa Songwe na wilaya 36 ambazo hazina vyuo ili kufanya wilaya zote 138 kuwa na chuo cha Ufundi (VETA). **Waheshimiwa wabunge, Huyo ndio SAMIA.**

**62. Mheshimiwa Spika**, kwa sasa wanafunzi wa kidato cha tano ni takriban 90,825 na kidato cha sita ni 56,880. Mahitaji ya fedha ni shilingi **10,339,350,000**. Ili kuwapunguzia gharama watoto hao kama **Mheshimiwa Rais** alivyoielekeza Wizara, **napendekeza kufuta ADA kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Kwa hatua hiyo, Elimu bila Ada ni kuanzia shule za msingi mpaka kidato cha sita.** Serikali itajipanga kuangalia namna ya kusaidia vyuo vya kati **kadiri** hali ya uchumi itakavyotengemaa. Nani kama SAMIA? Nani kama Mama? Nani kama CCM? CCM ni Na. 1.

### **Sekta ya Afya**

**63. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Serikali imewezesha ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya afya ikiwemo: majengo 66 ya wagonjwa mahututi - ICUs; majengo 100 ya dharura - EMDs; nyumba 150 kwa ajili ya watumishi wa Afya; Hospitali za Rufaa za Mikoa 7 na hospitali maalum 1 (Mirembe); na vituo vya Afya 304 ili kuboresha huduma ya mama na mtoto. Aidha, Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 23.32 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kukamilisha ujenzi wa maboma 564 ya zahanati. Serikali pia imeendelea na ujenzi wa hospitali 99 na kuanza ujenzi wa hospitali mpya 28. Vilevile, Serikali imewezesha ujenzi wa vituo vya afya 234 kwa kutumia tozo ya miamala ya simu yenye thamani ya shilingi bilioni 86.0.

**64. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za afya kwa kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa ambapo hadi sasa katika hospitali zetu mbalimbali kuna jumla ya mashine 11 za *CT scan*, mashine 7 za MRI na mashine 105 za *digital X Ray* zinazofanya kazi. Kati ya hizo, mashine 42 za *digital X Ray* zipo katika hospitali za ngazi ya taifa, kanda na maalumu na rufaa za mikoa na mashine 63 zipo katika hospitali zilizo chini ya OR-TAMISEMI. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika eneo hili ambapo

ununuzi zaidi wa vifaa vya uchunguzi wa magonjwa umekamilika na vifaa hivyo vitasimikwa katika hospitali na taasisi zetu mbalimbali. Vifaa ambavyo vimeshaagizwa ni pamoja na, MRI 4; *CT "Scan 31; Digital X Rays"* 130; *mini angio suite* moja na "*Echo Cardiography*" 7. Aidha, Serikali inaendelea na usimikaji wa vinu ya kuzalisha na kujaza hewa tiba ya oksijeni ambapo hadi sasa vinu 13 vimesimikwa katika hospitali zetu mbalimbali na hivyo kusogeza huduma za kitabibu kwa wananchi.

**65. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM inayoongozwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM itaendelea kuboresha sekta ya afya kwa kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya kutolea huduma za afya ikiwemo: Ujenzi wa Hospitali Maalum ya Mama na Mtoto Jijini Dodoma; kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi; kukamilisha ujenzi wa Hospitali (5) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa mipya ya Katavi, Geita, Njombe, Songwe na Simiyu; na kukamilisha upanuzi wa hospitali nane (8) za Rufaa za Mikoa. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa na Kanda kwa kuimarisha miundombinu na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika Taasisi ya JKCI, Hospitali za Rufaa za Kanda za Chato, Mtwara, KCMC, Bugando na Mbeya.

## **Sekta ya Maji**

**66. Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais wetu amewezesha kukamilika kwa miradi 303 ya maji vijijini na miradi 40 mijini ikiwemo miradi mikubwa ya Misungwi, Orkesumet, Chalinze- Mboga na Longido; kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka asilimia 72.3 vijijini na 86 mijini mwaka 2020/21 hadi asilimia 74.5 vijijini na 86.5 mijini; kuimarika kwa usimamizi wa rasilimali ya maji kwa kuendelea kutambua, kuweka mipaka na

kuhifadhi vyanzo 178 vya maji pamoja na kuandaliwa kwa mipango ya utunzaji wa maeneo ya vidakio vya maji katika mabonde yote nchini.

**67. Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imekamilisha taratibu za ununuzi wa seti 25 za mitambo ya kuchimba visima ambayo itasambazwa kwa kila mkoa isipokuwa Dar es Salaam; seti 5 za mitambo ya ujenzi wa mabwawa ambazo zitapelekwa kwenye kila kanda; na seti 4 za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi. Mitambo hii inatarajiwa kupokelewa mwishoni mwa mwezi Juni, 2022. Aidha, mnamo tarehe 6 Juni 2022, Serikali ilisaini mikataba ya kusambaza maji kwa miji 28, ambazo ni fedha za mkopo wenye thamani ya dola za Marekani milioni 500 kutoka Exim bank - India. Kati ya fedha hizi, dola milioni 35 zitatekeleza miradi ya maji Zanzibar.

### **Sekta ya Mali Asili na Utalii**

**68. Mheshimiwa Spika**, Aprili mwaka huu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua filamu ya "*The Royal Tour*" ambayo imelenga kuonesha uwezo na fursa zilizopo Tanzania katika sekta ya utalii na uwekezaji. Hivyo, kupitia Bunge hili, napenda kuendelea kuwakaribisha *diaspora* wa Tanzania na wawekezaji kutoka kona zote za dunia kuja kutalii na kuwekeza katika fursa za uwekezaji zilizopo nchini kwani Tanzania tuna "**JAMBO LETU**" kwenye kuinawirisha sekta binafsi katika uwekezaji. Tumejipanga na kujizatiti kuifanya Tanzania kuwa "**KITOVU na MFANO**" wa sehemu ya uwekezaji salama, haraka, rahisi, wenye tija na manufaa kwa pande zote. Kufuatia ziara hiyo kwenye kanda za utalii Tanzania, tayari *booking* zimejaa mpaka Desemba 2022 kwenye maeneo mengi. Naomba kutoa wito kwa **wawekezaji wote** kuwa, **Tanzania kumenoga, milango iko wazi, njooni muwekeze kwa maslahi mapana ya pande zote.**

## Sekta ya Madini

**69. Mheshimiwa Spika**, chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, mchango wa sekta ya madini umeongezeka kutoka asilimia 6.7 mwaka 2020 hadi asilimia 7.2 mwaka 2021 ambapo ukuaji huu uliifanya sekta hii kushika nafasi ya tano miongoni mwa sekta nyingine za kiuchumi nchini. Aidha, kasi ya kukua kwa shughuli za madini hapa nchini imekuwa ikiendelea kuongezeka ambapo katika mwaka 2021, sekta ya madini ilikua kwa asilimia 9.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2020, na hivyo kuwa ya tatu miongoni mwa sekta nyingine kwa kiwango cha ukuaji katika kipindi hicho. Mwenendo huu wa ukuaji wa sekta umetokana na ongezeko la uwekezaji uliofanyika kupitia uchimbaji mkubwa, wa kati na mdogo nchini. Lengo la Serikali ni kuona sekta ya madini inachangia asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

**70. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa wachimbaji wadogo kushiriki uchumi wa madini, Serikali imezihamasisha taasisi za fedha na benki nchini kutoa mikopo kwa wachimbaji hao ili kuwawezesha kukua na kufanya uchimbaji wenye tija. Baadhi ya benki ikiwemo NMB, NBC, CRDB na KCB zimeridhia na kuanza kutoa mikopo ambapo jumla ya shilingi bilioni 36 zimekopeshwa kwa wachimbaji hao. Hizi ni miongoni mwa juhudi ambazo Serikali imezifanya ili kuhakikisha wachimbaji wadogo wanakua na kufikia hadhi ya kiwango cha kati na hatimaye wakubwa, wanashiriki uchumi wa madini na kuchangia katika Pato la Taifa. Aidha, kufuatia Serikali kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo, mchango wao katika maduhuli ya Serikali umeongezeka hadi kufikia takriban asilimia 40 ya maduhuli yote. Kutokana na mchango wao, Serikali itaendelea kuwawezesha ili waendeleo kuchangia zaidi katika uchumi wa Taifa.



**71. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia Tanzania - GST imeweza kufanikisha ugani wa jiolojia kwa asilimia 96 ya nchi nzima, ugani wa jiofizikia kwa skeli ndogo (Low Resolution) asilimia 100 na skeli kubwa (High Resolution) asilimia 16 na ugani wa jiokemia asilimia 25 ya nchi nzima. Kupitia tafiti hizo Serikali imefanikiwa kugundua maeneo mapya yenye rasilimali madini na kuyatangaza kwa lengo la kuvutia uwekezaji mkubwa. Baadhi ya rasilimali zilizogunduliwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita ni pamoja na dhahabu (Malinyi - Morogoro na Liwale - Lindi), gesi ya helium (Masware - Babati na Ziwa Natroni - Arusha), chokaa na feldispa (Kiteto - manyara), chokaa (Mkalama - Singida).

**72. Mheshimiwa Spika**, migodi mikubwa iliyopo kama GGML, Bulyanhulu North Mara na mgodi mpya wa Kabanga Nikeli na Nyanzaga imetokana na taarifa za awali za jiolojia zilizofanywa na GST miaka ya nyuma. Kutokana na mafanikio hayo, Serikali itaendelea kuiwezesha GST ili iweze kufanya utafiti zaidi wa jiofizikia kwa skeli kubwa (*High Resolution*) kwa lengo la kufikia asilimia 65 kutoka asilimia 16 iliyopo sasa. Manufaa yanayotarajiwa ni pamoja na; Uwezekano wa kuanzishwa kwa migodi mipya ambayo itachangia Pato la Taifa kupitia sekta ya madini; ukuaji wa sekta mtambuka ambazo hutegemea sana sekta ya madini kama vile kilimo, ujenzi na maji; uanzishwaji wa viwanda vinavyotegemea upatikanaji wa malighafi za madini kama vile viwanda vya saruji, mbolea na marumaru; na kuongezeka kwa ufahamu zaidi wa jiolojia ya nchi na hivyo kuchochea shughuli za utafiti na uchimbaji wa madini ambao utachangia katika maendeleo ya Taifa.

**73. Mheshimiwa Spika**, kila mtanzania mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 na mwenye kipato anatakiwa kulipa kodi. Ili kutimiza amza hiyo, Serikali inakusudia kutoa namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) kwa kila mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 au

zaidi. Kwa kuwa utaratibu wa usajili wa namba ya utambulisho wa Taifa (NIDA) unamtaka kila mwananchi mwenye umri wa miaka 18 au zaidi kujisajili NIDA, napendekeza kuwa wale wote wenye NIDA kwa sasa (wanaofikia milioni 19 nchi nzima) wapatiwe namba ya TIN na itumike kwenye miamala yote inayofanyika katika ununuzi na mauzo yanayofanyika ndani ya nchi. Kila mwenye namba ya mlipakodi atapata makadirio yake kwa njia ya simu na kulipa kodi husika kwa njia ya mtandao.

**74. Mheshimiwa Spika**, vijana wetu wa bodaboda wanapata shida kufuata leseni yalipo makao makuu ya mkoa, yaani mtu atoke Mererani kwenda Babati makao mkuu ya mkoa wa Manyara, atoke Kakonko kufuata leseni Kigoma, atoke Wilaya ya mwisho kule mpakani na Lindi, Mtwara na Ruvuma kufuata leseni Morogoro ili hali taarifa zake zote ziko kwenye kitambulisho cha NIDA. Napendekeza taarifa zilizopo kwenye kitambulisho zitumike kutengeneza leseni, akishakufuzu ajiandikishe atoe namba yake ya NIDA, TRA na Jeshi la Polisi wafanye kazi ya kuoanisha taarifa na wamtumie mhusika leseni yake kwa simu. Aidha, napendekeza wananchi wote wenye namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) wapeleke ritani za kodi Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka mara moja. Utaratibu huu utachachua utamaduni wa kulipa kodi miongoni mwa Watanzania na hivyo kuiongezea Serikali mapato yatokanayo na sekta ambazo hazichangii kwenye makusanyo ya Serikali kwa sasa licha ya kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kama vile sekta za mifugo, kilimo, uvuvi na nyinginezo.

## **Bunge**

**75. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua uzito wa majukumu ya Bunge na hivyo itaendelea kuhakikisha kwamba Bunge linawezeshwa kifedha na kujengewa uwezo ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa

majukumu yake ya msingi ya kutunga sheria, kushauri na kusimamia Serikali. Kwa kulitambua hilo, katika mwaka wa fedha 2022/23, Bunge limeongezewa kiasi cha shilingi bilioni 5 kwa ajili ya matumizi mengineyo ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake **ikiwemo kuwajengea uwezo wabunge ili waweze kuisimamia vizuri Serikali. Serikali pia imeongeza bajeti ya mfuko wa Jimbo ili kuwawezesha wabunge kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kuchochea maendeleo katika majimbo yao.** Serikali itahakikisha kuwa fedha kwa ajili ya shughuli za Bunge zinatolewa kwa wakati. Aidha, Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu kwa kulipatia taarifa zote muhimu zinazohitajika na kwa wakati ikiwepo taarifa za kila robo mwaka za kitengo cha Tathmini na Ufuatiliaji ili zivasaidie wabunge wanapofanya ziara za kukagua miradi kama nilivyopendekeza awali.

## **Utawala Bora**

**76. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mahakama, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa mfumo ya haki na utoaji haki kwa kuendelea kuwezesha mhimili wa Mahakama kuongeza kasi ya kusikiliza mashauri na hivyo kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani. Aidha, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya utoaji haki kupitia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama ikiwa ni pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA hususan mfumo wa mkutano mtandao na mfumo wa kielektroniki wa usimamizi na uendeshaji wa mashauri. Utekelezaji wa masuala haya unalenga kuboresha ufanisi wa mahakama na kufanya usimamizi wa mahakama kuwa wa kisasa zaidi na hivyo kuwawezesha wananchi kupata haki sawa na kwa wakati.

**77. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea kugharamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

zinazolenga katika utoaji haki kwa wananchi na kupambana na rushwa. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa vituo jumuisi vya utoaji haki na kutafsiri sheria ambapo kiasi cha shilingi bilioni 5.7 zimeongezwa kwenye bajeti ya awali. Aidha, Serikali imeongeza kiasi cha shilingi bilioni 20 kwenye bajeti ya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali kwa ajili kugharamia mashahidi wa makosa ya jinai na ujenzi wa vituo jumuisi vya utoaji haki.

### **Ulinzi na Usalama**

**78. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Serikali kupitia majeshi yetu imeendelea kudumisha amani na usalama nchini na hivyo kuwezesha watanzania kutembea kifua mbele na kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi bila wasiwasi. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi mbalimbali na tunaamini kuwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vitaendelea kutimiza wajibu wake wa kulinda mipaka na amani ya nchi yetu kwa moyo wa kizalendo na hivyo kuzidi kuimarisha mazingira ya amani na utulivu ya kuvutia biashara na uwekezaji. Katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea kuimarisha na kuvijengea uwezo vyombo vya ulinzi na usalama ili kuendelea kutekeleza wajibu wake kwa weledi na uzalendo.

**79. Mheshimiwa Spika**, sambamba na zoezi la anuani za makazi linaloendelea, Serikali itaimarisha shughuli za usalama ngazi ya kaya ili kujidhatiti na aina mpya ya uhalifu ambao tumeusikia kwa baadhi ya majirani zetu. Utaratibu huo ni pamoja na kuhakikisha viongozi wa mitaa na shehia wanahusika kwenye upangishaji wa nyumba za kuishi ili kila nyumba ya kupanga itumie mkataba wa Serikali ya vijiji/mitaa uliopigwa muhuri wa ofisi ya vijiji/mitaa husika. Kadhalika, mauziano ya mali zisizohamishika lazima zihusishe uongozi wa Serikali husika hata kama wahusika wana mawakili binafsi ila viongozi wa serikali za vijiji/mitaa wawe na taarifa za mambo yanayoendelea katika maeneo yao.

## Uhusiano wetu na Washirika wa Maendeleo

**80. Mheshimiwa Spika**, jitihada za kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo pamoja na mataifa mbalimbali duniani zinazofanywa na **Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan**, zimewezesha kusainiwa kwa mikataba ya misaada na mikopo mbalimbali. Baadhi ya mikataba ya miradi iliyosainiwa ni pamoja na: Uboreshaji wa Umiliki wa Ardhi; kuboresha Elimu ya Msingi; na mradi wa Maboresho ya Mahakama ili kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi. Aidha, baadhi ya mikataba ya miradi inayotarajiwa kusainiwa ni pamoja na: Mradi wa Kufungamanisha Uchukuzi ambao una lengo la kuboresha na kuunganisha njia kuu za barabara na viwanja vya ndege vya mikoja (TanTIP); na Mpango Kabambe wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu - TSMP II.

**81. Mheshimiwa Spika**, Serikali inakamilisha majadiliano ya upatikanaji wa mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia wenye thamani ya dola za Marekani milioni 500, sawa na shilingi bilioni 1,167. Aidha, Serikali imefikia makubaliano ya kupata mkopo nafuu wenye thamani ya shilingi bilioni 2,567, sawa na dola za Marekani bilioni 1.1 kupitia dirisha la *Extended Credit Facility (ECF)* chini ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF. Mkopo huo wa IMF utatolewa kwa awamu saba katika kipindi cha miezi 40 kuanzia Julai 2022 hadi Julai 2025. Fedha hizo zitaelekezwa katika kuimarisha sekta za uzalishaji, huduma za jamii pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji na kuinua sekta zilizoathiriwa na vita ya Ukraine na Urusi.

## Maslahi ya Watumishi wa Umma na Wastaafu

**82. Mheshimiwa Spika**, tuzo ya watumishi wachapakazi na wazalendo ni ipi? Matunda ya utumishi wa kujitoa na uadilifu wa watumishi hao ni

yapi? Lakini Je, ni nani wa kuyatambua na kuyapa thamani halisi mambo hayo? Sauti zenye maswali haya zilitawala masikio ya Mheshimiwa Mama yetu mwenye usikivu, unyenyekevu na anayejali, na hatimaye maswali haya yamejibiwa na kalamu yenye mamlaka ya Mheshimiwa Rais wetu kwa kuridhia nyongeza ya kima cha chini cha **mshahara kwa asilimia 23.3** kwa watumishi wa umma. Kwa kuendelea kuonesha kujali na kuthamini utumishi wa umma, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM** amefanya maboresho kwenye viwango vya posho. *Aaminie katika wema na kujali, hutenda na kuuishi wema.* Hivyo, Mheshimiwa Rais wetu ni mfano sahihi wa maneno haya katika jambo hili. Watumishi wa Umma wanauliza ***Nani kama Mama Samia? na wanasema Asante sana Mama!***

**83. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea na jitihada za kulipa madai ya Watumishi wa Umma pamoja na kupandisha madaraja watumishi wanaostahili. Tutaendelea kuboresha mazingira ya kazi na maslahi yao kadri uchumi wa nchi utakavyoruhusu bila kuathiri makundi mengine ya wananchi, huduma mbalimbali pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika kuhakikisha maslahi ya wastaafu wetu waliotumikia Taifa hili kwa uzalendo, uadilifu na bidii kubwa wananufaika na michango waliyochangia katika mifuko ya hifadhi ya jamii, Serikali sikivu ya Mama yetu imeridhia kuongeza malipo ya mkupuo kwa wastaafu kufikia asilimia 33 badala ya asilimia 25 iliyopendekezwa mwaka 2018.

**84. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea na mikakati mbalimbali ya kulipa madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii. Katika mwaka 2021/22, Serikali ilitoa hatifungani maalumu yenye thamani ya shilingi trilioni 2.18 kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma - PSSSF linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya

mwaka 1999. Mwaka 2022/23, Serikali itaendelea na uhakiki wa madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii na kulipa deni stahiki. Lengo ni kuhakikisha watumishi wanalipwa kwa wakati mafao yao mara baada ya kustaafu pamoja na pensheni zao za kila mwezi.

### **Mazingira ya Biashara ndogo na Sekta Binafsi**

**85. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha azma ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ya kuwapanga, kuwasimamia, kuwalinda na kuwawezesha wafanyabiashara wadogo inafikiwa, Serikali itaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha wajasiriamali hao wadogo wanaboreshewa mazingira ya kufanyia biashara. Aidha, Serikali itaendelea kuwatambua na kuwaunganisha na Taasisi za fedha ili waweze kupata mikopo nafuu. Vilevile, Serikali itaendelea kutenga maeneo na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wajasiriamali wadogo. Katika kuhakikisha utatuzi wa changamoto za machinga unakuwa shirikishi, Mheshimiwa Rais ameahidi kutoa shilingi milioni 10 kila mkoa kwa ajili ya kuimarisha uongozi wa machinga pamoja na ujenzi wa ofisi za machinga. Aidha, napendekeza kufanya mgao mpya wa mapato ya ndani ya halmashauri kama ifuatavyo: Asilimia 10 ya mapato ya vyanzo vya Halmashauri, napendekeza asilimia 5 iwe kwa ajili ya miundombinu na masoko ya machinga; asilimia 2 kwa vijana; asilimia 2 wanawake; na asilimia 1 kwa wenye ulemavu. Aidha, Serikali imetenga shilingi bilioni 45 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miundombinu na mtaji kwa machinga ambapo kila mkoa, machinga walioko kwenye maeneo yaliopangwa wawe na *revolving fund* ya shilingi bilioni 1 kwa utaratibu utakaowekwa.

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza jitihada za kurasimisha sekta isiyo rasmi ili inufaike na kuwa sekta rasmi, Serikali imepanga kuweka mazingira rafiki ya kisheria na kikanuni katika usajili na uendeshaji wa

biashara, kuharakisha usajili wa biashara kwa kuhakikisha usajili unakamilika ndani ya siku moja iwapo muombaji amekidhi masharti yanayohitajika, kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa biashara zinazorasimishwa, kuongeza upatikanaji wa huduma kama miundominu ya biashara, mafunzo teknolojia na masoko. Vilevile, Serikali imepanga kuongeza vituo atamizi vya kukuza biashara na maeneo maalumu ya viwanda.

**87. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika uwekezaji, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kupitia utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini ili sekta binafsi iweze kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa nchi. Mwaka 2021/22, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ilishiriki majadiliano ya kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo katika kufanya biashara katika masoko ya nchi mbalimbali ikiwemo Kenya ambapo vikwazo visivyo vya kikodi 42 kati ya 64 vimepatiwa ufumbuzi. Hali hiyo iliwezesha ustawi wa biashara baina ya Tanzania na Kenya. Aidha, kupitia Sheria ya Fedha 2022/23, Serikali inapendekeza kufanya maboresho ya jumla ya maeneo 19 ya sheria mbalimbali ili kuboresha zaidi mazingira ya biashara na uwekezaji kama nitakavyoeleza baadae.

**88. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuratibu ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji unaofanyika hapa nchini (**Local Content**) ambapo jumla ya ajira 72,395 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zilizalishwa katika mwaka 2021. Vilevile, miradi ya kimkakati ilitoa kandarasi ndogo ndogo kwa kuingia mikataba na kampuni 2,019 za watanzania kwa huduma za chakula, ulinzi, biashara, bidhaa za ujenzi kama vile saruji, nondo, kokoto, mchanga, kampuni za usafiri, kampuni za bima na kampuni za mafuta. Kadhalika, Serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha kuwa na mikataba



ya uwekezaji inasomana na sheria za kodi kwa ajili ya kutatua changamoto ya kutotekelezeka kwa baadhi ya miradi ya uwekezaji kutokana na kukinzana na sheria za kodi.

### **Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)**

**89. Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa miradi ya PPP, jumla ya miradi mitano (5) ipo katika hatua ya ununuzi wa mbia. Aidha, napenda kulliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza umepata mbia wa uendeshaji ambapo hatua inayofuata ni majadiliano na mbia husika. Hatua hii itaongeza ufanisi wa uendeshaji na utoaji wa huduma na mradi huu utakuwa mradi wa kielelezo uliopitia hatua zote zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya PPP, Sura 103. Upatikanaji wa wabia katika miradi ya PPP utaleta ahueni katika bajeti ya Serikali na hivyo kuwezesha kuongeza rasilimali fedha katika maeneo mengine na hivyo kuwaletea maendeleo watanzania. Serikali itaendelea kufanya tathmini ili kuboresha na kuipa nafasi sekta binafsi kushiriki katika kutekeleza miradi ya Serikali kwa mfumo wa Ubia na hivyo Serikali kujikita zaidi katika kuweka mazingira wezeshi na kuboresha huduma za kijamii.

**90. Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara kwa kuimarisha miundombinu wezeshi ya usafirishaji na nishati; kuhakikisha uhimilivu wa viashiria vya uchumi jumla; na kuwianisha tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na Wizara na Mamlaka za Udhhibiti kwa lengo la kupunguza na kurahisisha ulipaji wake na kuzifuta baadhi ya tozo na ada za kero. Aidha, mwaka 2022/23, Serikali itaendelea kufanya marekebisho ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali. Marekebisho hayo yanalenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi,

hususan katika sekta ya viwanda, uwekezaji na biashara pamoja na kuongeza ajira, mauzo nje, mapato na akiba ya fedha za kigeni. Vilevile, katika kuepusha malimbikizo ya marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani - VAT na kupunguza mzigo wa madai ya fedha kutokana na ucheleweshaji wa marejesho kwa sekta binafsi, Serikali itaanza mchakato wa kuhakiki marejesho ya VAT kwa njia ya kielektroniki kuanzia mwaka 2022/23.

## Sensa ya Watu na Makazi

**91. Mheshimiwa Spika**, kipaumbele kingine katika bajeti ya mwaka 2022/23 ni ugharamiaji wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika **tarehe 23 Agosti 2022**. Ili kuwezesha zoezi hili muhimu, Serikali imetenga jumla ya shilingi billioni 400.9. Aidha, napenda kutumia nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kuhimiza wananchi wote kutoa ushirikiano siku hiyo hasa ukizingatia zoezi hili ni jukumu la kila mtu. Ushiriki wetu utaiwezesha Serikali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na sekta binafsi kupata takwimu sahihi zitazokuwa msingi wa kuandaa, kutekeleza na kutathmini sera na mipango mbalimbali ya maendeleo katika nchi yetu.

## Lugha ya Kiswahili

**92. Mheshimiwa Spika**, lugha ya kiswahili ndio lugha ya Taifa, ndio lugha ya ofisini, ndio lugha ya pili kwa watoto wa vijijini na lugha ya kwanza kwa watoto waliowengi wa sasa, ndio lugha ya msingi, ni lugha ya Bunge, na nikiwa Waziri wa Katiba na Sheria nilileta mapendekezo kuifanya kuwa lugha ya Mahakama na lugha ya hukumu. Aidha, Kiswahili ni lugha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambapo tumeipeleka wenyewe, ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU). Vilevile, UNESCO wameitambua na watakuwa wanaiadhimisha tarehe 7 Julai kila mwaka. Hii ndiyo lugha yetu, kwa nini usaili wa mtoto wa

kitanzania anapotafuta kazi unafanyika kwa lugha ya Kingereza? Yaani afisa kilimo, afisa mifugo, mtumishi wa Serikali anakazi ya kuhudumia watanzania tunapima akili zake kwa kupima kingereza chake kwa ajili ya nini? Napendekeza saili zote zifanyike kwa Kiswahili, na kumbi zote za mikutano na ofisi za Serikali ziwe na vifaa vya kutafsiria lugha za kigeni na watafsiri ili tuweze kuienzi lugha yetu ya Taifa.

### **Sekta ya Michezo**

**93. Mheshimiwa Spika**, Serikali itarejeshah bahati nasibu ya taifa kwa utaratibu wa kutumia Sekta Binafsi. Sambamba na hiyo Serikali kupitia Bodi ya Michezo ya kubahatisha, TRA na Sekta Binafsi wataanza kuendesha bahati nasibu kwa kupitia risiti za EFD ili kuchochea wananchi kudai risiti wanaponunua bidhaa. Aidha, Serikali itatumia sehemu ya Mchango wa Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (Corporate Social Responsibility) kwa kiwango kisichozidi asilimia 2 kwa ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha ili kuendeleza michezo nchini ambapo makampuni yataruhusiwa kukitambua kiasi hicho kwenye mapato yanayostahili kutozwa kodi. Nitumie nafasi hii kuwahakikishia watanzania kuwa tutaweka nyasi bandia kwenye viwanja vitano kwa kuanzia Mwanza, Arusha, Tanga, Dodoma na Mbeya ili kukuza mchezo hapa nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 msamaha wa kodi kwenye nyasi bandia na vifaa ambata vyake utakwenda mpaka ngazi ya Halmashauri. Nitumie fursa hii kuzipongeza timu zetu za Serengeti Girls na Tembo Warriors zilizokata tiketi za kuiwakilisha nchi kwenye mashindano ya Dunia. Niitakie kila la heri timu yetu ya Taifa Stars ambayo bado iko kwenye kampeni za kutafuta tiketi ya mashindano ya kimataifa.

### **Mkakati wa Uchumi wa Buluu**

**94. Mheshimiwa Spika**, uchumi wa buluu kwa hapa Tanzania siyo jambo jipya kwani shughuli mbalimbali

zimekuwa zikifanyika katika maeneo yenye fursa hizi za kiuchumi. Katika maeneo hayo, fursa za uwekezaji zinazopatikana ni za uvuvi wa samaki, ufugaji wa samaki, madini ya chumvi, utafutaji wa gesi na mafuta, kilimo cha mwani, utalii wa fukwe, usafiri na usafirishaji, utunzaji wa mazingira, na kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa fursa nyingi katika eneo hili, bado mchango wake katika uchumi ni mdogo ikilinganishwa na uwezo uliopo. Hii ni kutokana na kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kuongoza na kuelekeza uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali hizo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo. **Mheshimiwa Spika**, sekta zilizoko katika eneo hili hazijawa na uratibu mzuri na kila moja inajifanyia shughuli zake bila utaratibu maalum na ushirikishaji wa kutosha wa wadau katika tasnia hii. Kama fursa hizo zingetumika kikamilifu, zingeweza kuwa kichocheo cha kukua kwa uchumi, chanzo cha chakula na ajira, msingi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kukuza viwanda, kupunguza umaskini na kuongeza mapato ya Serikali.

**95. Mheshimiwa Spika**, kufuatia umuhimu wa sekta hii, Serikali inakamilisha maandalizi ya Mkakati wa Uchumi wa Buluu ili kutambua mchango wa sekta hiyo katika uchumi na ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Ibara ya 27. Mkakati huo unaandaliwa kwa njia shirikishi inayohusisha wadau wa sekta ya umma, sekta binafsi, washirika wa maendeleo na jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, shughuli nyingi zinazofanywa katika sekta za uchumi wa buluu ni biashara. Hivyo, sekta binafsi inatarajiwa kuwa na jukumu muhimu katika kufadhili mkakati huo. Serikali itajikita zaidi katika kujenga mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. Fedha za Serikali zitaelekezwa maeneo ambayo sekta binafsi ina hamu ndogo ikiwa ni pamoja na miundombinu wezeshi, kuweka mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi ya usimamizi na matumizi endelevu

ya rasilimali hizo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

## **Mikakati ya Kupunguza Makali ya Maisha kwa Mwananchi**

**96. Mheshimiwa Spika**, Serikali itachukua hatua za makusudi ili kupunguza makali ya maisha kwa mwananchi yaliyotokana na athari za vita. Hatua zitakazochukuliwa kukabiliana na hali hiyo ni kama ifuatavyo: **kuhusu ongezeko la bei za mafuta ya petroli**: Serikali imepunguza tozo mbalimbali zilizokuwa kwenye ukokotoaji wa bei ya nishati ya mafuta. Aidha, Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kupunguza bei za nishati ya mafuta hapa nchini. Vilevile, Serikali inachukua hatua nyingine katika suala hili ikiwemo: kuendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza bei ya nishati ya mafuta; kuruhusu watu wenye uwezo wa kuleta mafuta kwa bei nafuu; kuanzisha mfuko wa kuhimili ukali wa bei za mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund*) baada ya bei za mafuta kutulia katika soko la dunia; kuanzisha hifadhi ya mafuta ya kimkakati (*National Strategic Petroleum Reserve*); na kuanzisha upokeaji wa mafuta katika ghala moja (*Single Receiving Terminal - SRT*).

**97. Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la bei za mafuta ya kula**: Serikali itaweka mikakati ya kikodi ili kutoa unafuu wa uagizaji wa mafuta ghafi ya kula kwa wachakataji wa ndani kwa lengo la kuongeza uzalishaji, kupunguza bei ya bidhaa hiyo na kuongeza ajira. Aidha, Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo imesafisha na kusambaza kwa wakulima tani 2,000 za mbegu za alizeti zenye thamani ya shilingi bilioni 5.84 kwa utaratibu wa ruzuku kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula ambapo wastani wa tani 400,000 za alizeti na tani 100,000 za mafuta zinatarajiwa kuzalishwa. Vilevile, Wakala umezalisha mbegu-miche ya michikichi 121,292 ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya michikichi. Hatua hizi

kwa pamoja zitasaidia kuongeza upatikanaji wa mafuta na hatimaye kupunguza kasi ya kupanda kwa bei. **Napendekeza kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa nchini.**

**98. Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku ya mbolea:** Wote tunatambua umuhimu wa kilimo katika uchumi wetu na maendeleo ya wananchi. Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, tija ndogo pamoja na athari zinazoikumba dunia hivi sasa kutokana na vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine. Katika kuongeza tija na uzalishaji wa sekta hii na kumpunguzia mzigo mkulima, Serikali imejipanga kutoa unafuu wa upatikanaji wa pembejeo ikiwemo mbolea, zana za kilimo, viuatilifu, mbegu bora na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Katika kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbolea nchini, Serikali itatoa ruzuku ya mbolea na kuvipa kipaumbele viwanda vya ndani vya mbolea katika matumizi ya chokaa ili kupunguza gharama za uzalishaji. **Napendekeza kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye mbolea inayozalishwa nchini. Kiwango hiki kitahusu tu wazalishaji wa mbolea. Kadhalika, napendekeza kupunguza tozo ya mrahaba kwenye madini ya kuzalisha nishati na mbolea viwandani.**

**99. Mheshimiwa Spika,** Serikali inachukua hatua hizi zote ili kupunguza makali ya maisha kwa watanzania. Serikali imekubali kupunguza mapato yake ili mwananchi au mtanzania apate unafuu. Ruzuku kwenye nishati ni kwa ajili ya wananchi siyo kwa ajili ya makampuni. Wafanyabiashara tusitumie majanga kujinufaisha kwa gharama ya kuwaumiza wananchi kwa kutengeneza faida kubwa kuliko kipindi cha majanga. Kipindi cha matatizo ya kiuchumi kila mmoja anatakiwa kubadili makadirio yake ya kiuchumi. Tunatoa ruzuku ili kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo, kuleta unafuu kwa mwananchi.

**Naelekeza mamlaka zote zinazosimamia sekta za huduma wasimamie haki za wananchi ili azma ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ya kumpa nafuu mtanzania iweze kuwanufaisha watanzania.**

#### **IV. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA, TOZO NA HATUA NYINGINE ZA MAPATO**

**100. Mheshimiwa Spika**, kuanzia kipindi cha mwaka 2019/20, Dunia imepita kwenye changamoto kubwa ya kiuchumi kufuatia kuenea kwa janga la UVIKO-19 na baadaye kuzuka kwa vita ya Urusi na Ukraine Februari 2022. Hii imeathiri si tu upatikanaji wa bidhaa muhimu katika soko la Tanzania lakini pia imesababisha mfumuko wa bei, kupanda kwa gharama za maisha na kuathiri ukuaji wa uchumi nchini. Athari za kiuchumi zilizoanza kujitokeza ni pamoja na kupungua kwa uzalishaji viwandani na mashambani kulikosababishwa na changamoto ya upatikanaji wa malighafi muhimu za viwandani na kilimo kama vile ngano, mbolea na mafuta ghafi. Hatua za mapato kwa mwaka 2022/23 zinalenga *"Kuongeza kasi ya Kufufua Uchumi na Kuimarisha Sekta za Uzalishaji kwa ajili ya Kuboresha Maisha ya Watanzania"*.

**101. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maelezo hayo, napenda kuwasilisha mapendekezo ya kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi, ikiwemo baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali na kurekebisha taratibu za ukusanyaji na usimamiaji wa mapato ya Serikali. Marekebisho haya yamezingatia dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika. Vilevile, marekebisho yanatarajiwa kujibu maswali na kukidhi kiu ya jamii ya Watanzania yakilenga kuchachua shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ndani ya nchi kwa kuweka mkazo katika sekta za kimkakati kama vile kilimo, ufugaji na uvuvi, miundombinu ya umeme,

uchukuzi na usafirishaji na sekta za kijamii za elimu na afya ili kuboresha uzalishaji, kukuza uchumi jumla, kukuza ajira na hatimaye kupunguza ukali wa maisha ya wananchi. Aidha, hatua hizi zinalenga kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu sheria zifuatazo:

- (a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;
- (b) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;
- (c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;
- (d) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;
- (e) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290;
- (f) Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, SURA 263;
- (g) Sheria ya Madini, SURA 123;
- (h) Sheria ya Korosho, NAMBA 18;
- (i) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196,
- (j) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306;
- (k) Sheria ya Bima, SURA 394;
- (l) Sheria ya Magari ya Kigeni, SURA 84;
- (m) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, SURA 197;
- (n) Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;
- (o) Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (Blueprint) kwa kurekebisha Ada na Tozo mbalimbali; na
- (p) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.

**(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148**

**102. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:

- (i) Kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye miti ambayo haijachakatwa (standing tree).



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Lengo la hatua hii ni kuchochea ukuaji wa sekta ya misitu, kuongeza ajira na kuwa na usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu. Hatua hii **itapunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 8,814. Hata hivyo, mapato yatakayoongezeka kutokana na ukuaji wa sekta ya misitu na mnyororo wake wa thamani ni shilingi milioni 16,125 na hivyo kuleta ongezeko katika sekta hii kwa kiwango cha shilingi milioni 7,311;**

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi zinazotumika kuzalisha mitungi ya gesi zinazotambulika kwa *HS Code* 7229.90.00, 3810.90.00, 3401.19.00, 7904.00.00, 4016.93.00, 8481.10.00 na 8309.90.90. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa mitungi ya gesi na kulinda viwanda vya ndani. Aidha, msamaha husika utatolewa baada yamzalishaji kusaini Mkataba wa Utekelezaji (Performance Agreement) na Serikali;

(iii) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kutambua mikopo mbadala inayofuata misingi na taratibu zilizo nje ya sekta ya fedha kwa asili yake ishughulikiwe sawa sawa (treated) na mikopo inayotolewa na benki katika utaratibu wa kawaida. Lengo la hatua hii ni kuchachua ukuaji wa bidhaa nyingine zenye lengo la kuchochea ukuaji wa biashara na uchumi na kuweka usawa katika ulipaji kodi;

(iv) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa mwaka mmoja ili kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula iliyopanda kutokana na mdororo wa uchumi;

(v) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye mbolea inayozalishwa nchini kwa mwaka mmoja. Kiwango hiki kitahusu tu wazalishaji wa mbolea tu. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu

kwa wakulima hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa uchumi duniani;

(vi) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha, mamlaka ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa wawekezaji mahiri maalumu baada ya kuidhinishwa na NISC kwa mujibu wa kifungu cha 20(8) cha Sheria ya Uwekezaji SURA, 38 pamoja na kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la hatua hii ni kufanikisha maendeleo ya sekta ya uwekezaji nchini na kuondoa mgongano wa kisheria kuhusu utoaji wa vivutio vya ziada vya kikodi kati ya Sheria ya Uwekezaji na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani;

(vii) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 11 (10) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuhusisha bidhaa za mtaji zinazotambulika kwa *heading* 87.16 na *HS Code* 8701.20.90 kwenye bidhaa za mtaji (capital goods) zinazostahili kupata ahirisho la Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT deferment). Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uwekezaji na kuchochea maendeleo ya viwanda nchini;

(viii) Kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vya kupima kiwango cha maji na unyevunyevu kwenye udongo (chameleon sensor reader) zinazotambulika kwa *HS Code* 9026.10.00, kifaa cha kupima kiasi kilichochukuliwa na udongo hasa katika eneo la mizizi ya mmea (wetting front detectors) kinachotambulika kwa *HS Code* 9031.80.00, kifaa cha kupima kiwango cha chumvi katika maji (electronic conductivity meter) kinachotambulika kwa *HS Code* 9027.80.00, na kifaa cha kupima kiwango cha naitrojeni katika hali ya naitreti (nitrate test strips) kinachotambulika kwa *HS Code* 9027.90.00. Lengo la hatua hii ni kukuza utafiti na kuendeleza sekta ya kilimo kwa ukuaji endelevu pamoja na kuongeza tija.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Msamaha utatolewa baada ya kupata uthibitisho wa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kilimo ili kuhakikisha msamaha husika unatumika kwa manufaa ya wakulima na si vinginevyo. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 2,995**;

(ix) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyandarua vinavyotumika katika uzalishaji wa mbogamboga na maua (Agro- net) vinavyotambulika kwa HS Code 56.08. Lengo la hatua hii ni kukuza sekta ya kilimo na kuongeza tija kwenye uzalishaji;

(x) Kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vya kupima kiwango cha unyevunyevu (moisture meter) vinavyotambulika kwa *HS Code* 9003.18.00, kifaa cha kupima kiwango cha mvua iliyonyesha (rain gauge for weather stations) kinachotambulika kwa *HS Code* 9023.00.90, kifaa cha kupima hali ya alkaline na tindikali (PH meters) kinachotambulika kwa *HS Code* 3822.00.90; kifaa cha kuzalisha miche/mbegu kwa chupa (tissue culture equipment) kinachotambulika kwa *HS Code* 8419.89.60; na kifaa cha kupima uwezo wa kuvutika (*tension metters*) kinachotambulika kwa *HS Code* 9031.81.00. lengo la hatua hii ni kuboresha utabiri wa hali ya hewa, kufahamisha mipango sahihi na kupunguza hatari zinazohusiana na kutokuwa na uhakika wa hali ya hewa na hali ya udongo. Msamaha utatolewa baada ya kupata uthibitisho wa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kilimo ili kuhakikisha msamaha husika unatumika kwa manufaa ya wakulima na si vinginevyo. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 1,634.52**;

(xi) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye magari yenye jokofu (refrigerated trucks) yanayotambulika kwa *HS Code* 8704.21.90, 8704.22.90,

8704.23.90, 8704.31.90, 8704.32.90, 8704.90.90 na vyumba vya ubaridi (cold rooms) vinavyotambulika kwa *HS Code* 9406.10.10 na 9406.9010. Hatua hii inalenga kuzuia mazao kuharibika baada ya mavuno na kuchochea kilimo cha kisasa. Msamaha utatolewa baada ya kupata uthibitisho wa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kilimo na au Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mifugo na uvuvi ili kuhakikisha msamaha husika unatumika kama ilivyokusudiwa na si vinginevyo. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 3,744.47**;

(xii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi za kutengeneza mbolea zinazotambulika kwa *HS Code* 2528.00.00, 2710.99.00 na 3505.20.00 na mashine za kutengeneza mbolea zinazotambulika kwa Sura (Chapter) 84 na 85 ya Kitabu cha Ushuru wa pamoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbolea na kuvutia uwekezaji nchini. Msamaha utatolewa baada ya kupata uthibitisho wa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya viwanda ili kuhakikisha msamaha husika unatumika kwa manufaa ya wazalishaji wa mbolea na si vinginevyo. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 139**;

(xiii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vanilla ya kijani isiyochakatwa inayotambulika kwa *HS Code* 0905.10.00 ili kuleta usawa na mazao mengine yasiyochakatwa ambayo husamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hatua hii inalenga vanilla isiyochakatwa kutoka nje ya nchi kuingizwa na kuchakatwa hapa nchini na hivyo kuongeza ajira na fedha za kigeni. Vanilla inayolimwa hapa nchini haitoshelezi mahitaji ya kiwanda cha kuchakata zao hili. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 38**;

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(xiv) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye kamba za katani zinazozalishwa nchini. Lengo la hatua hii ni kukuza zao la katani na kuongeza ajira;

(xv) Kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mtindi (yoghurt) na maziwa yanayozalishwa kwa joto la juu na kudumu kwa muda mrefu (UHT Milk). Hatua hii inalenga kuwawezesha wazalishaji wa ndani kushindana kikanda na kimataifa, kuongeza ajira na kuboresha maisha ya watu. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 480**;

(xvi) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio vya maziwa (dairy packaging materials) vinavyotambulika kwa *HS Code 3923.30.00, 4819.10.00, 4819.20.00 na 4819.20.90*. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwenye sekta ya maziwa nchini na kuwawezesha wazalishaji wa ndani kushindana kwenye masoko ya kikanda na kimataifa. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 1,197**;

(xvii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye hereni za mifugo za kieletroniki (ear tag) zinazotambulika kwa *HS Code 3926.90.90*, meza za kuwekea hereni za mifugo (Automatic Turning Table/ Ear tag supporting table) zinazotambulika kwa *HS Code 8207.30.00*, *Ear tag Applicators* zinazotambulika kwa *HS Code 8456.90.00* na *Lessor beam Machines* zinazotambulika kwa *HS Code 9402.90.90*. Lengo la hatua hii ni kuleta ufanisi katika utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo nchini. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 794**;

(xviii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vya machinjio (stunning box) vinavyotambulika kwa *HS Code 8438.50.00* na *Skinning & dehidng pulling machines* zinazotambulika kwa *HS Code 8453.10.00*.

Hatua hii inalenga kuhamasisha ukuaji wa sekta ya mifugo, kuongeza ubora wa nyama na ngozi na kuhakikisha kuwa viwanda vya ndani vinapata malighafi za kutosha. Msamaha utatolewa baada ya kupata uthibitisho ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mifugo na uvuvi ili kuhakikisha msamaha husika unatumika kama ilivyokusudiwa na si vinginevyo. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 331.95**;

(xix) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mbegu za malisho zinazotambulika kwa *HS Code* 1209.25.00 (pasture grass seeds); *HS Code* 1209.21.00 (pasture legume seeds), *HS Code* 1209.29.00 (Pasture multiple tree seeds and pasture cuttings and rhizomes and stolons). Hatua hii inalenga kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za malisho za kutosha na kukuza sekta ya mifugo;

(xx) Kufanya marekebisho kwenye Kipengele cha 18 cha Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Msamaha ili kuhusisha vifaa na mashine zinazotumiwa na vyombo vya ulinzi na usalama (military and armed forces). Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ununuzi wa mashine na vifaa husika na kuimarisha mfumo wa ulinzi na usalama nchini. Msamaha utatolewa baada ya kupata uthibitisho wa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya ulinzi na usalama ili kuhakikisha msamaha husika unatumika kwa manufaa ya vyombo vya ulinzi na usalama na si vinginevyo;

(xxi) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa na mitambo ya hali ya hewa vinavyoingizwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA). Hatua hii inalenga kuimarisha mfumo ya utendaji kazi kwa kutumia vifaa vya kisasa kutabiri hali ya hewa kwa ajili ya mipango sahihi na usalama wa Taifa;

(xxii) Kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyavu za kuvulia (fishing net) zinazotambulika kwa *HS*

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

*Code* 3926.09.10; ndoano (fishing hooks) zinazotambulika kwa *HS Code* 9507.20.00; na kamba za kufungia ndoano (fishing lines) zinazotambulika kwa *HS Code* 9507.90.00 na 9507.30.00. Lengo la hatua hii ni kukuza wavuvi wadogo na kuchochea ukuaji wa Sekta ya Uvuvi;

(xxiii) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148 ili kuiwezesha Serikali kukusanya Kodi ya Ongezeko la Thamani katika biashara mtandao (digital services) bila kuathiri uwajibikaji chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332. Aidha marekebisho haya yanalenga kurahisisha utaratibu wa usajili wa walipakodi wanaotoa huduma za kidijitali bila ya kuwa na makazi hapa nchini (simplified registration). Hatua hii inalenga kwenda sambamba na mwamko wa shughuli za kibiashara duniani zinazofanyika kwa njia ya mtandao. Hatua hii inatarajiwa **kuiongezea** Serikali mapato ya **shilingi milioni 34,240**;

(xxiv) Kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye simu janja za Mkononi (Smartphones) *HS code* 8517.12.00, vishikwambi (Tablets) *HS Code* 8471.30.00 au 8517.12.00 na Modemu *HS Code* 8517.62.00 au 8517.69.00 kwa kuwa msamaha husika haujawezesha kupatikana kwa bidhaa hizo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara. Hatua hii inalenga **kuiongezea** Serikali mapato kiasi cha **Shilingi milioni 33,705**; na

(xxv) Kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za kukodi ndege (air charter services) kwani huduma hizi hutolewa kibiashara kama huduma za kukodi vyombo vingine vya usafiri ambazo kisheria hulipiwa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hatua hii inatarajiwa **kuiongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 36,545**.

Hatua zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 87,523.(b) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**103. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:

(i) Kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuweka kiwango cha asilimia 3.5 kwa walipakodi wenye mauzo yanayozidi shilingi milioni 11,000,000 lakini yasiyozidi shilingi milioni 100,000,000/= kwa mwaka (Presumptive Regime) kwa lengo la kuweka uwazi na kurahisisha makadirio na ulipaji wa kodi. Hatua hii itaongeza ulipaji kodi wa hiari na hivyo kuongeza mapato ya Serikali ambayo yanatarajiwa **kuongezeka** kwa **shilingi milioni 60,413.37**. Sambamba na pendekezo hili, inapendekezwa kufanya maboresho kwenye mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuwezesha malipo kufanyika kwa njia ya simu;

(ii) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ili kubainisha kuwa mikopo mbadala iliyoidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania inayotolewa na benki kwa wateja wake ambayo inahusisha ununuzi na uuzaji wa mali anazozihitaji mteja kwa faida inayowekwa juu ya gharama ya mali ni sawa na mikopo mingine ya kawaida. Hatua hii haimwondolei muuzaji wajibu wa kulipa kodi ya ongezeko la mtaji kwa mujibu wa Sheria katika muamala wa mauzo ya mali kwa mteja wa benki aliyenunua mali hiyo kupitia utaratibu wa mkopo mbadala. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanaweza kupata mikopo katika taasisi za fedha ikijumuisha wale ambao hawakubaliani na utaratibu wa riba;



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(iii) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 10 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha mamlaka ya kusamehe kodi ya mapato kwa wawekezaji mahiri maalumu baada ya kuidhinishwa na NISC kwa mujibu wa kifungu cha 20(8) cha Sheria ya Uwekezaji Sura ya 38, pamoja na kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la hatua hii ni kufanikisha maendeleo ya sekta ya uwekezaji nchini na kuondoa mgongano wa kisheria kuhusu utoaji wa vivutio vya ziada vya kikodi kati ya Sheria ya Uwekezaji na Sheria ya Kodi ya Mapato;

(iv) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuondoa msamaha wa kukata Kodi ya Zuo kwenye malipo ya upangishaji nyumba, vyumba na majengo ya biashara. Lengo la hatua hii ni kuwezesha wapangaji kukusanya kodi ya zuo kwenye pango na kuiwasilisha Serikalini. Aidha, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato ataingia makubaliano ya uwakala na OR - TAMISEMI juu ya usimamizi na ukusanyaji wa kodi hii;

(v) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Mtaji kwenye uhamishaji wa haki na taarifa za madini kwenda kwenye Kampuni za Ubia zinazoundwa baina ya Serikali na wawekezaji na uhamishaji wa hisa (Free Carried Interest) kutoka Kampuni ya Ubia kwenda kwa Serikali. Hatua hii inalenga kusaidia Serikali kutekeleza majukumu yake ya kimkataba na kuhakikisha kuwa uhamishaji na ubadilishaji wa haki na taarifa za madini unafanyika kwa wakati;

(vi) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Mtaji kwenye hisa ambazo Serikali imepata kupitia Msajili wa Hazina. Lengo la hatua hii ni kutatua changamoto zilizopo na kuhakikisha kuwa zoezi la ubadilishaji umiliki wa hisa hizo linafanyika kwa wakati;

(vii) Kusamehe kodi ya zuio kwenye Kuponi za Hati Fungani za Makampuni na Manispaa (Coupon for corporate and municipal bond). Pendekezo hili linalenga kuongeza vyanzo mbadala vya kugharamia miradi ya maendeleo (alternative financing);

(viii) Kupunguza kiwango cha kodi ya zuio kwenye tasnia ya filamu kwa malipo yanayofanyika kwenda kwa watoa huduma wa nje ya nchi kutoka asilimia 15 hadi asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kukuza tasnia ya filamu na kuchochea uhamishaji wa ujuzi kwenye tasnia hiyo kwa lengo la kuongeza ajira na kuboresha maisha;

(ix) Kutoza Kodi ya Mapato ya asilimia 2 kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wa kigeni. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 4,889.35**;

(x) Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo ya wachimbaji wadogo wa madini (Small Scale Miners). Hatua hii inalenga kuweka utaratibu maalum wa utozaji kodi kwa wachimbaji hao na kutatua changamoto zilizopo kwenye ukusanyaji kodi katika sekta hiyo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 37,290.40**;

(xi) Kutoza kiwango cha mfuto (flat rate) cha shilingi 3,500,000 ikiwa ni kodi ya mapato inayopaswa kulipwa kwa kila magari ya mizigo na mabasi ya abiria kwa mwaka. Lengo la hatua hii ni kuongeza uwazi katika makadirio ya kodi baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipakodi, kuweka mfumo wa kodi unaotabirika na kuongeza mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajiwa **kuongezea** Serikali mapato yanayokadiriwa kuwa **shilingi milioni 141,052**;

(xii) Kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya awali ya mapato (advance income tax) ya shilingi 20 kwa lita kwa wafanyabiashara rejareja wa mafuta ya petroli nchini itakayokusanywa na waingizaji wa mafuta hayo kwa jumla na kulipwa Serikalini. Lengo la hatua hii ni kurahisisha ulipaji kodi ya mapato kwenye vituo vya mafuta na kupunguza gharama za matumizi hususan karatasi za kutolea risiti za kielektroniki; Hatua hii inatarajiwa **kuiongezea** Serikali mapato yanayokadiriwa kuwa **shilingi milioni 59,820**. Hatua hizi za Kodi ya Mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 102,593**.

**(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**104. Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kifungu cha 124(2), marekebisho ya viwango maalum vya ushuru wa *bidhaa (specific duty rates)* kwa bidhaa zote zisizo za petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Hata hivyo, kutokana na biashara za bidhaa hizi kuzorota kutokana na athari za kiuchumi zilizosababishwa na kupanda bei kwa bidhaa za mafuta, **napendekeza kutokufanya mabadiliko ya viwango maalum vya Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa zote zisizo za petroli**. Aidha, hatua hii inazingatia kiwango kikubwa cha mfumuko wa bei nchini na azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, na hivyo kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya viwanda, kuvilinda na hatimaye kukuza ajira na mchango wa sekta hiyo kwenye pato la Taifa.

**105. Mheshimiwa Spika**, napendekeza pia kufanya **marekebisho ya Ushuru wa bidhaa** kwenye bidhaa zifuatazo:

(i) Kupunguza ada ya leseni kwa wazalishaji na waingizaji wa bidhaa zinazotowwa Ushuru wa Bidhaa

kutoka shilingi 500,000/= hadi shilingi 300,000/=. Hatua hii inalenga kuwapa unafuu wazalishaji na waingizaji wa bidhaa hizo pamoja na kusaidia kurejesha ukuaji wa Sekta baada ya athari za UVIKO-19 na athari zinazotokana na msukosuko wa kiuchumi duniani. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 77.4**. Utaratibu wa ukusanyaji wa kodi kwenye vitenge unafanywa na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania chini ya Sheria ya Pamoja ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;

(ii) Kusamehe Ushuru wa Bidhaa kwenye vifungashio vya maua, matunda, na mbogamboga vinavyotambulika kwa *HS Codes* 3923.29.00 (puneet, plastic cryovac bags, modified atmosphere packaging - MAP bags, plastic sleeves, perforated bags, poly packaging bags), *HS Code* 3921.12.90 (cling firm), *HS Code* 3902.90.00 (plastic liners). Lengo la hatua hii ni kuwapunguzia gharama wazalishaji wa matunda, mbogamboga na maua, na kuongeza usafirishaji wa bidhaa hizo nje ya nchi na hivyo kuongeza fedha za kigeni. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 653.12**;

(iii) Kutoza ushuru wa bidhaa wa shilingi 700 kwa kilo ya bidhaa za sukari (sugar confectionery) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na shilingi 500 kwa kilo ya bidhaa za sukari zinazozalishwa hapa nchini zinazotambuliwa kwa *HS Code* 1806.31.00, 1806.32.00, 1806.90.00, (chokoleti), 1905.31 (biskuti) na 1704 (chingamu). Viwango tofauti vinapendekezwa ili kulinda viwanda vya ndani. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 34,453.87**; na

(iv) Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwenye betri za maji (Lead-acid battery) kwa kiwango cha asilimia 5 zinazotambuliwa kwa *HS Code* 8507.10.00, na 8507.20.00. Hatua hii inalenga kupunguza madhara

ya mazingira yanayosababishwa na matumizi ya bidhaa hizo. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa shilingi **milioni 1,864.85**;

Hatua hizi za Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 50,292**.

**(d) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**

**106. Mheshimiwa Spika**, Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 ili kumrejeshwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha na Mipango mamlaka ya kusamehe riba na adhabu baada ya kushauriwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Lengo la hatua hii ni kuondoa changamoto zilizopo katika kutoa misamaha hii na kurahisisha upunguzaji au uondoaji wa riba na adhabu ya madeni. Aidha, Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango atatoa utaratibu wa utoaji wa misamaha hii kwa njia ya kanuni au kwa namna atakavyoona inafaa.

**(e) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290**

**107. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:

(i) Napendekeza Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290 ili kugawanya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri katika utaratibu ufuatao: asilimia 5 ipelekwe kwenye miundombinu na masoko ya machinga, asilimia 2 kwa ajili ya mikopo kwa vijana, asilimia 2 kwa ajili ya wanawake na asilimia 1 kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Lengo la hatua hii ni kuendeleza juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita zinazolenga kuwawekea miundombinu wajasiriamali wadogo ili kuhakikisha wanapata maeneo ya kufanyia biashara kutokana na mikopo wanayopata;

(ii) Aidha, Halmashauri zihakikishe kuwa zinafanya tathmini ya vyanzo vya mapato kabla ya kuingia mikataba ya uwakala wa mapato kutoka kwenye vyanzo husika na kuhakikisha kwamba kiasi kinachokusanywa kinaendana na uwezo wa chanzo hicho. Sambamba na hilo naelekeza kuwa fedha zote zinazokusanywa kwa njia ya *Point of Sale* (POS) zinazojulikana kama mapato ghafi zihamishiwe benki katika kipindi kisichozidi siku saba kutokea kukusanywa kwa mapato hayo na Halmashauri zihakikishe kuwa fedha zinazokusanywa kwenye Halmashauri za Serikali za Mitaa zinahasibiwa kikamilifu;

(iii) Kusamehe Ushuru wa Mazao kwenye mbegu (seeds). Hatua hii inalenga kuwapa unafuu wakulima na kuongeza tija kwenye uzalishaji mazao mbalimbali;

(iv) Kupunguza Ushuru wa Mazao ya misitu (forest produce cess) kutoka asilimia 5 hadi asilimia 3. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu na kukuza sekta ya misitu;

(v) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 16(7) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura 290 ili kubainisha kwamba Makampuni/Taasisi/Biashara/ Watu binafsi wanaotakiwa kulipa Ushuru wa Huduma (service levy) kwenye Halmashauri moja wanatakiwa kulipa Ushuru wa Mazao (produce cess) kwenye Halmashauri nyingine ambako wananunua mazao ya kilimo au mazao mengine. Lengo la mapendekezo hayo ni kuhakikisha kwamba kila Halmashauri inanufaika na shughuli za kiuchumi zinazotekelezwa kwenye eneo lake la utawala ili kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa jamii; na

(vi) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 16 ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa mamlaka ya kuandaa Kanuni za ugawaji mapato yatokanayo na Ushuru wa Huduma kwenye

Makampuni/Taasisi/Bishara/Watu binafsi wanaotekeleza shughuli zao kwenye Halmashauri zaidi ya moja. Kifungu hiki kitamwezesha Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kutoa Mwongozo wa ugawaji wa mapato hayo kwa Halmashauri husika kulingana na hali halisi.

**(f) Sheria ya Mfuko wa Fidya kwa Wafanyakazi, Sura 263 108. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mfuko wa Fidya kwa Wafanyakazi kwa kupunguza kiwango cha mchango kwa sekta binafsi kutoka asilimia 0.6 inayotozwa sasa hadi asilimia 0.5 ya mapato ghafi ya wafanyakazi. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa katika uchangiaji kati ya wafanyakazi wa sekta binafsi na wa umma.

**(g) Sheria ya Madini, SURA 123 109. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Madini, Sura 123 kama ifuatavyo:

(i) Kupunguza kiwango cha mrabaha kutoka kwenye makaa ya mawe yanayotumika kama malighafi ya kuzalisha nishati viwandani kutoka asilimia 3 hadi asilimia 1. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji viwandani, kuchochea uwekezaji zaidi na kukuza ajira;

(ii) Kupunguza kiwango cha kutoza mrabaha (royalty) kutoka asilimia 6 hadi asilimia 4 kwa dhahabu inayouzwa kwenye vituo vya kusafishia madini (refinery centres). Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa vituo vilivyoanzishwa nchini vinapata malighafi ya kutosha kwa ajili ya kusafisha na hatimaye kuongeza ajira na mapato ya Serikali;

**(h) Sheria ya Korosho, Namba 18**

**110. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Korosho ili mapato

yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi yagawanywe kama ifuatavyo: asilimia 50 ipelekwe Wizara ya Kilimo kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo na Mfuko wa Kilimo (ADF); na asilimia 50 ipelekwe mfuko mkuu wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuchochea maendeleo ya Sekta ya kilimo na kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ruzuku na tafiti.

**(i) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196**

**111. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje kwa kuanza kutoza tozo ya asilimia 30 au dola za kimarekani 150 kwenye shaba chakavu (copper waste) zinazotambulika kwa HS Code 7204 na vyuma chakavu (scrap metals) zinazotambulika kwa HS Code 7404. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda husika. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 2,446**.

**(j) Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, SURA 437**

**112. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa kwa kupunguza tozo ya muamala kutoka kiwango kisichozidi shilingi 7,000 hadi kiwango kisichozidi shilingi 4,000 katika kila muamala wa kutuma au kutoa pesa. Punguzo hili ni sawa na asilimia 43 ya kiwango cha sasa. Sambamba na hilo, napendekeza kuongeza wigo wa tozo hiyo ili kuhusisha miamala yote ya kielektroniki. Lengo la hatua hii ni kupunguza makali ya maisha kwa mtanzania hasa katika kipindi hiki cha changamoto kubwa ya kiuchumi na kuweka usawa katika utozaji wa tozo hiyo.

**(k) Sheria ya Bima, SURA 394**

**113. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bima kwa kuongeza wigo wa bima ya lazima (mandatory insurance) kwa kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara,



bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje, vyombo vya baharini na vivuko. Hatua hii inalenga kuimarisha ushirikishwaji wa kifedha (financial inclusion) na kuongeza matumizi ya bima.

**(l) Sheria ya Magari ya Kigeni, SURA 84**

**114. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Magari ya Kigeni, SURA 84 ili kupunguza tozo ya magari yanayozidi ekseli 3 kutoka dola za kimarekani 16/100 km hadi dola za kimarekani 10/100 km. Lengo la hatua hii ni kuwianisha utozaji wa viwango vya tozo hizo katika ukanda wa EAC, SADC na COMESA.

**(m) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, SURA 197**

**115. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania kwa kuweka kiwango cha ukomo wa Serikali kukopa kuwa kiasi kisichozidi asilimia 18 ya mapato ya ndani yaliyoidhinishwa katika mwaka husika badala ya kiwango cha sasa cha moja ya nane ya mapato ya ndani yaliyokusanywa katika mwaka uliotangulia. Lengo la hatua hii ni kuwianisha kiwango husika na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuiwezesha Serikali kutekeleza Bajeti yake.

**(n) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

**116. Mheshimiwa Spika**, kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichofanyika tarehe 13 Mei, 2022 Mombasa Kenya, kilipendekeza kufanya marekebisho ya Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha (EAC-Common External Tariff) kwa mwaka wa Fedha 2022/23. Mapendekezo hayo yanalenga kuongeza kasi ya kufufua uchumi na kuimarisha Sekta za uzalishaji kwa ajili ya kuboresha maisha.

**117. Mheshimiwa Spika**, mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua

mpya na zinazoendelea ambazo zimekuwa zikitekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2021/22. Hatua hizo ni kama zifuatazo:

(i) Mapendekezo ya hatua mpya za Viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo: -

(a) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 au dola za Marekani 1.5 kwa kila mita moja ya mraba (square meter) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za marumaru zinazotambulika kwa HS Codes 6907.21.00; 6907.22.00; na 6907.23.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha marumaru, pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(b) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja (*Metric ton*) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye mabati yanayotambulika kwa HS Codes 7212.20.00; na 7226.99.00 kwa mwaka mmoja badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (*under-invoicing and under valuation*), na kulinda ajira pamoja na mapato ya Serikali;

(c) Kurejesha utozaji wa Ushuru wa Forodha wa kiwango cha asilimia 0 kutoka kiwango kilichokuwa kinatumika cha asilimia 25 kwenye mafuta ghafi ya kula (Crude Palm Oil) yanayotambulika kwa HS code 1511.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa mafuta ghafi hapa nchini ili wananchi waweze kupata mafuta ya kula kwa bei nafuu;

(d) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 0 kwenye mafuta ghafi ya soya, karanga, nazi na haradali zinazotambulika kwa HS

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

codes 1507.10.00; 1508.10.00; 1513.11.00; 1514.91.00; na 1515.11.00. Lengo la hatua hii ni kuonisha viwango vya mafuta haya ghafi vifanane na viwango vya mafuta ghafi ya alizeti, pamba na mafuta ghafi mengineyo ambayo viwango vyake ni asilimia 10. Aidha, hatua hii pia inalenga kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula nchini, kuongeza ajira pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi;

(e) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 500 kwa kila tani moja ya ujazo (*Metric ton*) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati na cha mwisho (semi-refined and refined) yanayotambulika kwa HS codes 1507.90.00; 1508.90.00; 1509; 1510.10.00; 1510.90.00; 1511.90.10; 1511.90.30; 1511.90.90; 1512.19.00; 1512.29.00; 1513.19.00; 1513.29.00; 1514.19.00; 1514.99.00; 1515.19.00; 1515.29.00; 1515.50.00; na 1515.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda na kuhamasisha uchakataji wa mbegu na mafuta ghafi yaliyoingizwa nchini ili kuongeza thamani ya bidhaa (value addition) na kukuza ajira;

(f) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye taulo za watoto (*Baby Diapers*) zinazotambulika kwa HS code 9619.00.90. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hii nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

(g) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (cotton yarn) zinazotambulika kwa *Headings* 52.05, 52.06 na 52.07 isipokuwa nyuzi za pamba zinazotambulika kwa HS Code 5205.23.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa

hiyo na kuongeza thamani ya zao la pamba (value addition) nchini;

(h) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwenye milango na madirisha ya *alluminium* na chuma yanayoagizwa kutoka nje yanayotambulika kwa HS Codes 7610.10.00 na 7308.30.00. Lengo la hatua hii ni kulinda wajasiriamali wa ndani wanaotengeneza bidhaa hizo, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

(i) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza viongeza ladha kwenye vyakula na vinywaji (*food flavors*) zinazotambulika kwa HS Code 1901.90.10; 3302.10.00; na 3505.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa bidhaa hizo nchini;

(j) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS Codes 4804.19.90; 4804.39.00; 4804.42.00; 4804.51.00; 4804.52.00; 4805.11.00; 4805.19.00; 4805.24.00; 4805.25.00; 4805.93.00; 4810.13.00; 4810.19.00; 4810.31.00; na 4810.32.00 zinazotumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio aina ya maboksi (corrugated boxes). Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa vifungashio hivyo hapa nchini ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi na kwa bei nafuu;

(k) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza vioo vizito (toughened glass) zinazotambulika kwa HS Codes 7005.10.00; 7005.21.00; 7005.29.00; na

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

7005.30.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa vioo hivyo nchini;

(l) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza nyaya za umeme (*electrical cables*) zinatambulika kwa HS Codes 7312.10.00; 7217.20.00; 7408.19.00; 7409.11.00; 7605.21.00; 2710.19.56; 3815.90.00; 5402.19.00; 5903.90.00; 7217.20.00; 7907.00.00; 7312.10.00; na 2712.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa nyaya hizo pamoja na kuvutia uwekezaji nchini;

(m) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (toilet soap) zinazotambulika kwa HS Code 3401.20.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni nchini, kuongeza ajira na mapato ya Serikali;

(n) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya kiwango cha asilimia 100 au dola za Marekani 460 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (*consumption sugar*) inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo (gap) la uzalishaji hapa nchini;

(o) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwenye hema za chuma (Prefabricated building) zinazotambulika kwa HS Code 9406.20.90 zitakazoagizwa na wafugaji, kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwenye sekta ya mifugo, kuvutia uwekezaji, kuongeza ajira, pamoja na mapato ya Serikali kutokana na uwekezaji;

(p) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwenye nywele bandia zinazotambulika kwa *Heading* 6704. Hatua hii inalenga kulinda wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo, kuongeza ajira pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(q) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwenye mafuta mengineyo ya petroli yanayotambulika kwa HS Code 2710.19.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu na kulinda watumiaji wa bidhaa hii;

(r) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 kwenye sigara za kielektroniki zinazotambulika kwa HS Code 8543.40.00. Lengo la hatua hii ni kulinda mnyororo wa thamani wa zao la tumbaku nchini, kulinda viwanda vya ndani, pamoja na kuongeza ajira;

(s) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kufanya marekebisho kwenye tafsiri (descriptions) ya HS Codes 7310.29.20 na 7612.90.10 ambapo awali zilikuwa zinatafsiri makasha ya kuhifadhia vinywaji pekee ambayo ushuru wa forodha ni asilimia 0 na sasa kujumuisha makasha ya kuhifadhia chakula ili yaweze kutozwa ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25. Lengo la marekebisho hayo ni kutoa unafuu kwenye vifungashio vya vyakula ili kulinda walaji.

(ii) Mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa Viwango vya Ushuru wa Forodha vya mwaka 2021/22 ni kama ifuatavyo; -

(a) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kwenye malighafi zinazotumika katika uzalishaji wa vifaa maalum vinavyotumika katika kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu (*UVIKO-19*) vikiwemo barakoa (*Masks*), kipukusi (*sanitizer*), mashine za kusaidia kupumua (*ventilators*), na mavazi maalum ya kujikinga yanayotumiwa na madaktari na wahudumu wa afya (*PPE*). Msamaha huu utatolewa kwa utaratibu wa "*duty remission*". Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wazalishaji wa vifaa hivyo hapa nchini ili kuongeza kasi katika kupambana na ugonjwa huo;

(b) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali (*Cash registers, Electronic Fiscal Device (EFD) Machines and Point of Sale (POS) machines*) zinazotambulika kwa HS Code 8470.50.00 na 8470.90.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya vifaa hivi katika kuhasibu mapato ya Serikali;

(c) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa maziwa kwa joto la juu yanayodumu kwa muda mrefu (*UHT Milk*) vinavyotambulika kwa HS code 4819.50.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa maziwa hapa nchini. Utaratibu wa *Duty Remission* utatumika kutoa unafuu huo;

(d) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifuniko vya chupa za mvinyo (corks and stoppers) vinavyotambulika kwa HS Code 4503.10.00 kwa kuzingatia kuwa havizalishwi hapa nchini. Hatua hii inalenga kuwapunguzia gharama wazalishaji wa mvinyo ili kuhamasisha na kuendeleza kilimo cha zao la zabibu nchini pamoja na ajira. Utaratibu wa *Duty Remission* utatumika kutoa unafuu huo;

(e) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 0 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye unga wa kakao unaoingizwa kutoka nje unaotambulika kwa HS Code 1805.00.00. Lengo ni kuchochea na kuhamasisha kilimo cha zao la kakao nchini pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(f) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia kahawa vinavyotumiwa na viwanda vya kusaga kahawa nchini. Vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika kwa HS codes 7310.21.00; 6305.10.00; 3923.50.10; 3923.50.90 na 3920.30.90. Hatua hii inalenga kuongeza thamani kwenye zao la kahawa na kuvipa unafuu wa gharama viwanda vinavyosaga kahawa hapa nchini. Utaratibu wa "*Duty Remission*" utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo;

(g) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia korosho. Vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS code 3923.21.00. Hatua hii inalenga kuongeza thamani kwenye zao la korosho na kuvipa unafuu wa gharama viwanda vinavyochakata korosho hapa nchini. Aidha utaratibu wa "*Duty Remission*" utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo;

(h) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia pamba (cotton lint). Vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika kama HS codes 3920.30.90; 6305.39.00 na 7217.90.00. Hatua hii inalenga kuvutia uwekezaji ili kuongeza thamani ya zao la pamba nchini;

(i) Kupunguza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 kwenye malighafi za



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kutengeneza taulo za watoto (*Baby Diapers*) zinazotumbulika kwa HS code 3506.91.00 *Hot Melt Adhesive; PE film* HS Code 3920.10.90, *Empty bag for Baby Diapers* HS Code 6305.33.00, *Plastic cask* HS Code 3926.90.90; na kiwango cha awali cha asilimia 10 kwenye *Super Absorbent Polymer* HS Code 3906.90.00, *Wet strength paper* HS Code 4803.00.00, *Non-woven* HS Code 5603.11.00, *Polyethylene laminated Nonwovens* HS Code 5903.90.00, *Spandex* HS Code 5402.44.00 na *Dust free paper* HS Code 4803.00.00. Aidha, msamaha huu utatolewa kwa utaratibu wa "*Duty Remission*". Hatua hii inalenga kutoa unafuu wa gharama za uzalishaji na kuongeza ajira;

(j) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifaa vinavyotumika katika kukata, kung'arisha na kuongeza thamani ya madini ya vito vinavyotambulika kwa HS Codes 6804.10.00; 7018.90.00; 7020.00.99; 3606.90.00; 6813.20.00; 8202.20.00; 8202.99.00; 8203.20.00; 8205.10.00; 8423.89.90; 8513.10.90; na 9002.19.00. Hatua hii inalenga kuchochea uongezaji wa thamani kwenye madini, kukuza ajira pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Utaratibu wa "*Duty Remission*" utatumika katika kuagiza vifaa hivyo;

(k) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya mbegu vinavyotambulika kwa HS codes 3923.29.00; 6305.10.00; 4 819.40.00; 7310.29.90; 6305.33.00; 6305.20.00; 6304.91.90 na 7607.19.90. Utaratibu utakaotumika kutoa unafuu huo ni wa "*Duty Remission*". Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbegu hapa nchini;

(l) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja ya ujazo (*Metric ton*) kwenye bidhaa za chuma kutegemea kiwango

kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 10 kwa mwaka mmoja. Bidhaa hizo ni *Flat - rolled products of iron or non-alloy steel and other alloy steel*. Bidhaa hizi zinatambulika kwa HS Codes 7209.16.00; 7209.17.00; 7209.18.00; 7209.26.00; 7209.27.00; 7209.28.00; 7209.90.00; 7211.23.00; 7211.90.00; 7225.50.0 na 7226.92.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya hapa nchini, kukuza ajira pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(m) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (*metric ton*) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (*metric ton*) kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS codes 7210.30.00; 7210.49.00; 7210.61.00; 7210.69.00; 7210.70.00 na 7210.90.00. Lengo la hatua hii ni kuwalinda wazalishaji wa bidhaa hizo hapa nchini kutokana na ushindani wa nje;

(n) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (*Metric ton*) kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika katika HS Code 7212.60.00 badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (*under-invoicing and under valuation*), pamoja na kulinda ajira na mapato ya Serikali;

(o) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (*Metric ton*) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (*Metric ton*) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

zinazotambulika kwa HS Code 7212.30.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (*under-invoicing and under valuation*), pamoja na kulinda ajira na mapato ya Serikali;

(p) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 250 badala ya kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (*metric ton*) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za chuma (*Reinforcement bars and hollow profile*) kwa mwaka mmoja. Hatua hii inahusu bidhaa zinazotambulika kwa HS Codes 7213.10.00; 7213.20.00; 7213.99.00; 7306.30.00; 7306.50.00; 7306.61.00; 7306.69.00; na 7306.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (*under-invoicing and under declaration*), pamoja na kulinda ajira na mapato ya Serikali;

(q) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 250 badala ya kiwango cha asilimia 10 kwenye bidhaa za chuma (*Flat-rolled products of other alloy steel, of a width of 600 mm or more*) zinazotambulika kwa HS Codes 7225.91.00; 7225.92.00; na 7225.99.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (*under-invoicing and under declaration*), pamoja na kulinda ajira na mapato ya Serikali,

(r) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 0 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za fito za plastiki zijulikanazo kama *PVC Profiles* zinazotambulika kwa HS Codes 3916.10.00; 3916.20.00; na 3916.90.00 ambazo hutumika kutengenezea fremu

za milango, madirisha n.k. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali;

(s) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini ambazo zinatambulika kwa HS code 4804.29.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha karatasi hizo hapa nchini;

(t) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa HS Codes 1001.99.10 na 1001.99.90 kwa utaratibu wa "*Duty Remission*" ambapo wanaonufaika na unafuu huu ni wenye viwanda vya kusaga ngano. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa viwanda vinavyozalisha unga wa ngano ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa za ngano kwa bei nafuu;

(u) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwenye bidhaa ijulikanayo kama "*Printed Aluminium Barrier Laminates*" (ABL) HS Code 3920.10.90 ambayo hutumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio vya dawa ya meno kwenye viwanda vya ndani. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa gharama kwa viwanda vinavyozalisha dawa ya meno nchini;

(v) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kutoka kiwango cha awali cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa "*Duty Remission*" kwenye malighafi ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama *RBD Palm Stearin* HS Code 1511.90.40 kwa viwanda vinavyotengeneza sabuni nchini. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda vya kuzalisha sabuni nchini;

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(w) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 1.35 kwa kila kilo moja ya viberiti (*safety match boxes*) vinavyotambuliwa kwenye HS code 3605.00.00 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha viberiti nchini dhidi ya bidhaa zenye ruzuku kutoka nje na hivyo kuwa na ushindani sawa katika soko;

(x) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo (*Metric ton*) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za chuma za misumari zinazotambulika kwa HS code 7317.00.00 (*nails, tacks, drawing pins, corrugated nails, and staples other than those of heading 83.05*) badala ya asilimia 25 pekee. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo nchini.

(y) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye maji ya kunywa (*mineral water*) yanayotambulika kwa HS code 2201.10.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha maji ya kunywa nchini;

(z) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye *Gypsum Powder* inayotambulika kwa HS code 2520.20.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa *Gypsum Powder* nchini;

(aa) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mitumba inayoingia kutoka nje badala ya asilimia 35 au dola za Marekani 0.40 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi kikubwa kwa lengo la kutoa unafuu kwa watumiaji nchini;

(bb) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza viatu vya ngozi na nguo. Lengo la hatua

hii ni kuhamasisha ukuaji wa sekta ya nguo na viatu vya ngozi nchini;

(cc) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotambulika kwa HS Codes 8702.10.99 na 8702.20.99 yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa mabasi hayo ili kurahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi;

(dd) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye matairi mapya ya pikipiki (new pneumatic tyres of rubber) yanayotambulika kwa HS Code 4011.40.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uzalishaji wa matairi hayo nchini kwa kuwa kuna malighafi za kutosha;

(ee) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye nyaya (wire of other alloy steel) zinazotambulika kwa HS Codes 7229.20.00 na 7229.90.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wazalishaji wanaotumia bidhaa hiyo kama malighafi;

(ff) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye *milk cans* zinazotambulika kwa HS Codes 7310.10.00 na 7310.29.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa vifungashio vya kuhifadhia maziwa ili kuwalinda walaji nchini;

(gg) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye *LABSA* (Organic surface-active agents - Anionic) inayotambulika kwa HS Code 3402.11.00 kwa utaratibu wa *Duty Remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni za unga na maji nchini;

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(hh) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuchakata ngozi zinazotambulika kwa HS Codes 3208.20.00 na 3210.00.10 kwa utaratibu wa *duty remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa ngozi nchini;

(ii) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mbolea zinazotambulika kwa HS Codes 2710.99.00, 2528.00.00 na 3505.20.00 kwa utaratibu wa *Duty Remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbolea nchini;

(jj) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya tumbaku iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Code 5310.10.00 kwa utaratibu wa *Duty Remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa tumbaku nchini;

(kk) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya chai iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Codes 4819.20.90, 5407.44.00 na 3923.29.00 kwa utaratibu wa *Duty Remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa chai (tea blenders) nchini;

(ll) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwa waunganishaji wa pikipiki za matairi matatu bila kujumuisha fremu ili ziweze kutengenezwana kuunganishwa hapa nchini (CKD for three-wheel motorcycles excluding chassis and its components) zinazotambulika kwa HS Code 8704.21.90 kwa utaratibu wa *Duty Remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waunganishaji wa pikipiki hizo nchini ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo;

(mm)Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mabomba ya plastiki (glass reinforced plastic pipes) zinazotambulika kwa HS Codes 3920.61.10, 7019.39.00, 7019.31.00,6006.90.00, 7019.12.00, 3920.10.10, 4016.93.00, na 3907.91.00 kwa utaratibu wa *duty remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa mabomba hayo nchini ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji; na

(nn) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kutoka kiwango cha asilimia 100 au dola za Marekani 460 kwa kila tani moja ya ujazo (metric tone) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya viwandani (*sugar for industrial use*) inayoagizwa kutoka nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuwezesha na kutoa unafuu kwenye viwanda vinavyotumia bidhaa hii kama malighafi.

(iii) Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikubaliana kiwango cha juu cha ushuru wa forodha cha zaidi ya asilimia 25 kuwa ni asilimia 35. Hivyo, Muundo mpya wa ushuru wa forodha wa EAC utakuwa katika mpangilio wa viwango vinne (Four Tariff Bands) yaani asilimia 0, asilimia 10, asilimia 25 na asilimia 35 na utekelezaji wake utaanza tarehe 1 Julai 2022. Bidhaa zitakazo tozwa ushuru wa asilimia 35 ni pamoja na nyama, samaki, bidhaa za mbogamboga na matunda, mafuta ya kula, Chai, magunia ya kitani, kahawa, siagi ya karanga, soseji (*sausages*), nyanya zilizosindikwa (*tomato sauces*), saruji, chumvi, sabuni, rangi za majengo, vinywaji, vipodozi na urembo, bidhaa za samani, bidhaa za ngozi, bidhaa za chuma, marumaru, pamoja na bidhaa za sukari kama vile chingamu (*chewing gum*), biskuti, peremende, na chokoleti (*chocolates*).



Hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 66,791**.

**(o) Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (Blueprint) kwa kurekebisha Ada na Tozo mbalimbali.**

**118. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufuta au kupunguza ada na tozo mbalimbali zinazotowwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hasa katika kipindi hiki cha changamoto kubwa ya kiuchumi kufuatia kuenea kwa janga la UVIKO-19 na baadaye kuzuka kwa vita ya Urusi na Ukraine. Hatua hizi ni sehemu ya mwendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment). Marekebisho hayo yatajumuisha:

**(i) Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

**(a) Sekta ya Mifugo**

Napendekeza kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye sekta ya mifugo kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Namba 5; na**

**(b) Sekta ya Uvuvi**

Napendekeza kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye sekta ya uvuvi kama ilivyoainishwa kwenye **Kiambatisho Namba 6.**

**(ii) Wizara ya Kilimo**

(a) Kufuta tozo ya shilingi 200 (impoundment fee) inayotowwa kwa kila mita ya mraba ya eneo la uso wa maji yaliyohifadhiwa kwenye mabwawa ya umwagiliaji. Hatua hii inalenga kupunguza gharama kwa wakulima wanaofanya kilimo cha umwagiliaji; na

(b) Kuongeza ada ya kibali cha kusafirisha mbolea nje ya nchi kutoka dola za kimarekani 0.2 kwa tani hadi dola za kimarekani 0.5 kwa tani. Lengo la hatua hii ni kuchochea uzalishaji wa mbolea nchini na kuongeza ajira. Hatua hii pia inaendana na dhima ya Serikali ya kuchochea maendeleo ya viwanda hapa nchini.

**(iii) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kuanzisha utaratibu wa kutoza ada ya shilingi 1,000 hadi 3,000 kwenye ada ya matumizi ya king'amuzi kulingana na kiwango cha matumizi.

**(iv) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**  
Napendekeza kuanzisha tozo ya asilimia 1.5 kwenye vifaa vinavyotumika kuzalisha, kusambaza, kudurufu na kutunza kazi za Sanaa, uandishi na ubunifu mwingine kama vile muziki, filamu, vitabu, picha na aina nyingine za kazi za ubunifu. Vifaa hivi ni *Radio/TV set enabling recording; Analogue audio recorders; Analogue video recorders; CD/DVD Copier; Digital Jukebox na MP 3 Player*. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 9,600**.

**(v) Shirika la Viwango Tanzania**

Kupunguza tozo ya kuthibitisha ubora wa shehena (Batch Certification Fee) za sukari zinazoingizwa nchini kutoka shilingi 6 kwa kilo hadi shilingi 2.5 kwa kilo. Lengo la hatua hii kupunguza gharama kwa waingizaji wa sukari nchini ili kutoa unafuu kwa wananchi.

**(vi) Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)**

Kufuta tozo ya kipimio cha mzio (peak expiratory flow test fee) inayotozwa shilingi 10,000 na tozo ya kipimo cha kilele (allergy test fee) inayotozwa shilingi 25,000. Pendekezo hili linatarajia kuchochea mazingira wezeshi ya biashara nchini hususan katika maeneo ya viwandani.

**(vii) Tume ya nguvu za mionzi Tanzania**

(a) Kupunguza ada ya Utambuzi wa Mionzi kutoka asilimia 0.2 ya Malipwani kwenda asilimi 0.1 ya Malipwani kwenye mizigo yote ya vyakula inayosafirishwa nje ya nchi ikiwa pamoja na mbolea, tumbaku na bidhaa za tumbaku na chakula cha msaada kinachoingizwa nchini. Lengo la hatua hii ni kupunguza tozo kero na gharama za biashara na hivyo kuchochea mauzo ya bidhaa nje ya nchi sambamba na kupunguza utoroshaji wa mazao hayo kwenda nchi jirani kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi ; na

(b) Kufanya Maboresho ya ada na tozo mbalimbali zinazotowwa na Tume ya Nguvu za Mionzi kama zilivyoainishwa kwenye *kiambatisho Namba 7* ;

**(viii) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji** Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi ya Zimamoto na Uokoaji Sura 427 kwa kupunguza ada na tozo mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye *kiambatisho Namba 8*. Lengo la hatua hii ni kupunguza tozo kero na gharama za biashara.

**(ix) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Jedwali la viwango vya tozo na ada la Kanuni za Michezo ya Kubahatisha chini ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Na. 41 kama ilivyoainishwa kwenye *kiambatisho Na 9*.

**(x) Idara ya Uhamiaji**

Mwaka wa fedha 2021/22 Serikali ilipitisha uamuzi wa kuondoa ada ya kibali cha kuingia nchini (VISA/PASS FEE) kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka nchi ya Msumbiji kwa ajili ya Mpango wa kubadilishana wanafunzi wa Elimu ya Juu baina ya Tanzania na Msumbiji (TAMOSE). Pamoja na uamuzi huo, napendekeza kuondoa tozo ya vibali vya ukaazi kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka nchi ya Msumbiji. Lengo la hatua hii ni kutekeleza matakwa ya

makubaliano kati ya nchi hiyo na Tanzania kuondoleana tozo hizo ambapo Msumbiji imeshaanza kutekeleza makubaliano hayo.

**119. Mheshimiwa Spika**, napendekeza pia kufanya maboresho ya Sheria mbalimbali ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kupunguza mwingiliano wa Sheria. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Kufuta kifungu cha 6(10) (b) (ii) na (iii) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ili kuwa na viwango vya kitaifa (National Standards) kwa kuzingatia kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Viwango Na. 2. Lengo la hatua hii ni kufanya jukumu la viwango vya kitaifa kubaki kwa Shirika la Viwango Tanzania pekee. Iwapo Mamlaka ya Mawasiliano itakuwa na mahitaji ya viwango, itashirikiana na Shirika la Viwango Tanzania;

(ii) Kufuta kifungu cha 7 (1) (b) (ii) na (iii) cha Sheria ya Udhhibiti wa Nishati na Maji, SURA 414 ili kubakisha jukumu la viwango vya kitaifa kubaki kwa Shirika la Viwango Tanzania pekee. Endapo kuna mahitaji ya viwango EWURA watawasiliana na Shirika la Viwango Tanzania;

(iii) Kufuta Kifungu cha 5(1) (c) (i) na (ii) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Na. 3 ili kazi ya viwango ifanywe na Shirika la Viwango Tanzania. Mahitaji ya viwango ya LATRA yatawasilishwa Shirika la Viwango Tanzania;

(iv) Kufuta Kifungu cha 5(2) (c) cha Sheria ya Pamba Na. 2 ya mwaka 2001 ili kubakiza jukumu la viwango kwa Shirika la Viwango Tanzania. Mahitaji ya viwango vya Bodi ya Pamba Tanzania yatawasilishwa Shirika la Viwango Tanzania;

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(v) Kufuta Kifungu cha 12(1) (b) na (c) cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania Na. 14 ya mwaka 2017 ili jukumu la viwango vya kitaifa libaki kwenye Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009. Mahitaji ya viwango ya TASAC yatawasilishwa Shirika la Viwango Tanzania;

(vi) Kufuta Kifungu cha 5 (1) (l) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na. 1 ya mwaka 2003 ili jukumu la viwango vya kitaifa libaki kwenye Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009. Mahitaji ya viwango ya TMDA yatawasilishwa Shirika la Viwango Tanzania;

(vii) Kufuta Kifungu cha 41 (1) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na. 1 ya mwaka 2003 ili kazi ya udhibiti wa machinjio ifanywe na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pekee;

(viii) Kufuta Kifungu cha 3(2) (g) cha Sheria ya Magonjwa na Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 ili chanjo zisajiliwe na TMDA pekee;

(ix) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 10 cha Sheria ya Tasnia ya Maziwa ili Bodi ya Maziwa iweze kufanya kufanya ukaguzi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania;

(x) Kufanya marekebisho kwenye maginal note ya Kifungu cha 46 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi ili kuondoa mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza majukumu ya Chama Cha Hakimiliki Tanzania. Aidha, napendekeza kuondoa neno "*society*" na kuweka neno "*Copyright Office*" kwenye Kifungu cha 46, 47, 48 na jedwali lake;

(xi) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 51 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi ili kuongeza sehemu mpya ya saba (PART VII) inayoweka hitaji la Collective Management Organisations kutoa taarifa ya hesabu zao zilizokaguliwa kwa Copyright Office kila mwaka na hivyo kuwa na uwajibikaji na kuimarisha

usimamizi wa masuala yanayohusu Hakimiliki na Hakishirikishi;

(xii) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Tasnia ya Pamba SURA 201 ili jukumu la kusimamia viwango vya pamba lifanywe na Shirika la Viwango Tanzania pekee;

(xiii) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 23 cha Sheria ya Utalii SURA, 65 ili kumpa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii mamlaka ya kutoa vibali baada ya kuridhiwa na Bodi;

(xiv) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 28 cha Sheria ya Mbolea SURA, 378 ili jukumu la kuandaa kanuni za viwango litekelezwe na Shirika la Viwango Tanzania pekee;

(xv) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 17 cha Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, SURA 297 ili kuweka sharti la OSHA kutoa leseni ndani ya siku 7 baada ya mwombaji kukidhi vigezo;

(xvi) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 35 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Urban Authority) SURA, 287 ili kuweka sharti la Mamlaka za Miji kuanzisha vituo vya pamoja kwa ajili ya uratibu, uhamasishaji na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara;

(xvii) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 113 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (District Authorities) SURA 288 ili kuweka sharti la Mamlaka za Vijiji kuanzisha vituo vya pamoja kwa ajili ya uratibu, uhamasishaji na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara;

(xviii) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 6, 7, na 8 cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa SURA, 290 ili kupunguza kiwango cha tozo ya kitanda siku (hotel levy) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 5; na

(xix) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 3 cha Sheria ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi SURA, 120 ili kuondoa mkanganyiko uliopo kati ya ngozi za wanyama wa majumbani na za wanyama pori.

**(p) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.**

**120. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa **Sheria ya Fedha ya mwaka 2022** na Matangazo ya Serikali (*Government Notices*).

**121. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hatua zilizobainishwa hapo juu, napendekeza kutoa tamko la biashara ya bima nchini kufanywa kwa ushindani kwa kufuata misingi ya soko huria kama ilivyo kwa biashara nyingine na kuyaelekeza mashirika ya bima yanayomilikiwa na Serikali ambayo ni Shirika la Bima la Taifa (NIC) na Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) kufanya biashara kiushundani kwa kutoa huduma bora tofauti na maelekezo yaliyopo sasa yanayoipatia NIC pekee fursa ya kupata biashara kutoka kwenye Taasisi za Umma.

**(q) Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi.**

**122. Mheshimiwa Spika**, hatua hizi za kikodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2022, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo.

## **V. SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2022/23**

**123. Mheshimiwa Spika**, Sura ya Bajeti kwa mwaka 2022/23 inaonesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 41.48 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika. Jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 28.02, sawa na asilimia 67.5 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuwa

shilingi trilioni 23.65 na mapato yasiyo ya kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 4.37.

**124. Mheshimiwa Spika**, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 4.65, sawa na asilimia 11.2 ya bajeti yote. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 5.78 kutoka soko la ndani ambapo shilingi trilioni 3.30 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na kiasi cha shilingi trilioni 2.48 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vilevile, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 3.03 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**125. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 41.48 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 26.48 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63.8 ya bajeti yote, ikijumuisha shilingi trilioni 11.31 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na gharama nyingine za Mfuko Mkuu na shilingi trilioni 9.83 kwa ajili ya mishahara ikiwemo nyongeza ya mshahara, upandishaji wa madaraja kwa watumishi na ajira mpya. Aidha, shilingi trilioni 5.34 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ikijumuisha shilingi bilioni 200.0 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi na wazabuni.

**126. Mheshimiwa Spika**, matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 15.0, sawa na asilimia 36.2 ya bajeti yote. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 12.31 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 82.0 ya bajeti ya maendeleo na shilingi trilioni 2.70 ni fedha za nje. Fedha za maendeleo za ndani zinajumuisha: shilingi trilioni 1.11 kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha Standard Gauge; shilingi trilioni 1.44 kwa ajili ya kugharamia mradi wa Kufua



**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Umeme wa Maji wa Julius Nyerere; shilingi trilioni 1.18 kwa ajili ya Mfuko wa Barabara; shilingi bilioni 944.1 kwa ajili ya mifuko ya Reli, Maji na REA; shilingi bilioni 570.0 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; shilingi bilioni 230.0 kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madeni yaliyohakikiwa ya wakandarasi; na shilingi bilioni 346.5 kwa ajili ya kugharamia elimumsingi bila ada.

**127. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza hapo awali, sura ya bajeti kwa mwaka 2022/23 ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.1.**

**Jedwali Na 1: Mfumo wa Bajeti Kwa Mwaka**

		<i>Shilingi Milioni</i>
<b>Mapato</b>		<b>BAJETI 2022/23</b>
<b>A.</b>	<b>Mapato ya Ndani</b>	<b>28,017,867</b>
	(i) Mapato TRA (kodi na yasiyo ya kodi)	23,652,758
	(ii) Mapato yasiyo ya kodi (MDAs na TR)	3,352,824
	(iii) Mapato ya Halmashauri	1,012,286
<b>B.</b>	<b>Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo</b>	<b>4,648,561</b>
	(i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS	1,949,480
	(ii) Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi	2,576,958
	(iii) Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta	122,123
<b>C.</b>	<b>Mikopo ya Ndani na Nje</b>	<b>8,814,152</b>
	(i) Mikopo ya Nje	3,034,004
	(ii) Mikopo ya Ndani	2,480,148
	(iii) Mikopo ya Ndani: Rollover	3,300,000
	<b>JUMNA YA MAPATO YOTE (A+B+C)</b>	<b>41,480,580</b>
	<b>Matumizi</b>	
<b>D.</b>	<b>Matumizi ya Kawaida</b>	<b>26,475,748</b>
	o/w (i) Mfuko Mkuu wa Serikali	11,308,365
	Malipo ya Riba Ndani	1,770,159
	Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover)	3,300,000
	Malipo ya Mtaji Nje	2,916,041
	Malipo ya Riba Nje	1,100,802
	- Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii	1,655,652
	Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu	565,710
	(i) Mshahara	9,830,753
	(ii) Matumizi Mengineyo (OC)	5,336,630
	Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa	200,000
	Matumizi ya Halmashauri (own source)	617,485
	Matumizi mengine	4,519,145
<b>E.</b>	<b>Matumizi ya Maendeleo</b>	<b>15,004,833</b>
	(i) Fedha za Ndani	12,305,752
	o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa	230,000
	o/w Ugharamiaji wa SGR	1,113,000
	o/w Ugharamiaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere	1,435,000
	o/w Matumizi ya Halmashauri	394,801
	o/w Miradi mingine	9,132,951
	(ii) Fedha za Nje	2,699,081
	<b>JUMLA YA MATUMIZI YOTE (D+E)</b>	<b>41,480,580</b>

*Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango*

## VI. HITIMISHO

**128. Mheshimiwa Spika**, maendeleo endelevu ya Taifa lolote duniani hujengwa kwa ushiriki wa wananchi wote chini ya uongozi madhubuti na shupavu. Bajeti hii ni muendelezo wa kuiishi dhana hiyo kwani imeandaliwa kwa kushirikisha makundi yote katika jamii yetu ya Tanzania. Makundi hayo ni wawakilishi wa wananchi ambao ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo, watalaamu mbalimbali kutoka taasisi za umma na binafsi pamoja na wananchi wa kawaida. Maoni yaliyowasilishwa na makundi hayo yamesaidia kuboresha maandalizi ya bajeti hii katika kupanga vipaumbele na sera zinazolenga kutatua changamoto mbalimbali katika nchi yetu. Kwa msingi huo, ni dhahiri kabisa hii ni **“Bajeti ya Wananchi”**, ni **“Bajeti Yetu Wote”** kwa ajili ya maendeleo yetu.

**129. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, bajeti ya mwaka 2022/23 inalenga kuongeza kasi ya kufufua uchumi na kuimarisha sekta za uzalishaji kwa ajili ya kuboresha maisha, hivyo nguvu kubwa itaelekezwa katika maeneo hayo chini ya kaulimbiu ya **“Kazi lendelee”**.

**130. Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele nilivyoviainisha awali, wote tunafahamu kuwa tafsiri ya dhana ya ukuaji wa uchumi ni lazima ifungamane na maendeleo ya mtu mmoja mmoja na familia za Watanzania wote na tunajua kuwa, **“Mama hawezi kumuacha mwanae apate tabu, Mama ana huruma, Mama anajali na Mama ana upendo kwa wanae”**. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya **“MAMA YETU”** Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imehakikisha kuwa, bajeti hii inaenda kugusa na kuboresha maisha ya watanzania wa hali zote kwa kuboresha sekta za uzalishaji. Hii itasaidia kuongeza ajira na vipato, kukabiliana na changamoto

mbalimbali ikiwemo mfumuko wa bei uliotokana na mabadiliko ya kiuchumi duniani na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**131. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kujenga misingi ya Taifa letu kujitegemea kiuchumi. Matunda ya mikakati hiyo yatafikiwa na kutunufaisha wote ikiwa kila mtanzania kwa nafasi yake atashiriki kwenye shughuli za uzalishaji mali zinazofuata sheria za nchi na kuchangamkia fursa za kiuchumi ili kujiongezea kipato na kuongeza mapato ya ndani ya Serikali. Hivyo, nawahimiza wananchi wote, taasisi za umma na binafsi kudai risiti sahihi wanapofanya ununuzi wa bidhaa na huduma ili kuhakikisha kuwa Serikali inakusanya kodi stahiki kutoka kwenye shughuli zinazofanyika. Vilevile, nawahimiza wafanyabiashara na kampuni zote kuwajibika kwa hiari katika ulipaji wa kodi kwa Serikali kutokana na shughuli wanazozifanya.

**132. Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza majukumu ya kuiletea maendeleo nchi yetu. Aidha, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa kuendelea kusimamia na kuratibu kazi za kila siku za Serikali na utendaji wa Serikali Bungeni kwa umahiri mkubwa pamoja na kumsaidia vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuiletea Taifa letu maendeleo. Vile vile, ninampongeza Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha

wa Mwaka 2022 na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Mwaka 2022.

**133. Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuwa mwanamke wa pili kushika uongozi wa Mhimili huu wa Bunge. Kipekee, nampongeza Naibu Spika ambaye ameungana nawe kuchaguliwa kwa kishindo katika nafasi za kuliongoza Bunge letu Tukufu. Tunategemea kuwa umakini, weledi, busara na hekima kubwa mliyodhihirisha katika nafasi mlizokuwa nazo zitaendelea kukua zaidi mnapotekeleza wajibu wenu katika nafasi hizi kubwa zaidi. Vilevile, nawapongeza Wenyekiti wa Bunge kwa kusimamia kwa ustadi wa hali ya juu kazi waliyopewa ya kuongoza vikao vya Bunge letu, kwa hakika mmekuwa msaada mkubwa sana katika uendeshaji wa Bunge kwa ujumla. Vilevile, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Daniel Baran Sillo - Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua - Mbunge wa Kilindi kwa maoni na ushauri wao mzuri katika kuboresha utendaji wa Wizara pamoja na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23.

**134. Mheshimiwa Spika** napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Hamisi Juma, **Jaji Mkuu wa Tanzania** kwa kazi nzuri ya kuongoza mhimili wa Mahakama. Kazi yenu ni nzuri sana na ni ya muhimu sana kwenye usitawi wa jamii, upendo na amani ya nchi. Neno la Mungu linasema, ***HAKI HUINUA TAIFA, BALI DHAMBI NI AIBU YA WATU WOTE (MITHALI 14:34)***. Endeleeeni kusimamia sheria na kutenda haki mtekelezapo majukumu yenu. Niwapongeze vyombo vya Ulinzi na Usalama vikiongozwa na JWTZ kwa kazi nzuri mnazozifanya, mmeiheshimisha Nchi yetu na kuifanya kuwa nchi ya tofauti duniani kote. Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kila wakati

anatuelekeza Wizara ya Fedha na Mipango tutekeleze bajeti zenu sawasawa na mahitaji yenu ili mtekeleze majukumu yenu kwa manufa ya watazania wote, nasi tutaendelea kufanya hivyo.

**135. Mheshimiwa Spika**, nawashukuru waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na wataalam wa Wizara zote na Taasisi za Serikali kwa michango waliyotoa ili kukamilisha Bajeti hii. Kwa unyenyekevu mkubwa, nawashukuru viongozi na waumini wa dini zote kwa kuendelea kuliomba Taifa letu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwaomba viongozi na waumini wa dini zote kuendelea kumuomba Rais wetu pamoja na viongozi wote wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mungu aendeleo kuwajalia afya njema, hekima, unyenyekevu na dhamira njema katika kusimamia rasilimali za nchi yetu katika utekelezaji wa majukumu yao.

**136. Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mheshimiwa Khamad Hassan Chande, Mbunge wa Jimbo la Kojani, ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano na msaada anaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, napenda kumshukuru Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa usimamizi wa kazi za kila siku za Wizara na uratibu mzuri wa maandalizi ya Bajeti hii, akisaidiwa na Naibu Makatibu Wakuu. Ninawashukuru pia wakuu wa taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango; Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara; pamoja na watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kukamilisha Bajeti hii.

**137. Mheshimwa Spika**, nipende kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya sita katika kuwaletea maendeleo wananchi wake. Washirika wanaotarajiwa

kuchangia bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23 ni pamoja na: Serikali za Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, Mashirika na Taasisi za Kimataifa zinazotarajiwa kuchangia bajeti hii ni Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Katika Afrika, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kuwait, Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria, Umoja wa Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Umoja wa Mataifa na mashirika yote yaliyopo chini yake, Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa, pamoja na Shirikisho la GAVI. Vilevile, ninapenda kuyatambua Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya ndani na nje ya nchi kwa michango yao kwenye sekta za kijamii kwa ajili ya ustawi wa watu wetu. Ninapenda kuwathibitishia kuwa, Serikali inathamini michango yenu na itaendelea kufungua fursa za ushirikiano.

**138. Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha,** nitumie fursa hii kuipongeza sana timu ya Yanga kwa mwenendo wao mzuri sana mwaka huu na nitumie fursa hii kumwomba radhi Bosi wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kitendo alichowafanyia mwanangu FEI TOTO kule Mwanza. Mniwie radhi, nilipompeleka FEI TOTO Yanga sikujua atakuja kuwafanyia kitumbaya hivi, mpaka nasikia anatafutwa maliasili eti kua mnyama bila kibali. Nakupongeza Mheshimiwa Anthony Mavunde wewe ndio ulikuwa Mwenyekiti wa kuisaidia Yanga ikiwa na mapito. Nampongeza GSM kwa kurejesha furaha ya wananchi hasahasa kwa udajili wa Fiston Mayele. Mayele amekuwa maarufu kuliko Makatibu wenezi wa baadhi ya vyama vya Siasa. Nawapongeza sana na marafiki zangu klabu ya Simba kwa kuwakilisha vyema kwenye mashindano ya Kimataifa, wananjua mara zote kimataifa tuko pamoja, siwezi kukana Bendera ya Taifa langu kwa ajili ya utani wa jadi.

**139. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuwasilisha hotuba hii. Kwa moyo wa dharti napenda kuishukuru familia yangu, mke wangu NEEMA NCHEMBA na watoto wangu, leo yupo Joshua MWIGULU na Mdogo wangu Peripetua Madelu, kwa kuendelea kunitia moyo na kuniombea wakati wote ninapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dharti wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya ubunge. Kadhalika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge na Watanzania Wote kwa kunisikiliza.

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA.  
KAZI IENDELEE!**

**140. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

CFS	8,643,560	9,532,987	
9,113,538	9,919,609		
9,656,017	10,663,278		
10,361,228	11,308,364		
Kulipa Madeni	7,234,530	8,133,063	
7,701,842	8,304,618	8,218,113	
8,878,420	8,612,067	9,087,002	
Malipo Mengine	1,409,030		
1,399,924	1,411,696		
1,614,991	1,437,904		
1,784,858	1,749,161		
2,221,362			

Matumizi ya Kawaida (Bila CFS)

9,501,407	9,462,087
9,663,058	10,286,658
10,917,280	13,048,841
12,867,625	15,167,383

Kiambatio Ika. 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato ya Semkali: 2016/17 -2022/23											Shilingi Milioni
	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22	2021/22	2021/22	2022/23	2022/23	
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Bajeti	Matarajio	Bajeti	Bajeti		
<b>Jumla ya Mapato ya Ndani</b>	16,639,933	17,944,887	18,527,293	21,069,957	20,594,735	25,691,735	24,350,024	28,017,867			
<b>A. Mapato yanyotokana na Kodi</b>	14,126,590	15,191,421	15,511,330	17,622,822	17,624,654	21,778,103	20,811,234	23,652,758			
1. Ushuru wa Faradha	998,164	1,109,205	1,201,045	1,253,272	1,266,114	1,504,414	1,444,238	1,629,283			
2. Ushuru wa Bidhaa	2,106,442	2,199,800	2,370,414	2,512,423	2,722,380	3,133,395	2,945,391	3,235,033			
3. Kodi ya Ongeseko la Thamani	3,912,674	4,425,968	4,736,876	4,987,319	5,029,231	5,940,766	5,406,097	6,361,863			
4. Kodi ya Mapato	5,117,862	5,157,106	5,072,402	6,490,240	6,015,741	6,866,152	7,072,137	8,091,001			
5. Kodi Nyingine	1,991,449	2,299,242	2,130,594	2,379,569	2,570,988	4,333,375	3,943,371	4,335,577			
<b>B. Mapato yasiyotokana na Kodi</b>	2,513,343	2,753,466	3,015,963	3,447,135	2,970,281	3,913,632	3,538,789	4,365,110			
1. Mchango na Gawio la Mashirika	893,935	803,502	682,331	738,810	636,399	779,033	755,662	2,572,075			
2. Wizaro Nyingine na Mkoa	1,107,690	1,408,464	1,674,534	1,991,076	1,576,826	2,270,741	1,884,715	780,749			
3. Mapato ya Halmashauri	511,718	541,499	659,098	717,249	757,055	863,858	898,412	1,012,286			
<b>Chanzo: Wizaro ya Fedha na Mipango</b>											



## Kiambalisho 2a: Mifumo wa Bajeti 2016/17 - 2022/23

Shilingi	Milioni	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22	2021/22	2021/22	2022/23
		Haliisi	Haliisi	Haliisi	Haliisi	Haliisi	Bajeti	Bajeti	Matarajio	Bajeti
I. Mopato Yote		25,417,791	26,439,542	28,962,515	29,515,050	32,274,882	37,992,548	37,992,548	36,347,273	41,480,580
Mipato ya Ndani		16,126,215	17,403,388	17,868,195	20,352,708	19,837,680	24,827,877	24,827,877	23,451,611	27,005,581
Mipato ya Halmashauri		511,718	541,499	659,098	717,249	757,055	863,858	863,858	898,412	1,012,286
Misaraada na Mikopo ya Bajeti		342,785	246,688	125,396	391,433	210,239	1,310,650	1,310,650	1,310,650	1,949,480
Misaraada na Mikopo ya Miradi		1,857,399	1,856,185	1,822,839	2,821,650	2,197,354	2,673,617	2,673,617	2,745,035	2,576,958
Mikopo ya Kieleta (Basket Loans)		104,991	74,681	44,281	166,027	77,107	59,736	59,736	52,090	122,123
Misaraada ya Kieleta (Basket Grants)		168,984	117,166	181,378	181,091	175,364	222,570	222,570	233,699	0
Mikopo ya Ndani (Borrower)		4,615,670	4,835,199	3,718,008	3,976,811	3,262,552	3,150,337	3,150,337	3,150,337	3,300,000
Mikopo ya Ndani (Financing)		1,300,000	869,200	3,037,177	376,924	3,359,220	1,838,796	1,838,796	1,838,796	2,480,148
Marekebisha		-838,731	-978,745	361,320	-1,290,936	-722,879	0	0	314,535	0
Mikopo ya kibikishara		1,226,760	1,474,282	1,144,822	1,822,093	3,121,190	3,045,107	3,045,107	2,352,107	3,034,004
II. Matumizi Yote		25,417,791	26,610,843	27,270,435	29,515,050	32,274,882	37,992,548	37,992,548	36,347,273	41,480,580
Matumizi ya Kawaida		18,144,967	18,995,074	18,776,596	20,206,266	20,573,298	23,712,119	23,712,119	23,228,853	26,475,747
CFS		8,643,560	9,532,987	9,113,538	9,919,609	9,656,017	10,663,278	10,663,278	10,361,228	11,308,364
Kulipa Madani		7,234,530	8,133,063	7,701,842	8,304,618	8,218,113	8,878,420	8,878,420	8,612,067	9,087,002
Matipo Mengine		1,409,030	1,399,924	1,411,696	1,614,991	1,437,904	1,784,858	1,784,858	1,749,161	2,221,362
Matumizi ya Kawaida (Bila CFS)		9,501,407	9,462,087	9,663,058	10,286,658	10,917,280	13,048,841	12,867,625	12,867,625	15,167,383
o/w Matipo ya Mshahara		5,999,246	5,544,384	5,699,188	5,939,616	6,141,566	6,912,184	6,912,184	6,843,063	8,619,577
Mshahara ya Mshahara		767,901	783,292	960,385	1,066,695	1,187,258	1,238,325	1,238,325	1,235,848	1,211,176
Fedha ya Halmashauri		251,484	216,600	349,322	419,428	447,419	533,325	533,325	554,658	617,485
Matumizi Mengine		2,882,775	2,917,811	2,654,163	2,860,918	3,141,037	4,365,007	4,365,007	4,234,057	4,719,145
Matumizi ya Maendeleo		7,272,824	7,615,768	8,493,838	9,308,784	11,701,584	14,280,429	14,280,429	13,118,419	15,004,833
Fedha za Ndani		5,141,451	5,397,034	6,535,879	6,840,104	9,251,759	11,324,506	11,324,506	10,192,055	12,305,752
Fedha za Nje		2,131,374	2,218,735	1,957,959	2,468,680	2,449,825	2,955,923	2,955,923	2,926,364	2,699,081
Pato la Taifa		113,553,41	122,835,22	132,049,54	143,297,78	152,349,15	155,005,47	155,005,47	167,286,24	188,202,76
		1	9	9	3	3	1	1	3	4
Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango										

Kiambalisho 2b: Mifumo wa Bajeti, Asilimia ya Pato la Taifa, 2016/17 - 2022/23											
	2014/17	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22	2021/22	2021/22	2021/22	2021/22	2022/23
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Bajeti	Bajeti	Matarajio	Bajeti	Bajeti	Bajeti
I. Mapato Yote	22.38%	21.52%	21.93%	20.60%	21.18%	24.51%	24.51%	21.73%	22.04%	21.73%	22.04%
Mapato ya Haimashauri	14.20%	14.17%	13.53%	14.20%	13.02%	16.02%	16.02%	14.02%	14.35%	14.02%	14.35%
Misada na Mikopo Natuu ya Bajeti	0.45%	0.42%	0.50%	0.50%	0.50%	0.56%	0.56%	0.54%	0.54%	0.54%	0.54%
Misada na Mikopo Natuu ya Mirafiki	0.30%	0.20%	0.09%	0.27%	0.14%	0.85%	0.85%	0.78%	1.04%	0.78%	1.04%
Mikopo ya Kisekta (Basket Loans)	1.64%	1.51%	1.38%	1.97%	1.44%	1.72%	1.72%	1.64%	1.37%	1.64%	1.37%
Misada ya Kisekta (Basket Grants)	0.09%	0.06%	0.03%	0.12%	0.05%	0.04%	0.04%	0.03%	0.06%	0.03%	0.06%
Mikopo ya Ndani (Rollover)	0.15%	0.10%	0.14%	0.13%	0.12%	0.14%	0.14%	0.14%	0.00%	0.14%	0.00%
Mikopo ya Ndani (financing)	4.06%	3.94%	2.82%	2.78%	2.14%	2.03%	2.03%	1.88%	1.75%	1.88%	1.75%
Marekebisha	1.14%	0.71%	2.30%	0.26%	2.20%	1.19%	1.19%	1.10%	1.32%	1.10%	1.32%
Mikopo yenye masharti ya kilaishara	-0.74%	-0.80%	0.27%	-0.90%	-0.47%	0.00%	0.00%	0.19%	0.00%	0.19%	0.00%
	1.08%	1.20%	0.87%	1.27%	2.05%	1.96%	1.96%	1.41%	1.61%	1.41%	1.61%
II. Matumizi Yote	22.38%	21.66%	20.65%	20.60%	21.18%	24.51%	24.51%	21.73%	22.04%	21.73%	22.04%
Matumizi ya Kawaida	15.98%	15.46%	14.22%	14.10%	13.50%	15.30%	15.30%	13.89%	14.07%	13.89%	14.07%
CFS	7.61%	7.76%	6.90%	6.92%	6.34%	6.88%	6.88%	6.19%	6.01%	6.19%	6.01%
Kulipa Madeni	6.37%	6.62%	5.83%	5.80%	5.39%	5.73%	5.73%	5.15%	4.83%	5.15%	4.83%
Malipo Mengine	1.24%	1.14%	1.07%	1.13%	0.94%	1.15%	1.15%	1.05%	1.18%	1.05%	1.18%
Matumizi ya Kawaida (Bila CFS)	8.37%	7.70%	7.32%	7.18%	7.17%	8.42%	8.42%	7.69%	8.06%	7.69%	8.06%
O/w Malipo ya Mshahara	4.93%	4.51%	4.32%	4.14%	4.03%	4.46%	4.46%	4.09%	4.58%	4.09%	4.58%
Mshahara ya Mshahara	0.68%	0.73%	0.73%	0.74%	0.78%	0.80%	0.80%	0.74%	0.64%	0.74%	0.64%
Fedha za Haimashauri	0.22%	0.18%	0.26%	0.29%	0.29%	0.34%	0.34%	0.33%	0.33%	0.33%	0.33%
Matumizi Mengine	2.54%	2.38%	2.01%	2.00%	2.06%	2.82%	2.82%	2.53%	2.51%	2.53%	2.51%
Matumizi ya Maendeleo	6.40%	6.20%	6.43%	6.50%	7.68%	9.21%	9.21%	7.84%	7.97%	7.84%	7.97%
Fedha za Ndani	4.53%	4.39%	4.95%	4.77%	6.07%	7.31%	7.31%	6.09%	6.54%	6.09%	6.54%
Fedha za Nje	1.88%	1.81%	1.48%	1.72%	1.61%	1.91%	1.91%	1.75%	1.43%	1.75%	1.43%
<b>Chanzo:</b> Wizara ya Fedha na Miungano											

Kimbatisho Na. 4: Kwenenda wa Mikopo ya Seikali (Millioni Shilingi)


	2020/21	2021/22	2022/23
<b>1. Jumla ya Mikopo mipya ya Ndani na Nje (a+b)</b>	<b>9,844,927.3</b>	<b>11,162,737.1</b>	<b>12,483,346.2</b>
<b>(a) Mikopo Mipya ya Ndani</b>	<b>4,904,247.6</b>	<b>4,989,132.9</b>	<b>5,780,146.1</b>
(i) Mikopo mipya ya Ndani (kupitia dharama za Seikali zilizoa)	3,316,078.4	3,150,336.7	3,300,000.0
(ii) Mikopo mipya ya Ndani (kubwa nakisi ya Bajeti)	1,588,169.2	1,838,796.2	2,480,146.1
<b>(b) Mikopo Mipya ya Nje</b>	<b>4,940,679.7</b>	<b>6,173,604.2</b>	<b>6,703,196.1</b>
(i) Mikopo yenye Mshahidi mawfu (Mkodzi ya Mwandiaji)	1,925,049.7	1,817,847.0	1,775,245.2
(ii) Mikopo yenye Mshahidi mawfu (Bajeti)	-	1,310,650.2	1,993,949.4
(iii) Mikopo yenye mshahidi ya kibabara	3,015,630.0	3,045,106.9	3,084,003.6
<b>(c) M alipo ya M ciani ya Ndani</b>	<b>4,946,747.0</b>	<b>4,711,974.1</b>	<b>5,070,159.0</b>
(i) M alipo ya M ciani ya Ndani za Seikali zilizawa (Railway)	3,316,078.4	3,150,336.7	3,300,000.0
(ii) Riba	1,630,668.6	1,561,637.4	1,770,159.0
<b>(d) M alipo ya M ciani ya Nje</b>	<b>3,703,194.5</b>	<b>4,146,445.8</b>	<b>4,016,845.5</b>
(i) Riba	1,259,913.84	1,151,376.3	1,100,802.0
(ii) M alipo	2,443,280.62	3,015,069.5	2,916,041.5
<b>(e) Ongeseko Hali la Mikopo ya Ndani (a-c)</b>	<b>1,588,169.2</b>	<b>1,838,796.2</b>	<b>2,480,146.1</b>
<b>(f) Ongeseko Hali la Mikopo ya Nje (b-d)(ii) / i</b>	<b>2,497,399.1</b>	<b>3,158,534.7</b>	<b>3,787,154.7</b>
<b>2. Ongeseko Hali la Mikopo ya Ndani na Nje (e+f)</b>	<b>4,085,568.3</b>	<b>4,997,330.9</b>	<b>6,267,304.7</b>

/ Ongeseko hii hujitishi hadha zilizozidolewa kupokolewa kwenye Mikopo ya zamani


Chanzo: Wazao ya Fedha na Mpango

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**Kielelezo Na. 3a: Vyanzo vya Fedha za Bajeti, 2022/23 Jumla**  
Shs. 41,480,580



**Kielelezo Na. 3b: Vyanzo vya Fedha za Bajeti, 2021/22**  
Jumla Shs. 37,992,548



(Hoja iliitolewa lamuliwe)

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ameshawasilisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali tayari kwa ajili ya Bunge kuyafanyia kazi katika kipindi cha siku zinazokuja hapo mbele, halafu baadaye tutaendelea na utaratibu wetu tutatoa maoni yetu na Serikali itatujibu na baadaye tutafanya maamuzi kwa maana ya kuhidhinisha kile ambacho tutakuwa tumekubaliana sisi Bunge, lakini pia na Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana hapo kwa muda mrefu sana ukizingatia alianza asubuhi, kwa hiyo nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nampongeza sana kwa mawasilisho hayo ambayo Waheshimiwa Wabunge tutaisikia Kamati yetu ya Bajeti baada ya kuyasikiliza haya na kuyasoma itatuletea maoni ya kamati halafu tutaendelea na michango hapo baadaye kwa mujibu wa taratibu zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wengi hapa ndani na mimi sitaki kuzungumzia alichokisoma Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwa utaratibu wetu tutazungumza hapo baadaye, ila nilikuwa tu nawatazama Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wanapiga makofi alivyosema anaongeza kodi kwenye nywele bandia. *(Kicheko)*

Nikawa natazama nasema mbona wanataka kunikatisha juhudi zangu maana niko katika safari moja hivi mheshimiwa Waziri itabidi anichangie.

Waheshimiwa Wabunge niwatangaze sasa wageni tulionao hapa Bungeni ambao wamekuja kuungana nasi siku

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ya muhimu sana siku ya leo. Tunaye kiongozi wetu wa kitaifa ambaye ni mstaafu Mheshimiwa Cleopa David Msuya ambaye ni Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu. Amepunga mkono pale nakushukuru sana, ahsante sana kiongozi wetu. *(Makofi)*

Lakini pia tunaye kiongozi wetu Mheshimiwa Balozi Hussein Kattanga ambaye ni Katibu Mkuu wetu Kiongozi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama yupo Jenerali Venance Salvatory Mabeyo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. *(Makofi)*

Jenerali inabidi usimame mpaka makofi yaishe, haya ahsanteni sana *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge kabla hajakaa ameniandikia barua kuhusu kustaafu kwake Jeshini, kwa hiyo hatutapata fursa kama hii ya yeye kuwepo hapa wakati nikisema haya na baadhi yenu mmeshamuona akionana na viongozi mbalimbali kwa ajili ya kuaga, lakini nichukue fursa hii kwa niaba yenu kwa sababu hapa ni Bungeni basi kwa niaba ya wananchi wa Tanzania kukushukuru sana kwa utumishi wako kwa Taifa hili. Ahsante sana na tunakutakia kila kheri katika yaliyombeke yako. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaye pia *IGP* Simon Sirro - Inspekta Jenerali wa Polisi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia ndugu Diwani Athuman Msuya, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Meja Jenerali Suleiman Mzee, Kamishna Jenerali wa Magereza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Dkt. Anna Makakala - Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Yupo pia John Masunga ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia CP Salum R. Hamduni ambaye ni Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Gerald Kusaya Musabila, Kamishna wa Kupambana na Dawa za Kulevya. *(Makofi)*

Yupo pia Luteni Jeneral Mathew Mkingule - Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Meja Jenerali Rajabu Mabele ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muwe mmeskiliza vizuri jina na cheo chake kwa sababu ndiyo mnaenda kukutana naye mnapoenda JKT, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaopia viongozi waandamizi wa Chama cha Mapinduzi na hapa tutaanza na Ndugu Daniel Chongolo ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Katibu Mkuu unasimama mpaka makofi yaishe. *(Makofi)*

Haya tunao Makatibu wa Bunge Wastaafu; Ndugu George Mlawa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Damian Foka naye ni Katibu wa Bunge Mstaafu, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi wengine waandamizi na wageni wetu mtuvumilie kidogo maana tunataka tuwatangaze wote na Waheshimiwa Wabunge pia mvumilie leo matangazo ya wageni hayaingii kwenye ile Kanuni tuliyobadilisha hapa.

Tunao wageni wengine Waandamizi, Mheshimiwa Antony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, karibu sana. Tunaye pia Profesa Devis Mwamfupe, Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Tunaye pia Ndugu Emmanuel Tutuba ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, karibu sana. Tunaye pia Dkt. Yamungu Kayandabila ambaye ni Naibu Gavana wa Benki Kuu, karibu sana. Tunaye Ndugu Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa TRA, karibu sana. Tunaye Ndugu Charles Kichere, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa. Sasa huyu amekuja kwa niaba yake, karibu sana. Tunaye Jaji Jacobs Mwambegele ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, karibu sana. Tunaye Brigedia Jenerali Andrew Chakila ambaye ni Mratibu Mkuu wa Baraza la Usalama la Taifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ipo pia familia ya Waziri wa Fedha na Mipango ambaye yeye ameshaitaja hapo wakiongozwa na Bi. Neema Nchemba, ambaye ni mke wa Waziri, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia viongozi wa dini, tutaanza na Askofu Nelson Kisare ambaye ni Askofu Mkuu wa Kanisa la Menonite na Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wa Dini Taifa, karibu sana; tunaye Sheikh Khamis Saidi Mataka, ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu BAKWATA na pia Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Viongozi wa Dini, karibu sana; tunaye Askofu Dkt. Fredrick Shoo, ambaye ni Mkuu wa KKKT na Mwenyekiti wa CCT, karibu sana; tunaye pia Askofu Peter Konki, ambaye ni Askofu Mkuu wa Makanisa ya Kipentekosti, karibu sana; tunaye pia Mchungaji Dkt. Canon Moses Matonya ambaye ni Katibu Mkuu Jumuiya ya Kikristo Tanzania, karibu sana; tunaye pia Askofu Antony Gasper Lagwen ambaye ni Askofu Mkuu Jimbo Katoliki Mbulu anamwakilisha Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), karibu sana; tunaye pia Sheikh Mustafa Rajabu ambaye ni Sheikh wa Mkoa wa Dodoma BAKWATA, karibu sana; tunaye pia Sheikh Jabir Nuhu Mruma ambaye ni Katibu Mkuu Baraza Kuu la Waislamu Tanzania BAKWATA, karibu sana. *(Makofi)*



Waheshimiwa Wabunge, tunao Mabalazi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa ambao wamewakilisha wenzao hapa; kwanza tunaye Mheshimiwa David Concar ambaye ni Balozi wa Uingereza nchini, sijui amekaa upande gani haya ameshasimama sawa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Leo Sacha Benmenni ambaye ni Balozi Mdogo wa Uswisi nchini, karibu sana; tunaye pia Mheshimiwa Trond Augdal ambaye ni Mwakilishi wa Balozi wa Norway nchini, karibu sana; tunaye Mheshimiwa Sandra Diesel ambaye ni Balozi Mdogo wa Sweden, karibu sana; tunaye Ndugu Lina Palmer, ambaye ni Mchumi Mkuu wa Sweden; tunaye pia ndugu Oscar Mkude, Mchumi na Mwakilishi wa Balozi wa Denmark Nchini, karibu sana; tunaye Ndugu Emmanuel Mungunasi, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkaazi wa Benki ya Dunia, karibu sana; tunaye Ndugu Zenah Amour, Mshauri wa Sera *UNICEF*, karibu sana; tunaye Ndugu Godfrey Mulissa, ambaye ni Mshauri Mwandamizi, akimuwakilisha Mkurugenzi Mkazi wa *UNDP*, karibu sana; tunaye Ndugu Francis Sampa ambaye ni Mchumi wa Ubalazi wa Uingereza karibu sana; yupo Silvester Ernest ambaye ni Mshauri wa Masuala ya Siasa Ubalazi wa Uingereza, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao watendaji wa taasisi pia za Serikali tutaanza na Jaji Sivangwilwa Mwangesi ambaye ni Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, karibu sana; tunaye Ndugu Gerson Mdemu, Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Kanda ya Dodoma, karibu sana; tunaye Dkt. Wilson Charles, ambaye ni Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema wageni tunao wengi na kwa namna ileile niliyosema tutatamani wote tuwatangaze sasa wako viongozi wengine wa Chama cha Mapinduzi ukiacha Katibu Mkuu; yupo Dkt. Edmund Mndolwa, ambaye ni Mwenyekiti Jumuiya ya Wazazi Chama cha Mapinduzi, karibu sana; yupo pia Ndugu Gaudensia Kabaka, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania, karibu sana; yupo pia Ndugu Gilbert Kalima ambaye ni Katibu Mkuu

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Jumuiya ya Wazazi, karibu sana; yupo pia Dkt. Philis Nyimbi, ambaye ni Katibu Mkuu Umoja wa Wanawake Tanzania, karibu sana; yuko pia Ndugu Musa Mwakitinya ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Vijana Tanzania, sioni jina hapa lakini Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana yupo ama yupo Naibu, sawa ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Salum Reja ambaye ni Katibu wa Sekretariat ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, karibu sana. Nimeambiwa hawa wapo na Maafisa wengine Ndugu Mary Mwenisongole na Ndugu Enock Joseph, karibuni sana wageni kutoka Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine yuko Ndugu Stella Manda ambaye ni Mtaalamu wa Bunge (*UN Women*), karibu sana; yupo Ndugu Usu Mallya ambaye ni Mshauri wa masuala ya Sera wa *UN Women*, karibu sana; yupo Ndugu Sharmistha DasBarwa, *UN Women*, karibu sana; yupo Ndugu James Mloe, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma *PSSSF*, karibu sana; yupo Ndugu Gilbert Kamanga, Mkurugenzi Mkuu wa *World Vision Tanzania*, karibu sana; yupo Ndugu Joseph Mayala, Mkurugenzi Mwandamizi *World Vision*; yupo Ndugu Chabu Mishwaro, Meneja wa Kanda CRDB Dodoma, karibu sana. Yupo Ndugu Grace Adam, Meneja Tawi la Bunge la *CRDB*, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Nelson Eden Mbunde, Meneja Mipango wa NMB Makao Makuu, karibu sana; yupo Ndugu Mesia Mwangoka, Mkurugenzi wa Mahusiano *TBL*, karibu sana; yupo Boma Rabala ambaye ni Afisa Mkuu wa Biashara CRDB, karibu sana; yupo Ndugu Msiba Mgaya, Mkuu wa Kitengo cha Fedha CRDB; yupo Ndugu Noelina Kivaria, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Serikali CRDB, karibu sana; yupo pia Patricia Mhando, Mkurugenzi wa Mahusiano ya Umma *TCC*, karibu sana; yupo pia Ndugu Tuse Mwaikasi, ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Umoja wa Mabenki, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ipo orodha pia ya Makatibu Wakuu walioko hapa Bungeni; tunaye Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Ikulu, karibu sana; yuko pia Dkt. Laurean

Ndumbaro, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, karibu sana; yuko pia Profesa Riziki Silas Shemdoe ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, haya ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mary Ngeleja Maganga ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, karibu sana; yupo Dkt. John Jingu ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, karibu sana; yupo Profesa Adam Katundu ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi wa Waziri Mkuu, Kazi Ajira Vijana na wenye Ulemavu, karibu sana; yupo Ndugu Emmanuel, huyu tulishamtambulisha. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Faraji Mnyepe, Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana; yupo Ndugu Mary Makondo, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, karibu sana; yupo Balozi Joseph Sokoine, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, karibu sana; yupo Ndugu Andrew Wilson Massawe, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, karibu sana; yupo Ndugu Tixon Nzunda, Katibu Mkuu Mifugo, karibu sana; yupo Dkt. Rashid Tamatamah, Katibu Mkuu Uvuvi, karibu sana; yupo Dkt. Allan Kijazi, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, karibu sana; yupo Dkt. Francis Michael, Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mhandisi Felchesmi Mramba ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, karibu sana; yupo Ndugu Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, karibu sana; yupo pia Mheshimiwa Balozi Mhandisi Aisha Amour ambaye ni Katibu Mkuu Ujenzi (Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi), karibu sana; yupo pia Ndugu Gabriel Joseph Migire, Katibu Mkuu Uchukuzi (Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi), karibu sana; yupo Profesa Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, karibu sana; yupo pia Dkt. Abel Nkono Makubi, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, karibu sana; yupo Profesa Eliamani Sedoyeka, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, karibu sana; yupo Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama,

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

karibu sana; yuko Dkt. Zainab Chaula, Katibu Mkuu, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Makundi Maalum, karibu sana; yupo Mhandisi Anthony Damian Sanga ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Maji, karibu sana; yupo pia Dkt. Hassan Said Abbas, Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, karibu sana; yupo pia Dkt. Jim Yonaz, Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, amesimama pale kwa niaba yake. *(Makofi)*

Wapo pia watendaji wa Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zake na hapa niwatambue Ndugu Jenifa Christian Omolo, Naibu Katibu Mkuu - Huduma za Hazina, karibu sana; yupo pia Ndugu Lawrence Mafuru ambaye Naibu Katibu Mkuu - Usimamizi wa Uchumi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Amina Khamis Shaabani ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Fedha za Umma, karibu sana; yupo pia Ndugu Julian Banzi, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, karibu sana; yupo pia Dkt. Albina Chuwa, Mtakwimu Mkuu Wa Serikali, karibu sana; yupo pia Ndugu Elijah Mwandumbya, Kamishna wa Sera, karibu sana; tunaye pia Ndugu Ncha Hassan Ncha, Naibu Kamishna TRA, karibu sana; tunaye pia Ndugu Japhet Justin, Kamishna wa Usimamizi wa Madeni, karibu sana; tunaye pia Dkt. Charles Mwamwaja, Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha, karibu sana; tunaye Dkt. Mursali Milanzi, Kamishna wa Mipango Kitaifa, karibu sana; yupo pia Dkt. Frederick Mwakibinga, Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Dkt. John Mboya ambaye ni Kamishna wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Binafsi, karibu sana; tunaye Ndugu Leonard Mkude, Mhasibu Mkuu wa Serikali, karibu sana; yupo pia Ndugu Athumani Selemani Mbutuka ambaye ni Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali, karibu sana; yupo pia Profesa Geraldine Rasheli ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Ununuzi Serikalini; yupo pia Ndugu James Mbalwe ambaye ni Mtendaji Mkuu Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, karibu sana; yupo pia Ndugu Bahati Ndeserua ambaye ni Katibu wa Bodi, Baraza la Rufani za Kodi,

karibu sana; yupo Ndugu Khadija Said ambaye ni Naibu Kamishna *TIRA*, karibu sana; yupo pia Ndugu Saimon Solomon CPA, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi; yupo pia Ndugu Eliakim Maswi, Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma, karibu sana; yupo pia Ndugu Florida Mapunda, Katibu Mtendaji, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma, karibu sana; na yupo pia Mgonya Benedicto, Msajili wa Hazina, karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Frank Nyabundege ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Kilimo, karibu sana; yupo pia Dkt. Tumaini Katunzi, Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki kwa Afrika (*EASTC*), karibu sana; lakini pia yupo Ndugu Simon Migangala, Mtendaji Mkuu wa *UTTAMIS*, karibu sana; yupo pia Ndugu Christopher Illomo, *SELF Microfinance Fund*, karibu sana; yupo pia Ndugu Profesa William Pallangyo, Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania, karibu sana; yupo Daktari Cairo Mwaitete, ambaye ni Kaimu Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha, karibu sana; yupo Ernest Mchanga, Katibu Tume ya Pamoja ya Fedha; yupo pia Ndugu Fatma Simba ambaye ni Kamishna Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; yupo pia Dkt. Emmanuel Mnzava, Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha, karibu sana; yupo pia Dkt. Elirehema Doriye, Mtendaji Mkuu, Shirika la Bima la Taifa; yupo pia Ndugu Godfrey Mbanyi, Mkurugenzi Mtendaji, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi; yupo pia *CPA* Nicodemus D. Mkama ambaye ni Mtendaji Mkuu, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, karibu sana; yupo pia Ndugu Mohamed Magati ambaye ni Msajili, Baraza la Rufaa za Kodi; yupo pia Ndugu Godfrey Malekano, Mtendaji Mkuu, Soko la Bidhaa Tanzania; yupo pia Dkt. Tausi Kida, Mkurugenzi Mtendaji, Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Jamii, karibu sana; yupo pia Ndugu Chotto Sendo, Mkurugenzi Mtendaji wa Usimamizi wa Mali za Serikali, karibu sana; yupo pia Ndugu Robert Mtengule, Kaimu Kamishna wa Fedha za Nje; na yupo pia Noela Nyasembwa, Naibu Katibu Mkuu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Alfred Mregi Kamishina Walipakodi Wakubwa; yupo pia Herbert Kabyemela Kamishina wa Kodi za Ndani; Ndugu Said

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Athuman - Kamishna wa Ushuru wa Forodha; yupo pia Ndugu William Mhoja Kamishina Msaidizi wa Sera; yupo pia Mariam Issa - Mratibu Kitengo cha Pensheni za Viongozi; yupo Ndugu Yudica Saruni - Kamishina Msaidizi wa Sera; yupo pia Ndugu Shumbi Mkumbo - Kamishina Msaidizi wa Sera na pia Dkt. Suleiman Misango ambaye ni Mtendaji wa Benki ya Taifa. *(Makofi)*

Sasa nimeletewa orodha hapa kwamba wapo viongozi wengine wa dini ambao hawakutambulishwa wakati wale wengine wakitambulishwa. Mmojawapo ni Askofu Brown Mwakipesile, Askofu wa Mkanisa ya *EAGT*, karibu sana kiongozi wetu na wageni wengine ambao nitakuwa sikuwataja nia ilikuwa ni kuwataja wote, kama kuna ambaye hajatajwa basi pengine majina hapa mbele yatakuwa hayajakamilika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo Watendaji wengine wa Mkoa wa Dodoma na hawa wanaongozwa na Ndugu Fatuma Mganga ambaye ni Katibu Tawala wa Dodoma. Karibu sana. Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaye pia Kanali Justace Kitta ambaye ni *Base* Kamanda wa JWTZ Dodoma, karibu sana; tunaye pia Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma Ndugu Benard Mpepo, karibu sana; tunaye pia Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini Jabiri Shekimweri, karibu sana Mheshimiwa; tunaye pia Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda - Mkuu wa Wilaya ya Bahi; tunaye pia Mheshimiwa Gift Msuya - Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Remedius Emmanuel - Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, karibu sana; tunaye Mheshimiwa Josephat Maganga - Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, karibu sana; tunaye Mheshimiwa Simon Chacha - Mkuu wa Wilaya ya Chemba, karibu sana; tunaye pia Mheshimiwa Dkt. Hamisi Mkanachi 0- Mkuu wa Wilaya ya Kondo, karibu sana; tunaye pia Brigedia Jenerali Andrew Chakila ambaye ni Mratibu

Mkuu wa Baraza la Usalama wa Taifa, huyu nadhani nilishamtaja mwanzo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge naambiwa kuna mgeni mwingine kutoka NMB Ndugu Juma Kimori - Afisa Mkuu wa Fedha, karibu sana; yupo pia Ndugu anaitwa Innocent Yonazi - Idara ya Mahusiano ya Biashara, karibu sana; yupo pia Vicent Mnyanyika ambaye anatoka Idara ya Mawasiliano, karibu sana; yupo pia Grace Matemu - Meneja wa Tawi la NMB Bunge. (*Makofi/Vigelele*)

Haya ahsanteni sana, lakini nimeletewa hapa taarifa kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Ndugu Kadio tunaye humu ndani pia, karibu sana, sana, sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Wakuu wa Vyombo vya Habari yupo Ndugu Gerson Msigwa - Msemaji Mkuu wa Serikali, karibu sana sijui yupo upande gani? Haya ahsante sana; yupo Dkt. Ayub Ryoba - Mkurugenzi Mkuu *TBC*, karibu sana; tunaye pia Dkt. Regina Mengi ambaye ni Mkurugenzi *IPP Media*, karibu sana; tunaye pia Ndugu Tido Mhando - Mtendaji Mkuu wa *Azam Media*, karibu sana. (*Makofi*)

Hawa wengine siwaoni humu ndani lakini labda wapo, Ndugu Nasib Abdul - Mkurugenzi wa *Wasafi Media*, haya sasa hapa orodha ni ndefu ya hawa viongozi wa vyombo vya habari na sijui kama wote wapo, lakini kwa ajili ya kutenda haki wacha niwataje asije akarukwa mtu ambaye yupo hapa ndani.

Ndugu Bakari Machumu - Mhariri Mkuu *Mwananchi Communications*, karibu sana; yupo pia Ndugu Tuma Abdallah ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji *TSN*, karibu sana; yupo pia Ndugu Shaaban Kisu ambaye ni Mkurugenzi Mkuu *Channel Ten* karibu sana, haya ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tunaye Ndugu Deodatus Balile - Mwenyekiti Jukwaa la Wahariri (*TEF*), karibu sana; tunaye Ndugu Kajubi Mkajanga

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT) NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

- Katibu Mtendaji Baraza la Vyombo vya Habari, karibu sana; tunaye pia Ndugu Ernest Sungura - Mkurugenzi Mkuu *Uhuru Media*, karibu sana; tunaye pia Ndugu Pascal Shelutete ambaye ni Mwenyekiti wa *TAGCO*, karibu sana; yupo Ndugu Salome Kitomari -Mwenyekiti *MISA Tanzania*, karibu sana; tunaye pia Ndugu Jacqueline Woisso ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji *Multichoice Tanzania*, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine hapa na hawa ni taasisi mbalimbali na Mashirika ambayo tuliyaalika; tunaye Ndugu Maharage Chande - Mtendaji Mkuu *TANESCO*, karibu sana, naona amewakilishwa; Ndugu Masha Mshomba - Mkurugenzi Mkuu *NSSF*, karibu sana; Ndugu Abdul Majid Nsekela - Afisa Mtendaji Mkuu CRDB nadhani amewakilishwa na viongozi wa CRDB; yupo Ndugu Ruth Zaipuna nadhani pia amewakilishwa na viongozi wa NMB. *(Makofi)*

Lakini yupo Mkurugenzi Mkuu wa *NHIF* Benard Konga; yupo Mtendaji Mkuu wa NBC Ndugu Theobald Msabi, karibu sana; yupo Ndugu Maduhu Kazi Mkurugenzi Mkuu *TIC*, karibu sana; yupo pia Ndugu Nehemia Mchechu - Mkurugenzi Mkuu *NHC*, haya ahsante sana; yupo pia Waziri Kindamba... *(Makofi)*

Haya jamani sasa majina hapa nadhani hawa wasaidizi wamechanganya mambo kidogo, lakini majina ya wakuu wa mashirika na taasisi za kifedha Waheshimiwa Wabunge tukubaliane wale waliotajwa wanawakilisha wenzao na watuwie radhi kwa sababu naona majina yamechanganywa kidogo hapa. Lakini sijui kama yupo Mkuu wa Chuo cha Biashara *(CBE)* Profesa Emmanuel Mjema, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Profesa Hozen Mayaya Mkuu wa Chuo cha Mipango, karibu sana; yupo pia Profesa Timoth Simalenga - Makamu Mkuu wa Chuo cha Mtakatifu John, karibu sana; lakini pia yupo mwakilishi wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Dodoma Ndugu Michael Salali Hosea, karibu sana, sana, sana. *(Makofi)*



Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni mwingine anaitwa James Ikechukwu Esomugha ambaye ni maarufu kama Jim Lyke, huyu ni muigizaji na maarufu kutoka Nigeria na mfanyabiashara pia sijui amekaa upande gani sijamuona sehemu aliyokaa, lakini tunawakaribisha wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulioko nao hapa ndani na wageni wetu karibuni sana, sana Bungeni, kwa wale ambao hatukuweza kuwasoma majina yao hapa mbele itakuwa tu ni bahati mbaya, lakini nia yetu ilikuwa tuwape heshima kama ninyi mlivyotupa heshima hii kubwa sana. Haya kwa hiyo, tunawashukuru sana, lakini naambiwa hapa yupo pia Askofu Dkt. Dickson Chilongani wa Kanisa la Anglikana Dodoma, karibu sana Askofu wetu. *(Makofi)*

Sasa kwa namna ya kipekee hawa viongozi wetu wa dini jamani wanatuombea sana, nadhani wote wasimame kwa pamoja, ili tutambue uwepo wao hata wale ambao tutakuwa hatukuwataja majina, hata waliotambulishwa wote tu wasimame kwa pamoja. Haya ahsanteni sana viongozi wetu kwa maombi yenu kwetu Wabunge, lakini pia kwa viongozi wa Taifa hili na kuliombea Taifa letu kwa ujumla tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge liko tangazo hapa mbele ambalo nilitangaza leo asubuhi niwakumbushe siku ya kesho saa 4.00 asubuhi tutakuwa na mdahalo katika Ukumbi wa Msekwa kuhusu hali ya uchumi, lakini pia kuhusu bajeti aliyoiwasilisha hapa Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana tukawasikilize wataalam, lakini na sisi tuchangie yale ya kwetu.

Waheshimiwa Wabunge, pia humu ndani siku ya leo wapo Menejimenti ya Bunge, hebu wasimame wote kwa pamoja, viongozi wetu wa Bungeni hapa hawa watendaji, tunawashukuru sana. Ahsanteni sana. Wanaongozwa na Katibu wa Bunge sasa Katibu wa Bunge yupo hapa ndani, kwa hiyo, hawezi kusimama nikiwa mimi nimesimama hapa mbele. Ahsanteni sana kwa kazi nzuri tunashukuru kwa kuja kuungana nasi muda huu. *(Makofi)*

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)NAKALA  
MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Nimeambiwa Mhandisi Ladislaus Matindi yuko humu ndani Mkurugenzi Mkuu wa *ATCL*, karibu sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu kwa Kanuni zetu siku ya kesho ni kwa ajili ya kutafakari Hali ya Uchumi lakini pia kutafakari bajeti. Kwa hivyo, kesho hakutakuwa na Bunge kwa maana ya humu ndani, tutakutana Msekwa kwa ajili ya kuendelea na tafakuri ya yale ambayo tumeyasikia siku ya leo.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Alhamisi saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 16 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*